

Hans-Jörg Ronsdorf

KUBADILI UPANDE

KUTOKA UTU WA **ZAMANI** HADI UTU **MPYA**



Kubadili Upande

Kutoka Utu wa Zamani hadi Utu Mpya
Hans-Jörg Ronsdorf

Christliche Literatur-Verbreitung e. V.

Postfach 11 01 35 · 33661 Bielefeld

Toleo la kwanza 2011

© 2011 by CLV · Christliche Literatur-Verbreitung

Postfach 11 01 35 · 33661 Bielefeld

Mtandao: www.clv.de

Muundo wa jalada: Andreas Fett, typtop, Meinerzhagen

Upangaji wa maandishi: CLV

Uchapishaji na ujalidi: GGP Media GmbH, Pößneck

ISBN 978-3-86699-310-5 (toleo la Kijerumani)

Yaliyomo

Dibaji	12
1. Safari ya ndege ya kuzunguka	14
2. Tumetua – na sasa tuendelee vipi?	25
2.1 Uhuru au utumwa – lakini si vyote viwili	25
2.2 Amri za uhuru	26
2.3 Kukimbia na kupinga	27
2.4 Hisia	27
2.5 Meli yenye nahodha wa zamani na nahodha mpya	28
2.6 Mbele kwa nguvu zote!	29
2.7 Baba yetu	30
2.8 Mungu anataka nini	31
2.9 YEYE hana budi kuzidi – bali mimi kupungua!	32
2.10 Maisha mapya katika mchoro	32
2.11 Yote kwa pamoja kwa mtazamo mmoja	35
2.12 Matembezi milimani	36
2.13 Kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo	37
2.14 Ni nini kilipaswa kutokea kwanza kwa ajili ya wokovu wetu?	38
3. Warumi 5:12-21: Kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo	39
3.1 Mstari wa 12: Jinsi yote yalivyoanza	40
3.1.1 Dhambi na matendo ya dhambi	40
3.1.2 Dhambi na mauti	41
3.1.3 Anguko na dhambi ya asili	42
3.1.4 Amri moja rahisi	43
3.2 Mstari wa 13: Dhambi kabla ya kutolewa kwa sheria	44
3.3 Mstari wa 14: Adamu, mfano wake yeye atakayekuja	45
3.3.1 Adamu na Kristo	45
3.4 Mstari wa 15: Kwa njia ya Kristo hasara inarekebishwa, na zaidi ya hapo	46
3.5 Mstari wa 16: Matokeo ya kosa na matokeo ya karama	46
3.6 Mstari wa 17: Utawala wa mauti unakomeshwa na Kristo	47
3.7 Mstari wa 18: Hukumu ya adhabu na kuhesabiwa haki kwenye uzima	48

3.8 Mstari wa 19: Nafasi ya kisheria ya wenye dhambi na nafasi ya wokovu ya wenye haki	49
3.9 Mstari wa 20: Sheria inafichua dhambi zote	50
3.10 Mstari wa 21: Kutoka mautini hadi uzima wa milele	51
3.11 Mapitio ya jumla ya Warumi 5:12-21	52
4. Warumi 6: Huru mbali na nguvu ya dhambi	53
4.1 Kubadili upande: Kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo	53
4.2 Mistari ya 1-2: Je, neema ni ruhusa ya kutenda dhambi?	54
4.2.1 Tumeifia dhambi na nguvu yake!	54
4.3 Mistari ya 3-4: Tumebatizwa katika Kristo na katika mauti yake	55
4.3.1 Ubatizo katika mauti	56
4.4 Mstari wa 4: Tumeufuliwa ili tuenende katika upya wa uzima	58
4.5 Mstari wa 5: Tumeunganika naye katika mauti yake na katika ufufuo wake	59
4.6 Mstari wa 6: Utu wa zamani umesulubiwa pamoja naye	60
4.6.1 Utu wa zamani	61
4.6.2 Kusulubiwa kwa utu wa zamani	62
4.6.3 Mwili wa dhambi	63
4.7 Mstari wa 7: Ameachiliwa huru mbali na dhambi	64
4.8 Mistari ya 8-9: Kushiriki mauti na uzima pamoja na Kristo	65
4.9 Mstari wa 10: Kristo aliifia dhambi	66
4.10 Mstari wa 11: Kujihesabu kuwa wafu kwa dhambi, bali walio hai kwa Mungu	67
4.11 Mstari wa 12: Utawala wa dhambi juu ya mwili unavunjwa	68
4.12 Mstari wa 13: Kujitoa sasa kwa Mungu	69
4.13 Mstari wa 14: Si chini ya sheria, bali chini ya neema	69
4.14 Muhtasari	70
4.15 Msalaba wa Golgotha na dhambi	71
4.16 Warumi 6:15-23: Waliowekwa huru wanaoishi chini ya neema	71
4.17 Ukweli wa wokovu na agizo la wokovu	72
4.18 Mstari wa 15: Lengo la neema	75
4.19 Mstari wa 16: Watumwa wa dhambi au wa haki	75
4.20 Mstari wa 17: Watiifu kwa moyo – si watumwa wa dhambi tena	75
4.21 Mstari wa 18: Watumwa wa haki	77
4.22 Mstari wa 19: Kujitoa kwa ajili ya haki na utakatifu wa Mungu	77

4.23 Mistari ya 20-22: Kutoka kukosa matunda hadi uzima wa milele	78
4.24 Mstari wa 23: Uzima wa milele badala ya adhabu ya milele	79
5. Sheria katika Waraka kwa Warumi	81
6. Warumi 7: Huru mbali na sheria	85
6.1 Maana ya Warumi 7 na nafasi yake	86
6.2 Vita vya Roho dhidi ya tabia ya mwili?	86
6.3 Wenye haki na wenye dhambi wakati mmoja?	87
6.4 Amezaliwa mara ya pili au la?	87
6.5 Warumi 7: Uzoefu wa lazima?	88
6.6 Mtu wa Warumi 7 ni nani?	90
6.7 Warumi 7:1-6: Tumeifia sheria	90
6.7.1 Mstari wa 1: Sheria inawahusu walio hai tu	90
6.7.2 Mistari ya 2-3: Njia pekee ya kuiepuka sheria	91
6.7.3 Mstari wa 4: Yeye ambaye sasa sisi ni mali yake – Kristo	91
6.7.4 Mstari wa 5: Sheria haizalishi haki, bali matendo ya dhambi	92
6.7.5 Mstari wa 6: Utumishi mpya usiotegemea sheria	93
6.8 Warumi 7:7-14: Sheria iliyo kamilifu	94
6.8.1 Mstari wa 7: Kuijua dhambi huja kwa njia ya sheria	95
6.8.2 Mstari wa 8: Sheria inaichochea dhambi	96
6.8.3 Mistari ya 9-11: Kukutana na sheria kunaleta mauti	96
6.8.4 Mstari wa 12: Hata hivyo sheria ni njema	98
6.8.5 Mstari wa 13: Kwa mara nyingine – kazi ya sheria	98
6.9 Warumi 7:14-25: Uzoefu wa Mkristo aliye chini ya sheria	99
6.9.1 Mistari ya 14-15: Nia njema na tabia ya mwili iliyo dhaifu	99
6.9.2 Mstari wa 16: Kukubaliana na sheria	99
6.9.3 Mistari ya 17-21: Dhambi ikaayo ndani yangu	100
6.9.4 Mistari ya 22-23: Sheria mbili na matokeo yake	101
6.9.5 Mstari wa 24: Kukata tamaa	101
6.9.6 Mstari wa 25: Somo la Warumi 7	102
7. Warumi 8:1-11: Huru hatimaye!	105
7.1 Tayari sasa – bado	106
7.2 Kupenya kizuizi	107
7.3 Mstari wa 1: Kuachiliwa huru – hakuna tena hukumu ya adhabu	108

7.4 Mstari wa 2: Tumewekwa huru kwa sheria ya Roho wa uzima	110
7.5 Mstari wa 3: Mungu anatatua tatizo la dhambi pale Golgotha	110
7.5.1 Mungu anakuwa mwanadamu	111
7.5.2 Golgotha	112
7.6 Mstari wa 4: Sheria ya Mungu inatimizwa sasa hata hivyo	113
7.6.1 Sheria ya Musa na uhalali wake	114
7.7 Mstari wa 5: Kufuata tabia ya mwili au kufuata Roho	116
7.8 Mstari ya 6-7: Mauti na uzima, uadui na amani	116
7.9 Mstari ya 8-9: Kuwa katika tabia ya mwili na kuwa katika Roho	117
7.10 Mstari ya 10-11: Roho wa Mungu na wokovu wa mwili wetu	118
7.10.1 Nafasi yetu ya wokovu – ukweli wa wokovu – “tayari sasa”	118
7.10.2 Kuishi na kufa	119
7.10.3 Roho wa Mungu na mwili	120
7.10.4 Kwa nini bado hatujawa wasioweza kufa sasa?	120
8. Warumi 8:12-17: Agizo la wokovu – maisha ya ushindi	122
8.1 Mstari wa 12: Si wadeni wa tabia ya mwili tena	122
8.2 Mstari wa 13: Uzima au mauti	123
8.2.1 Ahadi na maonyo, na wokovu wa milele	123
8.2.2 Kuyafisha matendo ya mwili kwa Roho	127
8.2.3 “Kujihesabu kuwa wafu” au “kufisha”?	128
8.2.4 Kufisha – kunafanyikaje?	129
8.3 Mstari wa 14: Wana wa Mungu wanaoongozwa na Roho	131
8.4 Mstari wa 15: Roho wa kufanywa wana analia ndani yetu: “Baba mpendwa!” ...	133
8.5 Mstari wa 16: Sisi ni watoto wa Mungu!	134
8.6 Mstari wa 17: Sisi ni warithi wa utukufu wa Kristo	134
9. Warumi 12: Fikiria zinafanywa upya!	136
9.1 Lengo la Mungu kwetu	137
9.2 Warumi 12:1-2: Ibada – jambo lenye mantiki!	137
9.2.1 Miili yenu!	138
9.2.2 Ulimwengu: rafiki au adui?	139
9.2.3 Kubadilishwa kwa njia ya fikira mpya	141
9.2.4 Metamofosisi	142
9.2.5 Kwa nini kufanywa upya?	143

9.2.6 Kufanywa upya kunatokea?	143
9.2.7 Uwanja wa vita wa mawazo	144
9.2.8 Tunawezaje kushinda vita hivi?	145
9.2.9 Ndoto za mchana na matamaniao	146
9.2.10 Mapenzi ya Mungu – yamejaribiwa na kuonekana kuwa mema!	147
9.3 Warumi 13:13-14: Kumvaa Kristo – bila kuiandalia tabia ya mwili nafasi	148
9.4 Hitimisho	149
10. Ya kale na mapya – mapitio ya jumla	151
11. Tabia ya mwili ni nini?	153
11.1 Dhambi na tabia ya mwili	154
11.2 Tabia ya mwili na mtu asiyeamini	155
11.3 Tabia ya mwili na Mkristo	156
12. Tabia ya mwili dhidi ya Roho	159
12.1 Tatizo lilikuwa nini?	159
12.2 Utendaji wa tabia ya mwili	160
12.3 Mkristo katika Waraka kwa Wagalatia	161
12.4 Sheria na tabia ya mwili – magurudumu mawili ya meno katika mashine moja	162
12.5 Mgogoro wa kale wa ulimwengu mzima na mgogoro wa sasa wa kibinafsi	163
12.6 Ishini na enendeni kwa Roho!	163
12.7 Kazi ya Mungu na kazi yetu – je, zinapingana?	165
12.8 Mmeitwa mpate uhuru – lakini ni uhuru wa namna gani?	165
12.9 Roho anapigana kwa ajili yetu	166
12.10 Katikati ya vita	166
12.11 Virusi na chanjo	168
12.12 Matendo ya tabia ya mwili ni nini?	168
12.13 Tunda la Roho wa Mungu	170
12.14 Tabia ya mwili ni ya kusulubiwa msalabani	171
12.15 Mtu ni nani baada ya kusulubiwa pamoja na Kristo?	172
12.16 Kujitwika msalaba kila siku	174
12.17 Kuishi na kuenenda kwa Roho: kuwa na kutokuwa	175
12.18 Kuenenda kwa Roho – kunawezekanaje?	176
12.19 Kujikwaa na kuinuka	177

12.21 Msaidizi wetu mbinguni	178
12.22 Itakuwaje tukiwa tumetenda dhambi?	179
12.23 Kuungama	181
12.24 Mkristo wa kiroho na Mkristo wa tabia ya mwili – je, wapo kweli?	182
12.25 Kiini cha mgogoro kati ya Roho na tabia ya mwili	183
13. Utu mpya na utu wa zamani: Ya kale yamepita, yamekuwa mapya	185
13.1 Utu mpya katika Waraka kwa Waefeso	186
13.2 Utu mpya katika Waraka kwa Wakolosai	187
13.3 Utu wa zamani katika Waraka kwa Waefeso na kwa Wakolosai	187
13.4 Historia ya kuumbwa kwa utu mpya	189
13.5 Wengi ni mtu mmoja mpya	190
13.6 Kila mtu binafsi anakuwa utu mpya	191
13.7 Utu mpya ni nini?	193
13.8 Kiumbe kipya	194
13.9 Ni nini kiliumbwa upya?	195
13.10 Je, utu mpya unahitaji kufanywa upya?	196
13.11 Utu mpya: tumeuvaa kama vazi	198
13.12 Muhtasari – picha moja	199
13.12.1 Mti wa zamani	200
13.12.2 Mti mpya	200
13.12.3 Mzizi wa zamani ambao bado uko hai	202
13.13 Kwa imani peke yake	203
13.13.1 Mtunza bustani mvivu	203
13.14 Wakati ujao wa utu mpya	204
13.14.1 Kuishi maisha ya wakati ujao tayari sasa	205
13.15 Wito	206
14. Kuzaliwa mara ya pili kwa uzima mpya	207
14.1 Asili ni nini hasa?	208
14.2 Washirika wa asili ya Mungu	209
14.3 Uzima wa milele ni uzima wa Kristo	210
14.4 Tunakuwaje washirika wa uzima wa Mungu?	210
14.5 Kuzaliwa mara ya pili – kuzaliwa na Mungu	211
14.5.1 Kuzaliwa kwa maji	211

14.5.2 Kuzaliwa kwa Roho	213
14.5.3 Unabii wa Ezekieli: mioyo mipya na roho mpya	213
14.6 Tumeokolewa kutoka mautini hadi uzimani: tumehuishwa	214
14.7 Siri ya kutokea na kukua	215
14.8 Ukuaji – uzima unakua	216
14.9 Kutunza	218
14.10 Burudani au wajibu?	219
14.11 Ukweli wa wokovu katika maandiko ya Yohana	220
14.12 Agizo la wokovu katika maandiko ya Yohana	221
14.13 Uzima wa milele – ubora na urefu	222
14.14 Dalili za uzima	222
14.15 Aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi	223
14.15.1 Hatua nne za historia ya wokovu: mwanadamu na dhambi	226
14.15.2 Kutotenda dhambi tena: inawezekana au haiwezekani?	226
14.16 Ukamilifu – ni nini?	228
14.16.1 Ukamilifu wa nafasi yetu ya wokovu	228
14.16.2 Ukamilifu (ukomavu) katika maisha yetu: kukua kuwa watu wazima	228
14.16.3 Ukamilifu wa mtu kwa ujumla wake katika ukamilisho ujao	229
14.17 Wajibu kwa ajili ya matendo yetu, si kwa ajili ya hali yetu ya kuwa	229
14.18 Asili mpya na asili ya zamani ziko ndani yetu wakati mmoja	230
14.19 Hitimisho	231
15. Hulka na tabia	232
15.1 Biblia na nadharia ya hulka	232
15.2 Tabia na kubadilika kwake	235
16. Neno la mwisho	237
17. Bibliografia	

Kwa watoto wetu, Felix, Laura, Alex, Peter na Annemarie – kwa shauku ya moyo kwamba mamshike Kristo na mashikwe naye.

Dibaji

Mada ya kitabu hiki imenishughulisha tangu ujana wangu. Ndiyo kiini cha kuwa Mkristo. Maisha yaliyowekwa huru yanawezekana tu kutokana na wokovu uliopokelewa kikamilifu na kueleweka. Ukomavu wa Mkristo unasimama au kuanguka pamoja na kile tulichoelewa kuhusu msalaba.

Kuwekwa huru mbali na dhambi si nadharia, bali ni uhalisi wa maisha ya kila siku. Karibu miaka 30 iliyopita kitabu “Das normale Christenleben” (Maisha ya Kawaida ya Mkristo) cha Watchman Nee kilinisaidia kupenya kizuizi. Ingawa nilikuwa muumini, nilikuwa nimevunjika moyo, kwa sababu sikuwa na chochote cha kupinga nguvu ya dhambi. Kitabu hiki kilinifungua macho, kama kilivyowafungua wengine wengi, nikauona uhuru ambao nilikuwa nao tangu zamani katika Kristo, lakini bado sikuwa nimeujua kwa kweli. Haihusu ngazi ya juu zaidi ya utauwa wala kuwa Mkristo wa kiwango cha mtaalamu. Inahusu kuelewa jinsi Mungu anavyotuona, na kile ambacho ametuwekea mikononi mwetu.

Mada hii ni kama chuma cha moto, hasa kwa yule anayeandika juu yake. Je, ninaweza kufanya hivyo kwa sababu nimefika asilimia 100? Kamwe. Ninajua wazi kwamba si wengi wetu wanaopaswa kuwa walimu, kwa kuwa watapata hukumu iliyo kubwa zaidi, maana sisi sote hujikwaa mara nyingi. Lakini bila mafundisho ya Biblia na kurudiwa kwake mara kwa mara hatuna nafasi yoyote ya kuwatia wengine moyo, wala ya kulishughulikia jambo hili ipasavyo sisi wenyewe. Kila kizazi kinapaswa pia kukabiliana na mada hizi chenyewe. Kitabu hiki hakitakuwa na jambo jipya, au karibu hakitakuwa na jambo jipya, ambalo wengine hawajaliandika tayari. Lakini kinakusudia kuwatia moyo mlihuishe somo hili kuu na kulizungumzia.

Nimepokea msaada kwa furaha. Zaidi ya yote ninamshukuru Thomas Jettell kwa kusahihisha na kwa mawazo ya kuchochea fikira, ambayo yamefanya mambo kadhaa yaeleweke zaidi. Ninawashukuru Josua na Brigitte Keller, wamisionari karibu na Nice, kwa mazungumzo yenye kujenga. Ninawashukuru pia Herbert Briem, Peter Streitenberger na Harry Graf kwa kulipitia kwa jicho la uchunguzi. Kuwatata ndugu hawa hakumaanishi kwamba tunakubaliana katika kila swali; kwa hiyo mimi mwenyewe ninawajibika kwa yaliyomo.

Isipokuwa mara chache, nimetumia Biblia ya Elberfelder ya mwaka 2003 (tafsiri ya Biblia ya Kijerumani; Edition CSV Hückeswagen). Mahali pasipotumika, kwa kawaida nimeonyesha.

Hans-Jörg Ronsdorf, Sulzberg, Novemba 2010

Yeye pekee yake ndiye mwamba wangu na wokovu wangu, ngome yangu iliyo juu.

Zaburi 62:6

Ndipo mtaishi salama, na mtakuwa na wingi wa wokovu, wa hekima na wa maarifa.

Isaya 33:6 (NeÜ, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani)

1. Safari ya ndege ya kuzunguka

Pandeni ndani na mfunge mikanda! Tutaifanya safari nzuri ya ndege ya kuzunguka. Lengo letu ni safu kubwa ya milima. Tunataka kutazama kundi la milima linalovutia sana kutoka juu, kama ndege aonavyo. Ninaishi pembeni kabisa mwa milima ya Alpi, na kutoka ofisini kwangu ninaweza kuitazama milima. Zaidi ya mara moja nimetamani kuruka angani na kuutazama uumbaji huu wa ajabu kwa muda mrefu kutoka juu. Hadi sasa nimefanya safari fupi moja tu ya kuzunguka, lakini imenitia hamu ya zaidi.

Leo ningependa kuwakaribisha katika safari kama hiyo. Ni safari isiyogharimu chochote. Inafanyika katika mawazo yetu. Mnaonaje: Ni milima ipi tunayoizungumzia? Fikirieni kwamba safu hii ya milima ni wokovu mkuu, yaani ukombozi mkuu wa Mungu wa milele na mwenyezi. Fikirieni kwamba mlima huu unawakilisha kile ambacho Mungu amekitenda ndani ya Yesu Kristo kwa njia ya kifo chake msalabani, kwa njia ya ufufuo wake na kwa njia ya kupaa kwake mbinguni. Si jambo dogo tu; ni *wingi wa wokovu*! Katika safari moja hamwezi kuona kila kitu kwa mara moja, lakini angalau mnaweza kuona mengi tayari. Na katika kila safari nyingine mngeweza tena kuona jambo jipya.

Ninawaahidi kwamba safari hii haitachosha, na si kwa sababu ndege ni ndogo na ina viti viwili tu. Ndege nyepesi kama hii inaweza kutikiswa sana, lakini kile tutakachoona kitakuwa kikubwa mno hata tutasahau mengine yote.

Rubani wetu anaijua njia kuliko mtu yeyote. Anazijua njia bora zaidi, malengo bora zaidi, mandhari nzuri zaidi, vimo sahihi vya juu na vya chini; anaijua hali ya hewa, na anaweza kuturudisha nyumbani salama. Kwa hiyo tunaweza kuiacha hofu ya kuruka chini ardhini bila wasiwasi.

Mlima tunaotaka kuufikia ni Elbrus, mlima mrefu kuliko yote katika milima ya Kaukasus, wenye urefu wa mita 5,642. Huo ni urefu mkubwa, na ndege inapaswa kujitahidi kweli ili kufika kimo hicho.

Mlima huu una jambo gani la pekee? Bila shaka unajulikana kwa kuwa mrefu kuliko yote katika Kaukasus, lakini pia ni volkano iliyozimika. Una kasoko kubwa ambayo zamani sana lava yenye moto mkali ilirushwa kutoka ndani yake. Kama tunavyojua hata leo, volkano ni nguvu za asili kubwa mno zisizoweza kudhibitiwa. Nguvu kama hizo za asili zililipuka pia wakati Mungu alipoufunika

ulimwengu kwa gharika katika siku za Nuhu. Biblia inasema kwamba chemchemi za vilindi na madirisha ya mbinguni yalifunguka (Mwanzo 7:11), ili kuzieneza duniani kote kiasi cha maji kisichoweza kufikirika. Huenda mabadiliko makubwa ya kijiolojia yaliyoambatana na gharika hii ya dunia nzima yalisababisha volkano kuanza kulipuka. Kwa vyovyote vile, maji yalipanda wakati huo hata juu ya vilele vya milima: Milima yote ilifunikwa (Mwanzo 7:20), na kilichoonekana ni maji tu.

Watu wa wakati huo walikuwa waovu sana. Walikuwa wamevuka *mpaka ambao baada yake hakuna kurudi tena*, na walikuwa wamejitenga mbali na Mungu, yaani mbali na kile alichokuwa amekikusudia kwa ajili ya uumbaji. Walifika mbali kiasi kwamba Mungu aliweka mstari wa mwisho. Sijui kina kizima cha uovu huo kilikuwa nini, lakini Mungu aliuona (Mwanzo 6:5). Na Yesu anasema kwamba siku kama hizo hasa zitarudi tena (Luka 17:26). Gharika ilipaswa kuwaua watu wote isipokuwa Nuhu na familia yake. Katika hukumu hii tunaweza kuona vizuri dhambi ina maana gani kwa Mungu. Mara nyingi sisi hatuna tatizo na dhambi, ingawa tunakabiliwa daima na matokeo yake mabaya na ya kutisha. Lakini Mungu anaifikirijae? Mungu anaichukia dhambi kwa sababu inawaharibu wanadamu, viumbe vyake, kama ugonjwa unaoua usioweza kuponywa, na kuwatenga naye. Dhambi inambadilisha mwanadamu kiasi kwamba anakuwa adui wa Mungu. Mungu anaichukia dhambi kwa sababu anatupenda. Anaichukia kabisa dhambi kwa sababu inapingana na asili yake yote, na upendo wake na utakatifu wake. BWANA anawaambia watu wa taifa la Israeli kwamba analia machozi kwa siri kwa sababu ya hali yao ya dhambi (Yeremia 13:17; 14:17). Dhambi inamgusa *yeye* moyoni; haimwachi bila kujali. *Yeye* anaijua kila dhambi na kuihisi hadi ndani ya moyo wake. Dhambi inawatenga wanadamu na Mungu, na wanadamu wao kwa wao. Ndiyo inayomshambulia Mungu na kuzidharau amri zake. Inaukata mshipa wa uzima unaotoka kwa Mungu kwenda kwa mwanadamu, kwa hiyo haiwezi kuleta kitu kingine isipokuwa mauti. Dhambi inaweza kuwa na uso wa kirafiki, lakini huo ni kinyago tu: Ni mbaya, na inaharibu kila mahali inapojitokeza. Imeenea kila mahali. Popote walipo wanadamu, inapatikana. Wote wameathiriwa. Inawang'ang'ania wote kama kupe, iwe wanakubali au hawakubali. Kama mbegu, imo ndani ya kila mtu tangu kuzaliwa, ingawa kwa mmoja imekua zaidi na kwa mwingine kidogo.

Mungu anaichukia dhambi, lakini anampenda mwenye dhambi! Huo ndio wokovu wetu! Lakini dhambi na mwanadamu wameshikamana na kukua

pamoja; wanaunda kitu kimoja ambacho hakiwezi kutenganishwa kwa njia yoyote inayowezekana kwa mwanadamu. Kama Mungu angeiangamiza dhambi, hukumu yake ya kuangamiza hatimaye ingetupata sisi! Amapata njia na amelitua tatizo! Si wanadamu walioshughulikia tatizo hili, kwa sababu wanaukana *ugonjwa wao wa dhambi*. Kwao dhambi haijumuishi kile ilicho kwa Mungu.

Yule wa Milele alipoumba ulimwengu, maneno yake ya kiuweza yalitoshia: “Na iwe!” Lakini ili kulitua tatizo la dhambi, maneno hayakutosha. Badala yake, jambo hili lilimgharimu upendo wake wote. Mungu habadiliki; yeye ni kama nuru safi, yeye ni upendo, yeye ni mtakatifu na mwenye haki, yeye ni safi na hana dhambi hata kidogo. Tunapozungumzia dhambi, tunapaswa kuzikumbuka sifa hizi za Mungu, tena kwa kipimo cha kiungu! Hatuzungumzii mawazo yetu yenye kuvumilia kila kitu na yanayojirekebisha kwa urahisi. Pale Golgotha, mahali ambapo Yesu aliuawa, mnaeweza kuona jinsi Mungu anavyoichukulia dhambi kwa uzito usioweza kufikirika. Hakuna mahali pengine panapoonyesha kwa wazi zaidi kwamba Mungu anampenda mwenye dhambi, lakini anaichukia dhambi bila kikomo. Mungu anamtoa Mwanawe mwenyewe kuwa dhabihu badala yetu sisi wanadamu. Kwa nini ilikuwa lazima dhabihu ya damu? Kwa sababu dhambi si kosa dogo tu la kupuuzwa, bali ni jambo linalomkwaza Muumba wetu na kumtukana. Kwa hiyo anadai kwa haki upatanisho kwa ajili ya dhambi na kulipwa kwa hasara tuliyo mtendea Mungu. Daima itabaki hivi: Mungu atamwadhibu mwenye dhambi kwa ajili ya dhambi yake. Watu wengi wanadhani kwamba adhabu kufuata uovu ni uvumbuzi wa kidini tu. Si hivyo hata kidogo! Ukweli huu ni, kwa mfano, msingi wa mfumo wetu wa sheria. Kwa Mungu tunapaswa tu kulifikiria jambo hili kwa namna iliyo safi zaidi na yenye haki zaidi. Yeye anajua yote na anayasoma mawazo yote. Yeye yuko kila mahali, na kwa hiyo yeye mwenyewe ni shahidi wa yote ambayo wanadamu wanawaza, wanasema na wanatenda. Hakuna kinachompita. Kama mngekuwa peke yenu duniani na mmetenda dhambi moja tu, hata hapo dhabihu ya Yesu ingehitajika. Hata dhambi moja tu haikubaliki kwa Mungu. Yeye ni mtakatifu mno na mtukufu mno kiasi kwamba hawezi kuipuuza hata dhambi moja tu.

Mungu hawachukuli wanadamu kama jaribio la uumbaji lililoshindwa. Hamwachi mwanadamu. Anataka kumhurumia mwenye dhambi na kumwokoa. Lakini kwa ajili hiyo anahitaji mtu ambaye *anaweza* kulipa deni. Je, yupo

mwanadamu anayeweza kulipa hesabu hiyo? Ndiyo! Huyu mmoja anakuwa dhabihu inayosimama badala yetu. Inalipa deni letu. Yesu, “Mwana-Kondoo wa Mungu”, anakuwa mbadala wetu. Mwanadamu mmoja anakuwa – kwa maana ya mfano – mwana-kondoo huyu wa dhabihu anayesimama badala yetu. Pale Golgotha Mwana wa Mungu, kwa hiari yake, alisimama pamoja na dhambi yetu karibu kabisa na Mungu, ili aipokee hukumu yetu na adhabu yetu. Mungu anaokubali utayari wa Mwanawe kujitoa dhabihu, wala hamwachilii katika hukumu hii ya adhabu. Je, sisi tungemtoa mwana wetu ili kuwakomboa adui zetu kutoka katika tatizo walilojiletea wenyewe? Je, badala ya kumwadhibu mwana wetu au binti yetu, hatungefanya kila kitu ili kuwahurumia? Mungu hakufanya hivyo. Ndiyo, ili kutukomboa ilipaswa kutokea mengi zaidi kuliko amri tu au neno la uumbaji.

Turudi kwa Nuhu: Maji ya hukumu wakati huo yalifunika vilele vya milima mirefu zaidi. Mungu aliichukulia dhambi kwa uzito, kwa uzito mkubwa sana! – Na zaidi sana pale Golgotha: Je, tunaelewa kidogo kuhusu hukumu iliyotekelezwa *pale*, kuhusu mzigo ambao Yesu aliubeba? Huenda sasa mnafikiria jinsi walivyomtendea vibaya, wakamkandamiza taji la miiba kichwani na kumpigilia misumari msalabani. Lakini hebu tungoje kidogo. *Hayo* hayakuwa mateso ambayo kwayo alizilipia dhambi zetu. Wanadamu ndio waliomtendea hayo. Hao hawakuchangia chochote katika wokovu. Walichokifanya kilithibitisha kwa mara nyingine jinsi wanadamu walivyopotoka. Hukumu ya Mungu na utekelezaji wa adhabu iliyostahili juu ya dhambi vilianza siku ile ya Ijumaa Kuu katika saa ya sita tu, yapata saa sita mchana. Hapo, jua lilipokuwa juu kabisa, giza nene likaingia. Wakati wa kulipa hesabu ya deni letu ulikuwa umefika. Hukumu ya ghadhabu ya Mungu iliangukia kwa nguvu zake zote juu ya Mwana-Kondoo wa dhabihu asiye na hatia. Kwa saa tatu Bwana wetu Yesu alijitoa chini ya ghadhabu ya Mungu juu ya dhambi (pia juu ya dhambi yangu), akajitwika kile kinachowapeleka wanadamu wote motoni milele. Hilo ndilo giza kwa maana halisi na ya ndani kabisa ya neno hilo. Hakuna aliyeshuhudia kile kilichotokea kati ya Baba na Mwana ili kulitatua tatizo la dhambi kwa nyakati zote.

Tunatazama chini kupitia dirisha la ndege, kwenye mlima huu ambao zamani ulikuwa volkano iliyotoa moto. Lava inayowaka kwa wekundu inanikumbusha lile ziwa linalowaka kwa kiberiti na moto, jehanamu ya milele. Ndiyo, Mwokozi wetu alivumilia mwenyewe badala yetu yote ambayo Mungu anayahisi mbele ya dhambi, yakiwa yamebanwa ndani ya saa tatu! Corrie ten Boom alitumia mfano

huu: Moto unapowaka msituni, daima kuna mahali ambapo moto hauwezi kupata tena kitu cha kuunguza – mahali ambapo moto umeshapita. Sasa Golgotha ndipo mahali ambapo mwenye dhambi anapata usalama, kwa sababu moto wa hukumu ya Mungu juu ya dhambi umeshapita hapo.

Mtunga zaburi, anayesema kinabii kuhusu hukumu hii ya Mungu pale Golgotha, anaonekana kuifikiria gharika: “Mawimbi yako yote na gharika zako¹ zimepita juu yangu” (Zaburi 42:7; taz. 88:7). Ngurumo za nguvu za asili katika siku za Nuhu (maji mengi, dhoruba, matetemeko ya ardhi, volkano na kadhalika) ni mfano dhaifu tu wa kile ambacho Bwana Yesu Kristo alikivumilia msalabani, na zaidi sana katika zile saa tatu za giza – alisulubiwa katika udhaifu, katika mwili ulioteswa vibaya na katika maumivu makali. Ilikuwa ni kuachwa na Mungu kabisa! Mungu alimhukumu Mwanawe. Mwana wa Mungu kati ya mbingu na nchi – amekataliwa na wanadamu na kukataliwa na mbingu! Alikwenda kwa ajili yetu katika giza la nje kabisa. Ni dhabihu kubwa kama nini! Chukueni muda kutafakari aliyowatendea ninyi. Niaminini: Kama mnataka kupata badiliko lolote maishani mwenu, linaanza kwa kuruhusu upendo wa Yesu uwaguse ndani kabisa. Upendo huo ni mkubwa kiasi kwamba unapita ufahamu wetu. Hivyo ndivyo Paulo pia anavyosema (Waefeso 3:19). Anazungumzia upana, urefu, kimo na kina cha upendo huu. Askari wa Kifaransa waligundua huko Hispania gereza la chini ya ardhi lililoachwa tangu zama za Baraza la Uchunguzi wa Kidini (Inkwizisheni). Walikuta mifupa ya mtu ambayo bado ilikuwa imefungwa kwa minyororo kwenye ukuta wa gereza. Ukutani palikuwa pamechorwa msalaba. Na kwenye ncha nne za msalaba yalikuwa yamechorwa maneno ya Waefeso 3: juu *kimo*, chini *kina*, kushoto *upana* na kulia *urefu*. Mfiadini aliyechora mchoro huu alikuwa amejaa upendo wa Yesu, hasa katika siku ngumu zaidi mwishoni mwa maisha yake yaliyojaa mateso. Alikuwa ameielewa maana ya msalaba – upendo wa Kristo unaopita ufahamu wote! Na mfiadini huyo wa Baraza la Uchunguzi wa Kidini alikuwa tayari, kwa ajili ya upendo huu, kuifuata njia hiyo na hivyo kumwiga Bwana wake.

Hadi sasa tumezungumzia hatia, dhambi na msamaha. Mtu anahukumiwa kwa ajili ya kile anachokitenda. Lakini vipi kuhusu tatizo la asili yetu mbaya? Je, tunaweza kweli kupewa msamaha, ingawa ukweli ni kwamba sisi *ni* wenye dhambi?

1. Mawimbi haya na gharika hizi ni mfano wa ghadhabu ya Mungu.

Kwa nini tukio la msalaba lilikuwa la kutisha kiasi hicho kisichopimika? Kwa sababu Bwana Yesu hakufa tu kwa ajili ya yale niliyoyatenda, bali pia kwa ajili ya kile nilicho. Hebu fikirieni kwamba mnachukua jukumu la hatia kubwa ya mtu fulani. Hilo lingestahili kupongezwa. Sasa fikirieni zaidi ya hapo kwamba watu hawangewachanganya tu na mtu huyu mwovu, bali wangewafanya kuwa sawa naye kwa makusudi! Huo ni mlinganisho dhaifu tu wa kile kilichohusika pale Golgotha. Biblia inaeleza asili yetu yote kuwa ya dhambi. Dhambi inakaa ndani yetu; imo katika kila kitu tunachokitenda. Haijalishi kama watu ni wenye dhambi “wakubwa” au “wadogo”; hilo halibadilishi jambo. Mniamini au msiniamini: Jambo hili mtu analiona hasa ndani yake mwenyewe anapokuwa ameamini kwa muda mrefu. Si kwamba hapo mtu anapaswa bado kuishi na dhambi isiyosamehewa. Lakini anajua zaidi na zaidi dhambi ikaayo ndani yetu. Kadiri mtu anavyoishi kwa muda mrefu katika imani, ndivyo anavyotambua zaidi jinsi dhambi ilivyo ya hila na ya kuchukiza. Na pia haileti tofauti yoyote kama mlikuwa mnaishi katikati ya ulimwengu au katika familia ya Kikristo mlipokuja kuamini.

Bwana Yesu Kristo alipokufa, alilitatua pia tatizo la dhambi iliyo *ndani* yetu. Tunapaswa kuelewa vizuri kwamba kwa sababu hiyo alifanywa kuwa dhambi. Mungu alimhukumu kana kwamba yeye ndiye aliyesababisha dhambi – si matendo tu, bali pia dhambi iliyoshikamana nasi. Si matunda tu yaliyokuwa mabaya; mti mzima ulikuwa umeoza na haufai kitu. Hivyo ndivyo Bwana Yesu Kristo alivyosimama hukumuni kwa ajili yetu. Baada ya zile saa tatu za giza alilia: “Imekwisha!” Hayo ndiyo maneno muhimu kuliko yote ambayo ulimwengu umewahi kuyasikia! Ili aipokee hukumu kikamilifu kabisa, Bwana Yesu anakufa. Mshahara wa dhambi, wa dhambi yetu, ni mauti – mauti yake yeye!

Fikirieni kwamba Mungu anawahesabia na kuwawekea katika akaunti yenu mauti haya ya Yesu kikamilifu kabisa. Au kwa maneno ya Biblia: Utu wetu wa zamani umesulubiwa pamoja naye! Maisha yetu ya zamani (yote tuliyoatenda na yote tuliyo) yalitolewa mautini pamoja naye msalabani miaka 2,000 iliyopita. Alikufa kwa ajili ya hayo. Kwa ajili ya yote! Hakuna tena chochote ambacho tunapaswa kukilipia. Hukumu ya adhabu ya Mungu haitatupata tena! Tazameni nje kupitia dirisha la ndege na mwangalie mlima huu mkubwa kwa makini! Volkano imezimika. Vivyo hivyo moto wa hukumu ya Mungu iteketezayo umezimika, kwa sababu Yesu alipokea juu yake. Mnaona nini sasa? Mlima mweupe! Kila kitu kimejaa theluji. Kama volkano ingekuwa bado hai, kileleni

pasingeweza kuwa na theluji. Lakini kile ambacho theluji inataka kutuambia ni wazi. Ni vitu vichache tu vinavyosema kwa wazi hivi kuhusu usafi na kutokuwa na lawama, ambavyo sasa ndani ya Kristo vimekuwa uhalisi kwetu.

Unitakase dhambi kwa hisopo², nami nitakuwa safi; unioshe, nami nitakuwa mwenpe kuliko theluji.

Zaburi 51:7

Njoni basi, tusemezane, asema BWANA. Dhambi zenu zijiapokuwa kama bendera, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijiapokuwa nyekundu kama damu, zitakuwa kama safu.

Isaya 1:18

Mungu ametuosha tukawa safi. Tungeweza kutaja hapa mambo mengi zaidi ambayo kazi kubwa mno ya Yesu imeyaleta. Hapa tutaje tu neno hili moja la Biblia:

Lakini kwa yeye ninyi mmekuwa ndani ya Kristo Yesu, ambaye kwetu sisi amefanywa kuwa hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi.

1 Wakorintho 1:30

Yote ambayo hatukuwa nayo katika maisha yetu ya zamani, sasa tunayo kwa njia ya Kristo, kwa sababu Mungu ametuhamishia ndani yake. Jambo hili linasikika la ajabu, lakini halimaanishi kitu kingine isipokuwa kwamba Mungu ametuunganisha na Kristo na kutufanya kitu kimoja naye kiasi kwamba yote ambayo Kristo ametenda na yote aliyo sasa kama Mwana wa Adamu aliyeinuliwa mbinguni yanatuhusu sisi. Mungu anatuona ndani ya kile alichokitenda Mwanawe na kile alichosasa! Hiki kweli ni kilele cha neema na cha wokovu, siyoyote? Utulivu na ukimya juu ya mlima huu, uliofunikwa kwa vazi jeupe kama theluji, vinatuonyesha kwamba sasa tuna amani na Mungu, na kwamba ndani ya Kristo tumeshahamishiwa mbinguni. Ndiyo, tuko ndani ya Kristo! Kwa hiyo hakuna tena hukumu yoyote ya adhabu dhidi yetu – wala kwa ajili ya yale tuliyoyatenda, wala kwa ajili ya kile tulicho tangu kuzaliwa. Mungu hakutaka kutuboresha; ameanzisha mwanzo mpya. Lakini ili kuanza upya, ya zamani yanapaswa kwanza kuondolewa njiani. Na kwa kuwa hapa si kitu bali ni wanadamu, swali linazuka: Jambo hili linawezaje kutokea? Kama tulivyokwisha kusema: Maisha yetu yangeweza kukomeshwa kwa njia ya kifo tu. Kristo alikufa

2. Hisopo ni mmea wenye majani uliotumika kunyunyizia maji na damu.

kwa ajili yetu (nasi tukafa pamoja naye). Hatukufa kihalisi, bali tulihesabiwa kifo cha mwingine. Kwa msingi wa haki yake mwenyewe, na kwa kukubaliana kabisa na madai yake ya haki juu yetu, Mungu ametuhamishia kabisa (kwa mtazamo wa kisheria tu) kifo cha Mwanawe kilichotokea badala yetu. Jambo hili linahesabika kana kwamba tumekufa kweli. Pale msalabani asili yetu ya zamani ilihukumiwa kifo, na hukumu hiyo ikatekelezwa juu ya Kristo.

Mlima huu mkubwa unatuonyesha ukuu wa haki ya Mungu, na wakati huo huo jinsi tulivyo wadogo: Ametenda yote ili kutuweka huru mbali na dhambi yetu, bila kuacha hata chembe moja ya haki yake:

Haki yako ni kama milima ya Mungu, bukumu zako ni vilindi vikuu.

Zaburi 36:6

Wakati mwingine tunaweza tena kuingiwa na hofu kidogo kama kweli haya yote yanatuhusu sisi binafsi kabisa. Je, labda tunajichukulia mengi mno? Ndege inaweza mara kwa mara kurushwa huku na huku, na mtu anaweza kushtuka. Lakini hata kama dhoruba ya hisia inatutikisa, mlima huu unabaki uleule. Hakuna dhoruba inayoweza kuuhamisha mlima huu wa wokovu. Mlima huu wa wokovu ni mlima wa neema, nao unafanana na mlima Sayuni:

Mlima wake mtakatifu umeinuka kwa uzuri, furaha ya dunia yote; mlima Sayuni, upande wa kaskazini kabisa, mji wa Mfalme mkuu.

Zaburi 48:1-2 (ER, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani; taz. Waebrania 12:18-20)

Tunapozungumzia milima, ninakumbuka jambo jingine, ambalo ni kama mlima kwa maana hasi. Grand Canyon ni korongo kubwa mno, bonde kubwa mno. Inavutia sana kweli kusimama mbele ya shimo hili na kutazama chini kwenye kina. Hiyo pia ni picha yetu: Hatukuwa kitu. Sisi ni mavumbi, na tutarudi mavumbini, kwa sababu dhambi imeingia katika maisha yetu. Mioyo yetu inafanana na shimo la uovu. Lakini sasa tunatazama juu kwenye ule “mlima wa wokovu”, ambapo palisimama msalaba. Msalaba ni mwisho, lakini pia ni mwanzo:

Kwa hiyo, mtu akiwa ndani ya Kristo, yeye ni kiumbe kipya; ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya.

2 Wakorintho 5:17

Rubani anapunguza kimo polepole, hivi kwamba sasa tunaweza kuona sehemu za chini zaidi za kundi hili kubwa la milima. Kwa sababu ya ukubwa wa milima

hii, hamwezi kamwe kuona kila kitu kwa mara moja. Tunaposhuka chini, rubani anaielekeza ndege karibu zaidi na mlima. Tunaona maporomoko makubwa ya maji, na kisha maporomoko mengine madogo zaidi. Ni tamasha kubwa kama nini mbele yetu! Jinsi maji mengi yanavyoporomoka bondeni kwa utukufu! Chini zaidi maporomoko haya yanaungana na kuwa mto. Theluji na barafu nyingi zinahifadhi mamilioni ya mita za ujazo za maji. Katika miteremko ya mlima Elbrus kuna barafuto zaidi ya 70 ambazo maji hutiririka kutoka kwake. Yanatiririka chini bondeni na kunywesha malisho, mashamba na misitu. Kilimo chote kinayategemea. Bila maji haya pasingekuwa na ukuaji mwingi katika maeneo hayo. Bila shaka mvua pia hunyesha huko, lakini hasa wakati theluji inapoyeyuka, maji yanayohitajika kwa ukuaji wa mimea wakati wa majira ya kuchipua hutiririka kwa wingi kuelekea bondeni.

Mikondo mikubwa ya maji inayoporomoka kutoka mlimani na kisha kukusanyika katika mito ni mfano wa Roho Mtakatifu. Bwana Yesu mwenyewe alitumia mfano huu. Alikuwa akiifikiria kiu kubwa ya mwanadamu – swali na utafutaji wa maana ya maisha, usalama na upendo – aliposema kwamba kila mwenye kiu aje kwake anywe. Anayekuja *kwake* anaizima kiu ya maisha yake, tena milele! Moyo wenye kiu unaweza kupata pumziko kwake.

Bwana Yesu anazungumzia maji yaliyo hai (yaani maji yanayotiririka), chemchemi ambayo ni yeye mwenyewe. Tunaruhusiwa kulichukulia Neno la Mungu kwa uzito; ni hakika: Roho wa Mungu wa milele, mtakatifu na mwenye nguvu tumepewa kwa wingi. Anaishi ndani yetu. Yeye ni chemchemi ya uzima, ya nguvu, ya uongozi na ya faraja, inayodumu na isiyokauka kamwe. Mungu mwenyewe tu ndiye anayeweza kuwa ndani yetu chemchemi inayobubujika daima.

Ninakumbuka pia mlima mwingine, ambapo Yesu alikuwa pamoja na wanafunzi wake watatu. Walikuwa wamepanda juu sana, labda hadi mpaka wa theluji wa mlima huo.³ Ghafila Yesu aligeuka sura mbele ya macho yao, akang'aa kama jua. Mavazi yake yakawa meupe kuliko theluji iliyowazunguka. Walipewa kuona mapema jinsi Bwana Yesu atakavyoonekana atakaporudi duniani. Lakini wakati huo huo ni picha ya jinsi tunavyoweza kumwazia Bwana Yesu sasa akiwa mkono wa kuume wa Nguvu. Aidha, Yohana anasema kwamba Roho Mtakatifu angeweza kuja tu baada ya Yesu kutukuzwa, yaani baada ya kukalia mahali hapo

3. Baadhi ya wafafanuzi wanakisia kwamba mlima Hermoni, ambao kuanzia kimo cha mita 1,800 hufunika na theluji kwa miezi kadhaa kila mwaka, ndio ulikuwa mlima wa kugeuka sura.

pa heshima mkono wa kuume wa Mungu. Roho wa Mungu alipaswa kutumwa hasa na Mwana wa Mungu aliyetukuzwa na kuvikwa taji, ili aushuhudie ushindi wake na utukufu wake na kuuimarisha ndani ya mioyo yetu.

Roho hataki kuwa mpangaji mdogo katika chumba cha pembeni cha maisha yetu. Hapana, ni kusudi la Mungu kwamba Roho huyu atujaze, amfanye Yesu kuwa mkuu ndani yetu, atuongoze na kutupa ushindi wa maisha ya washindi. Hayo ndiyo mambo halisi! Swali la kwa nini mara nyingi mambo hayaonekani hivyo, bila shaka tutalichunguza baadaye.

Hebu tuifurahie mandhari hii! Mlima mkubwa, kilele chake kikiwa cheupe kinachong'aa na kuumiza macho, na vijito vya maji yanayobubujika vinavyoporomoka kutoka juu kwenda bondeni. Nguvu ya ukuaji huanza mahali ambapo pana udongo mzuri.

Safari inakaribia mwisho polepole. Kwa kweli bado hatutaki kutua, lakini mafuta yanakwisha. Yanatosha tu kwa mizunguko michache juu ya ukijani, unaozidi kuwa mzito na wenye rutuba kadiri unavyoshuka bondeni. Kwanza ni vichaka tu na madoa machache ya kijani, kisha miti kadhaa, na kabla hatujatambua tunaruka juu ya msitu mnene. Kisha tunaona bondeni mashamba, makonde na mashamba makubwa ya mimea.

Je, mnajua kwamba hata ndani ya mioyo yenu maji ya Roho wa Mungu yameanzisha ukuaji wa kiroho, lakini halisi? Wokovu ni kitu kamili ndani yake wenyewe, lakini ndani yenu wakati huo huo ni mwanzo. Ndani ya mioyo yenu mbegu mpya imechipuka. Mmezaliwa mara ya pili. Ninyi si watu walewale kama zamani. Jambo hili haliwezi kuonekana kwa macho. Kwa nje tu (uzito wa mwili, sauti na kadhalika) kila kitu kwenu ni sawasawa kabisa na zamani. Lakini hata hivyo jambo kubwa mno limetokea. Mmezaliwa upya, tena mmezaliwa na Mungu mwenyewe. Mnaweza kuanza tena tangu mwanzo.

Mbegu hii ni Neno la Mungu la milele. Amepanda uzima wa milele ndani yetu, na uzima huu unakua. Mada hii tutaiendeleza zaidi katika sura inayofuata. Tunapouona ukijani wote wa mashamba, miti na mashamba makubwa ya mimea, tunatambua: Unashuhudia jinsi nguvu ambayo Mungu ameiweka katika uhai wa mimea ilivyo kubwa. Jua linapowaka, udongo ukiwa mzuri na maji yakitoka milimani, ukuaji hauwezi kuzuiwa. Je, tunadhani kwamba ukuaji wa kiroho ndani ya wanadamu una nguvu ndogo zaidi, ilhali hapa hatuzungumzii mimea, bali mwanadamu, “taji la uumbaji”?

Baada ya safari hii ya kusisimua tunatua. Bado tumeguswa sana na ukuu na uzuri wa mlima huu na mazingira yake. Tunakumbuka sisi ni nani: watoto wa Mungu. Hatia ya dhambi imeondolewa milele. Kile tulichokuwa kama utu wa zamani ni historia. Kimeondolewa kwa njia ya msalaba na kutupwa nyuma ya mgongo wa Mungu. Mahali pa utu wa zamani Mungu ameweka utu mpya, ambao ameuumba kwa mfano wa Yesu Kristo. Utu huu mpya una uzima wa milele. Kristo mwenyewe ndiye uzima wake – yeye aliye na maji yaliyo hai ndani yake, yanayoufanya ukue, ili ukomae na kuwa na nguvu katika imani.

Rubani anatua kwa mshtuko, nasi tuko tena ardhini. Je, tumeota ndoto tu, au ni kweli yote haya tuliyoyaona? Ndiyo, ni kweli. Neno la Mungu linasema hivyo.

Huenda safari hii ya kuzunguka imewafanya mtake kujua zaidi. Katika kurasa zinazofuata mtapata mengi zaidi kuhusu yale ambayo, kwa maana halisi ya neno, tumeyapitia juu juu tu kwa ndege. Ikiwa hadi sasa tumeruka tu, sasa mnakaribishwa kwenye matembezi milimani yatakayowafikisha mahali pazuri.

2. Tumetua – na sasa tuendeleo vipi?

Baada ya kutua kwa mtikisiko tunarudi kwenye ardhi ya mambo halisi. Ikiwa wokovu wa Mungu ni mpana hivyo, na si tiketi yangu ya kwenda mbinguni tu, swali linazuka: Unawezaje kubadilisha maisha yangu? Mungu mwenyewe anataka tuishi katika uhuru. Hatulindi tu na hukumu; anataka pia kutukomboza kutoka katika utumwa wa dhambi na kutoka katika udikteta wa maisha yetu ya zamani ya ubinafsi. Wokovu si jambo la kinadharia. Wokovu wa Mungu ni neno la msalaba – Injili, iliyo nguvu ya kuleta wokovu, na hivyo uzima, kwa kila aminiye!

2.1 Uhuru au utumwa – lakini si vyote viwili

Zamani Waisraeli walikuwa katika utumwa usio na huruma. Bila njia ya kutokea wala tumaini la uhuru. Lakini Mungu aliuona msiba wao, akawahurumia, akaingilia kati. Mwana-kondoo wa Pasaka aliyewalinda na hukumu hakuwa bado ndio ukombozi wenyewe. Waliupata ukombozi huo pale tu walipoiacha Misri nyuma yao. Jambo hili linataka kutuambia nini? Kwa wazi kabisa: Sisi pia tuko chini ya ulinzi wa damu ya Yesu, lakini zaidi ya hayo tumekombolewa na kuwekwa huru kwa ajili ya maisha mapya.

Jambo lifuatalo kutoka historia ya karibu linaonyesha kwa mfano kile kilicho muhimu. Marekebisho ya 13 ya Katiba ya Marekani⁴ yaliwasilishwa kwa majimbo tarehe 31 Januari 1865 ili yaidhinishwe, na yakaanza kutumika tarehe 18 Desemba 1865. Yaliukomesha utumwa kabisa katika eneo lote la Marekani.

Marekebisho haya yalipotiwa sahihi katika majimbo yote, sheria hii ilianza kutumika mara moja bila masharti yoyote. Sasa fikirieni watumwa wengi katika majimbo ya kusini, jinsi walivyokuwa wakiendelea na kazi zao siku hiyo. Ingawa kwa sheria sasa walikuwa huru na walikuwa na haki ya kuwaacha mabwana zao, wengi hawakufanya hivyo. Kwanza walipaswa kuijua sheria hii. Kisha walipaswa kuamini kwamba ni kweli, na hatimaye walipaswa kuudai uhuru huo na kuishi kama watu huru.

Ndivyo ilivyo kwetu. “Sheria hii ya ukombozi” ilitiwa sahihi miaka 2,000 iliyopita pale Golgotha. Sheria hii (kama ile ya kukomesha utumwa) bado

4. *The Thirteenth Amendment to the Constitution of the United States of America.*

inatumika hadi leo. Biblia inasema kwamba tumewekwa huru mbali na nguvu ya dhambi, kwa kuwa utu wetu wa zamani, kama tulivyokwisha kuona katika safari yetu ya ndege ya kuzunguka, ulisulubiwa pamoja na Kristo. Jambo hili lilitokea kwa ajili yangu pale Golgotha bila mchango wangu, kwa njia ya kifo cha Yesu kilichoshuhudiwa katika historia. Huu ndio ujumbe wa Injili: Uhuru! Baadhi ya watumwa hawakujua kwa muda mrefu chochote kuhusu sheria hii mpya, wakaishi kana kwamba haikuwa imeanza kutumika. Tunaona kazi ya utumwa isiyo halali kuwa jambo lisilokubalika kabisa, sivyo? Lakini Wakristo wangapi wanaishi, kwa kujua au bila kujua, kana kwamba ukombozi kwa njia ya Kristo haupo! Wangapi wanafurahi tu kwamba siku moja watakuwa mbinguni. Lakini “sheria hii ya ukombozi” ya Golgotha inatumika hapa na leo, si mbinguni tu! Mungu ameivunja nguvu ya dhambi. Maana yake ni kwamba tunaweza kuudai ukombozi huu kabisa kwa ajili yetu wenyewe kwa imani. Tunapaswa kuupokea kama ukweli kwamba tumeifia dhambi, yaani utu wetu wa zamani umekufa pamoja na Kristo. Jihesabuni kuwa wafu – ya kale yamekwisha! Hivyo ndivyo Paulo anavyosema, naye anatumia neno kutoka katika uhasibu wa fedha. Hapa tunazungumzia mantiki ya mambo halisi, si mantiki ya hisia zinazobadilika-badilika.

2.2 Amri za uhuru

Tunapaswa kuzielewa vizuri kanuni za uhuru ndani ya Kristo ili tuweze pia kuuonja. Kwanza kabisa hapa tunazungumzia mambo halisi ya wokovu, ambayo tunayategemea kwa imani kama mambo yanayotuhusu sisi, wala si hisia nzuri ya kuwa huru.

Jambo la pili linatokana na la kwanza: Ninapojaribiwa, dhambi inapovizia mlangoni, ninapolazimika kuchagua kati ya dhambi na Mungu, basi hili ndilo linalotumika: Si lazima mtende dhambi; ninyi ni huru! Kumbukeni ukweli huu. Mwombeni Mungu awakumbushe. Hatuhitaji kuganda kwa hofu mbele ya dhambi; badala yake Agano Jipya linatuagiza tuchukue hatua dhidi ya dhambi katika maisha yetu. Tunapaswa kuyaondoa mambo haya ya dhambi kabisa bila kusita. Ndivyo Mungu alivyofanya pale Golgotha, alipoihukumu dhambi katika Mwanawe.

Huenda tatizo kubwa kuliko yote la wakati wetu ni ubinafsi. Sisi wenyewe tuko katikati, na tunajizunguka sisi wenyewe. Jambo hilo halitusaidii katika

maisha pamoja na Mungu. Hebu tuache kujitazama sisi wenyewe, tumtazame Kristo. Huo ndio ushindi wetu!

- Utegemeeni wokovu wa Mungu unaowaweka huru kama ukweli wa kihistoria!
- Dhambi inapotaka kutawala, jikumbusheni tena na tena kwamba nguvu yake imevunjwa!
- Msiganda mnapojaribiwa, bali ikataeni dhambi kwa vitendo!
- Msiikazie macho dhambi na mapambano dhidi yake, bali mkazieni macho Kristo na nguvu ya Roho Mtakatifu!

2.3 Kukimbia na kupinga

Hata hivyo, katika mapambano kama hayo hatupaswi kujikadiria kupita kiasi. Kuna hali ambazo tunapaswa kuchukua hatua, na hali ambazo tunapaswa kushambulia. Mambo ya dhambi tunapaswa kuyahukumu, kuyaondoa au kuyaangamiza. Lakini jaribu la kutenda dhambi na mazingira yake ya karibu tunapaswa kuyakimbia. Hasa linapohusu vishawishi vya ngono, na pia tamaa ya mali na ibada ya sanamu. Yusufu ni mfano wa kukimbia wakati unaofaa. Hakuna kitu kingine isipokuwa kukimbia ambacho kingeweza kumzuia asipande kitandani kwa mke wa Potifa, aliyekuwa ameandaa kila kitu ili kufanya uzinzi.

2.4 Hisia

Kwa maana yake, Biblia inasema: Hesabuni hivyo, chukulieni kuwa hakika, daini kwa ajili yenu wenyewe kwamba mmeufia utumwa wa dhambi! Haki ya kuishi kama watu waliowekwa huru mmepelele! Mtumwa wa majimbo ya kusini angewatazama kwa mshangao kama mngesema: “Sihisi ukombozi huu.” Angewaambia kwamba hamhitaji kuuhisi hata kidogo, kwa sababu sheria iliyotiwa sahihi ni halali kisheria. Sheria hii haijali hata kidogo mnachokihisi. Inatumika daima – bila kujali ninachokihisi. Watchman Nee anatoa mfano unaofaa: “Hapo zamani Ukweli, Imani na Uzoefu walikuwa wakitembea mmoja nyuma ya mwingine juu ya ukuta mwembamba. Ukweli hakugeuka kulia wala kushoto wala kutazama nyuma, bali alisonga mbele bila kusita. Maadamu Imani, aliyekuwa nyuma yake, aliendelea kumkazia macho Ukweli, mambo yote yalikwenda vizuri. Lakini alipoanza kuhangaika kuhusu Uzoefu na kugeuka kumtazama, alipoteza usawa wake, akaanguka kutoka ukutani, na yule Uzoefu

mzee mwema akaanguka nyuma yake.”⁵

Bila shaka hisia zina nafasi muhimu katika maisha ya Kikristo. Hisia ni sehemu ya lazima na ya ajabu ya ubinadamu wetu. Furaha mtu huionja kama hisia (mhemko), na Mungu anataka tufurahi; hata anaamuru. Furaha anayoitoea yeye ni matokeo ya wokovu. Inaweza kuonjwa, kuhisiwa, nayo ni ya kweli. Lakini imani na kutumaini havijumuishi hisia, kwa sababu hisia hubadilika-badilika. Kwa imani, kilicho kweli na halisi ni kile ambacho Biblia inaiyahidi. Imani inadai kwa utulivu – iwe kuna hisia au hakuna – kile ambacho Mungu anaiahidi. Mpanda milima anapaswa kuamini kwa asilimia 100 maelezo ya mtengenezaji wa kamba zake za kupandia anaponing’inia juu ya shimo. Hisia zake hazina nafasi yoyote.

2.5 Meli yenye nahodha wa zamani na nahodha mpya

Hebu tuyalinganishe maisha yetu na meli. Kabla ya kuzaliwa mara ya pili, sisi wenyewe tuliamua mwelekeo na lengo. Lakini badiliko kubwa limetokea. Meli imenunuliwa; si mali yetu tena. Matokeo yake ni kwamba kuna nahodha mpya. Ni nani huyo? Bado ni mimi, lakini Mungu amenipa uzima mpya na Roho wake. Ndani ya Kristo nimekuwa utu mpya.

Nahodha wa zamani ana uzoefu mwingi na mazoea. Zamani kila kitu kilimtii yeye. Kulikuwa na desturi nyingi zilizoonyesha jinsi nahodha wa zamani alivyoiongoza meli. Lakini sasa ununuzi wa meli umekamilishwa mbele ya mthibitishaji wa kisheria, na kubadilika kwa mmiliki kumepangwa kwa mkataba. Haijalishi nahodha mpya ni kijana kiasi gani au hana uzoefu kiasi gani; amekuwa nahodha mpya kihalali. Nahodha wa zamani – tumlinganishe na dhambi, na tabia yetu ya mwili au na asili ya zamani ya dhambi – atabaki melini hadi siku ya ukombozi wetu kamili itakapofika. Hii ni hali ngumu kuielewa. Lakini huo ndio uhalisi wa kuwa Mkristo. Nahodha wa zamani bado yuko melini, lakini anapaswa kujiondoa aingie katika chumba chake. Haruhusiwi tena kuingilia uongozi wa meli. Hata hivyo, nahodha mpya anapaswa kuhakikisha kwamba yule wa zamani anabaki mahali anapostahili, na wakati huo huo kuukazia macho mwelekeo wa meli: Sasa yeye ndiye amesimama kwenye usukani. Yuko kwenye daraja la nahodha, mahali maamuzi yanapofanywa. Mmiliki mpya wa meli ni Kristo ndani yangu, anayetenda kazi kwa njia ya Roho wa Mungu. Agano Jipya linasema kwamba hawa wawili, yaani tabia ya mwili na Roho, wanapingana na

5. Watchman Nee, *Das normale Christenleben* (Maisha ya Kawaida ya Mkristo), uk. 47.

wote wawili wanadai kuyatawala maisha. Wakati tabia ya mwili inadai hivyo bila haki, dai la Roho wa Mungu ni halali, kwa sababu tumenunuliwa na Mungu.

Kwa mazoea, nahodha wa zamani anataka tena na tena kuingilia shughuli za nahodha mpya. Angependa sana kuichukua meli tena na kumfukuzia nahodha mpya katika chumba kile, mahali ambapo yeye mwenyewe anastahili kuwa. Hivyo mvutano unabaki melini. Mvutano huo unapungua sana nahodha mpya anapoutegemea mkataba tu, kwa urahisi kabisa – bila kujali anavyojisikia. Anapaswa kumrudisha yule wa zamani chumbani tena na tena. Asipofanya hivyo, akamwacha nahodha wa zamani azunguke-zunguke melini, mambo yanaweza kuishia vibaya. Kadiri nahodha wa zamani anavyopewa uangalifu, umakini na kujaliwa zaidi, ndivyo atakavyosimama mara nyingi zaidi tena kwenye usukani.

2.6 Mbele kwa nguvu zote!

Kauli mbiu ya nahodha mpya ni: Mbele kwa nguvu zote! Katika meli ya maisha yetu tumeshika uongozi. Ndani ya Kristo tunapaswa na tunaweza kutawala katika uzima. Hatimaye kujiamulia mambo yetu wenyewe maana yake ni kuishi maisha yanayoamuliwa na Mungu na yaliyojazwa Kristo. Na katika hayo tunaweka nguvu zetu, umakini wetu, mambo tunayoyapenda na malengo yetu. Sasa ni mali ya mmiliki mpya. Meli inafuata mwelekeo mpya, ina maana mpya ya maisha, inakwenda kinyume cha mkondo. Kutakuwa na dhoruba, vikwazo, maji kuingia melini, lakini hayo hayatatuzuia.

Nyaraka zote za Agano Jipya zinazungumzia mwendo usiokoma na nguvu ya mabadiliko, ambavyo ni sehemu ya maisha ya Kikristo:

- Pigeni mbio
- Fisheni
- Kueni
- Fuateni
- Jitakaseni
- Jazweni
- Mfanywe upya
- Zidini sana
- Vueni na mvae

Maagizo haya na mengine zaidi yanaonyesha wazi kwamba hakuna kinachotokea chenyewe. Mungu “haleti kwa uchawi” katika maisha yetu kile ambacho sisi wenyewe tunapaswa kukitenda (ingawa yote yako chini ya amri yake). Nguvu ya Mungu iko tayari kwa ajili yetu, na kumtumaini yeye ndiyo mfereji ambao kwa njia yake nguvu hii inatufikia. Hakuna kinachotokea, isipokuwa mtu akifanye! Ni neno la kweli, hata kuhusu utakaso wetu. Mungu anataka tujitoe kikamilifu. Wokovu wetu umezungukwa na maagizo haya; maagizo hayo na kuyatii ni sehemu yake kama kupumua kulivyo sehemu ya uhai. Maagizo haya kwa urahisi kabisa yanafuata “mantiki ya wokovu”.

2.7 Baba yetu

Maisha ya kujitoa kikamilifu hayafanikiwi kila siku. Sisi ni watu wa kuona mambo jinsi yalivyo, tukijua kwamba kila siku tunakabiliana na kushindwa katika mambo madogo au makubwa. Lakini maisha yetu yamo mkononi mwa Baba yetu wa mbinguni. Yeye si dikteta anayevizia makosa yetu. Sisi ni wanawe na binti zake, ambao amewanunua kwa gharama kubwa mno isiyo na kipimo, yaani uhai wa Mwanawe mwenyewe. Tunaishi kutokana na uhusiano huu wa neema. Hatuko chini ya sheria inayodai bila huruma, bali chini ya neema ya Baba yetu wa mbinguni. Yeye anatutia moyo na kutusaidia, anatumasisha na kutuchochea tena na tena. Anatupa kile tunachohitaji kwa maisha ya kumletea heshima. Katika maombi tunamwita “Aba” (Baba mpendwa). Hatulaumu jambo fulani linaposhindikana au udhaifu unapojitokeza katika maisha yetu. Kwake tunaziungama dhambi zetu, ambazo kwa bahati mbaya bado hutokea. Kila dhambi tunayoitenda bila kuiungama inaharibu ushirika wetu na Baba yetu wa mbinguni na Mwanawe Yesu Kristo. Kwa hiyo tunapaswa kuziondoa njiani. Mkikosa ujasiri na kujiona hamstahili, mkidhani kwamba ninyi ni watu walioshindwa, basi tieni moyo kwa maneno haya ya Mungu: “Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima” (Isaya 42:3).

Hatua ya kurudi mikononi mwa Baba inawezekana daima. Kwake kuna msamaha, neema na kurejeshwa, pamoja na mwanzo mpya. Kwake mtu anaweza kupona tena, hata kama imani ni dhaifu na kujitoa kumekaribia kuzimika. Samsoni alikuwa ameanguka chini kabisa, lakini alirudi katika hali njema tena. Nywele zake zilianza kukua tena, ingawa kwa bahati mbaya hakupata tena kuona kwa macho yake. Ilichukua muda hadi kufika hapo, lakini

siku ya ushindi wake mkuu kuliko yote ilikuja, hata ingawa kabla ya hapo alikuwa amepata kushindwa kukubwa kwa sababu ya dhambi.

2.8 Mungu anataka nini

Mungu hatudai chochote ambacho hatuwezi kukifikia! Anataka moyo wetu; anataka furaha na kuguswa ndani kabisa tunapomfikiria. Mungu anataka kutufanya tuwe na furaha. Hataki kututumia vibaya, wala kutunyang'anya furaha ya maisha. Wakati mwingine Wakristo wanaonyesha picha hiyo. Tunakuwaje na furaha kama Wakristo? Tunaipata katika maisha yaliyokabidhiwa kwake kabisa, wala si mahali pengine popote. Ninamnukuu Jay Adams: “Kwa Wakristo wengi tunaona upungufu mkubwa: Wanakosa ustahimilivu, wanakosa kudumu. Huenda ustahimilivu ndio ufunguo wa maisha yenye utaratibu yanayompendeza Mungu. Hakuna anayejifunza kuteleza kwenye barafu, kuteleza kwenye theluji, kupiga filimbi, kufunga kamba za viatu, kusoma, kuandika au kuendesha gari, asipojaribu kwa muda wa kutosha. Mtu hujifunza kwa kuendelea kwa bidii, licha ya kutokuwa stadi na kushindwa, hadi apate ujuzi aliokuwa akiutafuta. Mtu hujifunza kwa kurudia tena na tena kile anachotaka kujifunza. Biblia inatuambia kwamba ndivyo ilivyo pia kwa mwenendo wa maisha uliotakaswa.

Hatupaswi kuelewa vibaya kwamba Maandiko yanasisitiza sana juhudi zetu wenyewe; juhudi hii ina mizizi yake katika neema, wala si ‘tendo la tabia ya mwili’. Ni kwa Roho Mtakatifu peke yake tunaweza kupata ustahimilivu. Lakini utendaji wa Roho si wa ‘kifumbo’. Roho Mtakatifu anatuambia jinsi anavyofanya kazi: Maandiko yanashuhudia kwamba anafanya kazi kwa njia ya Maandiko.

Kwa kuyatii maagizo ya Biblia kwa hiari, kwa maombi na kwa kudumu, mienendo ya maisha ya kibiblia inakuwa sehemu yetu sisi wenyewe. Tunasoma Biblia na wakati huo huo tunamwomba Mungu atusaidie kuyatenda yale tuliyoyasoma. Kwa ajili hiyo ametupa Roho Mtakatifu. Neno ‘neema’ lina maana ya pande nyingi. Upande mmoja ni ‘msaada’. Roho Mtakatifu huwasaidia wale wanaolisoma neno lake na kisha kuthubutu kwa imani kutenda anachokisema. Hatuahidi nguvu kama malipo ya mapema. Mara nyingi nguvu huja (pale tu) tunapotenda kile tunachotakiwa kukitenda.”⁶

6. Jay E. Adams, *Grundlagen biblischer Seelsorge*, uk. 255.

2.9 YEYE hana budi kuzidi – bali mimi kupungua!

Hili lilikuwa lengo la maisha ya Yohana Mbatizaji, aliyekuwa mtangulizi wa Bwana Yesu. Ni mchakato ambao tunataka kuupokea kutoka kwa Yohana, tukijua kwamba utadumu maisha yetu yote! Mchoro unaonyesha kile ambacho sentensi hii rahisi, na pia ngumu, ya Yohana inasema: Alama ya kutoa inahusu maisha yetu ya zamani pamoja na malengo na mambo yetu wenyewe tunayoyapenda, wakati alama ya kuongeza kwa wazi kabisa inamhusu Bwana wetu!

(Mchoro: Mistari minili ya mikunjo inayokwenda kinyume juu ya mstari wa wakati; mkunjo unaosbuka umewekwa alama ya kutoa, unaopanda umewekwa alama ya kuongeza.)

- Kuvua utu wa zamani –
- Kuvaa utu mpya +
- Kufanana na Kristo kunakoongezeka na hivi karibuni kuwa kamili
- Uwanja wa mashindano ya imani
- Mchakato wa ukuaji maisha yote
- Kuzaliwa mara ya pili
- Kuja kwa Yesu na ufufuo

2.10 Maisha mapya katika mchoro

Michoro inayofuata (mraba, duara, pambetatu) inawakilisha watu mbalimbali. Mstari wa kwanza unaonyesha jinsi mtu anavyozaliwa, wa pili ukuaji wa maisha yake binafsi, na wa tatu kuzaliwa mara ya pili. Mistari ya nne na ya tano inaonyesha jinsi anavyokua katika imani au anavyoishi kwa kufuata tabia ya mwili, wakati mstari wa sita unaonyesha lengo, ukamilifu pamoja na Kristo.

Maumbo haya matatu yanatumika kutofautisha watu wowote kama wanavyozaliwa. Tofauti inaweza kuwa katika asili ya familia na mazingira ya kijamii, katika upekee wa mtu huyo, katika hulka tofauti na vipawa vya asili. Kwa jumla, yote yanahusu mtu binafsi jinsi anavyotofautiana na watu wengine. Huo ndio ulikuwa utambulisho wake alipozaliwa, bila yeye mwenyewe kuchangia chochote. Ni kile ambacho mtu mwenyewe, isipokuwa mara chache, hawezi kukibadilisha: muundo wake. Jambo hili linaonyeshwa kwa maumbo matupu katika mstari wa kwanza.

Maumbo hayabaki matupu. Mwanadamu anazaliwa akiwa mwenye dhambi, naye anatenda dhambi. Muundo wa haiba yake unaundwa na dhambi kuelekea upande usio sahihi. Mazoea ya dhambi yanaibuka, nayo kwa upande wake yanajenga tabia mbaya. Jambo hili linaonyeshwa kwa kile kinachoyajaza maumbo sasa. Hata kama kuna mema ya kimaadili ndani ya mtu, bado ameathiriwa na dhambi ikaayo ndani yake. Maumbo yaliyojazwa yanaonyesha mwanadamu kabla ya kuzaliwa mara ya pili.

Mungu hamrekebishi mwanadamu, bali anaumba kitu kipya. Kipya hicho kimeandaliwa kikamilifu kulingana na haiba ya mtu binafsi. Kama ndani ya Adamu aina zote za haiba za wanadamu zilikuwepo tayari, ndivyo ilivyo pia kwa Adamu wa mwisho, Bwana wetu Yesu Kristo. Alifanyika mwanadamu, na hivyo anaweza kuishi ndani ya kila mtu binafsi. Biblia inalinganisha jambo hili na mbegu inayopandwa ndani yetu: Inapaswa kukua tangu siku ya kwanza, ili asili yetu ibadilishwe kuwa asili ya Kristo. Mbegu ya kiungu inalingana kabisa na umbo la haiba. Hivyo sifa za mwanadamu alizopewa katika uumbaji (yaani alizorithi) hazibadilishwi na kuzaliwa mara ya pili. “Tunapaswa kukubali kwamba Mungu ana uwezo, kwa namna fulani, wa kuingiza ndani ya kila mtu kitu kipya kabisa kinacholingana kikamilifu na haiba yake, ambayo hakuwahi kukusudia kuiharibu.”⁷ Ndani ya haiba ya kila mtu binafsi sasa inaingia asili ya Kristo, nayo inakuwa hivyo onyesho la kipekee la asili ya Yesu. Huu ni udhihirisho wa utofauti na utajiri wa uumbaji mpya, kama ulivyokuwepo tayari katika uumbaji wa kwanza.

(Mchoro wenye mistari sita, kila mmoja ukiva na mraba, duara na pembetatu)

(Mstari wa 1: maumbo matatu ni ya kijivu na matupu)

Watu mbalimbali jinsi wanavyozaliwa wakiwa na haiba yao binafsi

(Mstari wa 2: maumbo yamejazwa maumbo mengi madogo meusi)

Kabla ya kuzaliwa mara ya pili, haiba ya mtu binafsi inajazwa na mambo anayoyapitia katika maisha ya kila siku. Tabia inajengeka. Mbali na sifa njema za tabia, mara nyingi kuna mienendo inayotoka katika moyo mwovu, ambayo wakati mwingine imetawaliwa zaidi na dhambi. Yaliyomo ndani ya mraba, duara na pembetatu yanalingana na kile ambacho mtu huyo amekuwa bila Mungu.

(Mstari wa 3: katikati ya kila umbo linaonekana umbo dogo jeupe la sura ileile)

Siku ya kuzaliwa mara ya pili, mbegu ya kiungu ya Neno la Mungu inapandwa ndani ya mwanadamu. Sasa Kristo mwenyewe ndiye uzima mpya wa kiroho wa

7. Custance, Arthur C., *Man in Adam and in Christ*, uk. 171.

muumini. Uzima huu mpya umefanywa ulingane na haiba ya mtu. Jambo hili linaonekana kwa kulingana kwa umbo dogo na umbo kubwa (kwa mfano, mraba mdogo na mraba mkubwa). Kuzaliwa mara ya pili hakubadilishi haiba ya mtu binafsi aliyopewa na Mungu katika uumbaji, bali kunajaza uzima mpya wa Kristo. Lengo la Mungu ni kuifanya upya na kuigeuza haiba iliyozaliwa katika dhambi ili ifanane na Kristo.

(Mstari wa 4: umbo jeupe limekua, maumbo mweni yamefungua)

Tangu siku ya kuzaliwa mara ya pili, mbegu ya uzima wa kiungu inaanza kukua. Kristo anazidi kuumbika ndani ya mtu huyo katika mchakato wa ukuaji usiokoma. Yaliyomo ya zamani, mwenendo wa zamani wa maisha na mitindo ya zamani ya tabia vinapungua na kutoweka zaidi na zaidi. Mbegu inaendelea kukua; yaani, asili ya Kristo inazidi kupenya, kumjaza na kumuunda yule aliyezaliwa mara ya pili.

(Mstari wa 5: katika mraba umbo jeupe limekuwa dogo tena na wengi umeongezeka; katika duara na pembetatu umbo jeupe linajaza karibu kila kitu)

Maisha ya Mkristo huyu hayakuendelea kukua. Maisha ya zamani yamerudi tena mbele.

Wakristo hawa wawili wamekua katika imani. Wamekuwa makini kuyafisha matendo ya tabia ya mwili, kumtumaini Kristo kama kiini na lengo la maisha yao, na kumtumikia YEYE.

(Mstari wa 6: mraba, duara na pembetatu ni mwenye kabisa)

Katika umilele kila muumini ana mwili wa ufufuo, yaani mwili wa utukufu. Katika mwili huo yeye yu sawa na Kristo. Wakati huo huo atakuwa milele mtu yuleyule binafsi ambaye Mungu alimruhusu kuwa kupitia vazazi wake, au alimuumba. Dhambi na tabia ya mwili yenye dhambi katika ukamilisho ni mambo yaliyopita kabisa, ni historia.

Mbegu iliyopandwa inapaswa kukua, ili Kristo na asili yake waipenye haiba zaidi na zaidi. Hilo ndilo lengo la Mungu. Yeye mwenyewe ndiye anayeleta ukuaji. Lakini kiwango na kasi ya ukuaji vinaathiriwa na sisi. Tunaagizwa kuuvua mwenendo wa zamani wa maisha, ili mtindo wa maisha wa utu mpya uzidi kuonekana kwa wale wanaotuzunguka. Maumbo katika mchoro yanabaki yaleyale daima; yaliyomo tu ndiyo yanayobadilika. Tunaagizwa kuziondoa kabisa bila kusita mbegu na mimea mingine yote isiyotoka kwa Mungu na kwa Roho wake na inayotokana na maisha ya zamani, ili mbegu ya Mungu iweze kukua.

Mstari wa tano unaonyesha wazi kwamba kwa bahati mbaya mambo yanaweza pia kurudi nyuma, na mbegu, yaani Kristo, haina tena nafasi muhimu kuliko zote katikati ya maisha yetu. Mbegu inakuwa ndogo, na maisha ya zamani ya ubinafsi yanaongezeka tena.

Au ukuaji ni wa kudumu, kama inavyoonyeshwa katika duara na pembetatu, ambapo haiba imeshikwa na kujazwa na Kristo kweli.

Mwishowe ataonekana Kristo peke yake, katika ukamilifu wa utukufu wa mbinguni. Tutakuwa milele sisi wenyewe kama Mungu alivyotuumba, lakini wakati huo bila dhambi yoyote, na hata hivyo tukiwa sawa na Bwana.

Mbegu ya Mungu katika maisha yangu ni kubwa kiasi gani? Imekua kwa kiasi gani?

2.11 Yote kwa pamoja kwa mtazamo mmoja

Mchoro huu⁸ ni muhtasari rahisi wa mambo muhimu ya maisha yetu ya Kikristo, ambayo yanaathiriana moja kwa moja na kutegemeana. Tumeamua kutoupokea wokovu kama tiketi tu ya kwenda kwenye umilele wa heri. Tunataka kuuonja uzima utokao kwa Mungu, upendo wake, furaha yake na amani yake tayari sasa. Kama Bwana Yesu Kristo alivyotoa vyote ili atumiliki, vivyo hivyo tunataka kumpa maisha yetu kwa shukrani.

Hili si jukumu lisiloweza kutekelezwa. Mungu anataka furaha yetu kamili na kuridhika kwetu, na tunavipata tu katika maisha ya kumwishia Mungu. Maisha kama hayo yana Kristo kama kitovu chake, kama kiini cha maisha, lengo la maisha na wakati ujao. Siku moja atajaza kila pembe ya ulimwengu, naye anatumia tayari sasa. Utumilifu huu unapenya hali yetu yote ya kuwa, na kutubadilisha siku baada ya siku zaidi kufanana na sura yake. Sisi wenyewe ndio tunaogundua kwa uchache kabisa badiliko hili jema, lakini Mungu anafanya kazi ndani yetu.

Mwanzoni yupo Roho Mtakatifu. Yeye ndiye nguvu na msingi wa matendo yote. Pamoja na hilo kuna mambo tunayoyapitia kila siku, yanayotuunda na kutupa changamoto ya kutenda mema, lakini pia kutujaribu tutende mabaya. Huu ndio uwanja wa imani, ambapo mambo makubwa ya maisha yetu yanatukia, tunapomtii na kumtumaini Bwana wa maisha yetu tusingemwona, na kumpenda.

8. Wazo kutoka kwa Dallas Willard, *The Divine Conspiracy*, uk. 347.

Katika yote yanahitajika kujitoa kwetu kikamilifu, juhudi zetu na nia ya kulichukulia jambo kwa uzito. Tunapaswa kumfuata Yesu kwa moyo usiogawanyika na uliojaa, tukiwa tayari na wenye nidhamu ya kuweka kando maisha yetu wenyewe, matakwa yetu na faida zetu, ili tupate uzima wa kweli.

(Mchoro: Pambetatu yenye mishale mitatu inayoelekea kutoka juu na kutoka pembe mbili za chini kwenye duara lililo katikati; maandishi juu, ndani ya duara, chini kushoto na chini kulia)

Utendaji wa Mungu katika neema, nguvu na msaada kwa njia ya Roho Mtakatifu, anayekaa ndani yetu na kusimama karibu nasi daima. Neno lake, Biblia, ndiyo hekima kwa maisha yetu. Anataka kutufikisha salama kwenye lengo la mwisho, lakini pia kulifikia pamoja nasi lengo lake binafsi kwa ajili ya maisha yetu hapa duniani.

Asili na uzima wa Yesu Kristo ndio kitovu na kiini cha kuwa Mkristo. Yesu anapaswa kuumbika ndani yetu. Mungu atatufanya tufanane na sura ya Mwanawe. Mchakato huu utakamilishwa wakati wa kuja kwa Kristo, lakini kwa upande wa maadili unaanza tayari hapa duniani!

Uhalisi wa maisha, uwanja wa mashindano ya imani: maisha ya kila siku pamoja na vishawishi vyake vyote vya dhambi na madanganyo, lakini pia majaribu na mashambulizi ya adui, na majaribu mbalimbali katika malezi ya Baba yetu wa mbinguni

Imani yetu na nia yetu, uamuzi wetu na juhudi zetu, bidii yetu, nidhamu na ustahimilivu, ili tuendelee na kuendelea kukimbia katika uwanja wa mashindano ya imani licha ya kutokuwa stadi kwetu, licha ya makosa, vikwazo na kushindwa, ili tulifikie lengo la mwisho la mbinguni

2.12 Matembezi milimani

Sasa, baada ya safari ya ndege ya kuzunguka kutuachia picha yenye nguvu, ninawakaribisha katika matembezi kadhaa ya “kiroho” milimani. Watoto wangu hawapendi sana matembezi ya miguu, na hata mimi mara nyingi ninapaswa kujilazimisha. Lakini jambo moja nimeligundua: Ninapoviona vilele vingi vya milima ya Alpi ya Allgäu kutoka chumbani mwangu ninamofanyia kazi, ni uzoefu usio na bei kuwa nimepanda mmoja wa vilele hivi kwa miguu na kufurahia mandhari yake. Wakati huo baada ya kupanda kwa taabu hauwezi kununuliwa; mtu anapaswa kuchukua hatua yeye mwenyewe. Kutazama kutoka

ndani ya ndege ni jambo moja, lakini kwenda milimani mwenyewe ni jambo jingine.

Matembezi haya milimani si matembezi mepesi katika nchi tambarare. Ninachowakaribisha kwacho ni matembezi ya kususimua milimani, ambapo tunapanda kwa subira, tukiwa na sehemu nyepesi na ngumu mbele yetu, lakini daima tukilikazia macho lengo kwa wazi: Ni yale mambo halisi ya wokovu ambayo tayari “*tumeyapitia juu kwa ndege*”. Sasa tunataka kuangalia mambo muhimu ya kina yaliyomo katika fundisho la Biblia kuhusu nafasi yetu ndani ya Kristo, na kuhusu ukweli wa maana ya “Kristo ndani yetu”. Matembezi haya milimani yana faida. Mimi mwenyewe nimekwisha kuyafanya nilipokuwa nikiandika mistari hii, na yalikuwa uvumbuzi wa kuvutia, wa kutikisa moyo, wa kuangaza, wa kuweka huru na wa kuhamasisha sana.

Kiongozi wetu wa milimani awe Roho Mtakatifu, ambaye amejitolea kutuingiza katika kweli yote ya Mungu, kweli ya Biblia. Anajikita katika kumshuhudia yeye, Mkombozi Yesu Kristo, na kumfanya kuwa mkuu katika maisha yetu.

Matembezi ya kwanza ni marefu na yenye kuchosha kuliko yote, lakini wakati huo huo ndiyo muhimu kuliko yote. Mtu akishafika kilele hiki, kinachofuata hakitakuwa kigumu hivyo tena. Waraka ambao Paulo aliwaandikia Warumi unaonyesha haki ya Mungu, lakini pia neema ya Mungu katika Injili. Waraka huu utatushughulisha kwanza. Hakuna mahali pengine ambapo maswali haya ya msingi ya wokovu yanayotuhusu yanafanuliwa kwa namna hii. Hiyo ndiyo pia sababu tunataka hapa kujitaabisha kupanda mstari kwa mstari hadi kileleni.

2.13 Kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo

Hatuingii katika Waraka kwa Warumi mwanzoni, bali katika “behewa” la tano la “treni hii ya neema”. Hata hivyo tunataka kuonyesha kwa ufupi yaliyomo katika sura za kwanza: Baada ya utangulizi katika 1:1-17, Paulo anazungumzia katika 1:18-5:11 *matendo ya dhambi* ya wanadamu wote, ambayo kwa sababu yake wanasimama mbele za Mungu wakiwa na hatia (1:18-3:20). Kwa upande wa Mungu, mambo mawili halisi ya wokovu yanawekwa mbele ya hali hii isiyo na njia ya kutokea:

- ukombozi ambao Mungu anatupa bila malipo yoyote kwa njia ya damu ya Yesu Kristo iliyomwagika msalabani (3:21-31)
- nguvu ya Mungu ya kufufua, iliyomrudisha Kristo uzamani (4:1-25).

Sehemu ya pili ya waraka inaanzia 5:12 hadi 8:39. Hapa Paulo analishughulikia swali la kile ambacho Mungu anakitenda kuhusu hali yetu ya dhambi isiyoweza kurekebisha. Anazungumzia dhambi kama kanuni, kama nguvu kubwa iliyo ndani ya mwanadamu. Swali ni: Mwenye haki anawezaje *kuishi* kwa imani (1:17)?

2.14 Ni nini kilipaswa kutokea kwanza kwa ajili ya wokovu wetu?

Je, kama mwanadamu ameharibika hivyo, haipaswi kitu fulani kutokea ndani ya mwanadamu? “Huo usingekuwa mtazamo sahihi. Mtume Paulo ana jibu tofauti kabisa katika Waraka kwa Warumi: Kwanza kabisa haikupaswa kitu fulani kutokea *ndani* yetu; ilipaswa kitu fulani kutokea *nje* yetu, ndani ya Kristo. Pamoja na kazi ya Kristo kwa ajili ya *matendo yetu ya dhambi*, tunapaswa kwanza kuifikiria kazi ya Kristo kwa ajili ya *dhambi* yetu, kwa sababu hilo pia ni jambo halisi la wokovu. Baada ya hapo, hapo tu na si kabla, inafuata kazi ya Roho Mtakatifu *ndani* yetu. Kazi ya Kristo *kwa ajili* yetu inapaswa kutofautishwa wazi na kazi ya Roho Mtakatifu *ndani* yetu. Kazi ya kwanza ilitokea kabisa nje yetu, nayo imekamilika; hakuna kinachohitaji kuongezwa tena. Ya pili inatokea ndani yetu, nayo bado iko mbali sana na kumalizika; bado kuna mengi ya kuongezwa. Lakini inapaswa kuwa wazi kabisa kwamba kutatuliwa kwa tatizo la dhambi (nguvu ya dhambi, mzizi wa uovu) ni sehemu ya mambo halisi ya wokovu, sawasawa kabisa na kutatuliwa kwa tatizo la matendo ya dhambi. Kwa maneno mengine:

- Kuwekwa huru mbali na dhambi kunatokea kwanza kabisa nje yetu, na hivyo ni sehemu ya kuhesabiwa haki (taz. neno ‘amehesabiwa haki’⁹ katika 6:7); hii ni kazi ya Kristo, iliyokamilishwa mara moja tu kwa nyakati zote.
- Baada ya hapo kuwekwa huru kunachukua umbo ndani yetu, na hilo ni sehemu ya utakaso, utakaoishia katika kutukuzwa kwetu (8:30); hii ni kazi ya Roho Mtakatifu, inayokamilishwa hatua kwa hatua katika muda wa maisha yetu hapa duniani.”¹⁰

9. Taz. maelezo katika ER (tafsiri ya Biblia ya Kijerumani).

10. H. P. Medema, *Romeinen 7 enzovoorts*, uk. 44.

3. Warumi 5:12-21: Kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo

Wakristo wa Rumi walipokuwa wamemsikiliza msomaji kwa hamu hadi 5:11, waliweza – ingawa walikuwa wamekwisha kuja kuamini na hivyo kupata wokovu – kupumua tena kwa faraja. Inaonekana kana kwamba jambo hilo limetokea sasa hivi: Walikuwa na amani na Mungu, na katika kesi hii ya mahakama ya Mungu hawakupatikana na hatia, bali walitangazwa kuwa wenye haki na Mhukumu wa dunia yote. Mada ya makosa, na ukweli kwamba sasa wao si wenye dhambi tena bali ni wenye haki, inaonekana kwa kweli kuwa imefungwa na mstari wa 11. Je, basi, maswali yote kuhusu dhambi na haki ya Mungu yamejibiwa kikamilifu? Ni wazi kwamba hapana. Mambo yanaanza upya kwa nguvu. Kwa mara nyingine mtume anajenga hali ya kusubiri kwa hamu, kama ile iliyoonekana pia katika sura za kwanza za waraka huu.

Dhambi ilitoka wapi? Mauti yalitoka wapi? Kwa nini wanadamu wote wameathiriwa? Sheria ya Mungu ina nafasi gani? Na bila shaka swali hili: Je, kuna njia ya kutoka katika mzunguko huu wa kishetani wa dhambi, mauti na hukumu ya adhabu? Huenda baadhi yao walitazamana kwa mshangao, kwa sababu je, Paulo hakuwa ametoka tu kuwafanya wasikie kelele ya shangwe ya wokovu? Kwa nini sasa aanze tena na dhambi na mauti? Jibu ni: Mada hii bado haijashughulikiwa kikamilifu. Mtu akiendelea kusikiliza, haraka inakuwa wazi kile kinachozungumziwa sasa. Haizungumzii tena yale ambayo wanadamu wameyatenda, ambayo kwayo wamejionyesha kuwa wasio haki na wenye dhambi. Sasa badala yake ni swali hili: Kwa nini iko hivyo? Sasa mada ni *mwanadamu ni nini*, kwa nini anatenda dhambi, chanzo cha matendo ya dhambi ni nini. Sasa Paulo anachimba kuutafuta mzizi, baada ya kuyashughulikia matunda mabaya kwanza. Mwenye dhambi hapaswi tu kuhesabiwa haki, yaani kuachiliwa huru, mbali na matendo yake ya dhambi, bali pia kukombolewa kutoka katika nguvu ya dhambi. Aliingia chini ya utawala wake kwa sababu ya kuunganishwa kwake na Adamu, kwa njia ya mti wa ukoo wa uhai, kwa kusema hivyo. Hili ndilo tatizo lake, naye ameshikiliwa katika muunganiko huu; hawezi kujiweka huru mwenyewe. Hadi Kristo alipokuja, hapakuwa na nafasi yoyote ya kuukwepa muunganiko huu.

Maandiko haya yanaonyesha msiba wa anguko na matokeo yake. Wakati huo huo, kwa njia ya tofauti na ulinganisho wa watu wawili wakuu (yaani Adamu na Kristo), yanaonyesha pia jinsi Mungu alivyoifungua kwa upana njia ya kuingia uzimani.

Katika maandiko haya Paulo anaweka msingi wa sura ya 6, 7 na 8. Kwa kweli maandiko haya ni utangulizi na maandalizi. Anayesoma hapa kwa makini hatapata ugumu mwingi hivyo katika sura zinazofuata.

3.1 Mstari wa 12: Jinsi yote yalivyoanza

Kwa hiyo, kama vile kwa njia ya mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa njia ya dhambi mauti, na hivyo mauti yakawafikia watu wote, kwa sababu wote wamefanya dhambi ...

Mtu mmoja tu aliifungulia dhambi mlango. Si katika maisha *yake* tu, bali katika ulimwengu. Maana yake ni kwamba kila kitu kinachoishi katika ulimwengu huu kimeathiriwa vilevile: Wanadamu wote wanakufa kwa sababu wote wamefanya dhambi. Kwa njia hiyo mtu huyu aliyaingiza pia mauti na taabu zote zinazoambatana nayo. Kama cheche, tendo la kwanza, lililoonekana kuwa dogo tu, liliwasha moto mkubwa unaoenea, unaowaka kwa ukali zaidi leo kuliko wakati wowote.

Mtu huyu wa kusikitisha ni Adamu wa kihistoria, mwanadamu wa kwanza, kama inavyoonekana mara moja. Paulo alijua kwamba hatua ya kwanza ya kutotii haikutoka kwa Adamu, bali kwa Hawa (1 Timotheo 2:14), lakini Adamu alinyamaza na kushiriki. Alimfuata mkewe, ingawa *yeye* ndiye aliyekuwa amepewa amri kabla Hawa hajakuwepo. Kwa hiyo yeye ndiye aliyewajibika kwa yote yaliyotokea.

Mada ya Paulo ni tofauti kati ya watu wawili wakuu, yaani Adamu na Kristo, ambao “*nazao*” wao wote wameunganishwa nao.

3.1.1 Dhambi na matendo ya dhambi

Dhambi ilikuwepo tayari kabla ya Adamu, kwa sababu Shetani alitenda dhambi tangu mwanzo (1 Yohana 3:8). Alimjia mwanadamu wa kwanza ili kumdanganya. Mjaribu, yule nyoka wa zamani, hatajwi hapa. Mwanadamu alitenda akiwa na wajibu kamili yeye mwenyewe.

Neno “dhambi” hapa si tu umoja wa “matendo ya dhambi”. Hapa ni jambo kubwa zaidi sana. Kama inavyoonekana katika mahali hapa na katika maandiko yanayofuata, hapa tunazungumzia dhambi kama kanuni inayompinga Mungu, nguvu inayosimama dhidi ya Mungu na amri zake. Tunazungumzia dhambi kama ugonjwa unaohatarisha uhai na unaoishia kifoni, ambao umewashika wanadamu wote. Mtume Yohana anasema: “Dhambi ni uasi” (1 Yohana 3:4). Kwa hiyo dhambi inajumuisha kuikataa mamlaka ya Mungu (fujo isiyo na utawala), kwa namna yoyote ile, iwe inaonekana au haionekani.

Watchman Nee analinganisha matendo ya dhambi na dhambi kwa njia iliyo wazi sana na hali ifuatayo: Mtu akitaka kulitatua tatizo la pombe kabisa, haitoshi kuitafuta pombe yote na kuiharibu. Vyanzo vinavyoleta pombe mpya, yaani viwanda vinavyotengeneza pombe, vinapaswa kufungwa na kuharibiwa. Hivyo pombe yenyewe inawakilisha matendo ya dhambi, wakati viwanda vinawakilisha dhambi.

3.1.2 Dhambi na mauti

Adamu na Hawa walijua kwamba dhambi ingelea mauti (Mwanzo 2:17). Mungu mwenyewe alikuwa ametangaza mauti kuwa matokeo ya kula tunda lililokatazwa la mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Mauti yalianza wakati uleule walipoivunja amri hii. Mauti haya yaliukatiza mara moja uhusiano usio na usumbufu na wa kuaminiana ambao Muumba alikuwa nao na viumbe vyake.

Mauti hayamaanishi kufutika au kukoma kuwepo. Yanamaanisha kutengana, na kubadilika, yaani kuharibika, kwa hali ya awali. Agano Jipya linazungumzia mauti ya kiroho. Mauti hayo hayamaanishi kufutika kwa moyo au roho ya mwanadamu, bali kushindwa kwake kuwa na uhusiano na Mungu. Hapa Paulo anazungumzia kifo cha mwili kama matokeo ya dhambi.

Mauti ni matokeo ya dhambi (yanayokuja baadaye) yasiyoepukika wala kukwepeka. Mauti yamewafikia wanadamu wote; hayakuweza kuzuiwa. Hilo lingewezekana kama mtu mmoja asingetenda dhambi na hivyo kuthibitisha kwamba hana asili ya Adamu. Jambo hilo halijawahi kutokea miongoni mwa wanadamu; hakuna hata mmoja ambaye hadi sasa imethibitishwa kwamba hana dhambi. Wote wameathiriwa, na mapema au baadaye wote wanakufa.

3.1.3 Anguko na dhambi ya asili

Hii haimaanishi kwamba anguko la Adamu linajirudia kwa kila mtu, kwa kuwekwa kama Adamu, akiwa hana hatia, mbele ya uchaguzi wa kutii au kufanya kosa. Kama ingekuwa hivyo, kungekuwa na uwezekano kwamba labda mtu mmoja angeweza kufaulu kutotenda dhambi, na kwa hiyo pia asingepaswa kufa. Paulo anataka kusema kwamba kila mwanadamu ameirithi asili ya dhambi ya Adamu, na hivyo maisha yake yameathiriwa na dhambi. Mstari wa uzao haujawahi kukatika. Kuna ushahidi wa aina mbili wa jambo hili: kwanza mauti, na pia ukweli kwamba kila mwanadamu ametenda dhambi. Hali hii inatofautiana na hali ya Adamu kwa kuwa mwanadamu wa leo tayari amedhoofishwa kimaadili (ndiyo, ameharibiwa) na asili ya dhambi aliyoirithi kutoka kwa Adamu, na kwa hiyo anatenda dhambi. Neno la kitheolojia “*dhambi ya asili*”¹¹ linatokana na maandiko haya.

Kwa sababu ya kosa la Adamu, dhambi imekuwa mwandani wa kudumu wa kila mwanadamu, kwa kuwa kama kanuni inayompinga Mungu imemwambukiza mwanadamu katika uhai wake wote kama ugonjwa usioponyeka. Imemshika mwanadamu mzima – roho yake, nafsi yake, moyo wake, akili yake, nia yake na mwili wake. Mauti kama matokeo ya dhambi yameishika sehemu ya mwanadamu isiyoonekana – utu wake wa ndani – na kuleta mauti ya kiroho “katika ... makosa na dhambi” (Waefeso 2:1), na pia yameiathiri sehemu inayoonekana (mwili). Huo nao unatawaliwa na mauti: Mwili umekufa kwa sababu ya dhambi (8:10).

Historia ya kila mwanadamu haiwezi kutenganishwa na baba yake wa kwanza. Historia yake haiandikwi upya kwa kumpa nafasi ya kuthibitisha kwamba si lazima atende dhambi. Yeye ni mtoto wa Adamu pamoja na matokeo yote ya kusikitisha. Hakuna mtoto anayezaliwa anayechitaji kujifunza dhambi. Dhambi imewekwa ndani yake tangu kuzaliwa, na ni malezi tu yanayoweza kuzuia dhambi isilipuke kabisa.

Wengine wanaelewa mstari huu kana kwamba sisi tulitenda dhambi (pamoja naye) ndani ya Adamu, yaani katika kosa lake. Kama ingekuwa hivyo, tungewajibishwa kwa tendo ambalo hatukulitenda kabisa. Jambo lenyewe ni kwamba kwa tendo hili Adamu aliiruhusu dhambi iingie maisha yake, nasi kama

11. Kwa Kiingereza *original sin*.

wazao wake tumeirithi asili hii bila kuweza kuepuka. Sisi wenyewe hatuwezi kubadilisha chochote katika jambo hili.

3.1.4 Amri moja rahisi

Kosa lililoleta matokeo ya kutisha namna hiyo halikuwa tendo la dhambi la kuogofya, si mauaji wala unyang'anyi – hapana, lilikuwa kuvunja amri rahisi kabisa. Tendo halikuwi dhambi pale tu linapokuwa la kutisha sana. Kila tendo (tangu chanzo chake katika mawazo hadi kutendwa kwake) ni dhambi, mara tu linapoikataa mamlaka ya Mungu, ambayo hapa inaonekana katika amri moja rahisi, au hata kuisahau tu.

Katika sura hizi, dhambi karibu haitajwi kwa njia ya matendo ya dhambi, bali karibu daima inatajwa kama kanuni iliyo nyuma ya matendo yote ya dhambi.

Dhambi ni kanuni inayomfanya mwanadamu ayashike maisha yake mwenyewe mikononi mwake na kutoyajali mapenzi ya Mungu, au hata kuwepo kwake kabisa. Jambo hili halileti lazima matendo ya dhambi “ya kuchukiza”. Maisha ya mtu mwenye maadili ya juu asiyejali mapenzi ya Mungu yamejaa dhambi sawasawa kabisa na maisha ya muuaji au mzinzi. Dhambi hii ndiyo inayozungumziwa katika sura zinazofuata. Mbegu ya dhambi imechipuka ndani ya kila mwanadamu, hata kama haijakua kwa kiwango kilekile kwa wote.

Swali kubwa ambalo Paulo analielekea ni kile ambacho Mungu amekitenda kuhusu tatizo hili la dhambi. Kwa jambo hili msamaha au kupatanishwa na Mungu havitoshi. Mungu hasamehe kile *nilicho*, bali kile *nilichokitenda*. Tayari katika nusu ya kwanza ya sura hii ya 5 mtume anasema waziwazi kwamba “*tulikuma* wenye dhambi”, yaani sasa sisi si wenye dhambi tena. Ni nini hasa kilitokea ili kulileta jambo hili? Na Mungu atahakikishaje kwamba dhambi haitawali tena katika maisha ya muumini, kama ilivyo bado kwa wote ambao bado wako katika “*familia ya Adamu*”?

Mstari wa 12 unakatzwa na maneno marefu ya kuingizwa katikati; unaonekana kukoma katikati. Kwa kuwa tunayajua maandiko yote, hapa tunaukamilisha kwa maneno yetu wenyewe ili tuelewe vizuri zaidi, kama ilivyo katika mstari wa 18, ambapo mstari huu wa 12 unaendelezwa baada ya sentensi ya katikati:

*Kwa hiyo,
kama vile kwa njia ya mtu mmoja dhambi ilingia ulimwenguni,*

*na kwa njia ya dhambi mauti,
na hivyo mauti yakawafikia watu wote,
kwa sababu wote wamefanya dhambi ...
... hivyo hivyo kwa njia ya mtu mmoja na tendo lake la baki (Golgotha)
baki ililingia ulimwenguni,
na kwa njia ya baki uzima (wa milele),
na hivyo uzima ukawafikia watu wote.*

3.2 Mstari wa 13: Dhambi kabla ya kutolewa kwa sheria

*... kwa maana kabla ya sheria dhambi ilikuwako ulimwenguni;
lakini dhambi haibesabini
pasipokuwapo sheria.*

Hapa yanaanza maneno ya kuingizwa katikati, yanayomalizika katika mstari wa 17 tu. Paulo anasisitiza kwamba hakuna njia ya kutoka katika muunganiko na Adamu – haijalishi ni wakati gani katika historia ya wanadamu, iwe pamoja na sheria au bila sheria.

Historia ya wanadamu ilianza na Adamu, na vilevile historia ya dhambi na mauti katika ulimwengu wa wanadamu. Hadi kufika Torati, sheria ya Musa, huenda zilipita karibu miaka 2,500. Sheria inaifanya dhambi ishikike na kuonekana wazi, lakini dhambi ilikuwepo tayari hata wakati ambapo sheria hii ilikuwa bado haipo. Kwa njia hii Paulo anaunga mkono kauli yake kuu, kwamba ni Adamu ambaye kwa njia yake dhambi ililingia ulimwenguni na kubaki ndani yake. Wazao wake wote wamekuwa kile alichokuwa yeye: Walijionyesha kuwa wenye dhambi. Tangu Adamu dhambi ilitawala, hata kama haikuweza kutajwa kwa jina na kuonyeshwa kwa njia ya sheria. Jambo hili halithibitishwi tu na kifo cha wanadamu wote wa wakati huo, bali pia na matukio ya wakati huo. Gharika kubwa ya wakati wa Nuhu huenda ndiyo mfano ulio wazi kuliko yote. Tena, Paulo mwenyewe ameieleza katika sura za kwanza za waraka wake hali ya uharibifu usio na tumaini ya wazao wa Adamu kabla ya wakati wa sheria. Na kama mtu angekitumia baadaye kipimo cha sheria kwa wakati ule ambapo hapakuwa na sheria, basi, pamoja na ushuhuda wa dhamiri, ukweli huu ungeonekana wazi: kwamba hata wakati huo wanadamu walitenda dhambi kwa sababu walikuwa wenye dhambi.

3.3 Mstari wa 14: Adamu, mfano wake yeye atakayekuja

*Lakini mauti yalitawala tangu Adamu hadi Musa,
hata juu ya wale ambao hawakufanya dhambi
kwa mfano wa kosa la Adamu,
aliye mfano wake yeye atakayekuja.
(taz. Hosea 6:7)*

Utawala wa mauti, ambao hakuna mwanadamu anayeweza kuukwepa, ni hakika, nao unathibitisha utawala wa dhambi usio na huruma vilevile. Hii ni ishara nyingine kwamba hata bila amri mahususi dhambi ipo. Zaidi ya hayo: Maneno haya yanaonyesha bila shaka yoyote kwamba wanadamu wa wakati huo hawakuwa wenye dhambi kwa sababu walitenda dhambi (ingawa hilo pia ni kweli), bali kwa sababu walikuwa wazao wa Adamu. Hata bila kosa mahususi wanadamu walikufa, na hivyo inathibitika kwamba muunganiko na Adamu ndio tatizo.

Watoto wachanga, wasiotenda dhambi kwa kujua, wanakufa kwa sababu ni wazao wa Adamu.

Jambo linalosisitizwa kwa nguvu ni kwamba muunganiko na babu yetu wa kwanza Adamu hauwezi kukatwa kwa mwanadamu yeyote (awe na sheria au bila sheria). Wote wanazaliwa wakiwa wenye dhambi, kwa sababu babu yetu wa kwanza kabisa alianguka dhambini. Kwa hiyo sentensi ifuatayo ni muhimu sana: Sisi si wenye dhambi kwa sababu tunatenda dhambi. Bali tunatenda dhambi kwa sababu sisi ni wenye dhambi na tulizaliwa hivyo.

Dhambi haikuingia ulimwenguni tu; imefika hadi ndani ya mioyo yetu. Yesu anasema kwamba matendo mabaya hutoka moyoni, kutoka ndani, kutoka katika kiini cha utu wa ndani kabisa (Marko 7:21-23). Yanatokana na ukweli kwamba “tumekuwa wenye dhambi” (taz. Warumi 5:19; Luther 1912, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani).

3.3.1 Adamu na Kristo

Sasa Paulo anajadili ulinganisho wa kuvutia kati ya Adamu na “yeye atakayekuja”. Yule atakayekuja ni wazi kuwa ni Kristo – wakati ujao ni mali yake. Kwa hiyo Adamu ni “mfano” unaomwelekea Kristo. Mtu angeweza kuuita mfano wa kinyume, kwa sababu ingawa wanafanana katika upana na matokeo ya

matendo yao, matendo hayo yanapingana kabisa. Adamu wa kwanza anasimamia dhambi na mauti, Adamu *wa mwisho* (1 Wakorintho 15:45) uzima na haki. Kufanana kwa watu hawa wawili ni kwamba kila mmoja anaweza kuitwa kichwa, chanzo au baba wa familia ya wanadamu. Wote wawili ni wawakilishi wa wazao wao au wa jamii yao.

3.4 Mstari wa 15: Kwa njia ya Kristo hasara inarekebishwa, na zaidi ya hapo

*Lakini je, karama si kama lile kosa?
Kwa maana ikiwa kwa kosa la yule mmoja
wale wengi walikufa,
zaidi sana
neema ya Mungu
na kipawa katika neema,
kilicho kwa yule mtu mmoja, Yesu Kristo,
kimewazidia wale wengi kwa vingi.*

Paulo anaueleza mfano wa Adamu kwa njia ya tofauti zake na Kristo. Kosa la Adamu linawaletea mauti wale wengi ambao yeye ni baba yao wa kwanza. Lakini Mungu wa neema hakuliacha jambo hapo. Kwa kweli ni neema tupu inayoishughulikia familia hii ya Adamu. Haiwahusu tu wale walioingia katika hali yao ya kupotea, yenye alama ya mauti na dhambi, kwa sababu ya kosa la Adamu bila kosa lao wenyewe, bali pia wale ambao wao wenyewe wanaishi kwa kufuata kauli mbiu ya dhambi.

Neema ya Mungu inaleta kipawa, yaani mwanadamu mmoja, anayewekwa kinyume cha Adamu. Kipawa katika neema ni mtu ambaye kwa njia yake neema ya Mungu inabubujika kiasi kwamba mabwawa yote yanavunjika, na kila mwanadamu (haijalishi yuko wapi katika sayari hii) anaweza kufikiwa. Neema iliyo katika nafsi ya Mwana wa Mungu, Adamu wa mwisho, ina nguvu kuliko yote yaliyolingia ulimwenguni kwa njia ya Adamu wa kwanza. Walikuwa wengi waliokufa, na wanaweza kuwa wengi watakaoishi. Mungu hakuwaacha wanadamu wake mikononi mwa mauti!

3.5 Mstari wa 16: Matokeo ya kosa na matokeo ya karama

Wala si kama kwa (yule) mmoja

*aliyefanya dhambi,
ndiyo kilivyo kile kipawa?
Kwa maana hukumu ilitoka katika moja (kosa) hata ikaleta adhabu,
bali karama ilitoka katika makosa mengi hata ikaleta haki (kuhesabiwa haki, au
hukumu ya kuhesabiwa haki).*

Uamuzi wa Adamu wenye matokeo makubwa unaleta hukumu ya adhabu juu ya wote – huu ndio urithi aliouacha. Kuanzia mstari wa 15 Mungu ndiye anayezungumziwa, na kwa hiyo pia hukumu ya adhabu. Mungu anatekeleza hukumu yake ya haki na adhabu juu ya mwenye dhambi, na hilo haliwezi kumaanisha kitu kingine isipokuwa hukumu ya adhabu. Lakini karama iliyo katika mtu Yesu Kristo inaleta kuhesabiwa haki kwa mwenye dhambi, kinyume kabisa cha hukumu ya adhabu. Hukumu hiyo ilimpata yule aliyesimama badala yetu. Sasa si kosa la Adamu peke yake linaloshtakiwa, bali pia makosa mengi ya wazao wake wengi. Hata wakati wa sheria sasa umejumuishwa.

3.6 Mstari wa 17: Utawala wa mauti unakomeshwa na Kristo

*Kwa maana ikiwa kwa kosa la yule mmoja
mauti yalitawala kwa sababu ya yule mmoja,
zaidi sana wale,
wapokeao wingi (kipimo kinachozidi) wa neema
na wa kile kipawa cha haki,
watatawala katika uzima (yaani katika nguvu ya uzima)
kwa yule mmoja, Yesu Kristo.*

Neema ya Mungu inabubujika; inajionyesha kwa wingi usioweza kupimwa. Kwa njia hiyo wazao wa Adamu wanapokea haki ya Mungu kama kipawa. Kwa njia ya Yesu Kristo, Adamu wa mwisho, wananyakuliwa kutoka katika utawala wa mauti. Sasa mauti hayawatawali tena; hapana, wao wenyewe wanatawala katika nguvu ya uzima wa Bwana wao aliyefufuka, kama sura inayofuata itakavyoonyesha. Kwa njia ya Yesu Kristo wanakuwa washindi – tayari sasa, na hivi karibuni bila kikomo katika mwili mpya, watakapokuwa sawa na Yesu.

Hapa yanamalizika yale maneno ya kuingizwa katikati yaliyoanza katika mstari wa 13, ambamo Paulo alilishughulikia suala la pekee la kuwepo kwa dhambi ingawa sheria haikuwepo. Amezikanusha hoja zote kwamba huenda kuna watu wasiohusika, ambao yale aliyoyatenda Adamu hayakuwaathiri. Wanadamu wote

bila kuepuka wameunganishwa na Adamu na wako chini ya matokeo ya kosa lake.

Ni ukweli kwa kila mwanadamu kwamba muunganiko na Adamu upo. Hilo linamhusu pia yule anayeitwa “mtu mwema”, anayejulikana kwa matendo mema – Myahudi na vilevile mtu wa mataifa. Hawezi kujiondoa mwenyewe katika muunganiko huo. Anapaswa kuukubali ukweli huu. Lakini, kama maneno yanayofuata yanavyoonyesha, hahitaji kubaki bila tumaini: Mungu amefungua njia ya kutoka. Kwa neema ya Mungu hairudishiwi tu hali ya Adamu ya kutokuwa na hatia, bali kwa njia ya muunganiko mpya na Kristo, “baba yake mpya wa familia”, anapokea mengi zaidi sana kuliko yale ambayo Adamu aliwahi kuwa nayo.

Agizo la Adamu lilikuwa kuutawala uumbaji. Lakini sasa yeye na wazao wake wote walitawaliwa na dhambi na mauti. Lakini wale wanaopokea kipawa cha haki watatawala katika uzima. Utawala huu maana yake ni kwamba wanaweza kuishi kama Mungu anavyotaka – katika uhuru na kwa utukufu wa Mungu. “Kutawala katika uzima” ndicho kiini hasa cha utimilifu wa uzima tulio nao sasa ndani ya Kristo. Katika hali hii mpya tunaweza kuwa wanadamu wanaotimiza kusudi lao, yaani watu wa Mungu wanaoishi pamoja naye na kwa uzima utokao kwake. Hawatawaliwi tena na mauti na dhambi katika matokeo yao yote juu ya mwanadamu; wamewekwa huru kutoka katika utumwa, ili sasa wawe kile ambacho Mungu amewakusudia kuwa. Jambo hili Paulo atalifafanua zaidi kwa undani.

3.7 Mstari wa 18: Hukumu ya adhabu na kuhesabiwa haki kwenye uzima

*Basi tena,
kama kwa kosa moja
watu wote
walipata hukumu ya adhabu,
vivo hivyo na kwa haki moja
watu wote
walipata kuhesabiwa haki kwenye uzima.*

Kwa mara nyingine tena tendo la kusikitisha la Adamu, katika upana na matokeo yake kwa wanadamu wote, linawekwa kinyume cha tendo moja la yule mmoja mwenye haki. Hukumu ya adhabu ni hukumu ya haki ya Mungu juu ya

wanadamu wote waliowahi kuwepo na watakaokuwepo. Lakini haki ile *moja*, tendo lile *moja* la haki, linasimama kwa nguvu ileile. Linajumuisha kifo cha Kristo cha dhabihu, cha hiari na cha utii. Tendo hili moja lisilo na kifani, lililotokea mara moja tu, litawaathiri vilevile wanadamu wote bila kumwacha hata mmoja. Linaleta kuhesabiwa haki kwa mwenye dhambi. Jambo hili lilikwisha kuelezwa katika sehemu ya kwanza ya waraka. Sasa linaendelea zaidi. Sasa *kuhesabiwa haki kwenye uzima* kunaingia katika mtazamo. Uzima ulio na nguvu kuliko mauti sasa unaingia. Hapa hatuzungumzii tu kesi ya mahakama ambapo swali la hatia linapaswa kujibiwa, yaani kile nilichokitenda. Hapa tunazungumzia zaidi kwamba mimi kama mwanadamu, kama mwenye dhambi aliyehesabiwa haki, nina uzima mpya, ambapo kitu fulani ndani yangu kimebadilishwa. Kama mwanadamu nimepokea haki ya Mungu, kwa sababu nina uzima utokao kwa Mungu, uzima wa yule Aliyefufuka. Nimeachiliwa huru, yaani nimehesabiwa haki, mbali na matendo yangu ya dhambi. Lakini pia uhai wangu, hali yangu mpya ya kuwa ndani ya Kristo, ina muhuri wa haki ya Mungu. Hukumu ya adhabu ya Mungu inanipata kwa haki si tu kwa ajili ya kile nilichokitenda, bali pia kwa ajili ya kile nilicho. Lakini sasa niko ndani ya Kristo na nina uzima mpya. Maandiko haya ni msingi wa yale ambayo Paulo atayaeleza kwa kina zaidi baadaye.

Kuhesabiwa haki kunaleta kipawa cha uzima. Kuhesabiwa haki kunaongoza kwenye uzima wa milele. Katika muunganiko wangu na Kristo aliyefufuka niko katika nafasi mpya kabisa, ambayo sasa inaamuliwa kabisa na Mtoaji mpya wa uzima, na kichwa kipya: na Kristo. Katika hali hii, hali yangu yote ya kuwa imejumuishwa katika kuhesabiwa haki na Mungu.

3.8 Mstari wa 19: Nafasi ya kisheria ya wenye dhambi na nafasi ya wokovu ya wenye haki

*Kwa maana kama kwa kuasi kwa mtu yule mmoja
wengi waliwekwa katika nafasi ya wenye dhambi,
vivo hivyo kwa kutii kwake yule mmoja
wengi watawekwa katika nafasi ya wenye haki.*

Nafasi ya mwenye dhambi ni hali ya kusikitisha ambayo ameingia ndani yake kwa hukumu ya Mungu: Nimetenda dhambi kwa sababu mimi ni mzao wa Adamu; katika uhai wangu wote mimi ni mwenye dhambi, na ninapaswa kuchukuliwa hivyo.

Mtu Yesu Kristo, ambaye tofauti na Adamu alitii hata mauti ya msalaba, anaweza kutufungulia njia ya uzima. Tunda la utii wake linaniwezesha kuchukua nafasi imara na salama ya mwenye haki.

Huu ni ulinganisho wa kinadharia kati ya watu wawili wakuu: Adamu na Kristo. Hapa hatuzungumzii jinsi ninavyoishi kama Mkristo. Ninajua kwamba ninashika nafasi ya mwenye haki. Mwanzoni mwa sura ya 5 ninatoka katika chumba cha mahakama nikiwa nimeachiliwa huru, kwa kusema hivyo. Sasa maisha yanaendelea. Mimi sasa ni nini? Hapo kwanza ilihusu kile nilichokitenda; sasa inahusu kile nilicho.

Mungu ameniweka katika nafasi ya mwenye haki, na anaichukulia kwa uzito nafasi hii aliyoiumba yeye mwenyewe. Anashika hukumu yake mwenyewe; yeye ni mwaminifu.

Wanadamu wote wanazaliwa “kiotomatiki” katika nafasi ya wenye dhambi. Nafasi ya wenye haki iko wazi kwa wote. Lakini wanaipewa wale tu wanaoamini (“wengi”, kwa bahati mbaya si wote).

3.9 Mstari wa 20: Sheria inafichua dhambi zote

*Lakini sheria iliingia kando,
ili kosa lipate kuzidi.
Lakini dhambi ilipozidi,
neema ilizidi kuwa nyingi zaidi ...*

Sheria haikuweza kubadilisha chochote kuwa bora. Haikuiboresha hali ya mwanadamu; badala yake iliifanya kuwa mbaya zaidi, kwa sababu kwa njia ya sheria dhambi imezidi hata zaidi. Badala ya kuikandamiza dhambi na kuizuia, dhambi imejitokeza wazi zaidi.

Sheria ya Musa (kiini chake ni zile Amri Kumi) ilionyesha wazi jinsi dhambi ilivyotawala kwa nguvu. Lakini Mungu hakuyafunua mapenzi yake kwa njia ya sheria ili kwa hiyo aseme neno la mwisho na kumwacha mwanadamu aangamie katika gharika ya matendo yake ya dhambi yanayozidi. Alijibu kwa neema yake, isiyo na mipaka. Kwa hiyo ulinganisho wa watu hawa wawili wakuu si tu kuwaweka kinyume, bali ni uthibitisho kwamba Mungu ni mkuu zaidi, si kwa nguvu tu, bali pia kwa neema.

Sheria ilifunua kile kilichokuwepo tayari kabla. Wanadamu walitenda dhambi tangu Adamu. Kwa sheria sasa matendo ya dhambi yanatajwa kwa majina yao.

Sheria ilionyesha wazi jinsi matendo ya dhambi ambayo mwanadamu anayafanya yalivyo mengi. Kwa sheria hii kuna kipimo cha kiungu, kisichobadilika na kisichoweza kupotoshwa, cha kile kilicho chema na kilicho kiovu.

3.10 Mstari wa 21: Kutoka mautini hadi uzima wa milele

... ili kama vile dhambi ilivyotawala katika mauti

(katika nguvu ya mauti),

vivyo hivyo neema itawale

kwa njia ya haki hata uzima wa milele

kwa Yesu Kristo,

Bwana wetu.

Kwa wale walio ndani ya Kristo, utawala wa dhambi hadi mautini sasa ni jambo lililopita. Kwao neema inatawala. Lakini neema ina haki ya Mungu kama msingi wake. Si neema rahisi isiyu na gharama inayopuuza kila kitu tu. Hapana, mambo yanakwenda kwa haki. Haki ya Mungu ndio msingi bora kuliko yote; kuna uhakika kamili wa kisheria.

Neno hili limebana mambo mengi na lina utajiri mkubwa sana katika kueleza kile ambacho sasa kimetimizwa ndani ya “Adamu wa mwisho” (Kristo), hata ni vigumu kulielewa kikamilifu.

Mtu angeweza kusema kwamba sasa neema pia inatawala kama zamani mauti yalivyotawala – ikishinda vizuizi vyote na bila kuzuilika. Hatuwezi kuyakwepa matokeo yake, kama vile mwenye dhambi asivyoweza kuyakwepa mauti. Lakini utawala huu wa neema tunaukubali kwa furaha!

Kwa mara ya kwanza katika muktadha huu uzima wa milele unatajwa, na hapa kinachomaanishwa ni kuumiliki wakati ujao katika ufufuo wa uzima. Uzima wa milele unaahidi wakati ujao ndani ya Kristo usio na mwisho. Waraka kwa Warumi ni uthibitisho wa jinsi Mungu anavyotupigania, ili tusipotee, bali tuwe na uzima wa milele.

3.11 Mapitio ya jumla ya Warumi 5:12-21

	Mwakilishi na kichwa cha uumbaji wa zamani; mwanadamu wa <i>kwanza</i>	Mwakilishi na kichwa cha uumbaji mpya; mwanadamu wa <i>pili</i> na Adamu wa <i>mwisho</i>
Mfano unaomwelekea Kristo	Adamu	Yesu Kristo
Tendo	Kosa	(Tendo la) haki Kazi kamilifu ya ukombozi ya Yesu
Matokeo	Dhambi na mauti	Haki na uzima
Athari kwa wazao wote	Hukumu na hukumu ya adhabu	Neema na kuhesabiwa haki kwenye uzima
Nafasi mbele za Mungu	Wenye dhambi	Wenye haki
Dai la zamani na dai jipya la kiti cha enzi	Utawala wa dhambi hadi mautini	Utawala wa neema kwa njia ya haki hadi uzima wa milele

4. Warumi 6: Huru mbali na nguvu ya dhambi

Wanadamu wote wanaozaliwa ni “kwa asili” (Waefeso 2:3; Warumi 11:24), wakubali au wasikubali, wa ukoo wa Adamu, babu yao wa kwanza. Kwa hiyo bila kuepuka wameambukizwa dhambi. Uthibitisho wa jambo hili ni wazi: Wanakufa, hata bila kuvunja amri fulani mahususi. Lakini neema ya Mungu haizuiliki. Amemtuma ulimwenguni Adamu “mpya”, naye ndiye jibu la Mungu kwa kushindwa kwa Adamu wa kwanza na kwa wanadamu wote kwa jumla. “Adamu wa mwisho” ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu mwenyewe, ambaye tofauti na Adamu alitii maisha yake yote katika hali ngumu kupita kiasi, hadi kilele cha kujitoa mwenyewe kwa hiari kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi. Tendo hili la haki (5:18) linaufungua mlango wa kuuendea mti wa uzima, uliokuwa umefungwa kwa sababu ya dhambi ya Adamu. Mti huu wa uzima sasa ni Kristo mwenyewe, yaani kama yeye aliyekufa na kufufuka. Ndani yake sasa kunazuka kizazi cha watu wapya, wanaohamishwa kutoka kwa Adamu na kuingizwa ndani ya Kristo kwa kuingilia kati kwa Mungu (1 Wakorintho 1:30). Linatokea badiliko la wokovu, kubadili upande, kunakoukata muunganiko na Adamu na kuumba muunganiko mpya na Kristo. Ni kana kwamba wanakatwa kutoka katika mti wa Adamu, na sasa wameunganika na Kristo na kukua pamoja naye (6:5); sasa wako “ndani ya Kristo Yesu” (6:11). Wanapokea uzima wa Adamu wa mwisho (1 Wakorintho 15:45), na ni wa familia mpya ambayo kichwa chake, mwanzo wake na chanzo chake ni mtu Yesu Kristo. Yeye si Adamu wa pili, bali ni Adamu “*wamwisho*”: Kamwe hakutakuwa na msiba mpya wala anguko jipya litakaloweza kuiingiza dhambi katika uumbaji huu mpya.

4.1 Kubadili upande: Kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo

Sasa Paulo anaiendelezaje mada hii? Sehemu ya pili ya Warumi 5 ni aina ya maandalizi kwa sura tatu zinazofuata. Sasa jambo linalozungumziwa ni jinsi kuhama huku kutoka ukoo mmoja kwenda mwingine kunavyotokea. Badiliko hili kutoka mautini hadi uzimani linatimizwaje? Ni nini kinawatokea watu hawa? Jambo hili lina matokeo gani kwa maisha ya watu kama hao? Ni nini kinaipata dhambi? Je, kwa kuongoka na kuzaliwa mara ya pili waumini sasa wanakuwa bila

dhambi? Maswali haya na mengine kama hayo yamo nyuma ya maelezo ya Paulo katika sura ya 6.

4.2 Mistari ya 1-2: Je, neema ni ruhusa ya kutenda dhambi?

Basi tuseme nini?

*Tudumu katika dhambi,
ili neema izidi kuwa nyingi?*

Hasha!

*Sisi tulioifia (kwa upande wa) dhambi,
tutawezaje kuendelea kuishi katika dhambi?*

Ni wazi kwamba waumini (Paulo anasema na watu kama hao hapa) bado wanaweza kudumu katika dhambi, na kwa hiyo swali la kama muumini hana dhambi tena limekwisha kujibiwa. Wingi wa neema, ambayo kwa sababu ya kazi ya Kristo itazishinda daima dhambi na matokeo yake, ungeweza kueleweka vibaya kwa makusudi au bila makusudi. Mtu anaendelea kuishi kama siku zote, kana kwamba bado ni wa familia ya Adamu, ingawa tayari yuko ndani ya Kristo. Bila shaka yoyote huo ni hitimisho lisilo sahihi na ni kujipinga, ambako Paulo anakupinga kwa nguvu. Hata hivyo inaonekana mawazo kama hayo yalikuwepo (huenda yalikuwa hoja za wale waliotaka kuwarudisha Wakristo chini ya desturi za Kiyahudi, dhidi ya Injili ya Paulo), na kwa bahati mbaya baadhi ya Wakristo hata leo wanaishi kwa kufuata kauli mbiu hii. Paulo anasema kwamba hatuna uhusiano wowote na hitimisho hili. Kuna sababu ya lazima kwa jambo hili:

4.2.1 Tumeifia dhambi na nguvu yake!

Muumini hapaswi kuishi maisha yanayotawaliwa na dhambi. Sababu ni nini? Ameifia dhambi, na kwa mantiki jambo hilo linapaswa kuleta matokeo kwamba dhambi haiwezi tena kuyatawala maisha yake. Mfu haitikii chochote.

Tunapaswa kusoma kwa makini: Si dhambi iliyokufa, bali *sisi* ndio tuliokufa. Lakini sasa ninaona kwamba bado niko hai kabisa na mwenye nguvu. Kifo hiki kinaelezwaje?

Maelezo hayo bado hatuwezi kuyapata katika mstari huu; yanafuata katika mistari inayofuata. Hapa, kama utangulizi, kwanza kabisa ni ukweli huu wenyewe: Kwa upande wa dhambi, sisi tumekufa.

Bila shaka tunajua tayari kwamba kifo hiki ni kifo cha Yesu Kristo, lakini hebu tumfuate Paulo jinsi anavyolikuza wazo hili hatua kwa hatua. Hapa tayari dokezo hili ni muhimu: Kifo tulichokufa hakukomeshi kuwepo kwetu – wala kuwepo kwa roho au nafsi, wala kuwepo kwa mwili. Ni kifo “cha pekee”; kinahusu dhambi tu. Kwa upande wa dhambi, kwa kuhusiana na dhambi au katika uhusiano na dhambi, sisi tumekufa. Hapa ni kifo cha Yesu, aliyejitwika hukumu ya Mungu ya kifo juu ya dhambi. Aliifia dhambi (mstari wa 10), kwa sababu alijitoa kuwa dhabihu na kwa ajili yetu akafanywa kuwa dhambi.

4.3 Mistari ya 3-4: Tumebatizwa katika Kristo na katika mauti yake

Au hamjui

ya kwamba sisi sote tuliobatikwa katika Kristo Yesu

tulibatikwa katika mauti yake?

Basi tulizikwa pamoja naye

kwa njia ya ubatizo katika mauti,

ili,

kama Kristo alivyofufuliwa katika wafu

kwa utukufu wa Baba,

vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.

Huenda Wakristo wa Rumi walijiuliza jambo hili la “kuwa wamekufa” lilipaswa kueleweka namna gani. Kwa hiyo Paulo anawakumbusha ubatizo wao. Walikuwa wamebatizwa katika Kristo Yesu. Kwa tendo hili walikuwa (ili kuendeleza uzi mwekundu wa Warumi 5:12-21) wametimiza, kama ungamo la hadharani, kubadili upande kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo. Kwa ubatizo katika mto au ziwa waliwajulisha wote walioona kwamba walikuwa na Bwana mpya. Ingawa hapa maji hayatajwi, hapa tunazungumzia ubatizo wa maji. Ubatizo wenyewe hauhusiani na uhalisi wa ndani wa “kuwa wamekufa”. Ubatizo kama tendo la nje hauleti kifo changu, wala hauleti kuzaliwa kwangu mara ya pili. Kwa kusema hivyo, ni upande wa nje wa uhalisi uliokuja kwa njia ya imani na kuzaliwa mara

ya pili.¹² Ubatizo ni picha ya kile kilichonitokea kiroho, na hivyo kwa kweli, nilipounganishwa na Kristo.

4.3.1 Ubatizo katika mauti

Hatukubatzwa tu katika jina la Kristo Yesu, bali pia katika mauti yake. Ubatizo ni ungamo la kuyakubali mauti ya Kristo, au la kubatzwa katika mauti hayo. Kumgeukia Kristo kwa yule anayebatzwa kulitokea hasa kwa sababu ya ukweli kwamba Kristo alikufa badala yake. Ingawa tunayastaajabia maisha kamili ya Yesu na hakuna kitu kinachoweza kulinganishwa nayo, ni mauti yake yanayotuokoa, si maisha yake matakatifu.

Kwa hiyo katika ubatizo wa maji tunamkiri Yesu Kristo na mauti yake. Aidha, yote mawili ni upumbavu kwa ulimwengu.

“Mwelekeo wa ubatizo” ni nafsi ya Yesu Kristo *na* mauti yake. Mwelekeo wa ubatizo unaonyesha ni mtu gani ambaye mtu anajifunga kwake kwa njia ya ubatizo (kwa mfano, kubatzwa kwa Musa; 1 Wakorintho 10:2). Mtu humfuata yule ambaye amebatzwa kwake tangu siku ya ubatizo.

Maana ya mfano wa ubatizo ni wazi: Kinachoonyeshwa kwa picha katika tendo la ubatizo si tendo la kuua. Ubatizo si “kumzamisha mtu hadi afe”. Ubatizo kwa urahisi kabisa ni mazishi ya mfano, kwa kusema hivyo, katika kaburi la maji. Maana yake ni kwamba anayebatzwa (anayezamishwa) ni mfu. Utu wetu wa zamani umesulubiwa (yaani umeuawa) pamoja na Kristo. Kwa hiyo ninapokiri katika ubatizo mauti ya Kristo kuwa wokovu wangu binafsi kutoka katika hukumu ya Mungu ya kifo, jambo hilo linajumuisha kukubali kwangu hadharani kwamba nimestahili hukumu ya Mungu ya kifo. Kwa ubatizo ninakiri kwamba katika kifo cha Yesu kilichotokea badala yangu, hukumu ya kifo ilitekelezwa juu yangu. Utu wa zamani, niliokuwa hadi kuongoka kwangu na kuzaliwa kwangu mara ya pili, kwa mfano unapelekwa kaburini na kuzikwa katika ubatizo. Kwa hiyo ninakiri kwamba maisha yangu bila Kristo yalistahili

12. Huu si ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ubatizo huo unatokea kwa njia ya Kristo. Yeye ndiye anayebatiza, anayewapa waaminio Roho Mtakatifu na kwa njia hiyo kuwaongeza kwenye ule mwili mmoja, yaani kanisa, au kuwaunganisha ndani yake (1 Wakorintho 12:13). Ubatizo wa maji unafanywa na wanadamu: Wakristo, wanaoitwa wanafunzi, wanabatiza na hivyo kulitimiza agizo la Yesu la kwenda kuwafanya watu wanafunzi. Tena ubatizo wa Roho hautokei kwa kuingia mautini, bali ni zaidi ishara ya uzima. Ubatizo wa maji ni ushuhuda wa hadharani, tendo la nje; ubatizo wa Roho ni tukio lisiloonekana la ndani, linalotimizwa mara moja tu pamoja na kumpokea Roho Mtakatifu, nalo kwa maana ya Agano Jipya linahusu tu kuwa sehemu ya kanisa.

mauti tu, na wakati huo huo yamekomeshwa milele. Maisha haya katika ukoo na mti wa ukoo wa Adamu sasa yamekomeshwa.

Picha ya moto wa nyika inaliezea wazo hili: Ili nijilinde na moto kama huo unaoenea, ninaweza tu kukimbilia mahali ambapo moto umeshapita. Vivyo hivyo, kama mtu anayekiri, kwa ubatizo ninaingia mahali ambapo hukumu imeshatekelezwa, yaani katika mauti.

Kwa mara nyingine inasemwa kwamba mazishi haya yalikuwa ya kuingia mautini. Maana yake Paulo anaieleza mara moja, anapoeleza uhalisi wa imani. Tayari kabla ya ubatizo, kwa njia ya imani, kuna hali mpya ya mambo kwa mtu huyo – hata wakati ambapo bado hajabatizwa. Ubatizo unapaswa kushuhudia kile ambacho tayari ni uhalisi wa ndani, na kile kilichotokea tayari miaka 2,000 iliyopita.

Lakini ubatizo hauonyeshi tu kwa mfano jambo la kiroho. Kama ungamo, kwa nje unatimiza kuachana kwangu na ukoo wa Adamu (na hivyo kujitenga kwangu na ulimwengu). Anayebatizwa, kwa kusema hivyo, anajitenga na ulimwengu kwa tendo la ubatizo. Jambo hili haliumbi uhalisi wa ndani, kwa sababu ni tendo rasmi la nje tu. Ubatizo hauokoi kwa ajili ya mbinguni, lakini “unamwoko” mtu kutoka katika ulimwengu. Kwa ubatizo kunatimizwa kujitenga kwa nje kabisa na ulimwengu, jambo linalolingana na uhalisi wa ndani wa imani ya yule muumini anayebatizwa. Hiki ndicho Petro anachomaanisha anaposema kwamba tunaokolewa kwa njia ya ubatizo (Matendo 2:40; 1 Petro 3:21).

Kusisitiza kwamba ubatizo unajumuisha ungamo la uhalisi wa kiroho ni lazima kwa sababu ya ufahamu usio sahihi wa kikanisa kuhusu ubatizo, unaofanya kuwa “sakramenti” na hivyo kuleta wazo kwamba ni wa lazima kwa wokovu. Lakini Paulo hakulijua tatizo hili, lililotengenezwa baadaye katika Ukristo. Inaonekana kana kwamba kwake pande zote mbili (upande wa nje wa ungamo na upande wa ndani wa imani ya kweli) zilikuwa zimesukwa pamoja, zikionyesha kitu kinachotegemezana na hata kuwekeana masharti. Huenda Paulo asingeuelewa kabisa utenganisho huu wa mambo ya ndani na ya nje, tunaousisitiza kwa haki. Kwake hapakuwa na Wakristo wasiobatizwa (yaani watoto wa Mungu wasiobatizwa waliopewa kuzaliwa mara ya pili), wala hapakuwa na wasio Wakristo waliobatizwa.

Hakuna mtu ambaye angekubali kubatizwa kama ungamo la kuingia mautini lingekuwa ndilo jambo pekee, na mauti yangekuwa na neno la mwisho. Ingawa

ubatizo ni “mazishi”, wakati huo huo ni ishara ya tumaini, uthibitisho wa uzima mpya. Kwa upande mmoja ni kuikubali hukumu ya Mungu ya kifo juu yangu kama mwenye dhambi, lakini pia unathibitisha hatua ya kuingia katika uzima mpya kwa njia ya yule Aliyefufuka:

4.4 Mstari wa 4: Tumefufuliwa ili tuenende katika upya wa uzima

*... kama Kristo alivyofufuliwa katika wafu
kwa utukufu wa Baba,
hivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*

Ubatizo unazungumzia kwanza mauti, lakini kisha pia uzima. Baada ya “kuwa tumekufa” pamoja na Kristo kunafuata kuunganishwa kwetu pia katika ufufuo wake. Muunganiko wetu na Kristo unaonekana katika jambo hili: kwamba tumeunganishwa naye (“tumekua pamoja naye” katika Warumi 6:5 [taz. ER, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani]) katika kazi yake yote – katika kusulubiwa kwake, kuzikwa kwake na kufufuliwa kwake, na hata katika kupaa kwake mbinguni na kukikalia kiti cha enzi (Waefeso 2:1-10) – hata kama jambo hili la mwisho halizungumziwi hapa (taz. Waefeso 2).

Utukufu wa Baba (maneno ambayo yanapatikana hapa tu) ulipaswa kuujibu utii huu wa kujitoa mautini, mauti ambayo Kristo aliyakufa kwa ajili ya wengine na si kwa ajili yake mwenyewe. Bila shaka ulikuwa pia ukuu mtukufu wa Baba na nguvu yake vilivyomfufua. Lakini tafsiri hii ni sahihi zaidi. Ilihusu utukufu wa Baba. Kwa kusema hivyo, mbele ya kujitoa huku kikamilifu kusiko na kifani, utukufu huo ulikuwa “umebanwa” umfufue Mwanawe mpendwa. Katika historia ya wokovu, na hasa katika wokovu wenyewe, daima jambo kuu ni utukufu wa Mungu. Unapaswa kulindwa na kubaki bila kuguswa. Hapo tu ndipo kunaweza kuwa na wokovu wa milele na ulio salama.

Hatuufikii utukufu wa Mungu (Warumi 3:23); sisi kama wanadamu wa asili hatuwezi kwa njia yoyote kulingana na utukufu huu wa kiungu wala kukubaliana nao kamwe. Lakini Kristo aliweza. Alimtukuza Baba kwa kuyatenda mapenzi yake, kuitafuta heshima yake, na mwishowe kuitenda kazi ambayo Baba alikuwa amempa aitekeleze. Ulikuwa ni utukufu wa Baba uliomfufua, kwa sababu haukuweza kunyamaza wakati mauti yalipomtawala (6:9) na yule wa pekee, Mwana wa upendo wake, alipokuwa kaburini.

Ikiwa sasa tumeunganishwa naye namna hiyo, tuna sehemu pia katika ufufuo wake. Jambo hili linasemwa hapa (ingawa si kwa maneno hayo hasa, lakini kwa njia isiyo ya moja kwa moja). Maisha ya zamani ya utu wa zamani yanakomeshwa. Sasa tunaweza, katika nguvu ya ufufuo wake, kuwa na uzima mpya na kutenda ipasavyo katika maisha ya kila siku. “Upya wa uzima” maana yake ni maisha tofauti kabisa yakilinganishwa na yale ya awali. Tunaweza kuishi maisha tofauti na ya zamani, kwa sababu tumepewa uzima mpya. Unatofautiana na ule tuliokuwa nao tulipokuwa wa familia ya Adamu. Hivyo ndivyo Paulo alivyosema hapo kwanza (“watatawala katika uzima”; 5:17). Uzima mpya wa Adamu wa mwisho umetuinua juu ya mauti na juu ya dhambi; umetuweka huru ili tutumikie. Kumtumikia Mungu kama wale “wanaojitoa kwake” (taz. 6:13) maana yake ni kutawala katika uzima.

4.5 Mstari wa 5: Tumeunganika naye katika mauti yake na katika ufufuo wake

Kwa maana ikiwa tumeunganika naye (tumekua pamoja naye) katika mfano wa mauti yake,

kadhalika tutaunganika naye katika (mfano wa) kufufuka kwake ...

Njia ya kuyaendea maisha mapya yanayompendeza Mungu inapita tu katika mauti, yanayoyakomesha maisha ya zamani. Jambo hili linaweza kufanywa na Mungu mwenyewe tu. Si sisi tunaoyakomesha. Bali huu ni utendaji wa Mungu na tendo lake peke yake. Ni yule tu aliyekufa na kuzikwa anayeweza kufufuka ili aenende katika upya wa uzima. Hilo nalo ni tendo la Mungu, ninalohesabiwa kwa njia ya imani katika Kristo.

Paulo anathibitisha kwamba muunganiko wetu na Kristo haumaanishi kifo chetu tu, bali pia ufufuo wetu. Kwa upande mmoja historia ya utu wa zamani inafikishwa mwisho kulingana na mapenzi ya Mungu na asili yake takatifu na ya haki; yaani, madai ya haki ya utakatifu wake yanatimizwa katika hukumu. Ni hilo tu, na si kitu kingine, ndilo msingi unaolingana na Mungu wa kuanza upya. Muunganiko na Kristo ni wa karibu sana – ndiyo, kana kwamba tumekua pamoja naye. Hapa haimaanishwi mchakato unaotunganisha na Kristo kwa karibu zaidi hatua kwa hatua, bali tukio la mara moja tu lililokamilika. Halihusu ukuaji wa kiroho, ambao mimi nina ushawishi juu yake, bali “tendo la mwisho” ambalo Mungu analihakikisha. Lilitokea nje yangu na *kwa ajili yangu* (si ndani

yangu) miaka 2,000 iliyopita katika kifo cha kihistoria¹³ cha Yesu pale Golgotha.

Ufufuo wake ni ufufuo wetu. Paulo hauelewi ufufuo huu kuwa ufufuo wetu wa wakati ujao.¹⁴ Tumekufa kiroho – si kwa maana halisi ya neno, yaani kimwili. Kwa hiyo maana ya ufufuo inahusu pia uzima wetu mpya wa kiroho, tulioupokea ndani ya yule Aliyefufuka. Paulo anasema: “Tutaunganika naye (hakika, yaani bila shaka yoyote) pia katika kufufuka kwake.”¹⁵ Jambo hili linakubaliana kabisa na yale ambayo Paulo anawaambia Wakolosai: “... mkazikwa pamoja naye katika ubatizo, na ndani yake mkafufuliwa pamoja naye kwa njia ya imani katika nguvu ya Mungu itendayo kazi” (Wakolosai 2:12; ER, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani).

Upya wa uzima (mstari wa 4) si kitu kingine isipokuwa kuwa tumefufuliwa pamoja na Kristo. Sisi ni walio hai, tuliotoka katika wafu (taz. maneno yanayofuata muda mfupi baadaye katika mstari wa 13).

4.6 Mstari wa 6: Utu wa zamani umesulubiwa pamoja naye

... tukijua neno hili,

ya kuwa utu wetu wa zamani ulisulubiwa pamoja naye,

ili mwili wa dhambi ubatilike (usiwe na nguvu),

tusiitumikie dhambi tena (kama watumwa).

Katika sentensi hii sasa Paulo anafikia kiini cha jambo. Haya ndiyo maelezo ya kile alichokisema mwanzoni mwa sura: “Tumeifia dhambi.”

Utu wetu wa zamani ulihukumiwa na Mungu ndani ya Kristo pale msalabani; hukumu ya haki ya Mungu ya kifo ilitekelezwa. Yeye, Bwana wetu, alipokea hukumu hii ya Mungu badala yetu. Mungu aliufanyia utu wa zamani kesi pale msalabani. Utu wa zamani haukufa tu kwa sababu ya udhaifu wa uzee; hapa ni kesi ya kisheria dhidi ya kile ambacho utu wa zamani ulikuwa na ulichokitenda.

13. “Kihistoria” hapa maana yake ni kifo halisi cha Yesu msalabani, kilichoshuhudiwa katika historia.

14. Baadhi ya wafafanuzi wanadhani kwamba katika sura hii kufufuliwa, yaani ufufuo, kunahusu daima mwili. Kwa haki wanasisitiza kwamba utu wa zamani unazikwa na haufufuki tena. Lakini ubatizo unaniunganisha na Kristo aliyekufa, lakini pia aliyefufuka. Kwa makusudi kabisa ubatizo huu unafanywa katika maji. Kwamba anayebatizwa, baada ya kuzamishwa, anatoka tena majini, kunaonyesha kama ushuhuda: Anaingia katika uzima mpya chini ya uongozi wa yule Aliyefufuka.

15. Kwa kweli si waumini wote watakaopitia kifo cha mwili, kwa sababu baadhi yao, kabla hawajafa, watabadilishwa na kunyakuliwa. Hata hao watakuwa na sehemu tayari katika ufufuo unaotelezwa hapa (yaani ufufuo unaobadilisha maisha kwa maana ya kiroho).

Matokeo ya kesi hii yalikuwa kutekelezwa kwa hukumu ya kifo bila kulegeza chochote.

Hiki ndicho kiini kigumu cha maisha yetu ya Kikristo: kwamba hapa ni jambo tunalolipata kwa “kujua” au “kutambua”. Hapa kitu fulani kilitokea nje yangu, badala yangu. Nilikuwa na wakilishi wangu katika hukumu hii, yaani Kristo, aliyesimama mbele yangu, ili hukumu isinipate mimi, bali impate yeye. Kilichotokea pale ni jambo nisiloweza kulihisi wala kulionja. Kazi hii ya Yesu kwa ajili yangu ni halali kwa asilimia 100 – bila kujali hisia na mihemko yangu.

Lengo la tukio la Golgotha ni kuivunja nguvu ya dhambi inayomtawala mwanadamu, tena katika maisha ya kila muumini.

4.6.1 Utu wa zamani

Miongoni mwa Wakristo neno hili linatumika kwa namna mbalimbali, kwa mfano kama *asili ya zamani* ambayo bado iko hai ndani ya Mkristo. Katika muktadha wa Warumi 6 hili linaweza kumaanisha tu kwamba ni mwanadamu au aina ya wanadamu walio wa Adamu. Utu wa zamani (kwa Kiyunani *palaios anthropos*) ni mwanadamu kabla ya kuongoka kwake, kabla ya kuzaliwa kwake mara ya pili. Utu wa zamani hauwezi kufanywa kuwa sawa na “tabia ya mwili” (kwa Kiyunani *sarx*; SUV: ‘mwili’), au na asili ya zamani, yaani dhambi. Ni mwanadamu aliye katika ukoo wa Adamu, yaani aliye wa familia ya Adamu na anayeamuliwa na dhambi. Akiwa hivyo amepotea. Na mwanadamu huyu wa dhambi alifikia mwisho wake pale msalabani. Kwa hiyo jambo lifuatalo ni muhimu: Hatuubebi tena utu wa zamani. Lakini tabia ya mwili, asili yetu ya zamani, bado iko ndani yetu, muda wote tunaoishi katika maisha ya duniani ya mwili wetu.

Maneno “utu *wetu* wa zamani” yanalifanya jambo kuwa la binafsi sana kwa kila anayehusika. Ni maisha *yangu* ya zamani, yaliyonitawala kama mtu mwenye wajibu kabla ya kuongoka kwangu, na ambayo niliyaishi kwa namna hiyo.

“Utu wa zamani” unatajwa mahali pengine pawili, na Paulo peke yake ndiye anayeutaja. Huenda ni neno alilolibuni yeye mwenyewe. Halikuwepo – wala katika Agano la Kale wala katika ulimwengu wa mawazo wa Wayunani. Linapatikana kwa namna hii na kwa maana hii katika Agano Jipya peke yake. Mahali hapo (Waefeso 4:20-24; Wakolosai 3:9-10) inasemwa kwamba tumeuvua

utu wa zamani (kama vazi). Mahali pote hapo patatu panaeleza tendo lililokamilika, lililotokea mara moja.

Hata hivyo mistari hii inasisitiza vilevile kwamba tunapaswa pia kuuvua kwa vitendo mwenendo wa zamani wa maisha ya utu wa zamani. Baada ya kuuvua utu wa zamani mara moja kunafuata kufanywa upya kwa kudumu kwa “utu mpya”, ambao, kwa kusema hivyo, unazidi kuusukuma nje “utu wa zamani”.

Kuwepo kwa utu huu wa zamani kunamweleza mwanadamu anayetawaliwa na dhambi. Ameiacha dhambi iunde akili yake, nia yake na nafsi yake (kwa ufupi, kila kitu kinachomfanya mtu huyu kuwa alivyo). Jambo hili si lazima liwe lilijidhihirisha kwa matendo ya dhambi yanayoonekana wazi, bali lilijitokeza tu katika maisha ya kujiamulia mwenyewe, yaliyotengwa na Mungu, ambayo yangeweza hata kuwa na sura ya kidini.

Katika Warumi 6 Paulo, tofauti na Waraka kwa Waefeso na Waraka kwa Wakolosai, hasemi waziwazi kuhusu “utu mpya” ulioingia mahali pa ule wa zamani. Lakini anamaanisha jambo lilile anapozungumzia “upya wa uzima” unaotuunda sasa.

Kwa maneno mengine Paulo anasema jambo lilile hivi: “Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini si mimi tena ninayeishi, bali Kristo yu hai ndani yangu” (Wagalatia 2:19-20). Hapa utu wa zamani unalinganishwa na “mimi”, inayosimama badala ya nafsi ya Paulo. Ni “mimi wake wa zamani”, maisha yake ya zamani kabla ya kuongoka, utu wake wa zamani, ambao sasa umechukuliwa nafasi na mimi mpya, yaani na Kristo mwenyewe.

4.6.2 Kusulubiwa kwa utu wa zamani

Maisha yetu ya zamani yalijumuisha yale tuliyo yatenda na kile tulichokuwa (na kile kila mwanadamu asiye na Mungu alichu). Yangeweza kukomeshwa tu kwa njia ya kifo. Jambo hili lilitokea badala yetu na nje yetu miaka 2,000 iliyopita pale Golgotha, katika kifo cha Yesu kilichoshuhudiwa katika historia. Kwa ajili hiyo Yesu Kristo alijitoa kwa hiari. Hukumu ilimpata yeye. William Kelly anaeleza kwa usahihi kilichotokea: “Yeye aliyekuwa ameitimiza sheria na aliyekuwa mrithi wa ahadi alichagua laana badala ya taji; badala ya ufalme wa Mungu alijitwika hukumu ya Mungu. Kisha likatimizwa tendo la ajabu kuliko matendo yote: kumwagwa kwa yote ambayo Mungu aliyahisi juu ya dhambi na aliyoweza kuyaonyesha, juu ya kichwa cha yule asiyejua dhambi. Yote ambayo Mungu

angeweza kuyatenda katika ghadhabu takatifu dhidi ya uovu yalimjia yeye ambaye hakuwahi kutenda uovu wowote, ambaye kinywani mwake haikuonekana hila. Yeye, aliyekuwa Mwanawe mwenyewe, mlengwa wa furaha yake kamilifu, wa fadhili zake kamili na za milele, alitolewa katika hukumu isiyo na huruma. Mungu mwenyewe alimtendea kama ambavyo hakuwahi kumtendea mtu yeyote kabla, wala hatamtendea mtu mwingine yeyote tena.”¹⁶

4.6.3 Mwili wa dhambi

Matokeo ya kusulubiwa kwa utu wangu wa zamani ni kwamba mwili wa dhambi umebatilika (au bora zaidi: umekuwa *bila nguvu*). “Mwili wa dhambi” maana yake nini? Je, ni neno jingine tu, au upande mwingine wa maneno “utu wa zamani”, au ni tabia ya mwili yenye dhambi inayozungumziwa?

Mwili wa dhambi ni mwili wetu wa kawaida, jinsi ulivyojiachia kutumiwa pamoja na viungo vyake kuwa silaha za udhalimu. Utu wa zamani ulijieleza na kujidhihirisha kwa njia ya mwili. Mwili ulijiweka wenyewe katikati ya maisha ya zamani kwa njia ya misukumo na tamaa zake. Mwili ulijenga mazoea ya dhambi, ukayalazimisha, ukayafanya kuwa sheria ya maisha. Paulo anazitaja mahali pengine “sehemu za utu wa mwanadamu”, akiweka roho mbele na mwili nyuma. Mpangilio huu ulibadilishwa. Mwili umechukua nafasi ya kwanza kama sehemu inayoamua, kisha tu inafuata nafsi, na mwishowe roho, ambayo ndiyo ilipaswa kuutambulisha na kuuamua ubinadamu wenyewe (1 Wathesalonike 5:23).

Bila shaka mwili wenyewe si wa dhambi, lakini ulikuwa umetiishwa chini ya dhambi, na ulikuwa jukwaa lililokuwa tayari kwa ajili ya dhambi. Mwili ulijenga maisha yake wenyewe ya dhambi. Uko mbali kabisa na kutoegemea upande wowote. Paulo anaposema kwamba anautesa mwili wake na kuutumikisha (1 Wakorintho 9:27), kwa utu wa zamani ni kinyume chake. Mwili unamtia mwanadamu utumwani kwa njia ya tamaa zake. Kwa hiyo mwili ni mali ya dhambi; umekuwa *mwili wa dhambi*. Hiyo ndiyo hasa sababu kwa nini sasa tunapaswa kumtolea Mungu viungo vyetu (Warumi 6:13, 19). Ndiyo, hata tunaagizwa kuuweka wakfu mwili kuwa dhabihu iliyo hai (Warumi 12:1).

Mwili haukusulubiwa. Bali utu wa zamani ndio uliosulubiwa, ili tangu sasa mwili usiwe tena silaha ya dhambi. Mwili huu sasa (kuhusu ukweli kwamba

16. William Kelly, *Die Lehre des NT über den Heiligen Geist*, uk. 191.

ulilazimika kutenda dhambi) hauna nguvu – kama mtu aliyepooza asiyeweza tena kujisogeza kwa uhuru. Hivyo dhambi katika kujieleza kwake kwa uhuru imewekewa kituo cha mwisho na Mungu pale Golgotha; dhambi haipaswi kutawala tena katika mwili wetu unaokufa (mwili wa dhambi na wa mauti; 7:24; 8:10) (6:12). Kwa maana hii mwili wa kawaida si silaha ya dhambi tena, kwa sababu kuanzia sasa uko tayari kwa ajili ya Mungu na ya haki. Jambo hili linaelezwa kwa undani na kwa vitendo katika sehemu ya pili ya Warumi 6, kama matokeo ya kuwekwa huru mbali na dhambi. Mwili umemaliza kazi yake kwa upande wa dhambi. Jinsi hilo linavyotokea, Paulo anaeleza katika yanayofuata. Sisi – kama walio hai, tuliotoka katika wafu – sasa tunapaswa kumtolea Mungu kila kiungo cha mwili (6:11-13, 19). Na kwa upande wa dhambi, tunapaswa kujihesabu kuwa wafu kwa dhambi, na kwa msingi huo kuyafisha matendo ya mwili (8:13), jambo ambalo litakuwa mada yetu baadaye.

4.7 Mstari wa 7: Ameachiliwa huru mbali na dhambi

Kwa maana yeye aliyekufa

ameachiliwa huru (amehesabiwa haki, au amefunguliwa)

mbali na dhambi.

Hakuna tena – kwa mtazamo wa haki au wa kisheria – muunganiko wowote kati yangu na dhambi. Haiwezi tena kunibebesha kama hatia; siwezi tena kushtakiwa kwa sababu ya dhambi. Hata kama bado iko ndani yangu, ni “kitu kigeni kilichotengwa”, kisicho na uhusiano wowote nami na hali yangu mpya ya kuwa, ambamo nimeunganishwa na Kristo milele. Matokeo ya kifo chake kwa ajili yetu, na ya kifo chetu pamoja naye, ni makubwa namna hii. Kwa mfano jambo hili linatangazwa kwa njia ya ubatizo: Sasa tuko upande wa pili wa “kaburi la maji”.

Kauli hii inapaswa kutazamwa kwanza, ikiwa si peke yake, kwa mtazamo wa kisheria. Kauli hii haihusu utakaso wetu, kwa sababu katika jambo hilo hata sisi wenyewe mara nyingi tunapitia mambo yanayopingana, au tunawaona Wakristo wanaoishi maisha ya tabia ya mwili, yaani ya dhambi. Inahusu kuhesabiwa haki (kuachiliwa huru) mbali na dhambi. Kuachiliwa huru huku hakuanzi kutumika baada ya kifo cha mwili tu, bali kwa kweli kunaeleza hali mpya ya kisheria ya muumini. “Dhambi haina tena haki ya kisheria ya kulazimisha utawala wake na

kumdhhibiti muumini, kwa sababu amekufa pamoja na Kristo.”¹⁷

Ni muhimu kabisa tusitafute hapa bado maelezo ya mwisho ya jinsi tunavyoweza kuishi maisha ya ushindi ya Kikristo. Hata kama mstari huu ni sababu ya kwamba hatuitumikii tena dhambi kama watumwa (mstari wa 6), Paulo bado hajafika mwisho wa mafundisho yake kuhusu kile ambacho mwanadamu alikuwa ndani ya Adamu, na kile kilichopaswa kutokea ili kutuhamisha kutoka huko na kutuingiza ndani ya Kristo. Kuhusu maisha ya ushindi ya Kikristo anazungumza katika sura ya 8, baada ya kuifafanua mada hii kikamilifu. Baadaye anazungumzia nguvu ya kuishi kwa njia ya Roho Mtakatifu na kile kinachotokea ndani yetu. Kwa maneno mengine, tukifika hapa, ni lazima kabisa tuendelee na matembezi yetu milimani. Kama kuhusu maisha ya ushindi kila kitu kingekuwa kimekwisha kuelezwa hapa, basi sura ya 7 na ya 8 zisingehitajika.

Kwamba hapa ni hali ya kisheria iliyombwa nje yangu miaka 2,000 iliyopita, inaonekana wazi kwa kuwa katika maisha yangu ya kila siku bado dhambi inatokea. *Kisheria* maana yake ni kwamba siwezi tena kushtakiwa kwa sababu ya dhambi, na kwamba haina tena haki ya kunitawala. Na ikiwa hiyo ndiyo hali yangu ya kisheria, basi hiyo ndiyo nafasi ya wenye haki (5:19), ambayo Mungu ameniweka ndani yake, na ambayo kwake ndiyo nafasi pekee halali ninayoishika. Hakuna tena nafasi nyingine – mimi si mwenye haki katika wakati mmoja na mwenye dhambi katika wakati mwingine, au yote mawili kwa wakati mmoja. Jambo hilo linajipinga lenyewe, na zaidi ya yote linaupinga wokovu mkuu wa Mungu.

Ili kulifanya wazi, mlinganisho tuliokwisha kuutumia unasaidia. Tarehe 18 Desemba 1865 sheria ya kukomesha utumwa ilianza kutumika Marekani. Ilimhusu kila mtumwa. Kisheria watumwa wote walikuwa huru tangu siku hiyo, hata kama hawakuwepo wakati sheria hii ilipotiwa sahihi. Jambo hili lilitokea bila mchango wao na mahali pengine, lakini hata hivyo lilikuwa halali kikamilifu. Sasa walipaswa tu kuisikia, kuidai kwa ajili yao wenyewe na kuwaacha mabwana zao.

4.8 Mistari ya 8-9: Kushiriki mauti na uzima pamoja na Kristo

Lakini ikiwa tumekufa pamoja na Kristo,

17. John A. Witmer, *The Bible Knowledge Bible Commentary*, Walvoord & Zuck (wahariri), uk. 463, Victor Books, 1988.

*twaamini,
ya kuwa tutaishi pamoja naye pia,
kwa kuwa twajua,
ya kuwa Kristo, akiisha kufufuliwa katika wafu,
hafi tena;
mauti haimtawali tena.*

Kwa mara ya pili Paulo anatoa hitimisho kutokana na ukweli kwamba tumeunganishwa na Kristo. Katika mstari wa 4, matokeo ya kufufuliwa kwa Yesu yalikuwa kwamba sisi, kama “waliofufuliwa pamoja naye”, tunaenenda katika upya wa uzima. Katika mstari wa 5 Paulo anathibitisha maana ya ufufuo wa Yesu kwa ajili yetu, si tu kwa kutazama wakati ujao, bali kwa kutazama maisha yetu hapa na sasa. Katika mstari wa 8 tena inahusu ufufuo, lakini sasa ni ufufuo wa wakati ujao, ufufuo wa mwili. Kwa kuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu, mwanadamu Yesu Kristo hawezi kufa tena; uzima wake wa ufufuo hauwezi kuvunjika. Tukiwa tumeunganishwa naye, tuna uzima uleule. Katika Adamu tulirithi mauti, katika Kristo uzima. Eneo, au ufalme, wa mauti (ule ulimwengu ambamo watu bado wako “katika Adamu”) tumeweza kuuacha kwa njia ya kifo na ufufuo wa Yesu.

Mauti ilimtawala Yesu alipokuwa kaburini. Hili ni tamko la ajabu kweli. Yesu alijinyenyekeza hata mauti ya msalaba, akakubali kufa kwa hiari yake; hata ilimbidi kuutoa uzima wenyewe mautini. Kisha, kwa muda mfupi, mauti ilikuwa mshindi juu yake. Lakini utukufu wa Baba haukuweza kufanya vinginevyo ila kumfufua Yeye aliye wa pekee na mkamilifu kwa uzima mpya.

Yaliyo kweli kwa Kristo yanatuhusu sisi pia. Utawala wa mauti umevunjwa, hata kama, kama mistari michache baadaye inavyosema, tuna miili inayokufa. Kwa hiyo katika ushindi juu ya mauti umo pia ufufuo wetu, siku ile miili iliyokufa na kuoza itakaponyakuliwa kutoka katika utawala wa mauti.

4.9 Mstari wa 10: Kristo aliifia dhambi

*Kwa maana kwa kule kufa alikokufa,
aliifia dhambi mara moja tu;
lakini kwa kule kuishi anakoishi,
anamwishia Mungu.*

Tukitaka kuelewa maana yake kwetu kwamba tumeifia dhambi, basi lazima tuelewe maana yake kwa Kristo kwamba aliifia dhambi. Alikufa kama dhabihu kwa ajili ya dhambi, kwa kuvumilia hukumu ya adhabu juu ya utu wetu wa zamani.

Hivyo kwa kifo chake alilitatua tatizo la dhambi: kwa upande mmoja alilipa hatia ya dhambi, lakini wakati huohuo aliivunja nguvu ya dhambi na kuiacha nyuma. Uzima mpya wa ufufuo hauko tena chini ya nguvu ya dhambi na ya mauti; bali ni uzima unaoongozwa na Mungu, tunaouishi kwa ajili ya Mungu, na uliowekwa wakfu kwake yeye peke yake.

Hakuna haja tena ya kulitatua tatizo la dhambi mara ya pili. Dhabihu ya pili kwa ajili ya dhambi haihitajiki tena, kama Waraka kwa Waebrania unavyothibitisha waziwazi.

“Tkiwa mshahara wa dhambi ni mauti, ni faida kubwa kiasi gani kwetu kifo cha yule ambaye yeye mwenyewe hakuwa na dhambi, ambaye Mungu alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye.

Si kwamba msalabani hakuwa mtakatifu kama alivyokuwa katika yote yaliyotangulia; lakini alijitoa mwenyewe ili ahukumiwe kwa haki kwa ajili ya yote aliyobebeshwa, ambayo kwa neema aliyachukua kuwa jukumu lake. Hakujihurumia katika jambo lolote; katika jambo lolote Mungu hakumhurumia, yeye aliyemwacha yule aliyejitambulisha na dhambi yetu na matokeo yake yote chini ya hukumu ya Mungu, ili sisi tupate kutoka huru.”¹⁸

Upekee huu wa dhabihu hii, na nafasi iliyo wazi inayotokana nayo, yaani kubadili upande kulikokwisha kufanyika, vinatuhusu sisi pia. Na huu ni ukweli ambao tunaweza na tunapaswa kuwa na uhakika nao milele. Kuutambua na kuupokea ukweli huu ndiko kunakoamua uhuru wetu, ambao ndani yake tunaruhusiwa kumtumikia Mungu.

4.10 Mstari wa 11: Kujihesabu kuwa wafu kwa dhambi, bali walio hai kwa Mungu

*Vivyo hivyo ninyi nanyi,
jihesabuni
kuwa wafu kwa dhambi,
bali walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu.*

18. William Kelly, *Notes on the Epistle to the Romans*, uk. 88.

Tunausimamia vipi ukweli ambao Paulo ameufafanua sasa hivi? Tunapaswa kuupokea kama jambo halisi, linaloaminika na lililo halali kwetu. “Kujihesabu” kunamaanisha pia kujiona kuwa ndivyo tulivyo. Hili ni neno la uhasibu: Mizania imesimama na imefungwa. Matokeo yake ni kwamba kazi ya Kristo imeingizwa kwenye akaunti yangu binafsi kwa asilimia mia moja. Kifo chake ni kifo changu, uzima wake ni uzima wangu.

Mstari huu *sí*, kama inavyosemwa mara nyingi, ufunguo wa vita dhidi ya dhambi. Jaribu la dhambi linaponijia, siwezi kujiambia kila wakati kwamba nimekufa. Ninatambua wazi kwamba sijafa hata kidogo; la sivyo nisingeitikia jaribu hata kidogo. Kile kinachopaswa kufanywa wakati wa jaribu, Paulo anakieleza katika sura ya 8.

Kwa hiyo hapa inahusu kwanza kuipokea kwa kuamini kazi ya wokovu ambayo Mungu amenitendea, si kuutekeleza ukweli huo kila siku. Sihitaji kuutekeleza, kwa sababu umekwisha kutendeka. Paulo hasemi kwamba tunapaswa kuifia dhambi kila siku, au kujifanya wafu jaribu linapokuja. Bali anaeleza kwamba *tumekwisha* kufa. Jambo hili lina matokeo katika maisha yangu, kwa sababu kwa hilo nguvu ya dhambi juu ya maisha yangu imevunjwa.

Anayejihesabu kuwa mfu kwa dhambi anaamini na kupokea kwamba maisha yake ya zamani yalikomeshwa msalabani, na kwamba kwa hiyo utawala wa dhambi katika maisha yake imevunjwa. Juu ya msingi huu wa wokovu, kwa imani ileile, ninalishika jambo halisi la wokovu kwamba sasa nina uzima mpya, ambao kwa huo nimewekwa huru, nami ninaweza kumwishia Mungu. Watchman Nee anasema kwa usahihi: “Kujua – kujihesabu – kujitoa: huo ndio mpangilio kwa kufuata utaratibu wa Mungu.”¹⁹

4.11 Mstari wa 12: Utawala wa dhambi juu ya mwili unavunjwa

*Basi, dhambi isitawale
katika mwili wenu unaokufa,
hata mkazitii tamaa zake.*

Haya ndiyo matokeo ya yale yaliyotokea msalabani. Hili ndilo lengo la Golgotha: Udikteta wa dhambi imevunjwa, iwe ni udanganyifu wake ambao karibu hauonekani, au utumiaji wake wa nguvu wa kikatili kabisa. Kazi ya Yesu ina nguvu ya kuivunja nguvu halisi ya dhambi katika maisha yangu. Kazi hii ndiyo

19. Watchman Nee, *Das normale Christenleben* (Maisha ya Kawaida ya Mkristo), uk. 58.

tunayoitegemea na kuisimamia. Hiyo ndiyo maana ya kujihesabu kuwa wafu kwa dhambi!

Mwili wetu unaokufa (sawa na sehemu isiyo ya kimwili ya mwanadamu, yaani utu wa ndani) uko chini ya matokeo ya dhambi. Mwili ndio chombo ambacho kwa njia yake dhambi inapata mikono na miguu. Dhambi yenyewe bado iko ndani yangu (yaani katika tabia yangu ya mwili; taz. 7:18), lakini haina tena haki ya kunitawala (6:6b, 14). Mwili umeathiriwa na dhambi kiasi kwamba unashawishiwa na dhambi, na tamaa na anasa, zinazodai kutoshelezwa kila wakati.

Paulo anasisitiza upande wa kisheria wa wokovu, ulio halali siku zote na kwa kila muumini. Lakini jambo hili halibaki kuwa nadharia tupu au jambo lisilo halisi. Upande wa kisheria wa wokovu ndio msingi ambao juu yake maisha yangu ya kila siku hayatawaliwi tena na dhambi.

4.12 Mstari wa 13: Kujitoa sasa kwa Mungu

*Wala msiendelee kuitolea dhambi viungo vyenu
kuwa silaba za dhuluma;
bali jitoeni wenyewe kwa Mungu,
kama walio hai baada ya kufa,
na viungo vyenu kuwa silaba za haki kwa Mungu.*

Sasa tunaagizwa kufanya jambo fulani. Hadi hapa hapakuwa na agizo lolote isipokuwa lile la kuipokea kazi ya Mungu na kuitegemea (6:11). Kutokana na hilo sasa linafuata tendo lenyewe. Kuvitoa viungo vya mwili maana yake ni kujitoa kuwa tayari kutumika. Mikono yangu na miguu yangu, macho yangu na masikio yangu, na kinywa changu (kwa ufupi, kuwepo kwangu kote kama mwanadamu pamoja na hisia zangu zote na uwezo wangu wote) sasa vinapaswa kutimiza kusudi lake. “Kuwa kile tulicho”²⁰ – hili si jambo linalojipinga, bali ni siri na pia mvutano wa maisha ya ushindi. Sisi ni walio hai baada ya kufa, kwa sababu katika Kristo Yesu tuna uzima wa Yeye aliyefufuka. Uzima huu wa Mshindi umewekwa wakfu kwa Mungu, si kwa dhuluma tena.

4.13 Mstari wa 14: Si chini ya sheria, bali chini ya neema

Kwa maana dhambi baitawatawala ninyi,

20. F. Godet.

*kwa sababu hamwi chini ya sheria,
bali chini ya neema.*

Ni ukweli kwamba dhambi haitutawali tena. Hali hiyo ni ya zamani. Tunatazama mbele, tunaingia katika uzima. Uzima huu hauongozwi na sheria ya Mungu, hata kama jambo hili linasikika kuwa la ajabu. Sheria, kama Paulo alivyokwisha kueleza, ilikuwa chombo ambacho kwa njia yake dhambi ilizidi sana. Lakini sasa maisha yetu yanaongozwa na neema ya Mungu. Sheria inadai kwa haki, lakini haitoi nguvu ya kutii. Neema tunayosimama ndani yake inatupa yale tunayohitaji ili tumwishie Mungu. Ni mazingira ya maisha yaliyo tofauti kabisa. Neema ya Mungu inatoa kwa wingi; sheria inadai. Mkristo anayefanya urafiki na sheria atapata yale yaliyoelezwa katika Warumi 7: kushindwa na kukata tamaa. Tulihihitaji neema ya Mungu kwa ajili ya wokovu, na vivyo hivyo tunaihitaji neema ya Mungu kwa ajili ya maisha. Tunaishi chini ya ulinzi, katika kukubaliwa, na katika nguvu ya neema ya Mungu. Kuwa chini ya neema ni sawa na ukweli wa kuwa “katika Kristo”, kama unavyozungumzwa katika sura ya 8.

“Tkiwa siko tena chini ya sheria, bali chini ya neema, basi hatimaye ninaweza kufanya na kuacha – kile ambacho Kristo anataka!”²¹

Hapa Paulo anaigusa sheria kwa ufupi tu, lakini katika sentensi hii moja anasema jambo lililo la maana kuliko yote juu yake, na analifafanua zaidi katika sura ya 7. Huenda wasikilizaji au wasomaji wa sura hii walifikiri moja kwa moja kwamba sheria ndiyo njia inayofaa ya kuuvunja utawala wa dhambi.

4.14 Muhtasari

Kubadili upande kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo kunatimizwa kwa njia ya msalaba. Maisha yangu ya zamani, yaani utu wangu wa zamani, yanahukumiwa na kuadhibiwa kama Mungu anavyotaka. Yesu Kristo amelichukua jambo hilo mahali pangu. Ndani yake sasa yanaanza maisha yangu mapya. Dai ambalo dhambi ilikuwa nalo juu ya maisha yangu limefutwa msalabani, na nguvu yake juu yangu ilivunjwa pale.

Katika maandiko haya, hadi hapa, haihusu kwanza kiasi gani sasa tunaishi maisha matakatifu au yasiyo na dhambi. Muumini bado ana dhambi inayobaki ndani yake, maadamu yuko katika mwili huu. Kwa bahati mbaya, maisha ya Mkristo yanaweza kutawaliwa na tabia ya mwili yenye dhambi, kinyume kabisa

21. Hans-Joachim Eckstein.

na yale ambayo Paulo anaandika hapa. Lakini hilo silo linalozungumzwa hapa (katika Warumi 6:1-14)! Paulo anaeleza badiliko kubwa na la msingi kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo, kutoka dhambini hadi hakini, kutoka mautini hadi uzimani.

Wakristo waliosahau jambo hili, au wanaojaribu wao wenyewe kujihesabu kuwa wafu kwa dhambi au kuifia dhambi polepole, wanapaswa kuyashika maandiko haya kwa ajili yao wenyewe kama yalivyoandikwa, katika ukamilifu wake wote.

Kwa Wakristo wanaoipenda dhambi, maelezo ya nafasi yao halisi, ile waliyo nayo katika Kristo, yanataka kuwaonyesha wazi kwamba wanaishi katika mgongano mkubwa. Ni jambo la kushangaza kuishi katika dhambi, ingawa mtu ameifia dhambi.

Kifo ambacho tumekufa – pamoja na Kristo – hakimaanishi kwamba tumefutiliwa mbali. Kwa maana ya Biblia, mauti (ya kiroho na ya kimwili pia) inamaanisha kutenganishwa kwa mambo yanayopaswa kuwa pamoja. Kwa kifo cha utu wa zamani, dhambi imetenganishwa nami na uhusiano umekatwa, hivyo kwamba nguvu ya dhambi imevunjwa.

4.15 Msalaba wa Golgotha na dhambi

Imefanyika kwa ajili yetu!

Warumi 1:1-5:11: Upatanisho kwa ajili ya dhambi	Warumi 5:12-8:13: Kuwekwa huru
Tatizo la matendo ya dhambi	Tatizo la dhambi
Matendo ya dhambi na swali la hatia	Dhambi kama chanzo cha matendo ya dhambi
Kwa damu ya Yesu Kristo iliyomwagika msalabani tuna msamaha wa dhambi.	Tumesulubiwa pamoja na Kristo. Utu wetu wa zamani ulitolewa kwa mauti.
Kristo alikufa kwa ajili ya matendo yetu ya dhambi.	Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi na asili yetu yenye dhambi, iliyoukawala utu wetu wa zamani kwa asili.

4.16 Warumi 6:15-23: Waliowekwa huru wanaoishi chini ya neema

Katika sehemu ya pili ya sura hii Paulo anasisitiza (akihitimisha kutokana na yale aliyoeleza katika sehemu ya kwanza juu ya kazi ya Mungu ya wokovu) kwamba mtu anaweza kumtumikia bwana mmoja tu, si mabwana wawili kwa wakati mmoja.

4.17 Ukweli wa wokovu na agizo la wokovu

Kile kinachoonekana kuwa kigumu kusoma kwa kweli ni namna ya kusema inayosaidia. Inahusu pande mbili za sarafu moja. “Indikativ” na “Imperativ” (kauli ya kueleza na kauli ya kuagiza) ni maneno mawili yanayotoka katika sarufi. Wanatheolojia huyatumia pamoja na neno “wokovu” ili kueleza kwa ufupi “pande mbili au mitazamo miwili ya wokovu” ni nini. Ukweli wa wokovu (yale ambayo Mungu ameshatenda; kwa Kijerumani *Heilsindikativ*) unaonyesha kile ambacho Kristo ametutendea, yaani uhalisi wa wokovu ulio nje yetu na usiotegemea hisia zetu. Upande huu unahusu wokovu usioweza kuguswa, ambao Mungu amempa kila muumini kweli kweli, nao ni halali.

Kutokana na wokovu yanatokea maisha yaliyobadilika na mapya. Wokovu unatulazimu kuishi na kuenenda katika upya. Hili ndilo agizo la wokovu (yale tunayoagizwa kutenda kwa sababu hiyo; *Heilsimperativ*), wito wa Mungu wa kuishi maisha matakatifu. Neema tuliyoipokea katika wokovu inatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia, na kuishi kwa haki na kwa utauwa (taz. Tito 2:12). Mtu hapokei wokovu bila kupokea pia wajibu wa kimaadili wa wokovu wa Mungu. Asiyelichukulia agizo la wokovu kwa uzito anapaswa kujichunguza kama ana haki ya kudai wokovu kuwa wake.

Ukweli wa wokovu unahusu tukio lililotokea kweli, na kwa hiyo unaeleza uhalisi wa wokovu. Agizo la wokovu ni amri na pia faraja ya kuishi maisha matakatifu. Yote mawili ni sehemu ya wokovu. Hata katika Warumi 6 pande hizi mbili zinaonekana wazi. Mistari ya 1 hadi 10 inaeleza ukweli wa wokovu, na kuanzia mstari wa 11 agizo la wokovu linazungumzwa.

Agizo la wokovu halituagizi kuustahili wokovu, bali kuishi kutokana na wokovu tuliokwisha kuupokea. Uwanja wake wa kujaribiwa uko chini ya utawala wa neema, ambako kuna msamaha na kurejeshwa kwa ukarimu. Wokovu haukutolewa ili kuwachagua wenye nguvu na kuwachuja wale wasioweza kufaulu. Maagizo yote ya wokovu yana kusudi kwamba tumtii Mungu kweli kwa imani; hayamaanishi kwamba imani inaweza kushindwa. Ingawa wokovu wetu ni wa hakika na hauwezi kupotea, maonyo na tahadhari za kuishi kwa kuufuata hazipingani na ukweli huo. Bali yanatakiwa “kutuweka katika njia” – katika njia nyembamba ya imani iendayo uzimani.

Mapitio ya jumla²²

Jambo halisi la wokovu – ukweli wa wokovu Zawadi: tumepewa kwa njia ya Kristo	Kuufanya wokovu kuwa wetu – agizo la wokovu Kazi: kwa ajili ya Kristo
Kile <i>tulicho</i> tayari katika Kristo ...	... tunaweza tu <i>kufanyika hiyo</i> katika Kristo.
Tumeifia dhambi. Warumi 6:2	Msijitoe kwa dhambi! Warumi 6:13
Tumekufa pamoja na Kristo. Wakolosai 3:3	Vifisheni viungo vyenu! Wakolosai 3:5; Warumi 8:13
Tumehesabiwa haki ... Warumi 5:1	... na tunapaswa kuishi kwa haki. 1 Timotheo 6:11
Hatumo tena katika tabia ya mwili. Warumi 8:9	Msiishi tena kwa kufuata tabia ya mwili! Warumi 8:12
Tumetakaswa mara moja tu kwa dhabihu ya Kristo! Waebrania 10:10	Itafuteni utakatifu, ambao hakuna mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao! Waebrania 12:14
Tumeitwa. Waefeso 4:1; Warumi 8:28	Enendeni kama inavyostahili wito wenu! Waefeso 4:1
Tumepewa yote ...	... kwa hiyo tunapaswa kuyafanya yote kuwa yetu.
Tumevaa utu mpya, yaani Kristo. Wakolosai 3:10-11; Waefeso 4:24	Mvaeni Bwana Yesu Kristo! Warumi 13:14
Tuna msamaha kamili. Waefeso 1:7	Tunawajibika kusameheana! Waefeso 4:32
Mungu alitupa upendo wake. Warumi 5:5	Enendeni katika upendo! Waefeso 5:1-2
Tuna amani na Mungu na amani ya Mungu. Warumi 5:1; Wafilipi 4:7	Itafuteni amani! 1 Petro 3:11
Tuna uhuru katika Kristo. Warumi 8:2; Wagalatia 5:1	Kwa hiyo dumuni katika uhuru, ili mtumikiane kwa upendo! Wagalatia 5:13
Mungu anatupa ushindi. 1 Wakorintho 15:57	Tunaufanya ushindi kuwa wetu tunapopigana. 2 Timotheo 2:5 n.k.
Sisi ni nuru katika Bwana. Waefeso 5:8a	Enendeni kama watoto wa nuru, au: Nuru yenu na iangaze! Waefeso 5:8b; Mathayo 5:16
Tunaupata utaratibu mpya wa wokovu ...	... na tunakingojea kiumbe kipya.

22. Kwa kufuata Peter H. Uhlmann, Heimenhausen, Uswisi, kwa idhini yake ya hisani.

Kristo ndiye uzima wetu. Wakolosai 3:4; Wagalatia 2:20	Tunangojea kufunuliwa kwa Kristo. Wakolosai 3:4
Katika Kristo tumekombolewa ... Waefeso 1:7	... na tunangojea ukombozi wa mwili wetu. Warumi 8:23
Mungu ametufanya kuwa watoto wake na wana wake ... Warumi 8:15; 1 Yohana 3:2	... na tunangojea jambo hilo lionekane wazi. Warumi 8:23; 1 Yohana 3:2
Utu mpya umeumbwa kwa mfano wa yeye aliyeumba: Kristo. Waefeso 4:24	Tunabadilishwa (katika maisha yetu) tufanane na mfano wa Bwana. 2 Wakorintho 3:18
Tuna uzima wa milele ... Yohana 3:36	... na bado: Shika uzima wa milele! 1 Timotheo 6:12
Kama kanisa sisi ni mwili mmoja. Waefeso 4:4	Kwa hiyo hifadhini umoja wa Roho. Waefeso 4:3
Tayari tumekamilika katika Kristo ... Wakolosai 2:10	... lakini bado hatujafikia ukamilisho. Wafilipi 3:12
Mungu anatenda yote – kwa asilimia mia moja!	Yafanye yote kuwa yako – kwa asilimia mia moja!

“Utimizezi wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka; kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.” Wafilipi 2:12

Tayari sasa	Bado
<i>Kuna</i> – nafasi ya imani	<i>Kufanyika</i> – imani inayotekelezwa
Ukuu na neema ya Mungu	Wajibu na matendo ya Mkristo

Tayari tumeokolewa kikamilifu – lakini bado hatujafikia ukamilisho!

Pande zote mbili zinaishia katika agizo hili: *Uwe kile ulicho!*

“Kila betri ina ncha hasi na ncha chanya. Tofauti hii ndiyo sharti la kuwepo kwa mvutano wa umeme. Hapo tu ndipo mkondo unaweza kutiririka, ili taa iwake. Vivyo hivyo, sisi tunakuwa Wakristo walio hai (na wanaokua) pale tu tunapozifahamu ‘ncha’ hizi mbili, yaani jambo halisi la wokovu na kuufanya wokovu kuwa wetu, na tunapoutekeleza wokovu katika maisha yetu. Mvutano huu unatupa nguvu ya kusonga ya uzima mpya.”²³

23. Nukuu ya Peter Uhlmann, Heimenhausen, Uswisi, kwa idhini yake ya hisani.

4.18 Mstari wa 15: Lengo la neema

*Ni nini basi? Tutende dhambi,
kwa sababu hatuvi chini ya sheria,
bali chini ya neema?
Hasha!*

Tena mtu angeweza kutoa hitimisho lisilo sahihi kutokana na yale ambayo Paulo alifundisha. Kwa hiyo maisha ya Mkristo sasa yako chini ya neema, si chini ya sheria tena. Je, hii inamaanisha kwamba mtu anaweza kuutumia vibaya uhuru huu na kuishi bila kujizuia? La hashu; hilo tena lingekuwa hitimisho lisilo na maana. Kwa maana mtu angesahau jambo lifuatalo:

4.19 Mstari wa 16: Watumwa wa dhambi au wa haki

*Hamjui ya kuwa
yeye ambaye mnajitoa kwake kuwa watumwa wa kumtii,
ninyi ni watumwa wa yeye mnayemtii:
ama wa dhambi iletayo mauti,
ama wa utii uletao haki?*

Yule anayeichukua neema na uhuru kutoka kwa sheria kuwa ruhusa ya kutenda dhambi, anasahau kwamba kwa kufanya hivyo anajitoa mikononi mwa dhambi na kuifanya tena kuwa bwana wake. Hakuna njia ya kati iliyo bora, ambamo mtu anaweza kuwaheshimu mabwana wote wawili bila mgogoro. Kuna utegemezi wa aina mbili tu – ama maisha yanayoongozwa na dhambi, ama mwenendo wa kumtii Mungu.

4.20 Mstari wa 17: Watiifu kwa moyo – si watumwa wa dhambi tena

*Lakini Mungu ashukuriwe,
kwa kuwa mlikuwa watumwa wa dhambi,
lakini mmekuwa watiifu kwa moyo
kwa mfano ule wa elimu
ambao mliwekwa chini yake!*

Paulo hawajaribu Warumi, wala hana shaka juu ya wokovu wao. Hawaulizi sasa wao ni watumwa wa nani, bali anatamka bila shaka yoyote kwamba utumwa wao, uliotawaliwa na dhambi, ni jambo la zamani. Anafurahi na kumshukuru Mungu. Tayari katika Warumi 5:8 alisema kwamba zamani *tulikuma* wenye dhambi, kwa hiyo sasa hatuko hivyo tena. Hapa analithibitisha hilo tena. Hata kama, kwa bahati mbaya, bado tunatenda dhambi sasa, hatuko tena katika utumwa wa dhambi.

“Uhamisho” huu ulikuwa kazi ya Mungu. Alituhamisha kutoka katika eneo la mauti na kutupa uzima. Eneo la uzima linaelezwa kwetu kwa namna inayogusa sana kwa njia ya “mfano wa elimu” katika sura hizi. Ni muhimu mno kulijua fundisho hili la Mungu juu ya wokovu katika Kristo. Fundisho hili ndilo msingi ambao juu yake mtu lazima kwanza azielewe kanuni za upya wa uzima, ili kisha aweze kuishi kwa kuzifuata. Fundisho haliji kutokana na uzoefu wetu, bali linatuonyesha njia. Kwa fundisho hilo tunaupima na kuuchunguza uzoefu wetu. Fundisho la Maandiko Matakatifu linatusahihisha sisi, si kinyume chake.

“Mfano wa elimu” ni ishara kwamba fundisho hili si aina ya kitabu cha sheria kilichojaa vifungu visivyo halisi. Ni “hekima ya maisha”, na kwa hiyo linataka kuyabadilisha maisha yetu. Ndiyo sababu mtume anasema hivi: Sisi “tuliwekwa chini ya mfano wa elimu ...” – yaani kwa kusudi kwamba ulete jambo fulani ndani yetu.

Kuna mafundisho na nadharia nyingi za kisayansi za wataalamu kwa ajili ya wataalamu. Fundisho la Mungu ni kwa ajili ya kila mtoto wa Mungu – haidhuru upendo wa Mungu umemtoa katika mazingira ya aina gani. Fundisho hili liko karibu na maisha, nalo ni la lazima kwa maisha. Sura hizi, ambazo hakika si rahisi kuzielewa kila wakati, si eneo la wanatheolojia peke yao, bali zina maswali ya msingi kabisa ya kuwa kwetu Wakristo. Mengi yanategemea kama tumezielewa. Mtu anaweza kupoteza miaka mingi ikiwa hajayajibu maswali hayo kwa ajili yake binafsi.

Mungu ametuweka chini ya mfano wa elimu; lakini wakati huohuo utii wetu kwa Injili ulikuwa sharti la Mungu kutenda. Utii huo ulitokea “kwa moyo”. Ulikuwa hatua ya utii iliyotoka ndani kabisa. Haukuwa utii wa juujuu, bali uamuzi wa maisha wa kweli na wa kudumu. Mungu anataka moyo wetu; anataka utii utokee kwa kusadiki kikamilifu na kwa furaha. Kila kitu kingine hakina thamani kwa Mungu, nacho ni umbo la nje tu na unfiki.

4.21 Mstari wa 18: Watumwa wa haki

*Na mipowekwa huru mbali na dhambi,
mlifanywa watumwa wa haki.*

“Uhamisho huu wa Mungu” kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo umetuweka huru mbali na dhambi. Jambo hili Paulo amelieleza katika sehemu ya kwanza ya sura ya 6.

Kuwekwa huru hakumaanishi “kuondolewa” kwa dhambi, kama vile kuondolewa kwa uvimbe mbaya wa saratani. Kwa kutumia picha hii, tunaweza kueleza maneno ya Paulo hivi: Uvimbe huo ulitibiwa kwa leza, kwa sababu dhambi imehukumiwa msalabani; ilihukumiwa katika tabia ya mwili (8:3). Lakini wakati huohuo mwili wa dhambi pia ulifanywa kuwa bila nguvu, yaani uvimbe huu hauna tena mwili (hauna tena uwanja wa kufanyia kazi) ambamo unaweza kuenea. Siitwi tena mgonjwa, ingawa uvimbe bado upo. Ukuaji wake umezuuliwa. Kwa maneno mengine: Ni kweli kwamba dhambi bado iko ndani yangu (katika tabia yangu ya mwili, katika asili yangu ya tabia ya mwili), maadamu niko katika mwili wangu unaokufa. Hata hivyo, kwa sababu hiyo mimi si tena mwenye dhambi kwa asili, bali ni mtakatifu katika Kristo.

Tumewekwa huru mbali na *utawala* wa dhambi; sisi si watumwa wa dhambi tena. Kinyume chake: Sasa tumekuwa watumwa wa haki ya Mungu.

4.22 Mstari wa 19: Kujitoa kwa ajili ya haki na utakatifu wa Mungu

*Nasema kwa jinsi ya kibinadamu,
kwa sababu ya udhaifu wa tabia yenu ya mwili.
Kwa maana kama vile mlivyovitoa viungo vyenu
kuwa watumwa wa uchafu
na wa uasi
hata mkafanya uasi,
vivyo hivyo sasa vitoeni viungo vyenu kuwa watumwa
wa haki
mpate kutakaswa.*

Mafundisho ya Paulo ni ya “kibinadamu” kiasi kwamba ni vigumu kumwelewa vibaya. Anajali udhaifu wa tabia yao ya mwili. Neno hili linaeleza hali dhaifu ya kiroho. Wapokeaji wa waraka hawakuweza kuielewa namna ya kusema ambayo

kwa kawaida Paulo angeichagua kwa mafundisho haya. Hali yao ya kiroho ilikuwa na upungufu na ilihitaji kukua na kufanywa upya, kama Paulo anavyoandika baadaye. Je, jambo hili halitusaidii sisi pia?

Linafuata wito, agizo la wokovu (yale tunayoagizwa kutenda kwa sababu ya yale ambayo Mungu ameshatenda; kwa Kijerumani *Heilsimperativ*), la kujitoka kwa haki kama watumwa, ili “upya wa uzima” uonekane kweli.

Lengo la “utakatifu”, au “utakaso”, linamaanisha badiliko letu la msingi la nafasi, lililotufanya kuwa watakatifu, yaani watu waliotengwa kwa ajili ya Mungu. Kwa upande mwingine, kwa wale waliohesabiwa haki na kutakaswa, kuna wajibu wa wokovu wa kuishi maisha yanayoelekezwa kikamilifu kwenye haki na utakatifu wa Mungu.

4.23 Mistari ya 20–22: Kutoka kukosa matunda hadi uzima wa milele

*Kwa maana mlipokuwa watumwa wa dhambi,
mlikuwa huru mbali na haki.
Basi, mlipata matunda gani wakati ule
kwa mambo yale ambayo sasa mnayaonea haya?
Kwa maana mwisho wa mambo hayo ni mauti.
Lakini sasa mkiisha kuwekwa huru mbali na dhambi,
na kufanywa watumwa wa Mungu,
mnayo matunda yenu, ndiyo kutakaswa,
na mwisho wake ni uzima wa milele.*

Kweli hii ni picha ya nyeusi na nyeupe ambayo Paulo anaichora hapa. Kwa maana kabla ya kuzaliwa kwao mara ya pili, kabla ya badiliko lao la nafasi, wapokeaji wa waraka hawakuwa na uhusiano wowote na haki ya Mungu, bali walikuwa watumwa wa dhambi. Haikuwa kwamba hapo awali kulikuwa na mchanganyiko wa vyote viwili – vivyo hivyo kama ambavyo sasa, wakiwa Wakristo, hakuna mchanganyiko wa vyote viwili kwao. Bwana Yesu alisema juu ya jambo hili kwamba mtu hawezi kuwatumikia mabwana wawili, bali bwana mmoja tu.

Sasa wapokeaji wa waraka walipaswa kutazama nyuma. Dhambi haikuwa mwandamani wa kinadharia tu katika maisha yao, bali ilikuwa imedai kodi yake na kuwaongoza kwenye matendo na mambo ambayo sasa wanayaonea haya.

Maisha ya namna hiyo yanaongoza mautini. Hakuna njia nyingine isipokuwa ile tu iliyoelezwa katika mstari unaofuata.

Kuwekwa huru mbali na dhambi na nguvu yake, pamoja na uhuru wa kweli wa kumtumikia Mungu sasa kama watumwa, kunahusu utambulisho mpya, nafasi mpya. Sasa nafasi hii inazaa mambo ambayo mtu hahitaji kuyaonea haya tena, bali yanayoleta katika maisha ya wahusika matunda ya kutakaswa. Upya wa uzima unazaa matunda kwa ajili ya Mungu, nao una uzima wa milele kuwa lengo lake. Uzima huu hauupati mtu kwa kustahili, kwa kumzalia Mungu matunda. Bali ni sehemu ya kudumu ya wokovu wa Mungu, kama mstari unaofuata unavyoonyesha.

Uzima wa milele hapa unamaanisha uzima wa wale waliofufuka katika Kristo, ambao tutaufikia wakati ujao. Mwishoni mwa maisha ya kumwishia Mungu hakuna nukta, bali kuna nukta mbili: Maisha ya utukufu usioweza kufikirika, katika ushirika usiosumbuliwa na Mungu, yanatungojea. Uzima wa milele unamaanisha kutoharibika. Kutoka katika Agano Jipya, na hasa kutoka kwa mtume Yohana, tunajifunza pia kwamba uzima huu hauhusu tu “urefu” au “wingi” wake, bali zaidi ya yote unahusu “ubora” wa uzima huu wa Mungu.

Lengo la maisha ya kumwishia Mungu ni uzima wa milele. Hilo ndilo tunalolielekea, nasi tunafurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu unaokuja.

4.24 Mstari wa 23: Uzima wa milele badala ya adhabu ya milele

*Kwa sababu mshahara wa dhambi ni mauti;
bali karama ya Mungu ni uzima wa milele
katika Kristo Yesu
Bwana wetu.*

Neno hili linafupisha katika sentensi moja si tu maudhui ya Warumi 6, bali pia Injili nzima. Mwanadamu wa kwanza “alijinunulia” dhambi. Kwa ajili ya hiyo lazima alipe. Au kwa upande mwingine: Analipwa kwa kazi ambayo haikuwa njema, bali mbaya. Lakini “biashara” hii haiwezi kurudishwa nyuma. Mauti haiwezi kurudishwa wala kubadilishwa kwa kitu kingine.

Mshahara au ujira ni kitu ambacho mtu amekistahili. Jibu la Mungu ni tofauti. Kutoka kwake inakuja karama, zawadi isiyostahiliwa. Jibu lake kwa mauti ni uzima. Lakini si kufutwa tu kwa kifo kama ilivyokuwa kwa Lazaro, ambaye Yesu alimfufua. Kwa maana Lazaro alikufa tena wakati fulani baada ya kufufuliwa

kwake. Karama ya Mungu, kinyume chake, ni uzima mpya kabisa, kwa sababu mtu anaupata katika Kristo Yesu. Uzima wa Kristo ni uzima wa Yeye aliyefufuka; ni uzima wa ufufuo ulio ng'ambo ya mauti, mbali sana mahali ambapo nguvu ya mauti haiwezi kuufikia.

Uzima huu ni wa milele kwa sababu ni uzima wa Mungu mwenyewe. Uliweza kuwa uzima wetu kwa sababu uzima huu umo “ndani ya Mwana”, aliyefanyika mwanadamu (1 Yohana 5:11-13).

Kristo Yesu, Mpakwa Mafuta wa Mungu, hayuko mbali nasi. Yeye ni Bwana wetu binafsi, aliye katika uhusiano wa karibu nasi. Sasa yeye ndiye Mkuu wetu, yeye ndiye Mungu wetu.

5. Sheria katika Waraka kwa Warumi

Neno “sheria” linapatikana mara 72 katika Waraka kwa Warumi. Kwa jumla Paulo analitumia neno hili mara 119 katika Agano Jipya. Si kila mara ni sheria ya Musa, kama inavyoonekana katika muktadha wa kila mahali. Sheria ya Musa ni

mojawapo ya mada kuu za Waraka kwa Warumi. Mapitio haya ya jumla

yanaweza kusaidia kuelewa vizuri zaidi maana zake mbalimbali.

Neno	Maana	Orodha ya mistari
Sheria (pamoja na kibainishi na bila kibainishi), chini ya sheria, mapenzi ya Mungu, kielelezo cha kweli, maagizo ya haki ya sheria, amri, sheria ya Mungu (kwa namna mbili za kusema), sheria ya haki	Kwa ujumla daima ni sheria ya Musa. Katika Waraka kwa Warumi inamaanishwa sehemu ya kimaadili ya sheria, si sana au si kabisa maagizo ya dhabihu, yaani sheria za ibada. Sehemu hii ya sheria ilitolewa kwa Wayahudi peke yao.	2:12, 13, 14, 17, 18, 20, 23, 25 3:19, 20, 21, 31 4:13, 14, 15, 16 5:13, 20 6:14, 15 7:1, 4, 5, 6, 7, 8, 9, 10, 11, 12, 13, 14, 21, 22, 25 9:4, 31; 8:3, 4, 7 10:4, 5; 13:8, 10
“Kilichoandikwa (wengine wanatafsiri: katika hali ya zamani ya andiko , yaani katika [sheria] iliyoandikwa”)	Sheria iliyoandikwa, zile mbao mbili, pia vitabu vitano vya Musa	2:27, 29 7:6
Sheria ya imani	Kanuni ya imani na ya kutumaini, kinyume na matendo na haki inayotafutwa kwa matendo	3:27, 28
Sheria kwa nafsi zao wenyewe; kazi ya sheria iliyoandikwa moyoni; dhamiri	Sehemu ya kimaadili ya sheria, inayolingana na asili ya milele ya Mungu na madai yake (upendo; 13:10). Sheria hii baadhi ya watu wa mataifa walijua bila kuzijua amri za Musa. Kila mara mtu wa mataifa anapoitii sheria ya upendo kwa asili, anaitimiza; lakini pia anaikosea tena na tena.	2:14, 15
Sheria ya mume	Sheria inayomhusu mume (yaani sheria ya Musa inayomfunga mke kwa mumewe)	7:2, 3

5. Sheria katika Waraka kwa Warumi

Sheria ya akili yangu	Utendaji na kanuni ya uzima mpya, unaotaka kumtumikia Mungu. Ni kanuni ya asili ya uzima mpya kumtumikia Mungu, kwa sababu sheria ya Mungu imesimikwa katika uzima mpya.	7:23
Sheria ya dhambi na ya mauti	Kanuni isiyoweza kuvunjwa, ambayo kwa hiyo dhambi inamtawala mwanadamu kwa lazima, na dhambi inamwongoza mautini bila njia ya kutokea	7:23 8:2
Sheria ya Roho wa uzima	Katika Kristo, aliyeishinda mauti, yaani Yeye aliyefufuka, inafanya kazi sheria (kanuni, sheria ya nguvu) ya Roho Mtakatifu wa uzima; ina nguvu kuliko ile ya dhambi na ya mauti. Mfano: Kanuni ya asili ya mvutano wa dunia inaweza kushindwa tu kwa kanuni nyingine, ile ya aerodinamiki.	8:2

6. Warumi 7: Huru mbali na sheria

Katika jinsi mada inavyokua katika sura ya 5 na ya 6, kunasikika kupanda kwa nguvu, kunakoendelea hadi sura ya 7, mstari wa 6. Lakini kisha, katika sehemu ya pili ya sura ya 7, tunakutana na hali ya giza, ambayo haionekani kupatana hata kidogo na mtiririko wa mawazo.

Sura ya 7 ni kifungu cha kuingizwa katikati²⁴, ambamo Paulo anashughulikia uhusiano wetu na sheria, utendaji wake na lengo lake. Sheria ya Musa, Torati, alikuwa ameshaitaja mara mbili katika Warumi 6:14-15, lakini kwa matokeo ya kushangaza: Haiamui tena maisha ya Mkristo (awe Myahudi au mtu wa mataifa). Mkristo yuko chini ya neema, si chini ya sheria tena. Katika sentensi moja tu anatamka ukweli wa msingi wenye matokeo makubwa. Kwa mtu wa mataifa huenda jambo hili lilieleweka, lakini kwa Myahudi? Kwake hili lilikuwa uchokozi, kama si hata kumkufuru Mungu. Akitarajia majibu ya namna hiyo, Paulo hataki kuacha maswali yasiyojibiwa hapa, na kwa hiyo analishughulikia jambo hili katika sura nzima – sentensi ndefu ya mabano.²⁵

Kama Warumi 6:23 ingefuatwa moja kwa moja na 8:1, yaani kama kusingekuwa na sura ya 7, basi sisi (Wakristo kutoka katika mataifa) labda tusingekosa kitu. Hata hivyo mafundisho ya Warumi 7 hayawezi kukosekana katika muktadha mzima wa mada hii. Mkondo mkuu wa mawazo wa Warumi 5 hadi 8 unaweza kufupishwa hivi:

Kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo, kutoka katika maisha yasiyo na matunda hadi maisha yanayomzalia Mungu matunda na yasiyotawaliwa tena na dhambi. Mungu alifanyaje jambo hili, nami leo ninawezaje

kweli kuenenda katika “upya wa uzima”? Sasa linazuka swali kama kweli sheria haihitajiki kwa ajili ya jambo hili, kama ilivyokwisha kusemwa katika sura ya 6. Hata hivyo, ilitolewa na Mungu mwenyewe, ili kuonyesha jinsi mtu anavyopaswa kuishi.

24. Ninaiona sura nzima ya 7 kuwa sentensi ya mabano hadi 8:1. Kwa maana mistari ya 1-6 kwa mada yake si sehemu ya sura ya 6, bali ni utangulizi wa sentensi hiyo ya mabano.

25. Aidha, Paulo anafanya vivyo hivyo, kwa kuwajali Wayahudi, katika sura ya 9 – 11. Anaeleza kwa nini, kwa upande mmoja, Injili haiwahusu Wayahudi peke yao, bali watu wote. Lakini wakati huohuo anasisitiza kwamba ahadi zote kwa watu wa agano zititimizwa wakati ujao.

6.1 Maana ya Warumi 7 na nafasi yake

Sura hii ya Waraka kwa Warumi imeeleweka kwa namna zinazopingana. Swali kubwa ni hili: Sura hii inaeleza hali ya mtu wa namna gani? Maelezo yanayojulikana zaidi ni haya:

- hali ya kawaida ya Mkristo
- hali ya pekee isiyo ya kawaida na isiyotakiwa
- hali ya mtu ambaye hajazaliwa mara ya pili
- hali ya mtu aliyezaliwa mara ya pili ambaye hana Roho Mtakatifu.

Kweli, tafsiri ya sura hii inahusu jambo la msingi kabisa kwa maisha yetu ya Kikristo. Kwa maana mengi yako hatarini: Je, Injili inaweza kweli kuwabadilisha watu, tena kwa kudumu? Au tunajidanganya tu? Kutokana na sura ya 7 mtu angeweza pia kuhitimisha kwamba mara nyingi itabaki kuwa jaribio tu la kutenda mema. Je, yuko sahihi yule anayejua mtu wa uhalisia, anayedai kwamba ushindi juu ya dhambi upo mbinguni tu? Basi, Warumi 7 inapaswa kueleweka vipi?

6.2 Vita vya Roho dhidi ya tabia ya mwili?

Sura ya 7 *haielezi* mgogoro wa kudumu wa Mkristo, ambamo tabia ya mwili na Roho vinainukiana na kushindana, kama inavyoelezwa katika Wagalatia 5:16-25. Kwa maana huko inahusu ushindi katika nguvu ya Roho Mtakatifu, jambo ambalo halionekani mahali popote katika Warumi 7. Katika uzoefu unaoelezwa hapa mtu anaona kukata tamaa tu. Mtu huyu anaugua chini ya nguvu ya dhambi. Anajitazama mwenyewe tu na kuitafuta nguvu ndani yake mwenyewe peke yake. Kwa kweli ushindi ulikwisha kuelezwa katika Warumi 6. Lakini huo ni ushindi wa namna gani, ikiwa unaonekana kama kile ambacho sura ya 7 inaeleza? Warumi 7 haielezi maisha ya kawaida ya Mkristo, bali hali ya kusikitisha ya Mkristo aliyefanya sheria kuwa kanuni ya maisha yake na anayejaribu kuishika kwa nguvu zake mwenyewe. Haamini kile ambacho 6:14-15 inasema: Hatuko tena chini ya sheria. Kwa hiyo anapata uzoefu mchungu kwamba hawezi kufaulu. Jambo hili linamfikisha ukingoni mwa kukata tamaa kabisa (“Ole wangu, maskini mimi!”, mstari wa 24).

6.3 Wenye haki na wenye dhambi wakati mmoja?

Martin Luther alisema kwamba sisi ni “wenye haki na wenye dhambi wakati mmoja”²⁶. Kwa mujibu wa Luther, hasa katika Warumi 7 hali ya kuwa mwenye dhambi inaonekana wazi. Lakini tayari tuliona katika sura ya 5 kwamba sisi si tena “wenye dhambi”, bali tulikuwa hivyo (5:8; 5:19). Hivyo ndivyo Neno la Mungu linavyosema. Warumi 7 haisemi kwamba kwa nafasi yetu bado sisi ni wenye dhambi. Bali sura hii inaonyesha kwamba sheria ya Mungu si kipimo cha maisha ya kumpa Mungu utukufu. Tukiwa bado tunatenda dhambi, hiyo haimaanishi kwamba bado sisi ni wenye dhambi. Tunapotenda dhambi, tunafanya hivyo kama watakatifu – kama watu ambao hata hivyo wanabaki kuwa watakatifu.

Upya wa uzima katika Kristo na kwa njia ya Roho hauamuliwi na sheria ya Musa wala na sheria nyingine yoyote. Sheria inahusiana na utu wa zamani, si na utu mpya. Lakini mtu akiikubali sheria kuwa kipimo cha maisha, mapema au baadaye ataingia katika hali kama ile inayoelezwa hapa. Aidha, jambo hili linawahusu pia wale ambao katika uzoefu wao waliwahi kuiacha Warumi 7 na kuhamia Warumi 8. Kunaweza kutokea “kurudi nyuma” kila mara mtu anapokuwa mshika-sheria na kuifanya sheria kuwa kanuni ya Mkristo. Kwa maana hiyo, sura hii inaeleza pia uzoefu wa Mkristo anayejua kuwekwa huru halisi mbali na sheria, lakini hata hivyo anajaribu kuishika sheria kwa nguvu zake mwenyewe.

Maisha ya kawaida ya Mkristo yanaelezwa katika Warumi 8. Warumi 7 haielezi maisha ya kila siku ya Mkristo ambayo Mungu anayataka. Ingekuwa kukatishwa tamaa kuchungu, kama haya ndiyo yangekuwa matokeo ya wokovu mkuu wa Mungu, uliomgharimu kifo cha Mwanawe mwenyewe.

6.4 Amezaliwa mara ya pili au la?

Wakati uliopo kuanzia 7:14 (tofauti na wakati uliopita katika 7:7-11) unaonyesha wazi kwamba mtu huyu na uzoefu wake ni wa Mkristo.

26. Hoja ya Luther: Wenye haki na wenye dhambi wakati mmoja (*simul justus et peccator*). “Basi tazama, ni kama nilivyosema hapo juu: ‘Watakatifu, wakati uleule wanapokuwa wenye haki, ni wenye dhambi; ni wenye haki kwa sababu wanamwamini Kristo, ambaye haki yake inawafunika na kuhesabiwa kuwa yao. Lakini ni wenye dhambi kwa sababu hawaitimizi sheria (na) hawako bila tamaa ya dhambi, bali wako kama wagonjwa walio chini ya uangalizi wa tabibu’, wagonjwa walio wagonjwa kweli kweli, lakini kwa mwanzo na kwa tumaini wazima, au afadhali: wanaofanywa wazima, yaani walio katika hali ya kupona”, *Römerbriefvorlesung 1515/16*.

Wakati kuanzia sura ya 5:12 hadi mwisho wa sura ya 6 (au hata hadi sura ya 7:6) mikondo miwili mikubwa ya mawazo inaelezwa, Paulo anaikatiza ili aiendeleze tena katika sura ya 8. Katikati yake (yaani katika sura ya 7) tunakuta hali ya pekee, inayomhusu tu yule anayejua sheria. Mtu anayehusika anataka kumtumikia Mungu, jambo ambalo si lazima liwe kweli kwa mtu asiyeamini. Mtu asiyeamini anaweza kuwa wa kidini na kumtafuta Mungu, lakini mwishowe atafanya mapenzi yake mwenyewe. Tena, si lazima mtu wa kidini akubali kwamba yeye ni mbaya kabisa. Lakini mtu wa Warumi 7 anafikia kujijua huku. Kutambua kwamba sisi tumeharibika kabisa, lakini Mungu na sheria yake ni kamili kabisa, kunaweza kuja tu kwa nuru ya Roho wa Mungu. Kwa hiyo tunaweza kudhani kwamba hapa (7:14 na kuendelea) inamhusu mtu aliyezaliwa mara ya pili.

Wengine wanaeleza kushindwa kwake kwa kusema kwamba (bado) hana Roho Mtakatifu, ingawa Paulo, baada ya kumtaja mara moja tu katika mstari wa 6 (“katika hali mpya ya Roho”), anamzungumzia Roho Mtakatifu kwa kirefu katika sura ya 8 tu. Lakini Roho kutotajwa katika 7:7-25 kunatokana na kwamba Paulo (akiandaa sura ya 8) anataka kwanza kueleza uhusiano na sheria na kukosa nguvu kwa tabia ya mwili. Kuwepo kwa Roho ndani ya mtu huyu hakumsaidii, kwa sababu Roho hakuja ili kutusaidia kuishika sheria.

Kama Warumi 7 ingemhusu mtu ambaye bado hajazaliwa mara ya pili, somo la sura hii hatimaye lingekuwa marudio ya fundisho lililokwisha kuelezwa; kwa maana kwamba mtu asiye na haki – awe wa kidini au la – hawezi kabisa kumpendeza Mungu, tunakuta tayari kwa kirefu katika sura za kwanza za waraka huu. Paulo analenga zaidi ya hilo. Anachokieleza hapa ni asili ya tabia ya mwili na kushindwa kwake (hata ndani ya aliyezaliwa mara ya pili) kumpendeza Mungu. Inatakiwa kuonyeshwa kwamba hasa mtu aliyekombolewa, ambaye baada ya hapo bado anataka kumpendeza Mungu kwa njia ya sheria, ndiye anayepitia mtanziko huu wa 7:14-25 – tena muda wote anaotaka kuishika sheria kwa nguvu zake mwenyewe.

6.5 Warumi 7: Uzoefu wa lazima?

Pia kuna mtazamo kwamba Warumi 7 ni uzoefu wa kawaida, tena wa lazima, kwa kila Mkristo katika utakaso wa vitendo. Baada ya mtu kuongoka na kushukuru kwamba ana amani na Mungu, inasemekana kwamba baada ya muda fulani uzoefu wa Warumi 7 utamjia. Atasikia nguvu ya dhambi na hataweza

kuishinda. Kukata tamaa huku kutakoma tu wakati ule atakapoelewa maana ya Warumi 8: Kristo ametimiza yote. Hapo ndipo atakapotambua kwamba nguvu ya kushinda haiko ndani yake mwenyewe, bali katika yale ambayo Mungu ametenda na anayotenda kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Lakini mwenendo huu hauwezi kuchukuliwa kuwa aina ya kanuni ya lazima kwa maisha ya imani. Sura hii inamhusu kwanza yule anayeijua sheria, na kwa kawaida hao walikuwa Wayahudi. Hapa wanaozungumziwa kwanza ni Wayahudi (yaani Wakristo wa Kiyahudi). Watu wa mataifa hawakuwa chini ya sheria ya Musa.

Zaidi ya hayo, hakuna ulazima kwa Mkristo anayeyapokea kikamilifu na kuyatekeleza mafundisho ya Warumi 6 (si chini ya sheria, bali chini ya neema) na 7:1-6 (“tumeifia sheria”) kuingia katika taabu ya Warumi 7. Hapa ninasisitiza tena kwamba maisha ya Kikristo ya ushindi yanaelezwa katika sura ya 8 tu. Basi, kama mtu asiyeijua sheria pia asingeifahamu sura ya 7, huenda asingelijua tatizo linaloelezwa humo. Kwa hiyo hakuna ulazima wa kutoa kutoka katika sura ya 5 hadi 8 mchakato wa kawaida au hatua za maendeleo katika maisha ya Mkristo.

Lakini hatuwezi kuipita sura hii ya 7 kwa urahisi hivyo, kwa sababu uzoefu wa Wakristo wengi mara nyingi unalingana kabisa na hali inayoelezwa humo. Ikiwa inawahusu wale wanaoijua sheria, basi leo lazima tuseme kwamba si Wayahudi tu wanaoijua, bali pia Wakristo wote, na wengi wameifanya kuwa kanuni ya maisha yao. Kimsingi, Wayahudi na watu wa mataifa hawatofautiani kuhusu asili yao ya zamani ya Adamu na nafasi yao ya wokovu katika Kristo. Kwa hiyo uzoefu unaoelezwa, tunapoupitia leo, unaweza kuwa ule wa Wakristo wa Kiyahudi na pia ule wa Wakristo wa mataifa. Wakristo wengi wamepitia “uzoefu wa Warumi 7”. Wengi bado wako ndani yake, kwa sababu wanauona kuwa maisha ya kawaida ya Mkristo. Lakini pia wapo wengi waliopitia “uzoefu wa Warumi 8”. Mtume anaiona Warumi 8 kuwa maisha ya kawaida ya Mkristo. Inapaswa kuwa jambo la kawaida kwamba Wakristo wanaishi kwa Roho na hawaenendi kwa kufuata tabia ya mwili (taz. Wagalatia 5:16-26; 1 Wakorintho 3:1-3). Haya ndiyo maisha ambayo Mungu anayataka, na kwa ajili yake ameandaa kila kitu.

Lakini kwa nini wengi wetu tumepitia “uzoefu wa Warumi 7” wenye maumivu? Kwa sababu baada ya kuongoka kwetu tuligundua kwamba dhambi ni nguvu kubwa kiasi gani. Kisha tulijaribu kupigana nayo, lakini kwa silaha isiyofaa na tukitazama upande usiofaa. Tultumia nguvu zetu wenyewe.

Hatukutambua kwamba Kristo ametutimizia yote, na wakati huohuo anatupa kwa Roho wake nguvu yote ya kuwa washindi. Kwa maana hiyo tunaweza kushukuru sana kwamba tunayo sura hii, kwa sababu kwa hiyo tunaweza kuieleza na kuielewa kwa Neno la Mungu hatua hii ngumu ya kuwa kwetu Wakristo (kama kweli tuliipitia). Kisha tunaweza kuwaonyesha wengine wanaoishi katika dhiki hii njia ya kutoka.

6.6 Mtu wa Warumi 7 ni nani?

Watu wamekisia mengi kuhusu mtu anayeelezwa hapa ni nani. Je, kweli ni uzofu binafsi wa mtume Paulo, ambaye anazungumza kwa “nafsi ya kwanza”? Mambo kadhaa yanaweza kuunga mkono jambo hili, na mengine yanalipinga. Swali hili hatutaliendeleza hapa, hata kama linavutia kiasi gani.

Ninaamini kwamba Paulo anazungumza, kama mfano, juu ya yale ambayo Wakristo wengi wanayajua na wameyapitia. Jambo hili lina umuhimu mkubwa kiasi kwamba Paulo kwa sababu hiyo anajiweka mwenyewe katika “nafasi ya mimi”, jambo ambalo si geni kabisa (taz. pia Wagalatia 2:18; 1 Wakorintho 10:30).²⁷

6.7 Warumi 7:1-6: Tumeifia sheria

Mistari sita ya kwanza inaeleza kwa namna ya msingi uhusiano wa Mkristo na sheria. Kama ilivyo katika sura ya 6 kuhusu dhambi, hapa upande wa *keisheria* unaelezwa kwanza. Hatukufa kwa kweli sisi wenyewe, bali Kristo alikufa mahali petu. Kifo hiki tunahesabiwa sisi kana kwamba tulikufa kweli, na hapa matokeo yake ni kwamba tumeifia sheria.

6.7.1 Mstari wa 1: Sheria inawahusu walio hai tu

Ndugu zangu, banjui (maana nasema na watu wanaojua sheria) ya kuwa sheria humtawala mtu wakati wote anapokuwa hai?

Kweli mtu anapata picha kwamba hapa Paulo anazungumza kwa jinsi ya kibinadamu na anatoa mantiki rahisi kabisa, inayosaidia kueleza kweli muhimu

27. Kuhusu jambo hili, nukuu ya M. Arhelger, anayerejelea sarufi ya Kiyunani: “Ili kuonyesha kwa namna hai jambo linalowahusu wote kwa mfano wa mtu mmoja, kana kwamba ni jambo linalotokea sasa, lugha ya kawaida huchagua nafsi ya 1 na ya 2 umoja” (F. Blass, A. Debrunner, F. Rehkopf: *Grammatik des neutestamentlichen Griechisch*, Göttingen 1979, uk. 231 kuhusu § 281).

ya kiroho. Sheria, au kila sheria, inawahusu watu walio hai tu, wanaoweza kuitikia sheria kwa kuitii au kwa kutoitii. Mtu aliyekufa hana tena uhusiano wowote na sheria hata moja.

6.7.2 Mistari ya 2-3: Njia pekee ya kuiepuka sheria

Kwa maana mwanamke aliyeolewa amefungwa na sheria kwa mumewe maadamu yu hai; lakini ikiwa mume amekufa, amefunguliwa ile sheria ya mume. Basi, wakati mume yu hai, ataitwa mzinzji, akiwa mke wa mwanamume mwingine; lakini mume akifa, yu huru mbali na ile sheria, hata yeye si mzinzji, ajapokuwa mke wa mwanamume mwingine.

Mfano unatakiwa kuifafanua zaidi hali hii ya kisheria na kuongeza upande mwingine. Kama mtu angejaribu kujiondoa chini ya sheria (jambo linaloweza kutokea kwa njia ya kifo tu), kwa maana ya mfano angefanya uzinzi. Isipokuwa kwa kifo, hakuna njia ya kujiondoa katika mshiko wa sheria. Hivyo ndivyo mfano wa sheria ya ndoa unavyoonyesha. Sheria hii ya ndoa iliwaunganisha mume na mke kihalali kwa maisha yao yote bila kutenganishwa, kama lilivyokuwa kusudi la Mungu tangu mwanzo. Sheria ya ndoa haiwahusu tena wanandoa pale mmoja wao anapokufa, hapa katika mfano huu mume. Lakini mke akiwa pamoja na mwanamume mwingine wakati mume wake halali bado yu hai, anafanya uzinzi. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo hali ya yule aliye chini ya sheria: Hakuna kufunguliwa wala kuwekwa huru isipokuwa kwa njia ya kifo. Hapo tu ndipo uhusiano mpya wa ndoa unaweza kuwepo. Mtu akitaka kuiepuka sheria kwa njia nyingine isipokuwa kifo, atakuwa mkosaji zaidi, na kwa maana ya mfano atafanya uzinzi.

Katika picha hii mume anasimama badala ya sheria, wakati mke anawawakilisha Wakristo ambao Paulo anasema nao hapa. Basi, tunawezaje kuwekwa huru mbali na sheria?

6.7.3 Mstari wa 4: Yeye ambaye sasa sisi ni mali yake – Kristo

Vivyo hivyo nanyi, ndugu zangu, mliuawa kwa habari ya sheria kwa mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine, yaani, yeye aliyefufuka katika wafu, ili tumzalie Mungu matunda.

Kwa kuwa kuwekwa huru mbali na sheria kunawezekana tu kwa njia ya kifo, vivyo hivyo ni kwetu pia. Sasa Paulo anakitumia kifo cha Yesu Kristo, alichokwisha kukieleza katika sura ya 6 kuhusu dhambi, kwa uhusiano wetu na sheria.²⁸

Wahusika katika picha hii wanabadilika, na sasa inaonekana hivi: Muumini analinganishwa na mke. Mume anasimama badala ya sheria. Mara mume anapokufa, sheria inakoma kuwa halali.

Lakini si sheria iliyokufa (wala si dhambi; taz. sura ya 6), bali sisi ndio tuliokufa. Hata hivyo kifo hiki mwingine alikichukua. Mume mpya ni Kristo, ikiwa tunaendelea na picha hii. Alikufa mahali petu.

Neno “mliuawa” linatufanya tufikirie kuuawa kwake. Hivyo ndivyo Paulo anavyomaanisha anaposema kwamba kwa njia ya sheria aliifia sheria (Wagalatia 2:19-20). Mkosaji wa sheria lazima afe. Zamani Paulo aliikosea sheria, lakini Paulo alikufa – katika Kristo, aliyejitwika matokeo haya ya kisheria ya kuikosea sheria. Lakini katika kufa huku pamoja naye, wakati huohuo ilikuwemo pia njia ya kutoka, ya kuliepuka eneo ambamo sheria inatenda kazi.

Kifo cha Yesu Kristo kilikuwa kifo cha yule aliyefanywa kuwa dhambi mahali petu. Kutajwa kwa mwili wake kunatufanya tufikirie hofu yote ya kuuawa kwake na ya hukumu ya Mungu msalabani. Kilikuwa kifo cha kutisha, ambamo utu wetu wa zamani ulisulubiwa pamoja naye.

Hapa pia inazungumzwa juu ya kubadilishwa. Uhusiano na sheria unavunjwa, na uhusiano mpya unaumbwa, ambao hapa unalinganishwa hata na agano la ndoa. Tumeunganishwa na Yeye aliyefufuka; sasa sisi ni mali ya Mtu aliyekufa na kufufuka. Mwanamke anayeolewa anapokea jina na hadhi ya mumewe; vivyo hivyo nasi, kwa maana kwa uhusiano huu sasa tuko “katika Kristo”.

6.7.4 Mstari wa 5: Sheria haizalishi haki, bali matendo ya dhambi

Kwa maana tulipokuwa katika tabia ya mwili, tamaa za dhambi, zilizokuwako kwa sababu ya sheria, zilitenda kazi katika viungo vyetu, ili kuizalia mauti matunda.

Kuhusu maisha yetu ya zamani kabla ya kuongoka, Paulo analeta neno jipya. Tulikuwa “katika tabia ya mwili” (kwa Kiyunani *sarx*; SUV: ‘mwili’; taz. 8:8-9).

28. Katika Wagalatia 6:14 tunakuta matokeo ya tatu ya kufa kwetu pamoja naye: Tumeufia ulimwengu.

Hapa haimaanishi mwili wetu wa kimwili, bali hali fulani: Tulikuwa katika ukoo wa Adamu. Kwa hiyo tabia ya mwili lazima ihusiane na dhambi: “Katika tabia ya mwili” “tamaa za dhambi zilitenda kazi”. Tabia hii ya mwili inaeleza hali ya kuwa ya mwanadamu iliyojaa dhambi na tamaa zake. Hapa haihusu tabia ya mwili iliyo ndani yetu, bali *kuwa katika tabia ya mwili*. Hali hii ya kuwa mzao wa Adamu ina mazingira yake ya maisha katika tabia ya mwili yenye dhambi tu, na haiwezi kutenda kitu kingine isipokuwa dhambi. Ndiyo sababu Bwana Yesu, anapozungumza juu ya ulazima wa kuzaliwa upya, anasema: “Kilichozaliwa kwa tabia ya mwili ni tabia ya mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho” (Yohana 3:6). Ingawa mahali hapa kuzaliwa mara ya pili si mada inayozungumzwa, kimsingi inahusu jambo lililele: Matunda kwa ajili ya Mungu hayawezi kutoka katika tabia ya mwili. Kwa hiyo kuzaliwa upya ni lazima.

Sheria ilifanya dhambi “izidi sana” (5:20). Haikuionyesha dhambi tu, bali iliichochea dhambi. Jambo hili linaeleza wazi kinachotokea Mkristo anapojiweka chini ya sheria. Hilo litaonekana katika sehemu inayofuata ya sura hii, ambapo uzoefu huu hasa unaelezwa.

6.7.5 Mstari wa 6: Utumishi mpya usiotegemea sheria

Lakini sasa tumefunguliwa sheria (tumeondolewa chini yake), kwa kuwa tumeifia ile iliyokuwa ikiinfunga, bata tunatumika katika hali mpya ya Robo, wala si katika hali ya zamani ya andiko.

Sheria haijamwachilia mtu yeyote wala kumwachilia huru; siku zote imetoa hukumu yake (ya haki) ya hatia. Lakini kwa sababu sisi (yaani utu wetu wa zamani) tumekufa, njia iko wazi ya kuingia, kana kwamba, katika “uhusiano mpya wa ndoa”, ambao hautakomeshwa kamwe tena kwa kifo.

“Andiko” (kwa neno kwa neno: *kilichoandikwa*) ni sheria, inayodai utii bila kutoa nguvu inayohitajika ya kuutumiza. Lakini sasa “tumeondolewa” chini ya sheria; tumehamishwa upande mwingine. Sasa tuko katika Kristo Yesu, tuna uzima ndani yake na Roho Mtakatifu ndani yetu. Kuhusu utendaji, nguvu na sauti ya Roho huyu, Paulo ataandika baadaye. Katika mstari wa 6 Roho anatajwa mara moja tu katika sura hii, tofauti kabisa na sura ya 8.

Kama vile katika sura ya 6 inahusu *upya wa uzima*, hapa ni *hali mpya ya Robo* (tafsiri nyingine: “jambo jipya, [yaani] Roho”). Ya kale yamepita, yamekuwa mapya. Tuna uzima mpya, na tuna Roho wa Mungu.

6.8 Warumi 7:7-14: Sheria iliyo kamilifu

Baada ya uhusiano wa Mkristo na sheria kuelezwazwa wazi (tumeifia sheria, ili tuwe mali ya mwingine, yaani Kristo), kwa kweli mtu angeweza kwenda moja kwa moja hadi sura ya 8:1. Lakini sasa kinakuja nini? Kinafuata kuitetea sheria. Utetezi huu unaelekezwa kwa Mkristo wa Kiyahudi, lakini pia kwa kila mtu ambaye ama hajaelewa uhusiano wa muumini na sheria (taz. 7:1-6), ama anadhani kwamba anaweza hata hivyo kujaribu kufikia lengo kwa msaada wake. Mtu huyu anajihusisha na sheria – kwa matokeo mabaya kabisa. Sasa uzoefu wake unaelezwa.

Kama tungehamishia mfano wa ndoa ambao Paulo ameutumia sasa hivi kwa Mkristo huyu, tungeweza kusema: Kwa namna fulani anafanya uzinzi; kana kwamba ameunganishwa na mume mpya, yaani Kristo, huku akijihusisha na uhusiano na sheria (Wagalatia 2:18).

Sheria si kanuni ya maisha ya Mkristo (au: si mazingira yake ya kuishi, kama vile nchi kavu isivyo mazingira ya samaki). Hili ni kweli hata pale ambapo – na haiwezi kuwa vinginevyo – yeye kama Mkristo kwa kawaida anazitimiza amri za kimaadili za sheria ya Mungu (8:4). Lakini kuitimiza sheria ya Musa si kazi ya maisha yake. Mkristo hayuko chini ya utawala wa Musa. Sasa inahusu kuwa na Kristo mwenyewe kuwa kiini cha maisha na kanuni ya maisha, kuunganishwa na Kristo, na kuwa na nguvu ya Roho wake. Upya wa uzima na “hali mpya ya Roho” havijengwi kwa makatazo, ambayo ndiyo yaliyokuwa alama ya sheria. Kristo mwenyewe anaumbika moyoni mwetu na anaonekana kwa njia ya tunda la Roho. Kuwa Mkristo hakuhusu kushika amri, bali kubadilishwa kutoka ndani – kuelekea kufanana na Kristo. Haihusu amri, bali Mtu. Yeye ndiye lengo.

Lakini sasa hatujawa watu wasio na sheria hata kidogo: Tunamtumikia Yesu Kristo. Tunamtumikia kama watumwa, au kama watumishi walio mali yake – yeye aliye Bwana wetu na Mkuu wetu, ambaye sisi ni mali yake halali. Amri zake tunazishika; hizo ndizo “sheria ya Kristo” (Wagalatia 6:2; taz. 1 Wakorintho 9:21). Tuko chini ya Kristo, chini ya sheria yake.

Katika sura hii inaonekana wazi kwamba sheria (hasa kwa sababu mara nyingi ni makatazo) haielekezwi kwa wale waliohesabiwa haki katika Kristo. Ndiyo sababu Paulo anasema kwamba sheria haikuwekwa kwa ajili ya mwenye haki, bali kwa ajili ya waasi (1 Timotheo 1:9), ili kuifichua dhambi yao na kuwaongoza kwa Kristo.

6.8.1 Mstari wa 7: Kuijua dhambi huja kwa njia ya sheria

*Tuseme nini basi? Je! Sheria ni dhambi? Hasba! Lakini mimi nisingalijua dhambi isipokuwa kwa sheria. Kwa maana nisingalijua kutamani kama sheria isingalisema, "Usitamani."*²⁹

Swali hili linajitokeza lenyewe kwa nguvu! Ikiwa sheria ni kitu ambacho mtu anawekwa huru mbali nacho kwa njia isiyo ndogo kuliko kifo cha Bwana Yesu msalabani, basi lazima kuna kitu kisichokuwa sawa na sheria. Tena Paulo anasema “Hapana!” kwa uthabiti. Ikiwa kuna kitu kisichokuwa sawa, chanzo chake kiko kwa mwanadamu.

Ikiwa tayari tumejifunza kwamba hatuko tena chini ya sheria, na ikiwa wakati huohuo kila kitu kiko sawa na sheria hii, basi sasa Paulo ataeleza ni nini hasa habari ya sheria hii.

Sheria imefunua dhambi ni nini. Kwa kutumia sheria mtu angeweza kusema hasa dhambi, yaani kosa, ilikuwa nini. Kwa njia hiyo mwanadamu alipaswa kujua dhambi ni nini. Katika hali hii ni Myahudi, lakini mwishowe inamhusu kila mtu aliyekutana na sheria hii.

Paulo anaichukua amri ya mwisho kati ya zile Amri Kumi kama mfano, ili kuendeleza wazo lake. Huenda kuivunja amri ya kutotamani ndiyo dhambi iliyoenea kuliko zote – dhambi iliyofichika, ambayo kila msikilizaji au msomaji anajua kutoka katika maisha yake. Hatupaswi kutamani kitu chochote kilicho mali ya mwingine. Ni dhambi inayotokea kwanza moyoni mwangu tu, na si lazima itimizwe kwa tendo linalolingana nayo. Kwa maana sura hii haihusu matendo makubwa ya dhambi. Nguvu ya dhambi inasikika kwanza kwa nguvu ndani, wala haitambuliwi kwa matendo tu.

Tuufuate mstari huu pia kwa maana hii: kwamba tuihubiri sheria, kipimo cha Mungu, ili kuwaletea waliopotea kuijua dhambi. Bila kuijua dhambi, hawataelewa kwamba wanamhitaji Mwokozi.

29. Kutoka 20:17; taz. Kumbukumbu la Torati 5:21.

6.8.2 Mstari wa 8: Sheria inaichochea dhambi

Lakini dhambi ilipata nafasi kwa ile amri, ikafanya ndani yangu kila namna ya kutamani; kwa maana pasipo sheria dhambi imekufa.

Amri inapomkuta mwanadamu, utii haufuati mara moja, ingawa hilo ndilo jibu lililokusudiwa. La, dhambi inajionyesha kuwa nguvu ya ukaidi. Dhambi inaichukua amri ya Mungu kuwa nafasi ya kufanya kile hasa ambacho sheria inakataza. Si tu kwamba dhambi inaamshwa kama mbwa aliyelala. Sifa *kuu* ya dhambi ni kuiasi amri ya Mungu.

Tamaa haielekei kwenye kitu kimoja tu. Inalenga kila kitu kinachotamanika; katika hilo ina sura nyingi, na ni kama sumaku yenye nguvu inayojaribu kuvuta kila kitu kwake.

Katika sura ya 5 ilikwisha kuonyeshwa wazi kwamba dhambi ilikuwepo pia bila sheria (na bila kutegemea sheria). Ila haikuwa imefunuliwa kama ilivyo, yaani kama kanuni inayompinga Mungu.

Bila sheria dhambi “imekufa”; bila sheria mtu hawezi kumshtaki mtu yeyote kwa sababu ya dhambi.

Basi kwa nini Mungu alitoa sheria, ikiwa bila sheria dhambi ilikuwa imekufa? Je, bila sheria isingebaki imekufa milele? Sheria iliingia *kando*, ili dhambi izidi sana (taz. 5:20). Ugonjwa wa dhambi, uliompata kila mwanadamu tangu Adamu, haukuweza kuponywa kwa sheria, kwa kusema hivyo; ulitambulishwa tu kama ulivyo. Paulo anawaambia Wagalatia kwamba sheria ilikuwa “kiongozi wa kutuleta kwa Kristo” (Wagalatia 3:24; ER, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani); kwa hiyo sheria ilionyesha ulazima wa dhabihu ya Yesu (Wagalatia 3:23-26). Kwa maana hii tunapaswa pia kuitumia katika uinjilisti wetu.

6.8.3 Mistari ya 9-11: Kukutana na sheria kunaleta mauti

Mimi nalikuwa hai bapo zamani pasipo sheria; lakini ilipokuja ile amri, dhambi ilibuika, mimi nikafa. Na ile amri iliyoletwa iwe uzima, nimeona ya kuwa ilileta mauti. Kwa maana dhambi ilipata nafasi kwa ile amri, ikanidanganya, na kwa hiyo ikaniua.

Paulo, kama mfano (yaani si lazima kama jambo alilopitia yeye mwenyewe, kwa maana kama Farisayo huenda hakuwahi kuishi “pasipo sheria”), anaonyesha tena kutolewa kwa sheria: “... lakini ilipokuja ile amri”.

Mwanadamu hajui dhambi bila sheria, kwa sababu hawezi kuitambua. Akipewa sheria, matendo ya dhambi yanafunuliwa kwake zaidi na zaidi: Kwa maana hii “dhambi ilihuika”. Zaidi ya hayo, kwa jumla matendo ya dhambi yanatendwa zaidi, kwa sababu dhambi inachochewa na sheria, na kwa asili yake inatenda kinyume cha sheria.

Kwa hiyo kuna hali ambazo dhambi inahuika, ingawa muumini hataki hivyo hata kidogo (kwa maana anataka kuitii sheria). Hapo anajiona kana kwamba anakufa. Analijua neno linalosema kwa maana hii: “Fanyeni haya, nanyi mtaishi!” Lakini bila nafasi yoyote ya kufaulu anaikubali hukumu ya sheria juu yake na “kufa”. Kufa huku si kifo cha Yesu Kristo, kinachotuweka huru mbali na dhambi na sheria (wala si kufa pamoja na Kristo); ni kifo kinachojumlisha kushindwa kwote na udhaifu wote mbele ya sheria.

Pamoja na kushindwa huku, inaweza kumaanishwa pia kifo kwa njia ya sheria, kama Paulo anavyosema: Kwa njia ya sheria ameifia (sheria). Dhambi inaua. Amri ya Mungu haionyeshi tu jinsi ninavyoitikia kwa uasi, bali pia kwamba matokeo ya uasi wangu ni mauti – bila njia ya kuepuka. Kwa maana hiyo dhambi inaua.

Dhambi ni adui aliyeitumia sheria kwa faida yake. Dhambi ilidanganya vipi? Je, ilimdanganya Mkristo na kumshawishi ajikaze kwenye sheria kama kanuni ya maisha, ambayo eti sasa, akiwa Mkristo, angeweza kuitimiza? Maneno kadhaa katika sura hii yanatufanya tufikirie hali ya bustani ya Edeni, ambako pia alikuwepo yule aliyedanganya, mwongo tangu mwanzo.

Si sheria iliyoua; dhambi ndiyo iliyoua. Katika kifungu hiki inahusu kuitetea sheria ya Mungu. Ilitolewa iwe uzima, lakini mwanadamu lazima akiri kushindwa kwake: Hawezi kuishika sheria kwa kiwango cha kumfanya kuwa mwenye haki mbele za Mungu.

Katika Biblia sheria haionekani tu katika mwanga huu “hasi”. Kama inavyoonekana mara nyingi katika Agano la Kale (fikirieni tu Zaburi 19 na 119), sheria ilikuwa zawadi ya pekee kwa Israeli. Sheria ilikuwa baraka kubwa. Katika Warumi 7 kazi maalumu ya sheria ya kuijulisha dhambi inasisitizwa, inayoonyesha kushindwa na kukosa uwezo kwa mwanadamu. Hiyo ndiyo maana

ya mwanga “hasi”: Sheria ni njema, lakini haisaidii, kwa sababu mwanadamu si mwema.

Maswali yanayoulizwa hapa hayapatikani hivyo katika Agano la Kale. Kuwatwika Wakristo sheria kulikuwa udanganyifu wa Wayahudishaji (waliotaka kuwalazimisha Wakristo desturi za Kiyahudi), waliomfuata Paulo kila mahali ili kuyachanganya makanisa aliyoyaanzisha.

Ni pale tu Injili ya neema ilipoanza kuenea ndipo mgogoro huu ulipoanza kati ya ya kale na mapya, kati ya sheria ya Musa na neema ya Injili. Jambo hili lilimsukuma hasa Paulo, aliyekuwa mjuzi wa sheria aliyethibitika, kusimama wazi kabisa katika nyaraka zake kwa Warumi, Wakorintho, Wagalatia na Wakolosai “dhidi ya” sheria ya Musa kama njia ya wokovu na kanuni ya maisha ya Mkristo.

6.8.4 Mstari wa 12: Hata hivyo sheria ni njema

Basi sheria ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya baki, na njema.

Tatizo si sheria, bali dhambi iliyo ndani ya mwanadamu. Sheria ina sifa zote alizo nazo Mungu mwenyewe kama Mtoaji wa sheria.

Muhtasari huu unaonyesha wazi chanzo cha sisi kuifia sheria na kuwa tangu sasa chini ya neema: Si ubora wa sheria, bali kushindwa kwa mwanadamu kuishika.

6.8.5 Mstari wa 13: Kwa mara nyingine – kazi ya sheria

Basi je! Ile iliyo njema ilikuwa mauti kwangu? Hasba! Bali dhambi,³⁰ ili ionekane kuwa dhambi, ilinifanyia mauti kwa ile iliyo njema, ili kwa ile amri dhambi izidi kuwa mbaya mno.

Hata hivyo swali linazuka: Sheria ya Mungu, yaani mapenzi ya Mungu, inawezaje kumaanisha kifo changu? – Jibu: Si sheria inayoleta mauti; la, dhambi ndiyo inayoleta. Dhambi haikandamizwi wala haifunikwi na amri iliyo njema, bali inafichuliwa.

30. Maneno ya mstari huu, ambayo mahali hapa katika tafsiri kadhaa za Biblia za Kijerumani (miongoni mwake pia Elb na ER) hayaleti sentensi kamili, yanapaswa kueleweka hivi: “Basi je! Ile iliyo njema ilikuwa mauti kwangu? Hasba! Bali ilikuwa dhambi ...” (taz. kwa mfano Schlachter, Schl 2000 na Menge).

Je, dhambi inaweza kuwa mbaya zaidi kuliko ilivyo? – Dhambi haiwezi kufanywa mbaya zaidi kuliko ilivyo tayari, lakini hapa inahusu swali la jinsi tunavyoiona na kuipima dhambi. Mtu anaweza kuifanya dhambi ionekane ndogo, anaweza kuilevya dhamiri yake. Lakini sheria takatifu ya Mungu inanirudishia namna sahihi ya kuiona na kuipima dhambi. Kusudi la sheria ni kuiona dhambi kama Mungu anavyoiona, ili kunisukuma kwa Mwokozi.

6.9 Warumi 7:14-25: Uzoefu wa Mkristo aliye chini ya sheria

6.9.1 Mistari ya 14-15: Nia njema na tabia ya mwili iliyo dhaifu

Kwa maana twajua kwamba sheria ni ya rohani; bali mimi ni wa tabia ya mwili, nimeuzwa chini ya dhambi; kwa maana silijui (sikubaliani na) nifanyalo; kwa sababu lile nilipendalo silitendi, bali lile nilichukizalo ndilo nilitendalo.

Sasa mwanga wa tochi unahama kutoka kwa sheria na kumwangazia mwanadamu. Sheria ni ya rohani: Inatoka kwa Mungu. Lakini mwanadamu ni wa tabia ya mwili: Hali yake, yaani asili ya mwanadamu, ina dhambi. Anajua kwamba ameuzwa chini ya dhambi, ameachwa peke yake kama Yusufu katika kisima chenye giza. Mwanadamu amenaswa katika mgongano ambao hana maelezo yake. Haelewi kwa nini kila kitu kinakwenda tofauti na anavyotaka. Kwa maana alikuwa amemchagua Mungu na sheria yake. Lakini sasa kwa nini hivi: Hawezi kutenda anachotaka (yeye anayetaka kumtumikia Mungu), na analazimika kutenda kinyume chake. Hili ndilo hasa linaloonyesha nguvu na udikteta wa dhambi, ambayo “ameuzwa” chini yake.

6.9.2 Mstari wa 16: Kukubaliana na sheria

Basi ikiwa nakitenda lile nisisilipenda, nakiri ya kuwa sheria ni njema (bora kabisa).

Katika hali hii mwanadamu analazimika hata kukubali kwamba sheria ni bora kabisa, ya rohani na njema. Kujijua kwa mwanadamu kunaongezeka hatua kwa hatua. Mwanadamu anaitetea sheria, na kwa hiyo anamtetea yeye aliyeitoa. Sasa anaweza kukibaini chanzo cha ubaya. Hataki kuta mahali popote tu, bali ndani yake mwenyewe:

6.9.3 Mistari ya 17–21: Dhambi ikaayo ndani yangu

Basi sasa si mimi tena nifanyaye, bali ni dhambi ikaayo ndani yangu. Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya tabia yangu ya mwili, halikakai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema sipati (sikubaliani nalo). Kwa sababu lile jema nilipendalo silitendi; bali lile baya nisololipenda ndilo nilitendalo. Lakini ikiwa nalitenda lile nisololipenda, si mimi tena nilitendaye, ila ni dhambi ikaayo ndani yangu. Basi nimeona sheria hii kwangu, ya kuwa mimi, nitakaye kutenda lililo jema, ubaya upo kwangu.

Chanzo cha ubaya kimebainishwa: dhambi ikaayo ndani ya mwanadamu. Katika sura ya 5:12 Paulo anaeleza jinsi dhambi ilivyoingia ulimwenguni kwa njia ya Adamu. Hapa inaelezwa kama kanuni inayokaa ndani ya mwanadamu tangu siku ile. Dhambi si kanuni isiyo halisi katika ulimwengu unaonizunguka, ambayo mtu anaweza kuikimbia (kwa mfano katika nyumba ya watawa). Dhambi imejipatia haki ya kukaa ndani ya mwanadamu, moyoni mwake. Dhambi yenyewe ndiyo inayotenda ubaya. Mtu anayeelezwa hapa katika Warumi 7 amekibaini chanzo. Lakini hautupi wajibu wa dhambi yake kwa mwingine, kana kwamba hahusiki nayo. Dhambi haibebi wajibu; mwanadamu mwenyewe anawajibika kwa yale anayoyatenda na anayoyaacha. Ndani yake inakaa dhambi, na kwa hiyo katika tabia yake ya mwili hakuna “jema” (ER) linaloweza kupatikana. Kujijua huku kumekuja kwa njia ya sheria.

Lililo jema ni kuishika sheria. Hapa kimsingi inazungumzwa juu ya sheria ya Mungu, yaani sheria ya Musa. Lakini kila kanuni ninayojitwika mwenyewe kama sheria ina matokeo yaleyale ya sheria (taz. namna ya kusema “sheria” bila kibainishi katika 7:8-9). Sura hii inamhusu mtu aliyezaliwa mara ya pili, anayejikweka kanuni njema na sahihi ili kumpendeza Mungu. Lakini kosa lake ni kwamba anajaribu kuzitimiza kanuni hizi (sheria ya Mungu) kwa nguvu zake mwenyewe, na kwa kufanya hivyo anaichokoza dhambi iliyo ndani yake, bila kuuelewa uhusiano huo. Anayejikweka chini ya kanuni ya “lazima”³¹ anajitazama mwenyewe na kanuni zake, bila kumtazama Kristo na nguvu ya Roho.

31. H. P. Medema, *Der Brief an die Römer*, uk. 111.

6.9.4 Mistari ya 22-23: Sheria mbili na matokeo yake

Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani; lakini naona sheria nyingine katika viungo vyangu, ikipigana na sheria ya akili yangu, na kunifanya mateka wa sheria ya dhambi ikiyo katika viungo vyangu.

“Kujichunguza” huku hakuishii tena katika kuitambua dhambi ikaayo ndani, ambayo haipo tu, bali pia inajilazimisha kwa kanuni yake. Kwa maana kama vile kuna chanzo cha ubaya, ndivyo lazima pia kuwe na sababu kwa nini mtu huyu anafurahia yale yatokayo kwa Mungu. Chanzo chake ni kuwepo kwa “utu wa ndani”. Utu huu unasimama mkabala na dhambi, na – kwa kupatana na mistari mingine inayolingana (Waefeso 3:16; 2 Wakorintho 4:16), ambapo pia “utu wa ndani” unazungumzwa – unawakilisha uzima mpya wa muumini. Utu wa ndani haupingani tu na utu wa nje, yaani mwili. Kwa “utu wa ndani” haimaanishi tu nafsi au roho, kwa maana hivyo kila mwanadamu anayezaliwa anavyo. Utu wa ndani haupaswi kueleweka kwanza kwa mtazamo wa jinsi mwanadamu alivyo (kianthropolojia), unaoeleza upande wa ndani wa mwanadamu.³² Bali utu wa ndani unapaswa kueleweka kwa mtazamo wa wokovu (kisoteriolojia). Wokovu bado haujaushika mwili wetu; kwanza tulipewa uzima wa kiroho, ambao bado hauonekani kwa nje. Ukamilisho wa mwili utatokea tu katika ufufuo au katika kubadilishwa. Hapa jambo jipya limeanza ndani ya mtu huyu, linalomtafuta Mungu. Amezaliwa mara ya pili.

Utu wa ndani una “akili” (kwa Kiyunani *nous*, yaani akili ya kufikiri). Ni fikira zilizofanywa upya na Roho Mtakatifu. Kwa akili hii ya kufikiri ni sheria ya asili kutaka kile ambacho Mungu anataka. Lakini dhambi, hapa kama adui mshindi ndani ya mwanadamu, ina nguvu zaidi. Nayo imeleta “kanuni ya asili” yake. Dhambi inatenda dhambi; hiyo ndiyo sheria yake (kanuni yake). Jambo hili linasikiwa na mtu aliyekata tamaa, kama mstari unaofuata unavyosema:

6.9.5 Mstari wa 24: Kukata tamaa

Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?

32. Jürg Buchegger, *Der neue Mensch in Christus und seine tägliche Erneuerung*, uk. 199, katika: *Ein Mensch – was ist das?*, Wuppertal, 2004.

Kujichunguza kwa mwanadamu kunafika mwisho, na kunatokea kilio hiki cha mateso. Hataki tu kuuacha mwili wake, kana kwamba suluhisho la Wagiriki wa kale ndilo jibu la tatizo la dhambi. Suluhisho hilo lilikuwa kuuona mwili kuwa chanzo cha uovu wote, na kuutafuta uhuru katika roho. “Mwili wa mauti” ni mwili wa mwanadamu chini ya utendaji wa dhambi, inayoenea na kuutawala uwepo wake wote wa kibinadamu.

Mwili wa mauti, kama mwili wa dhambi katika sura ya 6, kweli ni mwili wa kimwili wa mwanadamu. Kwa sababu ya dhambi umeandikiwa mauti (Warumi 8:10-13). Tofauti na suluhisho la Kiyunani ni kwamba Mkristo anaukubali mwili (ingawa umeandikiwa mauti) na kuutoa kwa Bwana. Anaweza kufanya hivyo kwa sababu sasa Kristo mwenyewe anakaa katika mwili huu kwa njia ya Roho Mtakatifu. Suluhisho la mwisho kisha liko katika ufufuo wa mwili (si katika kutoka nje ya mwili); lakini kwa sasa mwanadamu anaruhusiwa kwa Roho kuyafisha matendo mabaya ya mwili (Warumi 8:12-13).

Kwa kilio hiki kilichopo hapa, mtu huyu hatamani tu ukombozi, bali zaidi ya yote Mkombozi! Andiko la sheria lilidai bila hisia, bila kutoa nguvu. Mkombozi, Bwana wetu Yesu Kristo, ndiye aliyetoa uhai wake kwa neema na upendo kwa ajili ya kila mtu binafsi, naye anatoa nguvu (Wafilipi 4:13; 2 Wakorintho 12:9 n.k.).

6.9.6 Mstari wa 25: Somo la Warumi 7

Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu! Basi, kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa tabia ya mwili sheria ya dhambi.

Kwa mara ya kwanza Mwokozi anatajwa kwa jina. Huu ndio ufunguo wa mlango wa gereza lile kuu, ambamo muumini amejifungia mwenyewe. Ikiwa yuko mmoja anayeokoa kutoka katika hali hii, ni Yesu Kristo, Bwana wetu. Jambo hili linaonyesha kwamba ni muumini anayemzungumzia Bwana wake. Sasa hatimaye mwelekeo na lengo ni sahihi. Kuliko katika sura nyingine yoyote ya Biblia, katika Warumi 7 tunasoma “mimi” na “mimi” na tena “mimi”. Hapo ndipo lilipo tatizo. Huenda Paulo aliuchagua mfano huu hivi kwa makusudi, ili kuonya kwa uwazi mkubwa dhidi ya njia ya “mimi” na “nafsi yangu” na ya sheria. Maadamu tunakazia macho vita vyetu wenyewe vya ndani, hatuwezi kumwona Kristo na kuifuata njia ya Roho. Mkristo aliyekata tamaa sasa hatupi

tena nanga ndani ya mashua yake mwenyewe kama hapo awali, bali anaizamisha ndani ya Yesu Kristo.³³

Shukrani hii ya ghafla ndiyo badiliko katika taabu. Kushukuru kunamaanisha: Si mimi ninayefanya kitu, bali mwingine ananitendea kitu. Sura ya 8 inaonyesha shukrani hii ni kwa ajili ya nini, yaani kwa ajili ya kazi ya wokovu ya Mungu katika Kristo, iliyotatua si tu tatizo la hatia yangu, bali pia “tatizo langu la dhambi”. Kile nilicho kwa asili kiliondolewa na kukomeshwa. Kupanda kwa taabu juu ya mlima Sinai, mlima wa sheria, kumekwisha. Golgotha, na neema iliyotolewa pale kwa ajili ya wokovu na uzima, sasa ndiyo lengo!

Mwisho wa sura ya 7 unaziweka mkabala asili mbili zilizomo ndani ya muumini (7:25). Lakini mahali hapa si vita vya kudumu vya kila siku kati ya tabia ya mwili na Roho (kama vinavyoelezwa katika Wagalatia 5), bali ni utambuzi muhimu unaofungua njia mpya kwamba ndani ya muumini kuna kanuni mbili. Kuna kanuni mbili ndani yangu: Kwa upande mmoja – kwa tabia ya mwili – ninaitumikia dhambi. Chanzo cha kanuni hii sasa kimetambulishwa wazi: Ni dhambi ikaayo katika tabia yangu ya mwili. Kwa upande mwingine – kwa akili ya kufikiri iliyofanywa upya – ninaitumikia sheria ya Mungu. Chanzo hiki pia kinaeleweka: Ni utu wa ndani – uzima mpya uliotolewa na Mungu.

Tabia ya mwili ni nguvu inayoendesha ile “nafsi ya zamani”, isiyomcha Mungu na inayoshikamana na mambo ya dunia hii, ya majira haya ya sasa – naam, ya yote ambayo dhambi imeleta. Akili ya kufikiri ndiyo chombo ambacho kwa njia yake utu wa ndani unataka kuitenda sheria ya Mungu. Katika 7:25 Paulo anaufupisha mtanziko huu: Kwa njia ya fikira zilizofanywa upya anaifurahia sheria ya Mungu; kwa njia ya tabia ya mwili anaitumikia kanuni ya dhambi. Ni mtu mwenyewe, ile “mimi”, anayetumikia ama upande mmoja ama mwingine, tena akibeba wajibu kamili kwa uamuzi wake. Kwa hiyo tunaweza kuzungumza juu ya uwezo au nguvu mbili³⁴ ninazozitumia kwa yote ninayoyatenda. Mojawapo ya aina hizi mbili za uwezo inatenda kazi siku zote; hakuna kitu kisicho upande wowote. Kila tendo (kwa ufupi, kila kitu ninachofikiri na kutenda) linaamuliwa na mojawapo ya aina hizi mbili za uwezo. Basi, uwezo wa Roho unapenyaje na kushinda katika maisha yangu?

33. William MacDonald, *Kommentar zum NT*, Juzuu 1, uk. 641.

34. Charles C. Ryrie, *Ausgewogen statt abgehoben*, Dillenburger 1994, uk. 43. Neno la Kiingereza “capacity” lina pia maana ya “uwezo”.

Tuna hamu ya kuona jinsi Paulo atakavyojibu na njia gani atakayoionyesha. Lakini tunaweza kulitanguliza jibu na kulieleza kwa sentensi moja hivi: Kile ambacho sheria haikuweza kukifanya, sasa Kristo ametufanyia (kama tukio halisi la kihistoria), na Roho “anakitimiza” leo ndani yetu (kama uzoefu halisi).³⁵

35. Gordon Fee, *Der Geist Gottes und die Gemeinde*, Metzingen, 2005, uk. 188.

7. Warumi 8:1-11: Huru hatimaye!

Mfululizo wa hoja katika sura tano za kwanza, juu ya haki ya Mungu kwa upande mmoja na juu ya hatia na dhambi ya mwanadamu (awe Myahudi au mtu wa mataifa) kwa upande mwingine, uliongoza kwenye wokovu kwa damu ya Kristo (3:23-25). Mungu alimtoa Mwanawe kuwa dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. Damu ya Yesu inatimiza dai la haki la Mungu. Lakini Mungu, baada ya Yesu kujitoa kuwa dhabihu kwa ajili yetu, alimfufua kutoka kwa wafu kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu. Sasa Mungu, Hakimu mtakatifu na mwenye haki, anamhesabia haki yule anayemwamini Yesu Kristo *na* kumwamini Mungu aliyemfufua kutoka kwa wafu. Katika sura ya 5:1 Paulo anafupisha:

Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, tuna amani na Mungu!

Hadi hapo mtu angeweza kufikiri kwamba kilele cha waraka kimefikwa, hivi kwamba kilele kingine karibu hakiwezekani tena. Lakini kisha Paulo anachukua tatizo lililo ndani zaidi. Kuanzia 5:12 haihusu tena hatia na upatanisho kwa ajili ya dhambi, bali asili ya kimaadili ya mwanadamu. Inahusu dhambi kama nguvu na kama kanuni iliyoungana na kila mwanadamu bila kutenganishwa. Kile ambacho mtu *ametenda* anaweza kusamehewa. Lakini kile *alicho* (kwa mtazamo wa kimaadili) hakiwezi kusamehewa, kwa sababu kwa kufanya hivyo dhambi ingehesabiwa haki.

Katika sura ya 5 Paulo anaeleza chanzo na utendaji wa dhambi, katika sura ya 6 kuwekwa huru mbali na dhambi. Katika sura ya 7 Paulo amezungumzia uhusiano wa sheria na Mkristo. Katika nusu ya pili ameeleza uzoefu wa mtu ambaye tunaweza kudhani kwamba ni mtoto wa Mungu. Mkristo huyu anajaribu, kwa nia njema, kumpendeza Mungu kwa kuifanya sheria kuwa kanuni ya maisha yake. Lakini amesahau jambo la msingi: Mkristo ameifia sheria, kama vile alivyoifia dhambi. Hajaelewa kwamba sheria ya Sinai inasimama badala ya “mfumo” mzima, ambamo kanuni ya kustahili kwa matendo inatawala. Lakini sheria ilitolewa hasa ili kuthibitisha udhaifu na kushindwa kwa tabia ya mwili. Imeonyesha wazi kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi na anahitaji Mungu aingilie kati. Kwa njia ya sheria dhambi ilihuiika (7:9); kwa njia ya sheria dhambi ilizidi kuwa mbaya mno (7:13). Muumini akijihusisha na hali hii ya zamani ya

andiko, ataishia katika kukata tamaa, kwa maana dhambi iliyo ndani yake itakuwa na nguvu kuliko nia yake iliyofanywa upya.

Maneno “Ole wangu, maskini mimi!” yanatoka katika kutambua kwamba dhambi haiwezi kushindwa. Katika Warumi 7 Mkristo anajiona mwenyewe tu; haoni kwamba katika Kristo amehesabiwa haki, ameoshwa na ametakaswa. Hajautambua utambulisho wake mpya katika Kristo. Anayeutambua utambulisho wake mpya (kama ulivyoelezwa katika sura ya 8) hahitaji tena kusema: “Ole wangu, maskini mimi!” Hata hivyo: Kila mara anapojikwaa, au anapotenda dhambi, na hivyo “tendo la tabia ya mwili” (Wagalatia 5:19) linakuwepo kwake, anapaswa kulihukumu jambo hilo kwa unyoo mbele za Mungu na kuliungama. Kila maungamo ya kweli ya dhambi yanaambatana na huzuni na majuto. Hili ni sehemu ya ukuaji wa kiroho, tena ni sharti lake.

Warumi 8 inatufungulia mlango wa uzima kwa upana: kuachiliwa huru katika Kristo na uhuru katika Roho kama wana na watoto wa Mungu, tukiwa njiani kuelekea utukufu. Bado hatujafika; bado tuko katika mwili wa mauti na katika uumbaji uliowekwa chini ya uharibifu.

7.1 Tayari sasa – bado

Tumeokolewa katika tumaini (Warumi 8:24-25; ER, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani). Kuhesabiwa haki kwetu, kulikutufanya kutoka kuwa wenye dhambi hadi kuwa wenye haki, ni hakika, lakini kunapatikana kwa imani tu. Kile tulicho nacho kwa imani ndicho kile “tayari sasa”. Lakini ni wazi kwamba bado hatujaufikia ukamilifu. Lililo zuri kuliko yote bado linakuja, nalo ndilo tunaloliita “bado”.

Nyakati mpya za Kristo: Uzima wa milele, kazi ya Roho, neema, uhuru, ufufuo, kufanywa upya, amani, haki, ukamilisho

Kuja kwa kwanza kwa Kristo na kazi yake kunatimiza kile “tayari sasa”: kuhesabiwa haki, kipawa cha Roho

Maisha ya duniani katika imani na tumaini – Tayari sasa – bado

Nyakati za sasa

Kuja kwa pili kwa Kristo kunatimiza kile “bado”:

- Utukufu utakaokuja 8:18
- Kufanywa wana, yaani ukombozi wa mwili wetu 8:23
- Uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu 8:21
- Uumbaji umewekwa huru 8:21

Nyakati za Adamu: Dhambi, mauti, tabia ya mwili, sheria, utumwa, kuharibika, uharibifu, ubatili

Mchoro huu unakusudia kuonyesha wazi tofauti hii inayoonekana kuwa mgongano, na mvutano uliopo kati ya pointi hizi mbili. Duara ndilo eneo ambamo zinapishana, ambapo nyakati za Adamu bado hazijakoma, lakini zile za Kristo zimekwisha kuanza. Katika wakati huu watu wa Mungu wamekwisha kupewa uzima wa wakati ujao, wakati huohuo ukamilisho bado unangojewa.

Wakati huu wa imani, wa tumaini na wa kuvumilia katika imani unaambatana na maagizo ya wokovu (yale tunayoagizwa kutenda kwa sababu ya yale ambayo Mungu ameshatenda; kwa Kijerumani *Heilsimperativ*). Faraja zake, maonyo yake na maelekezo yake ya msisitizo yanatuhusu, nayo yanatakiwa kututia moyo kudumu hadi mwisho, ili tuweze kuimaliza mbio ndefu yote ya imani. Neema ya Mungu, kwa Roho wake, itatuwezesha kulifikia lengo. Hii ndiyo mada ya sura ya 8. Tumaini letu linahuika tunapokizingatia kwa uwiano ule *tayari sasa* – bado kwa Paulo na katika Agano Jipya lote. Sura ya 6 – 8 ni mfano ulio wazi wa wazo hili kuu.

Ukweli wa wokovu (yale ambayo Mungu ameshatenda; kwa Kijerumani *Heilsindikativ*) unalingana na *tayari sasa*, yaani na yale ambayo tumekwisha kupokea. *Agizo la wokovu* linaelekeza macho kwenye yale ambayo *bado* hayajawa, lakini tutayafikia: utukufu wa uzima wa milele na uumbaji uliowekwa huru. Wokovu wa Mungu hauondoi kutenda, kuamua na kuvumilia kwa mwanadamu. Tunapaswa kuwa kile tulicho. Onyo na ahadi, mawaidha na uhakikisho vinasimama kando kwa kando, wala havipingani kamwe.

7.2 Kupenya kizuizi

Huenda sura ya 8 ndiyo kilele “cha juu kabisa” katika waraka huu, na mojawapo ya vilele vya juu kabisa katika Biblia nzima. Baada ya kuwekwa huru mbali na dhambi kuelezwa kikamilifu, Paulo anaonyesha njia ya waliowekwa huru itaelekea wapi, na kupitia hali gani za maisha, ili kulifikia lengo la Mungu (ukamilisho).

“Sura hii inatuongoza katika mduara wa ndani kabisa na hadi moyoni mwa Ukristo; inazungumzia hali ya pekee ya heri, furaha iliyo safi kabisa na iliyofikia ufahamu, ambayo ulimwengu hauwezi kwa njia yoyote kutoa hata kitu kinachofanana nayo kwa mbali.”³⁶

36. C. J. Ellicott na W. Sanday (wahariri), *A Bible Commentary for Bible Students*, uk. 233.

7.3 Mstari wa 1: Kuachiliwa huru – hakuna tena hukumu ya adhabu

*Sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu (hakuna hukumu ya kulaaniva) juu yao walio katika Kristo Yesu.*³⁷

Hii ni mojawapo ya sentensi kubwa zaidi na zenye maana nyingi zaidi katika Biblia. Neno hili linafukuza kila hofu. Ni kelele ya shangwe katika ulimwengu uliopotea unaoelekea hukumuni. Kwa watu wanaoteswa na kukata tamaa kwa sababu ya kuijua dhambi yao, habari njema hii ina matokeo ya msingi kabisa kwa maisha: kuwekwa huru, amani, uhakika na usalama. Mahali hapa, au nafasi hii katika Kristo, ni salama kuliko handaki lolote la kujikinga na bomu la atomiki. Hakuna kitu kinachoweza kutupata katika Kristo, kwa sababu kingempata yeye kwanza. Naye anaweza kukabiliana na kila kitu. Hapa ni hukumu ya adhabu ya Mungu, ambayo ingetupata kwa haki kama yeye asingeichukua juu yake. Na kwa sababu tuko ndani yake na tutabaki ndani yake milele, tunapita katika maisha ya kila siku tukiwa na uhakika huu. Maswali yote ya kisheria yamejibiwa. Si tu kwamba tumewekwa kuwa wenye haki, bali tumeunganishwa na Kristo bila kutenganishwa: Kuwa katika Kristo maana yake si kingine ila kwamba Mungu, anapotutazama kutoka juu, hatuoni sisi, bali anamwona Kristo.

Tamko hili la msingi linatuhakikishia kwamba hukumu ya wakati ujao siku ya hukumu, na adhabu ya milele, kwetu sisi tulio katika Kristo zimehamishwa kutoka wakati ujao hadi wakati uliopita: Hukumu yetu imekwisha kutolewa.

Hukumu hii ya adhabu haikufutwa wala kubatilishwa kwa sababu tu Mungu ana neema kwetu. Asili ya Mungu haibadiliki. Hatauaacha wala kuukana kamwe utukufu wake, utakatifu wake na haki yake. Basi kwa nini hakuna hukumu ya adhabu kwa wale walio katika Kristo? – Kwa sababu hukumu ya adhabu juu yetu, yaani juu ya utu wetu wa zamani, ilitekelezwa juu ya Kristo (6:6; 8:3). Ilimpata yeye, si sisi. Ulinzi dhidi ya hukumu ya adhabu hauko katika ukweli kwamba Yesu alikuwa mkamilifu katika maisha yake na alitimiza sheria. La, hukumu ya adhabu haikupaswa kutamkwa tu, bali pia kutekelezwa, jambo

37. Kuna nakala za maandishi ya kale zinazoshuhudia tafsiri ifuatayo: *Basi sasa hakuna hukumu yoyote juu ya wale walio katika Kristo Yesu; (wao ni) watu wasioenenda kwa kufuata tabia ya mwili, bali kwa kufuata Roho.* Wale walio katika Kristo hawapati nafasi yao kwa sababu ya kuenenda kwao kwa kufuata Roho: Bali matokeo ya kimantiki ya kuwa katika Kristo ni kuenenda kwa kufuata Roho. Mara nyingi nafasi na hali vinatenganishwa mbali sana isivyo haki – jambo ambalo Paulo asingielewa. Tafsiri hii inalingana kabisa na umoja wa ukweli wa wokovu na agizo la wokovu. Kwa hiyo haihusu kuokolewa kwa matendo, bali kubadilika kwa maisha kama matokeo ya kawaida ya kuokolewa.

lililotokea msalabani na katika kifo cha Yesu. Si maisha yake matakatifu, bali kifo chake ndicho wokovu wetu.

Siku moja kila mwanadamu atalazimika kuingia mbele za Yeye aliye wa milele. Hiyo ndiyo siku ya ghadhabu na siku ya kufunuliwa kwa hukumu ya haki ya Mungu (Warumi 2:5). Siku hiyo mambo ya siri ya wanadamu yatahukumiwa (Warumi 2:16). Sisi sote tutasimamishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, na kila mmoja atatoa hesabu ya nafsi yake (Warumi 14:10). Wakati wowote saa hiyo itakapofika, sisi tuko katika Kristo. Tayari sasa tumefanywa kuwa wenye haki, hivi kwamba hatuhitaji kuogopa saa hiyo. Hatuna kesi ya mahakama ya kungojea. Hukumu imekwisha kufanyika. Ghadhabu ya Mungu (Warumi 1:18) haitupati; tumehesabiwa haki kwa damu ya Kristo, nasi tutaokolewa na ghadhabu (Warumi 5:9).

Kwa imani sasa tunaishika nafasi yetu ya wokovu katika Kristo. Lakini siku hiyo itafunuliwa wazi; hapo itakuwa uhalisi unaoonekana na tunaoupitia: kuachiliwa huru kikamilifu na kukubaliwa kama watoto pale mbele ya kiti cha enzi cha Mungu! Hapo tutakuwa tumetoka katika kuamini hadi kuona.

Mungu ametuweka ndani ya Kristo (1 Wakorintho 1:30). Huu ndio ulinzi kamili dhidi ya hukumu ya Mungu, lakini wakati huohuo pia ndio mwanzo wa uzima mpya kabisa ndani ya Yeye aliyefufuka. Kwa mada hii, ambayo yeye hasa anaishughulikia, Paulo anatumia usemi “kuwa katika Kristo”³⁸. Hiki ndicho kiini cha imani ya Kikristo, uhusiano wa karibu kabisa na Kristo, ambaye sasa yuko katika kiti cha enzi cha Mungu. Si chini ya hilo ndilo linalomaanishwa sasa na nafasi ya kisheria ya muumini mbele za Mungu, na vivyo hivyo mazingira yake mapya ya maisha ambamo sasa ameletwa. Jambo hili linaeleza nafasi yake, na pia kuhesabiwa haki na nguvu inayoendesha maisha yake. “Kuwa katika Kristo” maana yake ni “kuishi katika Kristo”. A. T. Pierson aliyalinganisha maneno “katika Kristo” na ufunguo mdogo unaoweza kufungua kufuli kubwa katika lango kuu la jumba la kifalme. Katika Kristo tumeletwa hadi kwenye kiti cha enzi cha Mungu. Huko tumekubaliwa katika Mpendwa, Mwana wa Mungu.

Haihusu hisia, wala juhudi zetu wenyewe, mtu anapotaka kuingia katika nafasi mpya (“katika Kristo”). Mkristo hahitaji kujitahidi ili kuifikia nafasi hii. Hilo lingekuwa kama mtu aliye ndani ya chumba, ambaye hata hivyo angejaribu tena na tena kuingia ndani ya chumba hicho, kama Watchman Nee alivyolinganisha.

38. Zaidi ya mara 190 neno hili na maneno yanayofanana nalo, yanayoonyesha uhusiano wetu na Kristo, yanapatikana katika Agano Jipya.

7.4 Mstari wa 2: Tumewekwa huru kwa sheria ya Roho wa uzima

Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ulio katika Kristo Yesu imeniweka huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti.

Muumini anakuta nini katika Kristo Yesu, katika “nyumba yake mpya”? Anashiriki nini sasa, akiwa katika Kristo? Huko anapata kushiriki nguvu yote ya uzima ambayo Kristo anayo katika ufufuo.

Sheria mbili – au kanuni mbili – zinawekwa mkabala. Nguvu moja inaelekea mautini, nyingine uzimani. Aliyeunganishwa na Kristo anaweza kuishinda dhambi na mauti. Sheria moja imeivunja nyingine, kwa sababu ina nguvu zaidi. Haihusu sheria mbili kukaa kando kwa kando, bali ushindi katika Kristo. Jambo hili linapaswa kuwa uzoefu wa Mkristo kwa vitendo kabisa, kama Paulo anavyoeleza pia katika sehemu inayofuata. Lakini kwanza ushindi lazima uwe umepiganiwa na kupatikana, ili mtu aweze kuidai kabisa sheria kama hii ya Roho wa uzima. Si Mkristo anayepaswa kupigana vita hivi; mwingine ameupigania ushindi huu kwa ajili yake: Kristo.

Sheria ya dhambi na mauti imelinganishwa na kanuni ya mvutano wa dunia. Ndege anaishinda kanuni hii kwa kanuni ya aerodinamiki. Ndege haanguki chini, bali anaruka popote anapotaka. Kuruka ni uwezo alio nao kwa asili yake, bila kujikaza kwa nguvu kwa ajili ya hilo. Hajui kwamba kwa kufanya hivyo anaivunja kanuni ya mvutano wa dunia. Anafanya kile alichoumbiwa. Vivyo hivyo sheria hii ya Roho wa uzima imemweka Mkristo huru, nayo inaendelea kutenda kazi ndani yake daima. Roho Mtakatifu ndiye anayetoa uhuru huu na kuudumisha ukiwa hai. Mkristo anaweza kuwa na uhakika wa utendaji wa sheria hii, nayo inapaswa – kama kwa ndege – kuwa jambo la kawaida kwake.

Sura ya 8 inamshughulikia hasa Roho Mtakatifu, wakati sura ya 7 inaishughulikia “mimi” wa kibinadamu. Roho Mtakatifu, Roho wa Kristo, ndiye Roho wa uzima. Katika Adamu na katika wazao wake wote ilitenda kazi sheria ya dhambi na mauti. Katika Kristo sasa wanatenda kazi, kwa nguvu kubwa zaidi kupita kiasi, Roho na uzima wa Yeye aliyefufuka.

7.5 Mstari wa 3: Mungu anatatua tatizo la dhambi pale Golgotha

Kwa maana yale ambayo sheria haikuweza kuyafanya, kwa kuwa ilikuwa dhatifu kwa sababu ya tabia ya mwili, Mungu aliyafanya, kwa kumtuma Mwana wake

mwenyewe katika mfano (usawa) wa tabia ya mwili yenye dhambi, na kwa ajili ya dhambi, alihukumu dhambi katika tabia ya mwili ...

Sheria haikuweza kulitatua tatizo la dhambi, wala kutoa uzima na nguvu ya kuishika na kuishi kwa kuifuata. Haikuweza kumfanya mwanadamu kuwa bora zaidi kimaadili wala kumfanya mpya. Tabia ya mwili (nguvu ya asili ya wazao wa Adamu, iliyo kwa hiyo ya dhambi na ya dunia hii) ilikuwa dhaifu na isiyoweza. Lakini Mungu aliweka kila kitu katika mwendo, kwa sababu yeye ni mwenye neema na mwenye rehema. Kile ambacho sisi hatukuweza kukifanya, yeye alikifanya. Ni neno lililoje linaloweza huru, ambalo katika muktadha huu linawahusu hasa wale ambao bado wanataka kufanya jambo wao wenyewe na wanajiweka chini ya shuruti ya kutenda na ya “lazima”!

7.5.1 Mungu anakuwa mwanadamu

Hilo ndilo Mungu alilofanya. Huu ndio mwisho wa kudumu wa kila kitu ambacho wanadamu wanaweza au wanataka kufanya. Mungu anafanya jambo kuu mno, lisiloweza kufikirika: Alimtuma Mwana wake pekee. Hakutuma malaika, wala mwanadamu. Alimtoa Mwana wake, ambaye ameunganika naye katika upendo usio na mwisho na ushirika wa milele. Mungu Mwana alifanyika mwanadamu. Hakuzaliwa ndani ya “tabia ya mwili yenye dhambi”, bali alitumwa katika “usawa” wa tabia ya mwili yenye dhambi. Alifanana na wanadamu, lakini bila dhambi. Bila dhambi, lakini alitumwa *kwa ajili ya* dhambi. Kazi yake ya Kimungu ilikuwa kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi. Usemi “kwa ajili ya dhambi” mara nyingi unatumika katika Agano la Kale kwa sadaka ya dhambi. Dhabihu hii hasa ndiyo aliyopaswa kuwa, kwa sababu dhabihu zote hadi wakati ule ziliweza tu kuwa ukumbusho wa dhambi! Kwamba angekuwa dhabihu hii ya mara moja tu kwa ajili ya dhambi, alilifahamu kila saa ya maisha yake yasiyo na dhambi.

Neno alifanyika mwili, lakini bila dhambi. Dhambi ilikuwa ndani ya wanadamu wote; asili yake inaitwa “dhambi katika tabia ya mwili”. Kwa Yesu ilikuwa kweli tu kwamba alikuwa katika mwili (katika kuwepo kwa kibinadamu), bila dhambi. Hilo lilikuwa sharti la lazima, lisiloweza kujadiliwa, ili aweze kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi kwa ajili ya wengine.

Usemi “mfano wa tabia ya mwili yenye dhambi” kwa upande mmoja unasisitiza kwamba Mungu Mwana alifanyika mwanadamu kweli (“usawa” hapa

unamaanisha zaidi ya “kufanana tu”, kwa sababu vinginevyo kungekuwa na nafasi ya kuutilia shaka ubinadamu wake wa kweli). Kwa upande mwingine usemi huu unamaanisha kwamba ubinadamu wake haukuwa umeshikwa na dhambi kama ilivyo kwa wanadamu wote.

7.5.2 Golgotha

Jambo lisiloweza kueleweka lilitokea: Mungu aliilaani (aliuhukumu) “dhambi katika tabia ya mwili”, na kwa ajili ya hilo akamchukua Mwana wake kuwa sadaka ya dhambi. Hivyo Mungu alitekeleza juu yake hukumu ya adhabu juu ya dhambi. Kristo alijitwika asili yetu ya dhambi (alijifanya mwenyewe kuwa kile tulichokuwa), akajiweka chini ya hukumu takatifu ya Mungu mahali petu. Mungu hakumhurumia Mwana wake (8:32)! Katika sura ya 6:6 Paulo anasema jambo lilelile: Tumesulubiwa pamoja naye. Katika sura ya 7:4 analieleza kwa maneno mengine (“mliuawa ... kwa mwili wa Kristo”). Msalabani kesi dhidi ya dhambi iliendeshwa, na hukumu ya kifo ikatekelezwa. Mwokozi ameichukua mahali petu hukumu ya adhabu, na pia mauti kama mshahara wa dhambi!

Ingawa yeye ni Mwana wa milele wa upendo wake, Mungu alimtendea msalabani kama mwenye dhambi mkuu kuliko wote – kama yule ambaye juu yake ilikuwa dhambi yote ya wanadamu. Ghadhabu ya Mungu ilimpata bila huruma yule aliyekuwa mtakatifu na mwenye haki, aliyeichukua dhambi. Alifanywa kuwa dhambi (na kuwa sadaka ya dhambi) kwa ajili yetu (2 Wakorintho 5:21). Tukio hili linahusu saa zenye giza kuliko zote katika historia ya wanadamu. Giza la ajabu lililoenea duniani kote, lililotawala siku ile kuanzia saa sita mchana hadi saa tisa alasiri, linashuhudia siri hii. Hakuna aliyeweza kuwa shahidi wa yale yaliyotokea. Mungu anampiga Mwana wake mwenyewe, ambaye kimwili amefika mwisho wa nguvu zake, lakini akiwa na ufahamu kamili anakutana na Mungu mtakatifu. Kisha anautoa uhai wake mautini. Mwokozi analitamka katika ulimwengu wote neno lililo muhimu kuliko maneno yote yaliyowahi kusemwa: “Imekwisha.”

Hivyo tunaelewa kwamba kwa wale walio katika Kristo Yesu hakuwezi kuwa tena na hukumu ya adhabu. Yeye ameichukua juu yake. Alijitoa mikononi mwa utakatifu na haki kamili ya Mungu, kwa kujitwika kile tulichokuwa kwa asili (alama zote za nafasi yetu “katika Adamu”), kana kwamba yeye ndiye aliyewajibika kwa hayo. Kila kitu nilichostahili, alikiondoa juu yangu. Ilikuwa

dhabihu ya Kimungu, nayo inawahusu wote walio sasa katika Kristo. Hili ndilo jibu la Mungu kwa kushindwa kwetu, kwa dhambi yetu na kwa kutoweza kwetu kumtumikia Mungu. Ameweka kuhesabiwa haki kwetu, kutoka katika matendo yetu ya dhambi na kutoka katika dhambi, juu ya msingi ulio wa haki kabisa, na kwa hiyo usioweza kupingwa. Dai la Mungu lilitimizwa. Ili kuumba jipya, ilikuwa lazima kuyahukumu ya kale: Dhambi ilipaswa kuhukumiwa katika mwili wa Yesu (katika Neno aliyefanyika mwili) kwa vipimo vya Mungu mwenyewe, kwa kupatana na haki yake, utakatifu wake na utukufu wake. Kwa hiyo Mungu alitukuzwa kwa kila namna, na madai yake yakatimizwa kikamilifu. Ufufuo na kutawazwa kwa Yesu katika kiti cha enzi ndio uthibitisho wa jambo hili. Mungu amepata pumziko kamili katika kazi ya ukombozi ya Mwana wake.

Lakini tuzingatie lengo la kazi hii ya wokovu ni nini:

7.6 Mstari wa 4: Sheria ya Mungu inatimizwa sasa hata hivyo

... ili maagizo ya haki ya sheria yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata tabia ya mwili, bali kwa kufuata Roho.

Wokovu kwa njia ya kifo cha dhabihu cha Yesu kilichotimizwa sasa unaishia katika maisha yetu ya vitendo, yaani mwenendo wetu. Lengo la wokovu ni kwamba sasa, hata hivyo (tofauti na sura ya 7), sheria inatimizwa na Mkristo. Mstari huu ndio jibu kwa Warumi 7! Baada ya kujifunza sura ya 7 swali lilibaki: Je, sheria ya Mungu haitavuka kamwe kazi ya kuifichua dhambi tu? Kwa kuwa sheria ya Mungu ni ya haki na njema kabisa, ingekuwa sawa na kushindwa kwa Mungu, kama hakuna mtu – isipokuwa Yesu, bila shaka – angeweza kuitimiza. Na ndivyo ilivyo: Sasa wale walio katika Kristo wanaitimiza sheria. Dai la sheria sasa linatimizwa ndani yao, tena kwa njia ya Roho wa Mungu.

Hapa haihusu kila amri ya sheria ya Musa. Tatizo la mwanadamu katika Warumi 7 halikuwa sheria ya ibada, bali sehemu ya kimaadili ya sheria ya Musa. Mtanziko wa hali yake anauonyesha kwa amri ya mwisho kati ya zile Amri Kumi (amri ya kimaadili): “Usitamani!” (7:7; Kutoka 20:17; taz. Kumbukumbu la Torati 5:21). Kwa amri za kimaadili dhambi inafunuliwa (taz. pia Yakobo 2:8-11). Kutamani, au anasa ya tamaa isiyo halali (ya kitu chochote kile), ni jambo tunalokutana nalo kila siku, nalo linaanza moyoni mwetu.

Amri hii sasa inatimizwa na muumini katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Kwa hiyo anaweza kuipinga tamaa na kuishinda. Zaidi ya hayo, atagundua jambo hili:

Anapoifuata njia ya Roho kwa makusudi, tamaa inazidi kupoteza mvuto wake kwake. Hataki tena kumiliki kitu kisicho halali na kilicho mali ya wengine – kile ambacho (kwa vipimo vya dunia) ni kikubwa zaidi, kizuri zaidi na bora zaidi.

Maadili “mapya” ya Paulo, yaani “hali mpya ya Roho” (7:6), hayajengwi kwa kanuni au sheria za zamani wala mpya. Bali katika nguvu ya Roho tayari leo tunaishi maisha ya wakati ujao – maisha yanayoieleza asili ya Mungu mwenyewe, kama tulivyoiuia katika Kristo Yesu. Kipimo cha maisha haya si sheria ya Musa, bali sheria ya Kristo (Wagalatia 6:2), ile kweli iliyo katika Kristo (Waefeso 4:20-22), tunayokutana nayo katika Agano Jipya lote. Bila shaka sheria ya Kristo na sheria ya Musa haziwezi kamwe kupingana, kwa kuwa zina chanzo kimoja na Mwandishi mmoja. Kiini cha sheria ya Musa ni upendo, nao ndio pia kitovu cha sheria ya Kristo. Lakini katika sheria hii ya pili upendo unakwenda mbali zaidi sana: Kristo mwenyewe na upendo wake ndio kipimo.

7.6.1 Sheria ya Musa na uhalali wake

Lazima tutofautishe kati ya “sheria ya milele ya maadili ya Mungu”³⁹ na sheria ya Musa, ambayo uhalali wake ulikuwa na mipaka ya wakati. Sheria ya milele ya maadili ya Mungu ndiyo kanuni kamili ya kile kilicho haki na kisicho haki mbele za Mungu. Ni kielelezo cha asili takatifu na isiyobadilika ya Mungu kwa mwanadamu. Sheria ya maadili ya Mungu imekuwepo siku zote, kwa sababu ndiyo madai ya asili yake ya milele. Wanadamu wanaweza kuishi kwa kupatana na sheria kamili ya maadili ya Mungu bila kuwa chini ya sheria ya Musa.

Hali hii mpya hasa ndiyo Paulo anayoieleza hapa. Mkristo amewekwa huru mbali na sheria ya Musa, kuhusu njia ya wokovu na pia kuhusu kipimo cha maisha. Lakini kwa sababu hiyo yeye si kamwe “asiye na sheria”. Sasa yuko chini ya Kristo, chini ya sheria yake (1 Wakorintho 9:21), na hapo zinatumika angalau kanuni zile zilizomo katika sehemu ya kimaadili ya sheria ya Musa.⁴⁰ Ni kweli kwamba “sheria ya Kristo” (Wagalatia 6:2), kama sheria ya Roho wa uzima (8:2),

39. Ernst G. Maier, *Die biblische Lehre von den Heilszeiten*, Hünfeld, 2007, uk. 80 na kuendelea. Usemi “sheria ya milele ya maadili ya Mungu” haupatikani katika Biblia, kama vile maneno mengine ya kithetologia (Utatu, asili ya zamani na asili mpya, n.k.), lakini unafaa ili kueleza kwa ufupi kweli ya Kibiblia.

40. Amri Kumi katika Agano Jipya: Isipokuwa amri ya Sabato, amri zile nyingine zote tisa (za kimaadili) katika Agano Jipya hazirudiwi tu, bali zinafanywa kuwa kali zaidi na/au zinabadilishwa kutoka katazo kuwa amri chanya! Amri ya 1: 1 Wakorintho 8:4-6; Amri ya 2: 1 Wakorintho 10:7, 14; Amri ya 3: Wakolosai 3:8; Amri ya 5: Waefeso 6:2; Amri ya 6: Mathayo 5:22; 1 Yohana 3:16; Amri ya 7: Mathayo 5:28; Waefeso 5:25; Amri ya 8: Waefeso 4:28; 1 Yohana 3:17; Amri ya 9: Waefeso 4:25; Amri ya 10: Waefeso 5:5; 1 Timotheo 6:10 n.k.

na ile amri (mpya) ya upendo (Yohana 13:34; 15:12 n.k.) zinaungana na sheria ya Musa, wala hazipingani nayo mahali popote; lakini zinakwenda mbali zaidi sana. Sasa waumini wamekuwa wafuasi wa mfano wa Mungu na wa Kristo. Inatumika hii: Enendeni katika upendo, katika upendo wa Kristo, uliojitoa hata mautini (Waefero 5:2)! Hili ni zaidi ya sheria. Hapa sheria ya Musa inabaki nyuma, kwa kusema hivyo, na haiwezi tena kukifuata kiwango kipya katika nuru ya kufunuliwa kwa Mwana wa Mungu na kazi yake ya ukombozi. Huu ni uhusiano, huku ni kufanywa wana, huku ni kuongozwa kwa kila mtu binafsi, huku ni kiumbe kipya (Wagalatia 6:15-16).

Kufunuliwa na kutumiwa kwa kanuni za milele za maadili ya Mungu kunabadilika katika nyakati mbalimbali za historia ya wokovu. Ingawa sheria ya Musa imepoteza uhalali wake, kanuni za milele za maadili ya Mungu zinazoonekana katika sheria ya Musa zinabaki. Kwa maana tunazikuta tena katika sheria ya Kristo. Paulo anatoa mfano katika Warumi 13:8-10. Amri ya uzima mpya ni kwamba tupendane. Kwa hiyo tunaitimiza pia sheria ya Musa, kwa sababu upendo ndio jumla ya sheria (Wagalatia 5:14-15; 1 Timotheo 1:5-11; Mathayo 22:34-40). Jumla hii, yaani upendo, inalingana pia na sheria ya Kristo.

Kwa upande mmoja Kristo ndiye mwisho, lakini pia lengo na utimilizi wa sheria ya Musa (Warumi 10:4). Yeye peke yake ndiye aliyeishika sheria ya Musa kikamilifu. Lakini zaidi ya hapo, katika mwanadamu Yesu Kristo sheria ya milele ya maadili ya Mungu inafunuliwa kikamilifu. Kristo, kama Neno wa milele (Yohana 1:1-3), katika nafsi yake ndiye kielelezo kamili cha mapenzi na sheria ya Mungu. “Sheria ya Kristo” ni ufunuo kamili wa sheria ya milele ya maadili ya Mungu, na kwa hiyo inaipita sheria ya Agano la Kale. Kwa hiyo kipimo cha Mkristo sasa si tena andiko la sheria ya Musa, bali ni Mtu: Kristo mwenyewe ameandikwa miyoni mwetu kwa Roho.

Kwa maneno mengine: Mambo halisi ya agano jipya yanaanza kutumika. Sheria inapandwa miyoni (yaani katika kitovu cha nia na cha maamuzi cha mwanadamu), ili wahusika waweze kuishi kwa kufuata sheria hii kutoka ndani, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Sheria hii haionyeshwi na mwingine yeyote isipokuwa na Kristo mwenyewe (Waebrania 8:10; 10:16; 2 Wakorintho 3:6, 18; Yeremia 31:31-34; 32:40; Ezekieli 36:24-27).

7.7 Mstari wa 5: Kufuata tabia ya mwili au kufuata Roho

Kwa maana wao waifuatao tabia ya mwili buyafikiri mambo ya tabia ya mwili; bali wale waifuatao Roho buyafikiri mambo ya Roho.

Paulo haachi kuiendeleza mikondo ile miwili ya mawazo aliyoianza katika Warumi 5:12. Katika muktadha huu haandiki juu ya kama Mkristo anaishi kiroho au kwa tabia ya mwili. Bado anashughulika na tofauti ya msingi. “Kufuata tabia ya mwili” maana yake ni kuwa bado katika jamaa ya Adamu. Lakini wale “waifuatao Roho” wako “katika Kristo”. Hata hivyo nafasi zote mbili si jambo la kinadharia tu. Maisha, fikira na matendo yanatengenezwa – ama na Roho, ama na tabia ya mwili. Tabia ya mwili inamtengeneza mtu asiyeamini, Roho anamtengeneza muumini.

Tabia ya mwili ni asili ya dhambi ya mwanadamu – kile ambacho amekuwa katika kuwepo kwake kote na namna yake ya maisha kwa sababu ya dhambi ikaayo ndani yake. Mtu asiyeamini ni “tabia ya mwili” (Yohana 3:6). Anaishi kutokana na tabia ya mwili na kwa kufuata tabia ya mwili; anajielekeza kwake mwenyewe na kwa mambo ya dunia hii. Hawezi kufanya vinginevyo, hata kama angetaka. Anaongozwa na tabia yake ya mwili. Nia yake, fikira zake na matendo yake vina alama ya nguvu ya mambo ya dunia hii, yanayoonekana na ya kidunia.

Lakini Mkristo, kinyume chake, “anaufuata Roho”. Hii inamaanisha kwamba Roho amempa wokovu, na kutoka huko anapata chanzo chake kipya: Kilichozaliwa kwa Roho ni roho (Yohana 3:6). Kwa sababu hiyo yanatokea mwelekeo mpya wa maisha, mambo mapya yanayomvutia, na kuyatazama mambo ya milele na ya mbinguni.

7.8 Mistari ya 6-7: Mauti na uzima, uadui na amani

Kwa sababu nia ya tabia ya mwili ni mauti; bali nia ya Roho ni uzima na amani; kwa kuwa nia ya tabia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haienyeyeki sheria ya Mungu, wala haiwezi kuinyenyekea.

Tofauti haiwezi kuwa wazi zaidi. Mwelekeo (nia) wa tabia ya mwili unabeba mauti ndani yake, yaani kuharibika na uharibifu. Mtu ambaye bado yuko katika tabia ya mwili haoni jambo hili. Anadhani anaweza kuishi kwa kujiamulia mwenyewe, lakini anaendeshwa na dhambi kwa hila. Hatambui kwamba maisha haya yanaongoza mautini (mauti ya kimwili na ya milele). Ingawa anaigopa

mauti, anaiona kuwa jambo la kawaida, wala hautambui uhusiano huu kati ya tabia ya mwili na mauti.

Lakini Roho wa Mungu analeta uzima na amani. Uzima huu si uhai wa kibijolojia, bali ni uzima wa kiroho, yaani uzima wa milele. Amani na Mungu ndiyo msingi wa uzima huu mpya. Amani ndiyo shauku ya wanadamu wote, lakini inapatikana tu katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Kuishi katika Roho kuna alama ya amani hii; ni amani inayomfanya muumini apumzike kwa kutumaini mkononi mwa Mungu. Katika nyaraka zake za mafundisho Paulo anaeleza jinsi uzima huu wa kiroho na amani hii vinavyoonekana katika kuwepo kwetu kwa kibinadamu. Hapa bado anabaki katika kulinganisha kwa msingi, kunakoonekana kuwa kwa kinadharia.

Asili ya tabia ya mwili yenye dhambi si jambo lisilotenda kitu. Hata kama haionekani hivyo, iko katika uadui juu ya Mungu. Tabia ya mwili inaikataa sheria. Mamlaka ya Mungu ni adui kwa tabia ya mwili. Ni asili ya tabia ya mwili kumfukuza Mungu nje ya maisha. Tabia ya mwili haiwezi na haitaki kuishika sheria ya Mungu. Jambo hili linamhusu pia Mkristo. Tabia yake ya mwili, au asili yake ya zamani ya tabia ya mwili, ambayo bado iko ndani yake hata katika nafasi mpya ya wokovu, inatenda vivyo hivyo (ikipewa uhuru wa kufanya hivyo), nayo pia haiwezi kuishika sheria. Hata tabia ya mwili *iliyo ndani yetu* ni uadui juu ya Mungu. Lakini sisi hatuko “katika tabia ya mwili”, kama mstari unaofuata unavyoonyesha:

7.9 Mistari ya 8-9: Kuwa katika tabia ya mwili na kuwa katika Roho

Lakini wale walio katika tabia ya mwili hawawezi kumpendeza Mungu. Lakini ninyi hammo katika tabia ya mwili, bali katika Robo, ikiwa kweli Roho wa Mungu anakaa ndani yenu. Lakini mtu yeyote asiye na Robo wa Kristo, huyo si wake.

Kwa maneno “kuwa katika tabia ya mwili” (kwa Kiyunani *sarx*; SUV: ‘mwili’) kunamaanishwa kile mtu alichwa kwa asili kama mzao wa Adamu. Maisha yake yanatiwa alama na kutawaliwa nacho katika yote aliyo na yote anayoyatenda. Ndiyo mazingira yake ya kuishi, kama vile maji yalivyo mazingira ya samaki. Paulo anasema kwamba ni lazima iwe wazi bila shaka yoyote kwamba katika tabia ya mwili mtu hawezi kamwe kumpendeza Mungu, hata kwa kutumia msaada wa sheria.

Mkristo hayuko tena “katika Adamu”, bali “katika Kristo”, na jambo hili hapa linalinganishwa na ukweli kwamba yuko “katika Roho”. Kwa kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani ya kila muumini, yeye pia yuko “katika Roho” tangu Roho huyu alipomfanya kuwa mali yake. Tukiwa katika Roho, basi tuko ndani ya nafsi ya Roho Mtakatifu, kama vile tulivyo ndani ya nafsi ya Kristo. Nafsi hii ya kimungu, Roho wa Mungu, anakaa ndani yetu kama vile Kristo anavyokaa. Kutokana na hilo, hali yetu sasa inaelezwa kuwa “katika Roho”. Tuko “katika Kristo”, na tuko “katika Roho Mtakatifu”. Kwa maneno mengine, tuko ndani ya Mungu (Wakolosai 3:3; 1 Wathesalonike 1:1; 2 Wathesalonike 1:2; 1 Yohana 4:15-16; Yuda 1). Hapo ndipo “nyumbani” kwetu kupya, mazingira yetu mapya ya maisha, yaliyojaa uzima, neema, amani na haki. “Kuwa katika Roho” kunamaanisha kwamba tangu sasa Roho wa Mungu anazaa tunda lake ndani yetu na kuiongoza nia, yaani kile tunachokitafuta. Roho huyu hafanyi kazi kwa namna tofauti au bila kumtegemea Yesu Kristo, ambaye tumewekwa ndani yake. Kwa hiyo Roho huyo huyo anaitwa pia “Roho wa Kristo”. Kristo ndiye kiini na lengo la maisha haya mapya, na Roho wa Mungu anajali sana kumfanya Kristo kuwa mkuu katika maisha yetu.

Ikiwa katika maisha ya muumini Kristo haonekani, na mtu huyo hampendi, matokeo yanaweza kuwa jambo moja tu: kwamba yeye si mali yake. Huu ni mwito wa kujichunguza, ili mtu yeyote asijidanganye kwa usalama wa uongo.

Hapa Roho wa Kristo anafanana na muhuri unaoonyesha mtu ni mali ya nani. Ingawa kutiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu hakutajwi hapa (taz. Waefeso 1:13), alama ya umiliki (yaani ukweli kwamba neno “wake” linatumika kwa maana ya kuwa mali ya Kristo) inaashiria upande huu.

7.10 Mistari ya 10-11: Roho wa Mungu na wokovu wa mwili wetu

Lakini Kristo akiwa ndani yenu, mwili umekufa kwa sababu ya dhambi, bali Robo ni uzima kwa sababu ya haki. Lakini ikiwa Robo wake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo katika wafu ataibusha pia miili yenu inayokufa kwa sababu ya Robo wake anayekaa ndani yenu (au: kwa njia ya Robo wake anayekaa ndani yenu).

7.10.1 Nafasi yetu ya wokovu – ukweli wa wokovu – “tayari sasa”

- Tuko katika Kristo Yesu.

- Tuko katika Roho.
- Tunaufuata Roho.
- Roho Mtakatifu yuko ndani yetu.
- Tunaye Roho wa Kristo.
- Kristo yuko ndani yetu.

Kuna mlingano wa kushangaza kati ya Kristo na Roho. Ni nafsi mbili tofauti, lakini zina lengo *moja*. Haiwezi kuwa vinginevyo katika Uungu, katika Utatu wa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Mungu wa Utatu alikuwa kazini katika wokovu wetu, na yuko kazini pia sasa katika utakaso wetu!

7.10.2 Kuishi na kufa

Katika sura ya 5 hadi 8 mauti inatajwa tena na tena. Kinachotangulizwa mbele ni kifo cha mwili, lakini hakiwezi kutenganishwa na mauti ya milele (matokeo ya hukumu ya adhabu ya Mungu). Mwili wetu bado uko chini ya matokeo haya ya dhambi. Ni wazi kwamba hapa Paulo anatofautisha upande wa ndani – Kristo ndani yenu – na upande wa nje, yaani mwili. Mwili huu umekufa (umeandikiwa mauti, unakufa) – kwa sababu ya dhambi. Lakini hilo halihusu upande wa ndani, kwa maana huo uko mkononi mwa Roho wa uzima. Wokovu wa Mungu unaugusa kwanza upande wa ndani wa mwanadamu. Upande huu wa ndani haufafanuliwi zaidi (kwa mfano kwa kutumia maneno “nafsi” au “roho”), bali unatajwa tu kwa kiwakilishi “ninyi” (“ndani yenu”). Roho anayetajwa hapa, katika muktadha huu, si roho ya mwanadamu, bali Roho wa Mungu. Yeye ndiye aliyeleta uzima kwa njia ya sheria ya Roho wa uzima (8:2).

Kama vile dhambi inavyohusika na mauti, vivyo hivyo kwa muumini haki ya Mungu inahusika na uzima. Haki ndiyo msingi wa uzima mpya. Tendo moja la haki la Yesu Kristo lilileta kuhesabiwa haki kwenye uzima (5:18); tumewekwa katika nafasi ya wenye haki (5:19).

Bado tuko katika mwili ambao kwa asili yake hautofautiani na mwili wa mtu asiyeamini. Kwamba Kristo yuko ndani yetu, jambo hilo halina athari kwa mwili katika maisha haya ya duniani. Kwa sababu hiyo mwili haufanywi kuwa usioweza kufa tayari sasa. Lakini hali hii ni ya muda tu, kwa maana nguvu ya ufufuo iliyo katika Kristo itaifikia pia mwili. Mwanadamu mzima, kama umoja kamili, ndiye lengo la wokovu wa Mungu. Haihusu tu “wokovu wa nafsi”, bali zaidi sana kurejeshwa kwa uumbaji wa asili.

Na hata hilo lingekuwa ni kusema kidogo mno, kwa maana wokovu haurejeshi tu hali ya kwanza ya Adamu aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu, bali utatubadilisha tufanane na mfano wa Mwanawe (8:29). Kwa maana inakuja siku ambayo tutafanana naye, Yesu (1 Yohana 3:2). Siku hiyo hatutauchukua tena mfano wa yule “wa udongo” (mfano wa Adamu), bali mfano wa yule wa mbinguni, yaani Kristo (1 Wakorintho 15:49). Ufufuo utaonyesha kwamba Mungu, kwa utukufu wake mwenyewe na kwa wokovu wetu, ameyashinda matokeo *yote* ya dhambi.

7.10.3 Roho wa Mungu na mwili

Roho wa Mungu anayekaa ndani yetu ndiye sababu ya sisi kufufuliwa siku moja. Roho huyu anakaa ndani ya mwili wetu, na ameuchukua mwili wetu kuwa wake. Mwili wetu umekuwa hekalu la Roho Mtakatifu; mwili ni mali ya Roho (1 Wakorintho 6:19)! Roho ndiye dhamana ya ufufuo wetu wa wakati ujao kutoka kwa wafu. Sababu ya ufufuo wa wakati ujao ni kwamba sasa, tunapoishi katika mwili wetu wa duniani, Roho anakaa ndani yetu. Roho anataka kukaa tena katika hekalu hili, kwa maana baada ya kifo cha mwili kutokea, ilimbidi aliache kwa muda. Bwana Yesu anasema kwamba Roho atakaa pamoja nasi hata milele (Yohana 14:16); atakaa pia katika mwili wetu wa ufufuo. Ni muhimu kuuona uhusiano huu wa Roho na *mwili* wetu, kwa sababu mara nyingi tunamhusisha Roho huyu na *roho* yetu ya kibinadamu tu.

Kwa upande mmoja Roho Mtakatifu ndiye *sababu* ya kufufuliwa kwa miili yetu, lakini vilevile atakuwa *chombo* cha Mungu cha kuifufua miili yetu.

7.10.4 Kwa nini bado hatujawa wasioweza kufa sasa?

Je, Mungu hangeweza kuupa mwili wetu kutokufa tayari sasa pamoja na wokovu wake? Kwa nini mwili huu (ikiwa Kristo hatarudi kabla ya hapo) wakati mwingine unapaswa kuugua na kupitia mauti? Jibu lake linaonekana kuwa hili: Mungu ana mpango kwa ajili ya ulimwengu. Lengo lake ni uumbaji mpya. Uumbaji huu umekwisha kuanza ndani yetu; sisi (waumini) tayari sasa ni sehemu ya uumbaji mpya, kwa namna fulani “onjo la mapema”, malimbuko. Enzi mpya imekwisha kuanza ndani yetu: “Tayari sasa” na wakati huohuo “bado” – hivyo ndivyo hali yetu ya mpito njiani kuelekea ukamilisho inavyoweza kuelezwa.

Hebu tuwazie kwamba tayari sasa tungekuwa wasioweza kufa. Basi kila mtu angependa kuwa Mkristo kwa sababu hiyo tu, ili naye asiweze kufa. Lakini Mungu anatuma Habari Njema ili watu watubu na kuamini. Swali hili haliulizwi moja kwa moja katika waraka huu, hata hivyo Paulo bado katika sura hii analishughulikia swali la mateso na dhiki, na ukombozi wa mwili wetu. Tunaishi katika mvutano wa “tayari sasa – bado”: Mwili bado uko chini ya magonjwa na mauti, lakini tumekwisha kupokea baraka kamili ya wokovu, ambayo ni onjo la umilele. Kwa swali lililoulizwa katika kichwa cha sehemu hii, Warumi 8:24 inatoa jibu: Tumeokolewa katika tumaini (taz. maneno ya ER, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani). Lakini tumaini linaloonekana (kwa mfano kwa namna ya mwili usioweza kufa) si tumaini.

8. Warumi 8:12-17: Agizo la wokovu – maisha ya ushindi

Wokovu wa Mungu haukomi pale jina letu linapoandikwa katika kitabu cha uzima, bali unaingia moja kwa moja katika maisha ya kila siku. Huko ndiko wokovu unakoonekana. Maisha mapya hayahusu tu “uhusiano mpya wa utumishi” (kutoka utumwa mmoja hadi mwingine), bali zaidi ya yote “uhusiano wa upendo”: Tumefanywa wana na Mungu, na hivyo tumekuwa watoto wa Mungu. Kama watoto hao, sasa tuko njiani katikati ya uumbaji ulioanguka na ulimwengu wenye uadui. Hali itakuwa hivi mpaka siku ile miili yetu itakapobadilishwa. Jambo hili linatokea kwa njia ya ufufuo (wa wale waliolala katika Kristo) au moja kwa moja (kwa kubadilishwa kwa wale watakaokuwa bado hai wakati huo) – yaani wakati wa kuja kwake Yesu. Hapo hatimaye kufanywa wana kwetu kutakamilika (8:23) na utukufu ujao utafikiwa (8:18).

Paulo hautili shaka wokovu wa Warumi. Anawaita ndugu, ambao Roho wa Mungu anawahakikishia kwamba wao ni watoto wa Mungu. Sisi ni watoto hao kwa nyakati zote, kwa maana wakati ujao utadhihirisha – na unapaswa kudhihirisha – kile ambacho sasa tunakishika kwa imani tu (na bado hakionekani). Ikiwa sasa (kama katika nyaraka zake zote) anazungumza juu ya “ikiwa” na “basi”, na kwa habari ya wokovu anatumia sentensi za masharti⁴¹, hasemi hivyo ili kuwatia wasiwasi. Kwa maneno hayo haonyeshi shaka wala uhakika. Badala yake anawahimiza wajiulize maswali ya kujichunguza: Mimi je? Ninaye Roho? Je, niko katika njia sahihi? Bila kusema waziwazi anachukulia kwamba watayajibu maswali haya kwa “Ndiyo”. Ni maonyo yanayotuhimiza – licha ya uhakika wa wokovu – tuwe kile tulicho. Tunapaswa kuishi maisha tuliopewa na Mungu. Maonyo haya yanatusaidia tulifikie lengo. Yanaelekeza macho yetu kwenye “bado” – mbele, kwenye utukufu wa Mungu mwenyewe, ambako tutakuwa nyumbani.

8.1 Mstari wa 12: Si wadeni wa tabia ya mwili tena

Basi, ndugu, sisi tu wadeni, si wa tabia ya mwili, tuishi kwa kufuata tabia ya mwili.

41. Yaani sentensi zenye masharti (“ikiwa ... basi ...”).

Ni wajibu kwa wote walio katika Kristo Yesu kwamba tangu sasa wasiishi tena kwa kufuata tabia ya mwili. Tabia ya mwili, yaani asili ya dhambi, Paulo amieleza kwa uwazi wa kutosha kwa kuilinganisha na Roho. Madaï ya tabia ya mwili ya kutumiliki yamepita: Tumewekwa huru. Tabia ya mwili, ikiwa sehemu ya ubinadamu wetu, haikuondolewa, bali ilifanywa kuwa isiyo na nguvu. Haina ruhusa tena ya kuyatawala maisha yetu. Kwa hiyo haiwezekani kabisa kwamba bado tuna wajibu wowote kwa tabia hii ya mwili. Lakini tabia ya mwili inajiendesha kana kwamba sisi ni wadeni wake, yaani tuna wajibu kwake, kama ilivyokuwa kabla ya kuongoka. Ukumbusho huu kwa ndugu ni wa lazima, kwa sababu bado tunaweza kushambuliwa: Sisi ndio wale wanaoweza kushambuliwa na jaribu la tabia ya mwili mpaka siku yao ya mwisho katika mwili.

Je, basi, sisi ni wadeni wa Roho? Kwa hakika tungetarajia Paulo aimalizie sentensi hii hivyo. Badala yake anaeleza jinsi maisha ya kufuata tabia ya mwili yanavyoishia, na jinsi maisha katika nguvu ya Roho yanavyoonekana:

8.2 Mstari wa 13: Uzima au mauti

Kwa maana mkiishi kwa kufuata tabia ya mwili, mtakufa (ni lazima mfe); bali mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi.

Maneno ya Paulo ni ya moja kwa moja, bila mapambo. Onyo ni wazi: Ndugu, mkiishi kwa kufuata tabia ya mwili, mtakufa. Asili ya tabia ya mwili, yaani uadui dhidi ya Mungu, inabaki bila kubadilika, hata kwa muumini. “Kuishi kwa kufuata tabia ya mwili” ni maelezo ya watu walio katika tabia ya mwili (8:5-8). Hili ni onyo linalokusudiwa kutulinda tusijidanganye. Mtu *akiishi* kwa kufuata tabia ya mwili, kuna uwezekano kwamba *yuko katika tabia ya mwili* – yaani katika njia pana iendayo kwenye uharibifu wa milele. Lakini hapa onyo hili linaelekezwa kwa ndugu (halisi)! Ingawa Paulo ana uhakika na wokovu wao na hautili shaka, anatoa onyo: Msiishi kwa kufuata tabia ya mwili, kwa maana hilo linaleta mauti! Na katika muktadha huu anamaanisha mauti ya milele.

8.2.1 Ahadi na maonyo, na wokovu wa milele

Onyo hili kwa ndugu linaonekana kuashiria uwezekano wa kuupoteza wokovu. Je, huu ndio uwezekano ambao Paulo anaufikiria kwa onyo hili? Sidhani. Alama za barabarani zinaonya juu ya matokeo yanayowezekeka, si juu ya matokeo yanayotarajiwa kutokea. Tunapoendesha gari barabarani, tunafanya

maamuzi yanayoathiri usalama wetu. Alama za barabarani zinaonya juu ya kona, upepo mkali wa pembeni na wanyama wanaovuka barabara. Hazipo ili kunitia wasiwasi. Hazikusudii kunitisha kwamba huenda nikasababisha ajali kwa sababu siwezi kuendesha vizuri vya kutosha. Badala yake zinaonya juu ya hatari mbalimbali zilizo halisi. Zinaamsha mawazo yangu juu ya kile kinachoweza kutokea nikiyapuuza maonyo hayo. Si jambo la kujipinga kuwa na ahadi ya Mungu kwa upande mmoja, na wakati huohuo kulisikia onyo, kwa sababu hatupaswi kulegea katika juhudi zetu za kuzishika ahadi hizo. Kutoka katika maisha ya Paulo kuna mfano wa kulinganisha unaosaidia. Katika safari yake kwenda Rumi meli inapatwa na dhoruba kali baharini, hata wote wanakata tamaa ya kuishi. Katika hali hiyo Paulo anawapa ahadi aliyoipokea kutoka kwa malaika, kwa maana hii: “Wote wataokolewa!” Baada ya siku kadhaa nchi kavu inaonekana, na baadhi ya mabaharia wanataka kukimbia kwa mashua ndogo ili wajiokoe

wenyewe. Paulo anawaonya askari wasiruhusu jambo hilo, kwa sababu bila mabaharia wote wangeangamia (Matendo 27). Je, Paulo alionya kwamba huenda ahadi ya Mungu isitimie? Au anaiamsha akili yao, kwa sababu anaona mbele kitakachotokea ikiwa mtu hashikamani na ahadi ya Mungu? Ahadi thabiti na onyo zito katika habari hii vinahusiana kwa namna ileile kama ahadi za Biblia (zinazotuhakikishia kwamba mwishowe tutaokolewa) zinavyohusiana na maonyo na mausia ya Biblia (yanayotudai tuvumilie katika imani kwa Yesu Kristo mpaka mwisho).

“Mungu anaonya juu ya matokeo yanayowezekana, si juu ya yale yanayotarajiwa kutokea. Ndivyo ilivyo pia kwetu. Maandiko yanatuambia kwamba Mungu anawashika salama wote walio katika Yesu Kristo (8:29-39). Wakati huohuo yanatuonya pia tuvumilie katika utii kwa Yesu Kristo, kwa sababu la sivyo tutapotea milele (8:12-13). Je, huku ni kujipinga kusiko na tumaini? Je, ni lazima kuzitilia shaka ahadi za Mungu ili tuweze kulitii onyo lake na kuamini? Hapana! Mungu anatushika salama katika Kristo kwa kutumia maonyo na mausia ambayo – sawa na mwito wa kwanza wa Injili – yanaelezwa kwa namna ya uwezekano au masharti. Mungu kamwe hazipingi ahadi zake ...⁴² Anaiamsha akili yetu, ili tukikabiliwa na uasi tumwamini na kumtii. Kwa hiyo Mungu anaitia nguvu imani yetu kwa kutuhakikishia kwamba atatulinda mpaka

42. Mwandishi wa nukuu hii anataka kuonyesha hapa kwamba ahadi na maonyo ya Mungu haviwezi kamwe kugonganishwa.

mwisho, lakini pia kwa kutukumbusha” kwa msisitizo “tubaki waaminifu kwa

Yesu Kristo kwa uthabiti.”⁴³

Baraka na ahadi – zilizofungamanishwa na masharti	
Warumi 8:13 Kwa maana mkiishi kwa kufuata tabia ya mwili, mtakufa; ...	... bali mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi.
Warumi 8:14 Kwa maana wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, ...	... hao ndio wana wa Mungu.
Warumi 8:17 ... ikiwa kweli tunateswa pamoja naye, ...	... ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.
1 Wakorintho 15:1-2 Basi, ndugu, nawajulisha ile Injili niliyowahubiri, ambayo mliipokea, ambayo mnasimama ndani yake, ambayo kwa hiyo mnaokolewa pia, ...	... mkiyashika sana maneno niliyowahubiri, isipokuwa mliamini bure.
Wagalatia 6:9 Tena tusichoke katika kutenda mema; kwa maana tutavuna kwa wakati wake, ...	... tusipozimia roho.
Wakolosai 1:21-23 Na ninyi ... sasa amewapatanisha katika mwili wa nyama yake kwa njia ya mauti, ili awasimamishe mbele zake watakatifu, wasio na mawaa wala lawama, ...	... ikiwa mnadumu katika imani, hali mmewekwa juu ya msingi na kuthibitika, wala hamhamishwi na kuliacha tumaini la Injili.
2 Timotheo 2:5 Tena mtu akishindana katika michezo, hapewi taji, ...	... asiposhindana kwa kufuata sheria.
2 Timotheo 2:12-13 Tukistahimili, ... Tukimkana, ... Tusipoamini – ...	... tutamiliki pamoja naye pia. ... yeye naye atatukana sisi. ... yeye hudumu kuwa mwaminifu, kwa maana hawezi kujikana mwenyewe.
Waebrania 3:6 ... bali Kristo kama Mwana juu ya nyumba yake, ambaye nyumba yake ni sisi, ...	... ikiwa tukishikamana na ujasiri na fahari ya tumaini letu kwa uthabiti mpaka mwisho.
2 Petro 1:10 Kwa hiyo, ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara wito wenu na uteule wenu; ...	... maana mkitenda hayo hamtajikwa kamwe.
Ufunuo 2:7 Yeye ashindaye, ...	... nitampa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu.
Ufunuo 2:11 Yeye ashindaye, ...	... hatadhuriwa na mauti ya pili.

43. Thomas Schreiner, *Mit Ausharren laufen – Gibt es Heilsgewissheit ohne Heiligung?*, Oerlinghausen, 2009, uk. 219.

Ufunuo 3:5 Yeye ashindaye, ...	... atavikwa mavazi meupe, wala sitaifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu na mbele ya malaika zake.
---------------------------------------	--

Maonyo na ahadi zinazofungamanishwa na masharti ya kuvumilia na kushinda hazikusudiwi kututia hofu na kitisho. Badala yake, kama vile ukweli wa wokovu (yale ambayo Mungu ameshatenda; kwa Kijerumani *Heilsindikativ*) na agizo la wokovu (yale tunayoagizwa kutenda kwa sababu hiyo; *Heilsimperativ*), ni pande mbili za sarafu moja.

Masharti haya hayapaswi kubatilishwa. Wala hayakusudii kututisha kwamba huenda tukaupoteza wokovu tena. Baraka na masharti vinaleta mvutano ambao ndani yake hatupaswi kulegea na kuwa wavivu, bali tunapaswa kuendelea mbele katika imani tukiwa macho na tukilenga lengo.

8.2.2 Kuyafisha matendo ya mwili kwa Roho

Tunapaswa kuinyima tabia ya mwili kila nafasi ya kujikuza, bila maaifikiano yoyote. Maisha katika Roho, yaani ushindi juu ya tabia ya mwili, ndiyo maisha ya kawaida ya Kikristo yanayokusudiwa na Mungu. Tabia ya mwili, yaani asili ya dhambi, bado ipo ndani ya muumini, na inajaribu daima kupata ushawishi. Eneo la ushawishi wake na uwanja wake wa kutenda ni mwili pamoja na hisia zake zote, kazi zake na uwezo wake. Bila shaka si mwili wenyewe ulio mbaya na unaopaswa kufishwa. Badala yake, mwili ni uwanja wa kuchezea wa tabia ya mwili; ni chombo cha tabia ya mwili, cha dhambi.

Tabia hii ya mwili bado inastahili mauti tu, nayo imekwisha kuhukumiwa pale Golgotha (8:3). Hapa Paulo haagizi kuifisha tabia ya mwili yenyewe, bali matendo (misukumo, mazoea, dalili za uhai) ya tabia ya mwili. Kila msukumo wa tabia yangu ya mwili ni lazima niuchukulie msimamo. Ni lazima niamue na nisimame upande fulani. Kwa ajili hiyo kuna kibali kutoka kwa Mungu cha kufisha. Ikiwa mwelekeo wa dhambi unataka kujipenyeza katika mawazo yangu na kuenea, ikiwa tabia ya mwili inataka kunisukuma kwenye hisia au tendo la dhambi, basi ni lazima niitikie nikiwa macho kabisa, na kila mara nionyeshe utaratibu uleule. Hapa haitakiwi kukaa bila kutenda, bali kukesha, yaani kuitikia mara moja. “Kufisha” kunamaanisha kutovumilia chochote kinachotoka katika tabia ya mwili. Hilo linaweza pia kumaanisha kukimbia mara moja, kwa mfano kukimbia jaribu la tabia ya mwili.

Lakini vita hivi si vyangu mwenyewe, bali ni vita katika nguvu ya Msaidizi mwenye nguvu, yaani Roho. Kwa usahihi zaidi, hapa haihusu vita, bali “kutekeleza hukumu ya kifo”. Hatulengi tabia ya mwili kwa ujumla wake (kama asili ya dhambi na asili ya Adamu), bali matendo yake. Matendo haya ni tishio la kudumu, lakini yanapaswa “kufishwa” tu pale yanapojitokeza. Tabia ya mwili ipo daima, lakini tendo la tabia ya mwili halipo daima. Kwa neno “kutekeleza hukumu ya kifo” hakuna kinachopambwa, kana kwamba pambano hili ni mchezo wa watoto au jambo la ushindi linalojiendesha lenyewe – lenye uhakika wa kushinda. Maisha yetu ya kila siku hayaendi kamwe kama tulivyopanga, ni vigumu kuyatabiri, na tena na tena yanakabiliwa na changamoto mpya. Vivyo hivyo hila na mbinu za tabia yetu ya mwili zinashuhudia daima kwamba inashambulia kwa ujanja na kwa ghafla. Rafiki wa tabia yetu ya mwili ni ulimwengu, yaani mwenendo mbaya wa zama hizi. Muungano huu hautufanyii mambo kuwa rahisi. Tabia ya mwili iliyo ndani yetu haitatulia na kurudi nyuma kwa pigo la kwanza. Itarudi tena wakati ambao hatuitarajii hata kidogo na wakati ambao hatuihitaji hata kidogo.

Tabia ya mwili ni ya ukaidi; haizeeki wala haichoki. Kwa habari ya jinsi tabia ya mwili ilivyo, hatupaswi kujidanganya hata kidogo.

Kwa hiyo si vita ambavyo ndani yake tunapaswa kuiangusha tabia ya mwili (kwa Kiyunani *sarx*; SUV: ‘mwili’) chini daima. Vita hivyo vilikwisha kupiganwa pale Golgotha. Katika ushindi huo, na kwa nguvu ya Roho, tunaweza kuyafisha matendo ya mwili. Tunaweza kutegemea kwamba (tukitumia pia uthabiti ule ulioelezwa sasa hivi) baada ya muda hatutaupata tena ushawishi huu na jaribu hili la tabia ya mwili kama mgogoro wa kudumu. Kwa kazi ya Mungu ndani yetu itakuwa namna yetu ya kufikiri na mazoea yetu kuliepuka ovu, kutolipa nafasi, na kwa kawaida kabisa kuchagua lililo jema, yaani mapenzi ya Mungu, kama kwamba ni mapenzi yetu wenyewe.

8.2.3 “Kujihesabu kuwa wafu” au “kufisha”?

Katika Warumi 6:11 Paulo alikwisha kusema kwamba tujihesabu kuwa wafu kwa dhambi, bali walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu. Lakini katika 8:13 anazungumza juu ya kufisha. Kwa mtazamo wa kwanza amri hizi mbili zinapingana. Amri ya kwanza ni ya kupokea zaidi, ya pili ni ya kutenda.

Kwa Warumi 6:11 bado halijasemwa kila kitu kuhusu ushindi wetu juu ya dhambi katika maisha yetu. Pambano dhidi ya dhambi na tabia ya mwili halishindwi kwa sisi kujihesabu tu kuwa wafu kwa dhambi. Tukijaribu kuukwepa ushawishi kwa “kujifanya wafu”, kwa sababu jaribu haliwezi kumshambulia mtu aliyekufa, huo ni mtazamo ulioenea sana, lakini hata hivyo si suluhisho. Tabia ya mwili bado inaishi ndani yangu; ninaweza kuitangaza kuwa imekufa, lakini nitagundua kwamba *bajjafa*. Jambo hilo linaniletea mgogoro unaochosha: Ninajikazia macho sana mimi mwenyewe na jaribu la kutenda dhambi, huku nikijaribu daima kujihesabu kuwa mfu. Hilo *si* jibu la Waraka kwa Warumi kwa tatizo la dhambi na la tabia ya mwili. Kujihesabu kuwa mfu kwa dhambi kunamaanisha nini? Ni kuipokea kazi ya ukombozi ya Kristo, ambayo ndani yake maisha yangu ya zamani, utu wangu wa zamani, ulisulubiwa (ukauawa) pamoja na Kristo. Kujihesabu “kuwa mfu kwa dhambi” hakuhusiani na jinsi ninavyopaswa kujiendesha ninapojaribiwa na dhambi; bali Warumi 6 inahusu kupokea kwa imani kile ambacho Mungu amenitendea mara moja tu kwa ajili ya wakati wote. Jambo hili lilitokea nje yangu miaka 2,000 iliyopita. Pale Mungu aliyahukumu maisha ya zamani na kuyakomesha katika mauti ya Kristo. Tendo hili la wokovu ninalipokea kwa imani kuwa langu kwa 100 %. Sasa ninaishi maisha mapya katika Kristo. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kujihesabu; hilo ndilo tunalopaswa kulitegemea kama waumini kuanzia sasa. Sehemu ya pili ya sentensi (“bali walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu”) inaeleza kile ambacho Mkristo anatenda: Anaishi katika nguvu ya Roho, kama inavyoelezwa katika sura ya 8. Sasa tu, katika Warumi 8, Paulo anaeleza kile ninachopaswa kukitenda kwa vitendo kabisa na tabia ya mwili yenye dhambi, na matendo yake na mazoea yake. Hapo haitakiwi kukaa bila kutenda (kujihesabu kuwa kitu fulani), bali kunatakiwa hatua thabiti. Kwa kweli ni hatua thabiti kuliko zote zinazoweza kuwaziwa: kufisha.

8.2.4 Kufisha – kunafanyikaje?

“Kufisha” kunaonekanaje? Kunahusu tabia ya mwili kutopata nafasi tena katika maisha yetu mapya. Mungu ametangaza vita dhidi ya tabia hii ya mwili, nasi tunapaswa kuufuata mfano huu, tena bila maafikiano. Kufisha kunamaanisha kwanza kwamba ni lazima mtu alitambue tendo fulani waziwazi kuwa tendo la tabia ya mwili. Ni lazima nijue wazi kile kinachotoka katika tabia

ya mwili. Roho Mtakatifu ananisaidia, kwa maana haitwi bure Roho Mtakatifu. Tujikumbushe tena na tena kwamba kila tunalolitenda – bila kubagua – linaongozwa ama na Roho ama na tabia ya mwili. Tabia ya mwili ni hatari hasa katika shughuli tunazozifanya kwa ajili ya Bwana. Tabia ya mwili ina pia “mshipa” wa kidini; inaweza kuwa ya kidini sana. Tabia ya mwili inajua kila namna ya kujificha! Kwa hiyo inafaa kujiuliza tena na tena: Tendo langu lina chanzo gani?

Tabia ya mwili inataka kutawala na kulazimisha tendo lake litendeke na kurudiwa. Kwa jambo hilo sasa tunasema wazi kabisa: “Hapana.” Tunajua tabia ya mwili; ni uadui dhidi ya Mungu. Kwa uongozi wa Roho tunasema bila maafikiano: “Simama!” Hakuna njia nyingine. Ama tabia ya mwili ama Roho inaongoza matendo yetu. Hatuiruhusu tabia ya mwili kuendelea na tendo lake. Kwa hiyo “kufisha” kunamaanisha kulihukumu tendo la tabia ya mwili: Kabla tendo lenyewe halijatokea, ninakataa waziwazi kila nia ya kulitekeleza. “Kufisha” kunaweza kuonekana kwa njia mbalimbali:

- Kusitisha
- kugeuka mbali
- kuacha
- kuungama
- kuondoa
- kuamua
- kukimbia
- kuacha kando
- kunyamaza
- kuhukumu
- kuondoka
- kugeuza macho
- kutaka
- kuharibu
- kushuhudia

– na mengine mengi –

Agano la Kale linatoa mfano unaofaa wa jinsi mtu anavyopaswa kumshughulikia adui kwa ukali wa mwisho. Egloni, mfalme wa Wamoabu, alikuwa mtu mnene sana na mwenye ubinafsi – kielelezo kamili cha tabia ya

mwili yenye dhambi. Ehudi, mwokozi wa Israeli, anamwangusha mfalme huyu kwa upanga wake katika tendo la ujasiri wa hatari, lakini lililolindwa na Mungu (Waamuzi 3:12-30).⁴⁴

Tusipoyafisha matendo ya mwili, yatatutawala. “Ua nyoka kabla hawajakuua.”⁴⁵

Mkakati huu mkali usio na huruma dhidi ya kila kinachotoka katika tabia ya mwili Paulo anaueleza kwa Wakolosai kwa uwazi uleule:

“Basi, vifisbeni viungo vyenu vilivyo katika nchi: uasherati, uchafu, shauku mbaya, tamaa mbaya, na kutamani (uchoyo), ndiko kuabudu sanamu.”

Mbele kidogo anaendelea na orodha hii: “... hasira, ghadhabu, uovu, matukano, aibu ya maneno ...” (Wakolosai 3:5-11).

Bwana Yesu mwenyewe anapendekeza mkakati uleule, na anauweka kwa maneno makali zaidi: “Kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake” (Mathayo 5:28). *“Basi jicho lako la kuume likikukosesha, ling’oe ulitupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako kimoja kipotee, wala usitupwe mwili wako mzima katika jehannam”* (Mathayo 5:29; taz. Marko 9:43-48).

Katika mgogoro na tabia ya mwili inapaswa kuwa wazi kwetu kwamba tunaweza kuyafisha na kuyang’oa matendo ya mwili katika nuru ya Golgotha tu na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Jambo hili halitatokea lenyewe; linahitaji uamuzi wetu wa kila siku. Mtazamo sahihi kuhusu tabia ya mwili tunaudumisha tu tukijikumbusha msalaba tena na tena (kama tunavyofanya pia katika Meza ya Bwana ya kila juma, yaani kumega mkate).

8.3 Mstari wa 14: Wana wa Mungu wanaoongozwa na Roho

Kwa maana wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.

Uongozi wa Roho unajionyesha kwanza kama ilivyoielezwa sasa hivi katika mstari wa 13: Kwa upande mmoja ni ushindi juu ya tabia ya mwili, na kwa upande mwingine ni ukweli kwamba mtu anazaa “tunda la Roho”, kama Paulo anavyolieleza katika Wagalatia 5.

Kuongozwa na Roho wa Mungu ndiyo alama *kuu* ya wana wa Mungu. Wana wanatambulika kwa kuwa wanayaelewa na kuyatenda mapenzi na lengo la baba

44. J. T. Mawson, *Überwinden ... aber wie?*, Schwelm, 1980, uk. 28-44.

45. Nukuu ya Jean Gibson.

yao. Katika jambo hili Yesu, Mwana pekee wa Mungu, alikuwa kielelezo kamili. Alizitenda kazi za Baba, na mapenzi ya Baba yalikuwa kama chakula chake. Roho alikuwa na sehemu kubwa katika hilo (Isaya 11:2; Mathayo 4:1; Marko 1:12; Luka 4:1, 14, 18; Waebrania 9:14; n.k.). Ndivyo inavyotokea pia kwa waumini, ambao ndani yao Roho hakai tu, bali pia anachukua uongozi.

Hapa Paulo haelezi hali maalum za maisha ambazo ndani yake tungepaswa kutimiza kazi maalum au kufanya maamuzi makubwa. Kama ilivyoonekana mara kadhaa katika sura hizi za waraka wake, anajali mambo ya msingi – kanuni, mikondo miwili ya mawazo inayotofautiana waziwazi.

Mtu asiyeamini anaongozwa na tabia ya mwili, muumini anaongozwa na Roho. Tena, hili si jambo linalojiendesha lenyewe kama roboti, linalomfikisha muumini kwa urahisi mahali pa kutokuwa na dhambi. Ni namna ya kawaida ya maisha ya Mkristo kuongozwa na Roho kutoka katika moyo wake na fikira zake zilizofanywa upya. Lakini daima yuko katika hatari ya kuifuata tabia ya mwili na kuongozwa nayo. Kwa hiyo mistari hii ni mwito wa wazi wa kuishi kwa bidii na kwa makusudi katika nguvu ya Roho huyu, na kuujua uwepo wake, nguvu zake na msaada wake. Yeye ni Roho wa Yesu, Roho wa kufanywa wana. Kwa maneno mengine: Wale wanaoongozwa na Roho wanaishi pia jinsi wana wa Mungu wanavyopaswa kuishi.

“Roho wa Mungu anaweza kufikia kila upande wa maisha yetu, na kwa hiyo si mkaaji asiyetenda kitu, bali anatumia nguvu ya kutenda ili kuwaongoza watakatifu wa Mungu.”⁴⁶ Uongozi na maelekezo ya Roho wa Mungu hayaiondoi haiba ya muumini, kana kwamba anajiendesha au anajisikia kama anaendeshwa kwa mbali au anachezewa. Roho anatoa nguvu ya kutenda yale ambayo Mungu anayataka. Mimi kama mtu ninabeba daima wajibu wa yale ninayoyatenda, na kwa hiyo daima mimi ndiye ninayefanya uamuzi. Mungu ashukuriwe kwamba mapenzi ya Mkristo yanafanywa upya daima (Warumi 12:2; Wakolosai 3:10), ili aweze kuyatambua na kuyatenda mapenzi ya Mungu. Fikiria hizi na matendo haya Roho anayaunga mkono. Kwa kawaida jambo hili linatoka bila mtu kuligundua au kulitambua. Zaidi ya hapo, kwa changamoto maalum za maisha yetu kunaweza kuwa na kazi maalum ya Roho – kwa njia ya hali maalum, kwa Roho kusema nasi, kwa njia ya ndugu katika imani. Juu ya jambo hilo Agano Jipya linasema mara chache tu.

46. Fred Stallan, *Was die Bibel lehrt*, Römerbrief, uk. 230.

Uongozi wa Roho si imani ya mafumbo ya kiroho (yaani kusikiliza daima sauti za ndani na hisia), wala hauhusishi “maadili ya kufuata hali”, ambapo katika kila hali tunahitaji ufunuo mpya au agizo jipya. Uongozi wa Roho unaimarisha haiba yetu na fikira zake zilizofanywa upya, ili tuyatambue mapenzi ya Mungu na kutenda lililo sahihi na lililo bora zaidi. Uongozi wa Roho unatenda kazi hasa ndani ya mipaka ya maagizo na amri za Biblia. Katika muktadha huu wa Warumi 8 inahusu ushindi juu ya tabia ya mwili na juu ya dhambi.

Hata hivyo: Roho hatoi nguvu tu; yeye pia ni “skauti” wetu, kiongozi wetu wa njia, njiani kuelekea utukufu. Tatizo letu ni kwamba haonekani, na kwa hiyo tunapaswa kuutegemea uwepo wake na kazi yake (yaani uongozi wake).

8.4 Mstari wa 15: Roho wa kufanywa wana analia ndani yetu: “Baba mpendwa!”

Kwa maana hamkupokea robo ya utumwa iwalettee hofu tena, bali mlipokea Roho wa kufanywa wana, ambaye kwa yeye tunalia: Aba, Baba!

Uhusiano mpya wa Baba na mwana si uhusiano wa utumwa. Jambo hili linakumbusha uzoefu wa sura ya 7. Chini ya sheria mtu yuko katika utumwa. Hofu ya bwana anayemtumikia na hofu ya kushindwa sasa zimepita. Roho wa kufanywa wana anatuwezesha kuishi katika ushirika na Baba. Ushirika huu unatiwa alama na maombi na kuabudu, kwa maana maneno yaliyo hapa (“Aba, Baba”) yanajumuisha ombi au kuabudu kwa namna fupi kuliko zote inayowezekana. Neno hili “Aba” linapatikana mara tatu tu katika Agano Jipya. Katika bustani ya Gethsemane (Marko 14:36) Yesu, Mwana wa Mungu, katika uchungu mkuu kabisa anamwita Baba yake kwa namna hii. Ni namna ya kumwita baba kwa ukaribu, inayoweza kulinganishwa na “Baba mpendwa” au kwa urahisi tu “Baba” (kama mtoto mdogo anavyomwita baba yake). Paulo anatumia maneno yanayofanana nayo pia katika Waraka kwa Wagalatia (4:6). Huenda ikashangaza kumwita Mungu Mwenyezi kwa jina hili la upendo, lakini linaonyesha jinsi uhusiano huu wa mwana, au wa mtoto, ulivyo wa moyo mchangamfu.

Kumtumikia Mungu sasa si jambo tena linalohusu hofu na kulazimishwa, wala kufuata kwa ukali amri na makatazo. Badala yake ni maisha tunayoyaishi katika uhusiano usiotawaliwa na woga na hofu, na yanayotoka katika uhusiano huo. Uhusiano huu umejaa upendo wa Mungu na kukubaliwa kikamilifu na

Baba, na uwepo wa Roho wake, ambaye kweli yuko ndani yetu, si kama mtazamaji aliye kimya, bali kama msaidizi anayetenda. Sisi ni wana wa Mungu, tumekubaliwa, tunaongozwa na kuelekezwa na Roho wake. Huo ndio ukweli! Kosa moja, dhambi moja, haiuvunji uhusiano huo; tunabaki wana na watoto. “Baada ya mwito wake wenye nguvu wa kuiishi imani yetu katika maisha ya kila siku, sasa Paulo anataka kuituliza mioyo yetu. Sijui ilivyo kwenu, lakini mimi ninahitaji kutiwa moyo huku. Kwa maana Mungu aliye juu ya ulimwengu wote ndiye yule ambaye, katika utulivu wa usiku au pale nilipoanguka matopeni, anaushika mkono wangu na kunikaribisha nimwite ‘Baba’.”⁴⁷

8.5 Mstari wa 16: Sisi ni watoto wa Mungu!

Robo mwenyewe husubudia pamoja na robo zetu kwamba sisi tu watoto wa Mungu.

Roho wa Mungu anashuhudia pamoja na roho yetu kwamba kweli tumeletwa katika uhusiano wa watoto na Mungu. Hapa haimaanishwi sauti inayoiita roho yetu kitu fulani. Badala yake inahusu kile kinachouongezea nguvu na kuuimarisha usadikisho, yaani uhakika wa wokovu, ambao tumekwisha kuupata kwa njia ya Neno la Mungu.

Ni mapenzi ya Mungu kwamba uhusiano thabiti na Baba uwepo katika mawazo yetu kila siku. Ni jambo la maana kubwa kwa maeneo yote ya maisha yangu kwamba ninajua kwamba Baba mwenye upendo amenikubali katika Kristo bila masharti. Baba ananipenda, nami nina thamani kubwa kwake kiasi kwamba alimtoa Mwanawe kuwa dhabihu kwa ajili yangu. Bila shaka ananiadibisha pia, jambo ambalo ni uthibitisho wa upendo wake (Waebrania 12:5). Haki ya kuwa mtoto (Yohana 1:12) inaleta pia wajibu, bila shaka. Tusisahau kamwe sisi ni nani sasa! Katika jambo hilo Roho Mtakatifu anatusaidia kila siku.

8.6 Mstari wa 17: Sisi ni warithi wa utukufu wa Kristo

Lakini ikiwa tu watoto, basi tu warithi pia – warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo, ikiwa kweli tumateswa pamoja naye, ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.

Si furaha tu ya uhusiano na Mungu tunayoruhusiwa kuihisi na kuionja. Sisi ni watoto pia “kwa maana ya kisheria”, yaani sisi ni warithi vilevile. Mungu

47. Francis Schaeffer, *Allein durch Christus*, uk. 216.

analichukulia kwa uzito kamili suala la sisi kuwa watoto wake na yeye kuwa Baba. Kile kilicho mali ya Mungu, na kile atakachompa Mwanawe, ndicho pia urithi wetu.

Mateso si sharti la kuupokea urithi katika siku ya utukufu. Kwa Wakristo wengi mateso kwa ajili ya Kristo ni mwenzi wa kudumu. Hayapaswi kuwa jambo geni kwetu, kwa maana Yesu ametutangulia katika njia hii ya mateso, aliyoyabeba kwa ajili ya haki. Katika Ujerumani na katika nchi zote za Magharibi, hadi sasa tumeepushwa na mateso haya, tofauti kabisa na ndugu zetu katika imani katika nchi nyingine. Ikiwa bado kitatujia kipindi cha mateso, basi hili ndilo la kufanya: Tulikumbuke neno hili, lililoandikwa na mtu aliyetaka kufanana na Kristo katika yote, hata katika kifo chake. Kupitia mateso hadi utukufu – hiyo ndiyo mara nyingi imekuwa njia ya waumini waaminifu katika historia ya kanisa.

“Tayari sasa” sisi ni watoto wa Mungu, na kwa hiyo warithi. Lakini “bado” hatujaupokea urithi wenyewe. Ukweli wa wokovu (yale ambayo Mungu ameshatenda; kwa Kijerumani *Heilsindikativ*) unaeleza kwamba sisi ni watoto; agizo la wokovu (yale tunayoagizwa kutenda kwa sababu hiyo; *Heilsimperativ*) linajumuisha mateso, ambayo si sharti la kuupokea urithi, lakini mara nyingi ni sehemu isiyoepukika ya kumfuata Yesu. Hili pia si onyo linaloashiria kushindwa kwa mwisho. Badala yake tunahimizwa tuwe watu wanaomkiri Yesu na kusimama naye kwa uaminifu.

9. Warumi 12: Fikiria zinafanywa upya!

Waraka kwa Warumi mtu angeweza kuuita kanisa kuu la fahari la Injili na la haki ya Mungu. Injili inaleta wokovu wa Mungu: kuachiliwa huru, kuhesabiwa haki, kuwekwa huru, kuunganishwa na Kristo, na kulindwa mpaka mwisho katikati ya shida zote, mateso na uadui!

Ili amtumikie Mungu, ilikuwa lazima mwanadamu awekwe huru mbali na hatia na nguvu ya dhambi, lakini pia apokee nguvu kwa ajili ya maisha mapya. Paulo amelieleza jambo hilo kwa namna ya kuvutia sana katika sura ya 8. Ulimwengu unaotuzunguka, na pia mwili wetu, bado havijabadilika, lakini hilo ni suala la wakati tu. Ahadi ya Mungu ya kuibadilisha miili yetu ni jambo lililokwisha kuamuliwa, ambalo atalitimiza wakati anaoujua yeye peke yake. Mpaka hapo Mungu yuko upande wetu: Ikiwa yeye yuko upande wetu, ni nani atakayethubutu kuwa juu yetu?

Kisha, kuanzia sura ya 9 hadi 11, Paulo anashughulikia maswali mengine, ambayo pia yanahusiana na haki ya Mungu. Katika sura ya 12 anarudi kwenye utumishi wetu kwa Mungu, ambao tuliwekwa huru ili tuufanye. Hapo tena inahusu maisha yetu binafsi, ambayo tunaweza kuyaishi katika upya na kwa Roho. Sasa haki ya Mungu, iliyofunuliwa katika wokovu, inapaswa kuonekana pia katika maisha ya kila siku. Katika sura ya 5 hadi 8 Paulo alikuwa amezungumza kwa namna ya kinadharia kiasi na ya kanuni. Ameuweka msingi, ameyaeleza mafundisho. Sasa anaonyesha jinsi upya huo unavyoonekana katika mambo madogo ya maisha. Anafanya hivyo kwa kutumia mausia, maagizo na miito – yaani amri za Agano Jipya. Amri hizi hazijachukua nafasi ya sheria ya Musa. Kwanza kabisa maneno haya yanatusaidia kuona jinsi maisha mapya yanavyoonekana. Ni vibao vya kuonyesha njia vya upendo wa Mungu. Hatuishi kwa kufuata amri hizi ili tuwe wenye haki, bali kwa sababu tayari sisi ni wenye haki! Amri hizi zinaonyesha Mungu ni nani, na Yesu Kristo ni nani. Amri zaidi ya 1,000 za Agano Jipya, mwishowe, zinaeleza ile kweli iliyo ndani ya Yesu. Uzima wake ndani yetu una alama zilezile hasa zinazoelezwa katika amri za Agano Jipya. Sasa Kristo yuko ndani yetu, na Roho yuko ndani yetu, ili tuweze kuishi hivyo. Imetupasa kuenenda kama yeye alivyoenenda (1 Yohana 2:6, 8).

9.1 Lengo la Mungu kwetu

Lengo la Mungu kwa kila mmoja wetu ni kutufanya tufanane na Mwanawe. Malengo mengine yote yako chini ya lengo hili. Siku moja jambo hili litakuwa kweli kikamilifu. Tutakapolifikia lengo, hatutaganda katika mfano huu, katika kufanana na Kristo; hatutakuwa kama sanamu za ukumbusho. La, tutakuwa watu wanaotenda – milele. Tutafikiri, tutatenda, tutasema na kupenda kama Mwana wa Mungu. Katika hilo tutabaki daima kuwa wale tuliokuwa tayari tangu kuzaliwa kwetu, kama watu binafsi walioumbwa na Mungu. Lakini hapo tutakuwa tumefikia kusudi letu, na tutaishi ndani yake milele. Tutakuwa wale tuliopaswa kuwa daima. Hiyo ndiyo furaha yetu kubwa kuliko zote. Furaha ya Mungu ni kutupa zawadi hii. Kwa njia hiyo Mwanawe anaheshimiwa. Hata sasa tunaweza kuwa wale ambao tumetamani kuwa daima. Ikiwa Kristo yuko ndani yetu, basi kujiamulia maisha yetu kunajumuisha ukweli kwamba *yeye* anaishi kupitia sisi!

Kubadilishwa kufanana na mfano wa Yesu, yaani kufananishwa naye, kulianza siku ya kwanza kabisa ya maisha yetu kama watu waliozaliwa mara ya pili. Ndiyo programu ya maisha ya Wakristo. Inahusu kujiandaa kwa ajili ya umilele. Kwa hiyo maisha haya ni muhimu sana, na pia jinsi tunavyoyatumia – au tuseme vizuri zaidi, jinsi Kristo anavyoweza kuyatumia.

9.2 Warumi 12:1-2: Ibada – jambo lenye mantiki!

Basi, ndugu, nawasibi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo utumishi wenu wenye mantiki (ibada). Wala msiifuatishie namna ya dunia hii (ya zama hizi), bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.

Huku ni kurudi moja kwa moja kwenye sura ya 6. Tunapaswa kuitoa miili yetu kuwa vyombo vya haki (kujitoa kwake). Sasa Paulo anaenda mbele zaidi, na anawahimiza Warumi (naam, Wakristo wote) waitoe miili yao kama dhabihu, kabisa kwa ajili ya utumishi kwa Mungu. Dhabihu hii, tofauti na dhabihu za wanyama za Agano la Kale, iko hai. Kwa hiyo inatolewa daima, si mara moja tu, kwa sababu tunaenenda katika upya wa *uzima* wa milele. Dhabihu yetu ni takatifu, kwa sababu tayari tumetakaswa na Mungu. Kwa hiyo ni dhabihu

inayompendeza. Mtazamo wa maisha wa kujitoa kikamilifu ndio matokeo ya kimantiki ya wokovu tuliopokea. Kwa hiyo Paulo anaita kwenye kujitoa huku kwa huruma za Mungu. Hatuhimizwi kwa njia ya sheria kuyatoa maisha yetu yote kwa Mungu, bali kwa njia ya huruma za Mungu. Huruma hizo zilijionyesha kwa namna halisi hivi: Yote tuliyokuwa tumeyakosa, na yote tuliyo (yaani watu waliouzwa chini ya dhambi), aliyaweka juu ya Kristo. Hakumwachilia Mwanawe! Rehema ya Mungu haikuuumba wokovu wetu tu; inabaki pia ikiwepo daima, kwa sababu yeye ni Baba yetu nasi ni watoto wake.

Haipaswi kupuuzwa kwamba hapa Paulo anatoa *usia* wa kindugu na wa upendo. Kwa kila Mkristo (awe yuko mwanzoni au amekuwa katika njia ya imani tangu zamani) dai hili la kujitoa kikamilifu ni changamoto na jambo la sasa tena na tena. Tunapaswa kulikubali tena na tena. Kila Mkristo mwaminifu atagundua kwamba, kwa bahati mbaya, kujitoa kwa maisha yake kunapanda na kushuka. Kujitoa ni mchakato unaohusiana na fikira zetu. Huko ndiko uamuzi unafanywa kama tuko tayari kujitoa, na tutafika umbali gani katika hilo. Kukumbushwa jambo hili kila siku kunasaidia.

9.2.1 Miili yenu!

Anayeutoa mwili wake kuwa dhabihu iliyo hai hatambuliwi kwa “tendo la ushujaa wa kupita kiasi”, kama lilivyotarajiwa na wapagani kwa miungu yao ya kipagani⁴⁸, bali anaishi maisha ya kawaida, yasiyo ya kuvutia macho, yanayoelekezwa kwa Mungu daima. Hakuna shaka kwamba maisha kama hayo pamoja na Mungu yana milima na mabonde, ushindi na kushindwa, kujikwaa na kuinuka. Lakini kuna uzoefu unaotia moyo kwa namna ya ajabu, na kuna matunda. Tukimkabidhi Mungu maisha yetu, na hivyo tukatembea tukiushika mkono wa Mungu wa milele, lakini asiyeonekana, maisha yetu yatakuwa ya kusisimua.

Lakini kwa nini Paulo anazungumza juu ya “mwili” unaopaswa kutolewa kuwa dhabihu? Je, fikira zetu (kama katika mstari wa 2) si sehemu yake pia? Bila shaka, inahusu kujitoa kwa uhai wetu wote, kwa maisha yetu yote. Lakini jambo hilo linaonekana hasa kwa njia ya mwili wetu. Mwili ndio kiungo kati yetu na ulimwengu tunamoishi. Na mwili huu, kabla ya kuokolewa kwetu, ulikuwa “mwili wa dhambi” (Warumi 6:6). Ulikuwa chombo ambacho kwa njia yake

48. Fred Stallan, *Was die Bibel lehrt, Römerbrief*, Dillenburg 2001, uk. 358.

dhambi ilipata mikono na miguu. Mwili ulijenga mazoea ya dhambi, uliishi maisha yake wenyewe ya dhambi, na ulidai utii. Hebu tuchunguze ni mara ngapi, au ni maeneo mangapi ya maisha yetu yanayotawaliwa au kuathiriwa na mwili wetu. Mifano michache tu inapaswa kuonyesha kwamba kwa urahisi tunaweza kudharau nafasi ya mwili wetu katika kujitoa kwetu. Inahusu mazoea, au swali la jinsi gani, kiasi gani, lini na nini tunakula na kunywa, mazoea ya kulala, na tabia zetu katika kutazama televisheni na kutumia mtandao. Mambo haya yote yanaathiri mwili wetu, na yanajiimarisha kuwa namna za kutenda zilizozama ndani yetu. Haihusu “orodha ya dhambi”, bali kuiona katika nuru sahihi nafasi ya mwili wetu, na ushawishi wake ambao mara nyingi hudharauliwa. Hapa mwili unatolewa kuwa dhabihu, yaani madai ya mwili wetu yanaachwa, ili badala yake mtu aweze kuutoa kwa Mungu.

Kwanza tunapaswa “kuyafisha matendo ya mwili” (Warumi 8:13). Neno hili pia linasisitiza nafasi ya mwili, lakini kwa kweli ni nafasi ya “kiadui”, kwa sababu mwili unataka kutenda mambo ambayo tunapaswa kuyafisha. Hayo ndiyo – tukitumia neno jingine la Paulo – matendo ya tabia ya mwili (kwa Kiyunani *sarx*; SUV: ‘mwili’) (Wagalatia 5:19), au pia viungo vilivyo katika nchi (Wakolosai 3:5). Mazoea ya dhambi yakishadhibitiwa kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, njia inafunguka ya kuutoa mwili huu zaidi na zaidi kwa Mungu. “Mwili wa dhambi” haukusulubiwa, kwa maana hapo tungekuwa tumekufa. Badala yake ulifanywa kuwa usio na nguvu pale Golgotha. Kile kilichokuwa zamani mwili wa dhambi, sasa ni “mwili wa haki”! Paulo anautia mwili wake utumwani (1 Wakorintho 9:27). Anayageuza mambo, na sasa ni lazima mwili umfuate yeye. Mwili haupaswi kuweza kulazimisha tamaa zake za dhambi na starehe iliyopita kiasi: Ni lazima mwili uwe mali ya Mungu na uwe chombo cha haki.

9.2.2 Ulimwengu: rafiki au adui?

Kwa mwili wetu tunaishi katika ulimwengu. Jamii (na hivyo ndivyo hasa Paulo anavyomaanisha kwa *ulimwengu*) kwa kiasi kikubwa imeufanya mwili kuwa jambo muhimu kuliko yote. Sekta nzima za viwanda zinatoa kila kitu ambacho mwili unahitaji au unapaswa kuhitaji: starehe ya kujitunza, utimamu wa mwili, michezo, afya, urembo, maisha marefu, chakula na vinywaji vizuri, dawa, upasuaji wa urembo. Kimsingi hakuna ubaya katika mambo kama hayo,

maadamu yanawekwa chini ya utawala wa Mungu. Swali ni: Tunaupa mwili nafasi gani? Je, ni mtumishi au ni bwana?

Hatari moja halisi, inayoweza kutuzuia tusijitoe kikamilifu, inavizia katika ulimwengu tunamoishi. Ni ulimwengu wa wanadamu unaotuzunguka na ambamo tunaishi na kutembea (ingawa, kama Yesu asemavyo, sisi si wa ulimwengu huo, kama yeye mwenyewe asivyo wa ulimwengu). Wanadamu wameyapanga maisha yao bila Mungu. Jamii, uchumi na biashara, viwanda, utamaduni, dini, muziki, falsafa, muda wa mapumzikio, anasa, chakula, elimu, maisha ya familia, maadili – kila kitu kinachounda maisha kimeambukizwa na kutiwa alama na hali ya kumsahau Mungu: Mwanadamu hataki Mungu awe ndani ya mashua yake (Warumi 1:28).

Kwa tabia yetu ya mwili ulimwengu unavutia na kupendeza. Kwa kweli tumetoka katika ulimwengu; tabia yetu ya mwili ilikuwa nyumbani huko. Sasa tunapaswa kujihadhari tusiishi kama ulimwengu (yaani kama watu wa ulimwengu). Namna ya maisha ya ulimwengu inapingana waziwazi na kujitoka kikamilifu kwa dhabihu iliyo hai! Watu wa ulimwengu wanaishi kwa ajili yao wenyewe, wala hawaulizi mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yao!

Ulimwengu (kwa Kiyunani *aion*) unatafsiriwa pia kuwa “zama hizi” au “mwenendo wa zama”. Muda wa ulimwengu unakwisha. Zama hizi za ulimwengu ziko karibu kufikia mwisho wake: Tunaishi “katika siku za mwisho”. Zaidi ya hayo, ulimwengu unakwenda katika mwelekeo usio sahihi – tena kwa kasi inayoongezeka. Unakwenda mbali na Mungu, si kumwelekea yeye. Kwa ujumla, mwenendo wa zama ni kama ile “njia pana” (Mathayo 7:13-14) inayoshuka hadi kwenye uharibifu. Mwenendo wa zama unafanana na mto ambamo samaki waliokufa wanachukuliwa na mkondo. Samaki aliye hai anaogelea upande wa pili; na hiyo ndiyo maana hasa ya kutoikubali namna (mfumo⁴⁹) ya ulimwengu. *Ulimwengu* unatafsiriwa pia kuwa “roho ya zama”. Mwelekeo wa fikira, yaani mtazamo wa ndani wa mwanadamu, ndio unaoufanya ulimwengu kuwa jinsi ulivyo. Tena Biblia inasema mara kadhaa na waziwazi kwamba Shetani mwenyewe ndiye mungu wa ulimwengu huu, mkuu wa zama hizi.

Ulimwengu na roho yake (ya zama) ni mbaya. Neno la Mungu haliachi shaka yoyote juu ya hilo (Wagalatia 1:4). Na anayetaka kuwa “rafiki wa dunia” (kwa

49. Kwa Kiyunani *schematizein*, yaani kujiunda kufuatana na mfumo fulani, au kuacha kuumbwa kufuatana na umbo lililowekwa tayari.

sababu maisha yanayojifananisha nayo ni rahisi zaidi) anajifanya kuwa adui wa Mungu (Yakobo 4:4). Bila shaka kuna viwango vya jinsi hali ya kidunia inavyoweza kwenda mbali. Si lazima iwe imeyashika maisha yote. Huenda inahusu eneo moja au jingine tu, eneo kubwa au dogo tu la maisha, lililotiwa alama na ulimwengu. Kwa hiyo kila mtu ajichunguze ni wapi namna ya kufikiri na namna ya kuishi ya ulimwengu imejipenyeza. Fedha yangu iko je? Mali yangu, malengo yangu ya kikazi, mwenendo wangu katika ndoa, mazoea ninayoyapenda zaidi, urafiki wangu – vyote hivi viko je?

Kutofuatisha namna ya ulimwengu, kutojifananisha nao, hakuanzi na mambo ya nje, bali kwanza na fikira. Kabla ya tendo huja wazo, kama vile mawazo yanavyotangulia kujifananisha na ulimwengu.

9.2.3 Kubadilishwa kwa njia ya fikira mpya

Mungu anataka kutubadilisha. Anataka tuwe kile tulicho! Kristo anapaswa kuumbika ndani yetu zaidi na zaidi. Kristo anapaswa kuzidi, bali sisi wenyewe kupungua. Kuishi kama ulimwengu (katika namna yake ya kufikiri na pia katika sura yake ya nje) ni kinyume kabisa cha kile ambacho Mungu anataka kukifikia. Jambo hili linawezaje kutokea? Kwa msingi wa yale yaliyokwisha kuelezwa katika sura ya 5 hadi 8, sasa kunatokea badiliko la hatua kwa hatua, mchakato wa kiroho wa kukua na wa utakaso. Mtu aliyekuja kuamini sasa hivi bado ana mitindo yake ya zamani ya kufikiri aliyoizoea. Haifutwi kwa kubonyeza kitufe. Kwa mchakato wa kufanywa upya inabadilishwa kuwa fikira zilizotiwa alama na Mungu.

Mara kadhaa Paulo anautaja mchakato wa kudumu wa kufanywa upya. Kinachomaanishwa ni zaidi ya tendo la kufikiri tu:

- 2 Wakorintho 4:16: kufanywa upya kila siku kwa utu wa ndani, katikati ya mvutano wa mateso na utukufu
- Waefeso 4:23: Mfanywe upya daima katika fikira zenu.
- Wakolosai 3:10: Utu mpya unafanywa upya daima.

Kubadilishwa kunaanzia katika fikira zetu. Nia (kwa Kiyunani *nous*) inajumuisha ulimwengu wa mawazo, akili, kufikiri, ufahamu, kituo cha kufikiri. Nyuma ya neno “nia” kuna zaidi ya kufikiri tu, yaani akili ya kupima mambo. Moyo, ambao katika Biblia pia unasimama kwa ajili ya kufikiri na mapenzi (wakati mwingine

pia kwa ajili ya hisia), hauwezi kutenganishwa na neno nia. Nia ni kituo cha uendeshaji kwa ajili ya kufikiri, kutaka na kutenda. Katika kituo hiki cha uendeshaji ndimo inamopita michakato ya kufikiri kwa kupanga, kwa kupima na kwa kugundua, pamoja na kufanya maamuzi. Kutenda ni matokeo ya kufikiri na kuamua. “Nia ni ... mahali ambapo mchakato wa kutambua unafanyika, na ambapo mawazo yanatoka. Kwa maana halisi ya neno hili, ni mahali ‘pa kuamua’ kwa ajili ya matendo yetu, na hivyo kwa ajili ya maadili ya vitendo kwa ujumla.”⁵⁰

9.2.4 Metamofosisi

Hili ndilo neno linalotumika katika maandiko ya Kiyunani kwa ajili ya “kugeuzwa”. Kufanywa upya kwa fikira kunaleta kugeuzwa huko. Neno metamofosisi (kugeuzwa kabisa) linasaidia katika mada yetu. Tunalijua neno hili kutoka katika ulimwengu wa wanyama. Tunajua kwamba kipepeo anapitia mojawapo ya michakato ya kubadilika inayoshangaza kuliko yote. Kutoka kwa kiwavi anayetambaa (ambaye si mara zote anaonekana mzuri), kupitia hatua ya buu, anatokea kipepeo anayeruka. Huu ni mchakato uliopangwa ndani yake, unaohitaji muda, lakini hauwezi kuzuiwa. Inashangaza kwamba sisi pia tunapaswa na tunaweza kupitia badiliko kubwa namna hiyo. Jambo hilo linaonyesha kwamba badiliko, jinsi Mungu anavyolitaka, linawezekana daima. Hakuna kitu kilichoachwa nje yake. Kisingizio kwamba hili au lile liko hivyo na litabaki hivyo hakifai, tukikumbuka kwamba kiwavi mbaya wa sura anaweza kuwa kipepeo mzuri ajabu. Mdudu anabaki mdudu; anabaki kiumbe yuleyule. Lakini anabadilishwa kabisa. Je, jambo hili halifanani na nguvu ya Injili, inayoweza kumbadilisha mwanadamu kweli na kwa kina (moyoni mwake na katika fikira zake)?

Neno hilohilo “metamofosisi” linatumika pale Yesu anapogeuzwa sura mbele ya wanafunzi juu ya mlima wa kugeuka sura, na kuchukua mng’ao wa nuru ya utukufu wa Mungu. Katika muktadha mwingine neno hilohilo linatumika kuhusu sisi: “Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiutazama utukufu wa Bwana, *tunabadilishwa* tufanane na mfano uleule, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa Bwana, aliye Roho” (2 Wakorintho 3:18). “Metamofosisi” yetu ina lengo la kufanana na kielelezo cha Kristo. Lengo hili la Mungu haliwezi kusisitizwa na kurudiwa vya kutosha. Si ndoto ya kutamani, wala si lengo

50. Jürg Buchegger, *Ein Mensch, was ist das?*, Wuppertal, 2004, uk. 211.

lisiloweza kufikiwa, wala si udanganyifu mpya ambao kwa huo Mungu anataka kutukatisha tamaa. Ni mpango wake na mapenzi yake, ambayo yanamfurahisha sana, na anataka kutushirikisha furaha hiyo. Kwa hiyo yatafanikiwa pia. Tukitaka, na tukimtazama Yesu Kristo (tukijishughulisha naye, na Neno lake, na ufalme wake), tukimfanya kuwa lengo letu, ikiwa kweli anayajaza maisha yetu, basi mchakato wa kubadilishwa umepangwa ipasavyo.

9.2.5 Kwa nini kufanywa upya?

Tangu kuzaliwa, kwa asili, tuna fikira na nia ambayo kiini chake si Mungu, bali nafsi yake yenyewe. Mtu anapotubu na kumgeukia Mungu, Mungu anaumba kitu kipya ndani yake; mbegu ya Neno inaota moyoni mwake; sasa Kristo ndiye uzima wake. Uzima huu sasa ni lazima ukue, kama ilivyo kwa mtoto mchanga. Ukuaji huu unauhusu utu wa ndani, na nia nayo imejumuishwa humo. Mchakato huu wa kufanywa upya unaendelea maisha yote. Ukuaji unatokea kwa msingi wa hali mpya ya kuwa katika Kristo. Katika Kristo tumefanywa wenye haki na watakatifu mbele za Mungu mara moja, kwa kitambo kimoja. Jambo hili halipaswi kubaki tu kuwa maelezo ya nafasi yetu, bali linapaswa kuyaenea maisha yetu ya kila siku. Kwa ajili hiyo kunahitajika kufanywa upya kwa kudumu, kunakofanywa na Mungu mwenyewe, na kunakozingatia kikamilifu hali tuliyomo, mazingira tunamoishi, na jinsi tulivyoyumbwa sisi wenyewe (tabia, hulka, vipawa, udhaifu, hali yetu ya maisha n.k.), na kunakolingana na mambo hayo.

9.2.6 Kufanywa upya kunatokeaje?

Kunatokea kwa Mungu mwenyewe. Kugeuzwa ni agizo, ambalo tunapaswa kuliacha litendeke ndani yetu. Kufanywa upya ni kazi ya Mungu. Hatuwezi kukuleta sisi wenyewe. Wajibu wetu ni kumkabidhi Mungu maisha yetu yote, na kutoifuatisha namna ya ulimwengu. Huo ndio mchango wetu katika mchakato huu wa kufanywa upya. Tukijishughulisha mno na ulimwengu, tukiziruhusu namna za kufikiri za kidunia ziingie katika kituo chetu cha uendeshaji kwa ajili ya kufikiri, kutaka na kutenda, na tukijifaninisha nao, basi sisi nasi tutabadilishwa, na (polepole lakini kwa hakika) tutaonyesha kufanana na ulimwengu. Jambo hili linatokea ndani, na kisha, kama matokeo yasiyoepukika,

pia nje. Mara nyingi mchakato huu unakwenda kwa kunyemelea, karibu bila kugunduliwa. Sumu ya ulimwengu inaua maisha ya kiroho polepole, hata mtu hauoni mchakato huo kwa urahisi.

Kinyume chake ni maisha katika “ulimwengu wa Mungu”, katika ufalme wake, katika ushirika na Mungu, ambapo ninamwachia yeye mwenyewe azijaze, azipange na kuzielekeza fikira zangu. Hata katika hali hii, si lazima mimi mwenyewe niuone mchakato wa kufanywa upya.

Kufanywa upya kunatokea kwa njia gani? Jambo hilo halizungumzwi hapa. Ni tendo la Mungu aliye mwenye mamlaka yote. Anatumia Neno la Mungu, linalosomwa moja kwa moja au kusikiwa katika mahubiri. Anatumia ukimya, maombi na kuabudu, kuyapokea kwa makusudi kufanywa upya na kusahihishwa. Anatumia ushirika wa waumini. Anatumia kila hali ya maisha, kila tukio. Yote ni malezi, mafunzo na mafundisho ya Baba. Kwa hiyo ninaweza kukuharakisha na kukuunga mkono huku kufanywa upya, lakini vilevile ninaweza kukuzuia. Ninaweza kuamua kuifuatisha namna ya ulimwengu zaidi, kama vile ninavyoweza kufanana na Yesu zaidi. Uamuzi huu hatuukabili mara moja tu, bali mwishowe kila siku.

9.2.7 Uwanja wa vita wa mawazo

“Nafikiri, kwa hiyo niko!” Mawazo yetu ndiyo alama za siri, yaani msimbo, wa maisha yetu. Kuyaathiri, au hata kuyaongoza, ndilo lengo kubwa kuliko yote la adui wa Mungu. Anayekitawala kituo cha uendeshaji ameshika kila kitu mkononi. Hilo pia si lazima liyahuu maeneo yote ya maisha, lakini linaweza kuwa na ushawishi mkubwa juu ya mwenendo wetu. Ibilisi anaweza kufaulu kujenga ngome katika ulimwengu wa mawazo yetu, kwa hatua moja kubwa au kwa muda mrefu kwa hatua nyingi ndogo (2 Wakorintho 10:3-5):

“Kwa maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa kufuata tabia ya mwili; kwa maana silaha za vita vyetu si za tabia ya mwili, bali zina uwezo katika Mungu baka kuangusha ngome (boma), tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka kijiinua juu ya elimu ya Mungu, na tukitoka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo.”

“Shabaha za kwanza za vita zinazopaswa kuangamizwa ni ‘ngome’ zilizo vichwani mwetu. Maana halisi ya neno la Kiyunani linalotumika hapa ni ‘boma’.

Maboma ni mitindo hasi ya kufikiri iliyochomwa ndani ya ubongo wetu, ama kwa kurudiwa-rudiwa daima ama kwa tukio lililoleta jeraha kubwa la moyo.”⁵¹

Mitindo ya kufikiri na namna za tabia au miitikio ya mazoea inatokea, miongoni mwa mambo mengine, kwa sababu ya athari za nje: “Athari hizi za mazingira kila moja ilikuwa fupi, lakini ilidumu. Miongoni mwake ni kwa mfano matukio fulani, mahali fulani na makutano fulani, pamoja na uzoefu wa kibinafsi. Zaidi ya hayo, tumeundwa na vitabu tulivyosoma, filamu tulizotazama, muziki tunaopenda kuusikiliza ... Tumejijengea njia ambayo huenda (au huenda isiwe) inalingana na mapenzi ya Mungu, ya jinsi tunavyoyashughulikia mambo haya na jinsi tunavyoitatua migogoro iliyoletwa nayo. Athari za kudumu katika maisha yenu zinatokana na mahusiano ya muda mrefu na mazingira yenu, kama vile athari ya familia, ya marafiki na wanaofahamiana nanyi, ya majirani, ya walimu, ya wafanyakazi wenzenu.

Katika kuzaliwa mara ya pili kiroho dhambi zenu zote zilioshwa kweli, lakini mitindo yenu ya zamani ya kufikiri na ya tabia, iliyotokana na kujifananisha na mazingira yenu, ilibaki imeota mizizi katika tabia yenu ya mwili. Kwa kweli mtu anaweza kuzaliwa mara ya pili na bado akaendelea kuyatunza maisha yake ya zamani ya ‘kutomjali Mungu’ (jambo hilo linawahusu vilevile wale waliokulia katika mazingira ya Kikristo; maelezo ya mwandishi). Kwa hiyo Paulo anatusihi kwa bidii tubadilishwe kwa kufanywa upya nia zetu (Warumi 12:2).”⁵²

Kila kitu tulichokizoea na kujifunza kinaweza kubadilishwa kwa njia ya kufanywa upya, ambako Mungu mwenyewe anataka kukufanya katika fikira zetu na maisha yetu, tukimruhusu. Kuna silaha kutoka kwa Mungu zinazotusaidia kubadilisha ile programu (kwa sehemu) ya tabia ya mwili iliyowekwa katika fikira zetu.

9.2.8 Tunawezaje kushinda vita hivi?

Kwanza tunahitaji ule mtazamo wa msingi uliotajwa hapo juu – kujitoa kwa Mungu, na kuukataa ulimwengu. Biblia inatoa maelekezo zaidi:

- kujiacha tujazwe Neno la Mungu kwa kusoma Biblia (kwa utaratibu)
- kuiacha amani ya Kristo itawale (Wakolosai 3:15)
- kuliacha neno la Kristo likae ndani yetu kwa wingi (Wakolosai 3:16).

51. Neil T. Anderson, *Neues Leben – neue Identität*, 1994, Lage, uk. 153.

52. Neil T. Anderson, *Kitabu kilichotajwa*, uk. 155.

Maboma na mawazo hayo ya kujitetea mara nyingi ni uongo wa Shetani. Ili kuufichua uongo huo, tunatumia silaha za nuru na za haki. Wazo au mtindo wa mawazo ukizuka, boma likifungua malango yake ya kushambulia, basi mwito ule wenye msisitizo unalenga kulikamata wazo hilo mara moja, liwe mateka chini ya utii wa Kristo. Kristo ana nguvu zaidi. Yeye ndiye mshindi.

Mifano ya maboma ya uongo:

- Hofu na mawazo ya kuwazia mambo yasiyo kweli
- Hofu ya wakati ujao na hofu ya kushindwa
- Hisia za kujiona duni na matatizo ya kujithamini
- Kukosa amani na wasiwasi
- Majaribu katika mawazo
- Mawazo yanayomlazimisha mtu
- Kutegemea watu, vitu, mambo, mali, milki, kinga za kibinadamu na tamaa.

Uongo huu wote ni lazima tuufichue na kuuteka nyara chini ya mamlaka ya Kristo. Mara nyingi jibu ni kwamba tuko salama katika Kristo, na kwamba milele sisi ni watoto wapendwa wa Mungu, na tunajua juu ya utunzaji wa Mungu. Dhambi haina haki tena ya kutukandamiza na kututesa. Kristo ametuweka huru.

9.2.9 Ndoto za mchana na matamanio

Uwezo wa fikira za mwanadamu unashangaza. Kwa mawazo mtu anaweza kusafiri bila kulipa hata senti moja. Mtu anaweza kujijengea ulimwengu wa pili, ambamo anajitimizia matamanio aliyonyimwa katika maisha halisi: Mtu anaweza kuwa nyota maarufu, kushinda bahati nasibu, kuwa na familia kamilifu, mke mwingine au mume mwingine; yote haya na mengi zaidi yanawezekana katika mawazo. Lakini tujihadhari! Mawazo haya hayaibi muda tu, bali yanatudanganya kwa kutuonyesha ulimwengu usiokuwepo. Ndoto hizi na matamanio haya, yakijiimarisha kuwa mazoea, yataathiri fikira zetu na maamuzi yetu. Sisi wenyewe ndio kiini na kitovu cha ndoto hizi! Ni hatari kujiwazia matendo yanayotokea katika ulimwengu wa ndoto tu. Mtu anapoteza uhusiano na hali halisi.

“Moyo wa mwanadamu ni moyo unaotangatanga, na moyo unaotangatanga ni moyo usio na furaha.”⁵³ Watafiti wa Kimarekani katika utafiti mmoja

53. Mwandishi hajulikani.

wamepata matokeo ya kushangaza. Kwa mujibu wake, nusu ya muda watu hawapo kwa mawazo. Wanafuata mawazo yao, wanatafakari hiki na kile, au wanaota tu. Tatizo ni hili: Inaonekana kwamba kutangatanga kwa mawazo kunawafanya watu wakose furaha. Hata kama jambo hili si kweli kila mara, linatufanya tufikiri kwamba adui wa nafsi zetu anaweza kuleta madhara kwa njia hii.

Tunafanya nini dhidi ya hili? Vidokezo kadhaa vinavyosaidia kushinda uzito na mwendo wa kujiendesha wa ulimwengu wetu wa mawazo:

- Kwa ujumla, na daima, hili ni kweli: Tukaze fikira kwenye kile tunachokifanya sasa, yaani kwenye wakati huu, ili tuzitimize vizuri kazi zetu na wajibu wetu!

Tukiwa huru kufanya tunachotaka:

- Tuombe kwa ajili ya kila kinachotujia akilini! Tufanye kila kitu kuwa ombi!
- Tusome Biblia au kitabu chenye thamani ya kiroho!
- Tukariri mistari ya Biblia, ili tuweze kulitafakari Neno la Mungu hata bila kuwa na Biblia mkononi! Huenda bado tukapitia kipindi bila Biblia!
- Tufikiri jinsi tunavyoweza leo kufanya huduma kwa ajili ya Bwana Yesu!
- Tumtafakari Bwana Yesu, tukitafakari tukio fulani kutoka katika Injili tunalolikumbuka!
- Tuinuke tufanye jambo la kutenda! Tujishughulishe, tufanye kitu!
- Tutafute mtu wa kuzungumza naye! Tumpigie mtu simu na kumwuliza hali yake!

9.2.10 Mapenzi ya Mungu – yamejaribiwa na kuonekana kuwa mema!

... mpate kujua bakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.

Mapenzi ya Mungu yanapingana na mwenendo wa zama za ulimwengu. Mwenendo huu wa zama (yaani watu wa ulimwengu) haujali sana Mungu anataka nini. Lakini huo ni mchezo wa moto – kwa maana halisi kabisa ya neno hili. Yohana anasema hivi (1 Yohana 2:15-17):

“Msipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake; kwa maana kila kilichomo duniani, yaani,

tamaa ya tabia ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake; bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele.”

Ulimwengu una tarehe yake ya mwisho wa matumizi. Na anayetazama kwa makini anaona kwamba tarehe hiyo karibu imekwisha kupita. Ulimwengu ambao mwanadamu amejijengea umeandikiwa maangamizi. Hakuna kitu juu yake wala ndani yake kinachoweza kuhalalisha kuongezewa muda. Harufu ya mauti imeshikamana nao. Na inavyoonekana, leo wapo Wakristo ambao hawaitambui tena harufu hiyo ya kuoza.

Mungu mwenyewe peke yake ndiye mwema na mkamilifu, na hilo ni kweli pia kuhusu mapenzi yake, ambayo zaidi ya hapo yanapendeza. Jambo hili linakumbusha dhabihu za Agano la Kale, ambazo zilipaswa kuwa bila kasoro na bila lawama. Hizo tu ndizo zilizoruhusiwa kutolewa. Vivyo hivyo, kwa kuyatambua mapenzi ya Mungu katika kila hali ya maisha, uhai wetu wote katika mwili (ambao utu wa ndani nao ni sehemu yake) unapaswa kutolewa kwa Mungu kuwa dhabihu. Kufanywa upya kwa daima kwa nia yetu kunawezesha kuyatambua mapenzi ya Mungu. Orodha za ukaguzi na mashauri mazuri huenda yakasaidia, lakini Mungu anataka pia kuumba katika fikira zetu yale yanayohitajika ili tuyatambue mapenzi yake.

9.3 Warumi 13:13-14: Kumvaa Kristo – bila kuiandalia tabia ya mwili nafasi

Na tuenende kwa adabu kama ilivyo wakati wa mchana; si kwa ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu (busuda); bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiiandalie tabia ya mwili nafasi, ili kuzitimiza tamaa zake.

Kabla hatujamaliza kujifunza Waraka kwa Warumi, tuangalie bado mstari huu, kwa sababu ndio mahali pekee baada ya sura ya 8 panapotaja “tabia ya mwili”.

Lengo la Mungu kwetu linabaki mpaka siku yetu ya mwisho: Anataka kutubadilisha tufanane na mfano wa Mwanawe. Haihusu kunakili maisha ya Yesu; hatupaswi kuwa maseremala. Badala yake inahusu kuipokea asili ya Yesu zaidi na zaidi katika maisha yetu, kulingana na haiba yetu ya kibinafsi. Hilo linajumuisha upendo wake, kweli yake, haki yake – mwishowe kila kitu tunachoweza kukitambua kwake kuwa sifa za kimaadili za asili yake. Amekwisha

kutupa uzima mpya; sasa ni lazima tumpe nafasi ya kukua, na tumwache Bwana awe mkuu katika maisha yetu, bali sisi wenyewe tujirudishe nyuma.

Neno hili linatuhimiza tumvae Bwana Yesu Kristo kama vazi. Kwa kweli huu ni mfano wenye nguvu, ambao haufafanuliwi zaidi. Katika usiku wa ulimwengu usiomcha Mungu, dhambi inatendeka kwa kila namna, wala watu hawaoni haya hata mbele ya hadhara. Kinyume cha hilo yanasimama mapenzi ya Mungu yanayoamua kila kitu. Kwetu haipaswi kuonekana tabia ya mwili, kwa sisi kuzikubali tamaa zake, bali Yesu Kristo.

Hapa pia tunaonyeshwa kwamba mengi yanaweza kutokea na kuruhusiwa katika mawazo, kabla tamaa haijaitimizwa kwa kweli na mtu kuanguka katika jaribu. Tabia ya mwili haipaswi kuhudumiwa wala kutunzwa. Schlachter inatafsiri bila kuacha shaka yoyote: “Msiitunze tabia ya mwili hata kuziamsha tamaa” (Schl 2000, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani). Tunapaswa kuyafisha mawazo na matendo ya tabia ya mwili! Inahitajika mtazamo usio na maafikiano, ambao Paulo ameueleza kwa kirefu katika Warumi 8. “Tamaa ya maisha ya starehe yasiyo na migogoro inaweza kutushawishi tuyakwepe maamuzi muhimu na hatua thabiti, ili tuiepushe tabia yetu ya mwili. Lakini kwa njia hiyo bila shaka tutaitunza, nayo itaweza kuzaa matunda bila kizuizi. Tabia ya mwili ikilelewa na kutunzwa, itaisimamisha udikteta wake katika maisha yetu. Ikiepushwa kwa kukosa uthabiti, na tamaa yake ikitoshelezwa, itazidi kuwa na njaa na shauku zaidi. Kuitunza tabia ya mwili hakusaidii (kama inavyodaiwa mara nyingi siku hizi) kujikubali na kukuza haiba, bali kunaamsha tamaa zinazopingana na mawazo ya Mungu.”⁵⁴

9.4 Hitimisho

Anayeutoa mwili wake na maisha yake juu ya madhabahu ya Mungu anayapoteza maisha yake, yaani maisha yake ya “mimi”. Lakini Bwana Yesu anasema nini, kwa maana hii? “Anayeyapoteza maisha yake ya ‘mimi’ atayapata” (taz. Luka 9:24; 17:33). Jim Elliot aliandika: “Si mpumbavu yule anayeutoa kile asichoweza kukubakiza, ili apate kile asichoweza kukipoteza.”⁵⁵

Tukiwa tayari, Mungu ataendelea kuzibadilisha fikira zetu. Hapo tutafika mahali ambapo sisi, kama watendaji wa mapenzi ya *Mungu*, tutaona kana kwamba tunatenda mapenzi *yetu*. Hiyo ndiyo sheria ya uhuru (Yakobo 1:25;

54. Walter Nitsche, *Versagen und innere Zerrissenheit*, uk. 76.

55. Maneno ya asili ni haya: “He is no fool who gives what he cannot keep to gain what he cannot lose.”

2:12): kutaka kwa hiari na kwa moyo kile ambacho Mungu anakitaka. Haya ndiyo maisha pekee yenye thamani ya kuishi. Bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele!

10. Ya kale na mapya – mapitio ya jumla

10. Ya kale na mapya – mapitio ya jumla

Ya kale	Mapya	Marejeo
Ya kale yamepita	Yamekuwa mapya	2 Wakorintho 5:17
Katika Adamu	Katika Kristo	Warumi 5:12-8:11 n.k.
Wenye dhambi	Wenye haki	Warumi 5:19
Utu wa zamani	Utu mpya	Warumi 6:6; Waefeso 4:20-24; Wakolosai 3:9-11
Mwili wa dhambi	Kuitoa miili yetu na viungo vyetu kwa Mungu	Warumi 6:6, 12-23; 8:13; 12:1-2
Katika tabia ya mwili	Katika Roho	Warumi 8:8-9
Sheria ya dhambi na ya mauti	Sheria ya Roho wa uzima	Warumi 8:2
Tabia ya mwili (ndani yetu)	Roho Mtakatifu (ndani yetu)	Warumi 8:1-11; Wagalatia 5
Dhambi – kutawaliwa nayo, kuuzwa chini yake	Kuifia dhambi: upya wa uzima; “walio hai baada ya kufa”	Warumi 6 (na Warumi 8)
Mauti ya kiroho	Uzima mpya wa kiroho, kuhuishwa	1 Wakorintho 15:45; 1 Yohana 3:14; Waefeso 2:5; n.k.
Tabia ya mwili (haifai kitu; mtu huyo hawezi kuitimiza sheria ya Mungu)	Kuzaliwa mara ya pili	Yohana 3; 6:63 Warumi 8:7
Mwisho wake: mauti	Lengo: uzima wa milele	Warumi 6:21-23
Kufa	Kufanywa upya	Warumi 6:21; Waefeso 4:22-24
Ya kidunia – viungo vilivyo katika nchi: uasherati, uchafu, shauku mbaya, tamaa mbaya, kutamani, hasira, ghadhabu, uovu n.k.	Ya mbinguni – wito, lengo	Wakolosai 3:1-11; 1 Wakorintho 15:48-49
Kujawa na nafsi zetu wenyewe: Ndani yetu hamna jema lolote, maadamu Kristo hayumo ndani yetu.	Kristo ndani yetu	Wakolosai 3:11; Wagalatia 2:19-20; n.k. Warumi 7:18

11. Tabia ya mwili ni nini?

Tabia ya mwili (kwa Kiyunani *sarx*; SUV: ‘mwili’) mara nyingi miongoni mwa Wakristo inaitwa “asili ya zamani”, kinyume cha “asili mpya” tuliyoipokea katika kuzaliwa mara ya pili. Majina mengine yanayotumika ni: *asili ya Adamu*, *asili ya dhambi*, *asili ya tabia ya mwili*, *asili ya kibinadamu*, au *ya kujikweza*, *ya dhambi*, *ya zamani*, au pia *ya kidunia*. Ingawa maneno haya yanasaidia, Agano Jipya daima linaiita “tabia ya mwili” (*sarx*).

“Tabia ya mwili” inamaanisha alama iliyowekwa na dhambi juu ya mwanadamu, kama ilivyoimarishwa katika uhai wake wa kimwili na wa kinafsi.⁵⁶

Neno hili (*sarx*) linatumika kwa maana mbalimbali. Mara nyingi linamhusu mwanadamu. Maana ya neno ni lazima ifafanuliwe katika muktadha wa kila andiko. Linaweza kuhusu upande wa kimaadili, au upande wa kiumbe na wa kimaada, au upande unaopita (Isaya 40:6-8), usio na msaada (Yeremia 17:5, 7), au dhaifu wa mwili wa mwanadamu; au linaweza kuhusu ushirika wa ndoa (Mwanzo 2:24; 1 Wakorintho 6:16), ukoo wa kifamilia (Warumi 1:3; 9:3) au wanadamu wote kwa ujumla (Warumi 3:20). Kwa jumla Paulo analitumia neno hili mara 78 (kati ya hizo mara 63 katika Nyaraka kwa Warumi na kwa Wagalatia) kama jina la asili ya kibinadamu iliyoanguka na yenye dhambi.

Kwa hiyo Paulo analitumia neno “tabia ya mwili” kwa maana ya kimaadili. Kwa maana hii linatumiwa vilevile na Petro (1 Petro 2:11; 2 Petro 2:10, 18) na Yohana (1 Yohana 2:16). Yakobo anazungumza juu ya tamaa (Yakobo 4:1-3).

Neno “tabia ya mwili” – kinyume cha “Roho” – lina maana ya msingi kwa mada ya *Kubadili Upande* (Seitenwechsel). Kauli kuu, tunapozungumza juu ya mgogoro katika maisha ya Kikristo, ni ile aliyoisema Paulo:

“Kwa maana tabia ya mwili hutamani ikishindana na Roho, na Roho ikishindana na tabia ya mwili; kwa kuwa hizi zimepingana” (Wagalatia 5:17).

Katika maisha ya Mkristo hazikabiliani pande mbili kama zile zilizopo kwa kiasi fulani ndani ya kila mtu. Haihusu tu mvutano kati ya ubaya na wema, unaotokea kwa kiasi fulani ndani ya kila mtu. Hapa inahusu kipimo kingine kabisa: Roho ni Roho Mtakatifu, Mungu mwenyewe, ambaye ameingia katika

56. Roland Antholzer, Gemeindeorientierte Initiative für biblische Beratung e.V. (GIBB).

maisha ya mtu aliyekuja kuamini, maisha yaliyotawaliwa na tabia ya mwili. Tabia ya mwili ni ile sehemu ya ubinadamu ambayo ndani ya Mkristo, baada ya kuzaliwa kwake mara ya pili, bado imebaki kutoka katika maisha ya zamani katika Adamu.

Katika maisha ya kila siku neno la Kijerumani *Fleisch* ('nyama'; katika Biblia pia 'mwili', *sarx*) linatumika tunapozungumza juu ya mchinjaji na chakula, na pia katika elimu ya maumbile ya mwili tunapozungumza juu ya tishu za mwili wa mwanadamu. Matumizi yote mawili yanalingana na jinsi neno hili linavyotumika katika Biblia. Mara nyingi kinachomaanishwa ni mwili wa mwanadamu tu (kwa mfano Warumi 2:28). Lakini maana ya neno hili inakwenda zaidi ya umaada mtupu. Tabia ya mwili (mwanadamu katika uhai wake wa duniani) si dhaifu tu, inayochakaa na inayopita. Zaidi ya hapo, kwa sababu ya dhambi imechukua sifa zinazopingana na asili ya Mungu. Maana ya tabia ya mwili, kama Paulo anavyolitumia neno hili katika Warumi 7 na 8 na mahali pengine, haielezi upande wa kimaada wa mwanadamu, bali upande wake wa kimaadili na wa kitabia. Kwa hiyo tabia ya mwili inamaanisha udhaifu wa uhai wa mwanadamu na hali ya kuanguka ya asili ya mwanadamu. "Tabia ya mwili ni asili ya kibinadamu jinsi ilivyokuwa kwa sababu ya dhambi."⁵⁷

Upande wa kimaadili na wa kitabia unaeleza *jinsi* mwanadamu alivyo: Msukumo wake ni nini, malengo yake ni nini, anajiendesha mbele za Mungu, na mbele za wanadamu wenzake? Inahusu asili yake, namna yake, tabia yake ya ndani kwa maana ya kimaadili, ikipimwa kwa asili na tabia ya Mungu. Tabia ya mwili (yaani asili na mwelekeo wa maisha ya mwanadamu) haimwelekei Mungu wa kweli, ingawa inaweza kuwa ya kidini. Bwana Yesu alimweleza Nikodemo wazi kwamba kuzaliwa upya ni lazima, kwa sababu kilichozaliwa kwa tabia ya mwili ni tabia ya mwili (Yohana 3:5-8). Kwa kuwa tabia ya mwili haifai kitu mbele za Mungu (Yohana 6:63), kuzaliwa na Mungu, kwa Roho, ni lazima ili kitu kipya kiumbwe.

11.1 Dhambi na tabia ya mwili

Dhambi ni kanuni inayoelekezwa dhidi ya Mungu na kuikataa mamlaka yake ya pekee. Kanuni hii ilikuwepo tayari wakati ambapo hapakuwa bado na "tabia ya mwili" (kwa Kiyunani *sarx*; SUV: 'mwili') kwa maana ya wanadamu walioumbwa, yaani viumbe wa nyama na damu. Ibilisi, ambaye huenda alikuwa

57. William Barclay, *Fleisch oder Geist*, Augsburg, 1968, uk. 19.

kiumbe wa kiroho wa juu kuliko wote, aliifuata kanuni hii kwa kuutumia vibaya uhuru wake. Adamu, mwanadamu wa kwanza, aliifungulia dhambi mlango kwa kuivunja amri moja rahisi. Kwa njia hiyo dhambi iliingia ndani ya mwanadamu, tena hadi kwenye kina cha asili yake na hali yake ya kuwa (moyoni mwake). Tangu hapo dhambi inakaa ndani ya kila mwanadamu (Warumi 7:17); yeye ni *mwenye dhambi*. Adamu aliwapa wazao wake wote asili yake. Hivyo tulikuwa wenye dhambi kwa kuzaliwa.

Tabia ya mwili ni mwanadamu mwenyewe, asili yake, haiba yake ya kibinafsi, inayotawaliwa na dhambi inayokaa ndani yake. Paulo analieleza jambo hili kwa ufupi anaposema: “Mimi ... ni wa tabia ya mwili, nimeuzwa chini ya dhambi” (Warumi 7:14). Hapa dhambi ndiye bwana na msimamizi wa watumwa, na tabia ya mwili (yaani mwanadamu) ni mtumwa wake. Dhambi na tabia ya mwili zimefumwa pamoja kwa karibu sana, karibu zinaweza kubadilishana nafasi.

Tabia ya mwili si kanuni tu ya kumwasi Mungu (kama ilivyo dhambi), bali inamaanisha pia kila mwanadamu asiye na Kristo katika upekee wake. Tabia ya mwili ni mchanganyiko wa sifa za haiba na za tabia. Kwa maana ya kimaadili, tabia ya mwili ni chombo cha dhambi. Mwili wangu, yaani umbo langu la kimwili, umefanywa mtumwa na dhambi. Matendo ya dhambi yanatendwa kwa njia ya mwili (yaani kwa mikono, kwa miguu na kwa ulimi). Kwa hiyo mwili si chombo kisichoegemea upande wowote tu, bali pia umetiwa alama na mazoea ya dhambi, na tamaa, na shauku mbaya.

11.2 Tabia ya mwili na mtu asiyeamini

Hakuna mahali popote ambapo “tabia ya mwili” inaweza kushuhudiwa kuwa na jambo jema. Kwa mtazamo wa Mungu tabia ya mwili haiwezi kurekebishwa. Dalili ya kwanza ya maana hii ya tabia ya mwili, inayofafanuliwa kwa kirefu katika Agano Jipya tu, ni kauli ya Mungu juu ya mwanadamu muda mfupi kabla ya gharika: “Mungu akaiona nchi, na tazama, imeharibika; kwa maana wote wenye mwili (yaani tabia ya mwili) wamejiharibia njia zao duniani” (Mwanzo 6:12; taz. pia mstari wa 3).

Mtu asiyeamini yuko “kwa kufuata tabia ya mwili” na “katika tabia ya mwili” (Warumi 8:5-8). Uhai wake wote, ukipimwa kwa utakatifu na haki ya Mungu, si kitu kingine ila “tabia ya mwili”, yaani si kitu kingine ila kiumbe chenye dhambi kinachotawaliwa na fikira zake mwenyewe, na tamaa zake (matakwa yasiyo halali), na misukumo yake. Mtu asiyeamini haitwi “wa tabia ya mwili”. Neno hili

linatumika kwa Wakristo tu, wanaoifuata asili ya zamani, ingawa kwa kweli – kwa sababu Roho anakaa ndani yao – wangepaswa kuishi kiroho (1 Wakorintho 3:1).

Mtu aliye mbali na Kristo anatazama yale yaliyo mbele ya macho (yaani yanayoonekana). Mataifa (ambayo yamenaswa katika “shughuli ... za maisha haya”⁵⁸) yanayatafuta mambo ya duniani, yaani mambo ya maisha haya tu, kwa kutumia kila kitu kwa ajili yake, bila kutambua kwamba Mungu ndiye mpaji wa vitu vyote (Mathayo 6:32). Kwa maana hii tabia ya mwili inaelekea maisha haya tu, na imeelekezwa kwenye yanayoonekana. Inashikamana na yanayoonekana – na kile kinachoonekana kuwa salama. Hii pia ni alama ya tabia ya mwili, ambayo kwa mtazamo wa kwanza haitambuliwi kuwa hivyo, kwa maana mara nyingi *wasiwasi wa hofu* juu ya maisha yetu tunauona kwa namna chanya kuwa ni kujali wajibu wetu kwa uzito.

11.3 Tabia ya mwili na Mkristo

Mkristo hayuko tena “katika tabia ya mwili”; yuko “katika Kristo” na “katika Roho”. Lakini tabia ya mwili bado ipo ndani yetu, ingawa haiko tena katika nafasi ile ambayo kwayo inaruhusiwa kuamua fikira zetu na matendo yetu. Inabaki kuwa adui wa kufa na kupona wa Roho Mtakatifu, na hivyo wa Mkristo. Hata bado ina uwezekano wa kuyaongoza na kuyatia alama maisha ya Mkristo, ikiwa hatukipokei kile ambacho Mungu ametutendea, na ikiwa sisi wenyewe hatutumii hukumu ya kifo juu ya matendo ya tabia ya mwili (Warumi 8:13). Katika Yesu Mungu alihukumu na kuisulubisha dhambi na tabia ya mwili. Jambo hilo tumelipokea kwa imani, nasi tunaiona tabia ya mwili iliyo ndani yetu kwa namna hiyo. Hata hivyo bado iko ndani yetu, bila kubadilika katika namna yake. Maonyo mengi yenye msisitizo ya kuishughulikia tamaa ya tabia ya mwili kwa uthabiti (yaani kutoipa tabia ya mwili nafasi yoyote) yanachukulia kwamba tabia hii ya mwili bado iko ndani yetu.

Yesu alimthibitisha Nikodemo kwamba tabia ya mwili haifai kitu wala haiwezi kitu. “Tena Yesu analigusa kiini cha tatizo, na kuonyesha kwamba haiwezekani kabisa kuifanya tabia ya mwili kuwa ya kiroho. Kile kilichozaliwa kwa tabia ya mwili ni tabia ya mwili, na kamwe hakitakuwa kitu kingine chochote. Inaweza kuwa tabia ya mwili iliyoelimika vizuri, tabia ya mwili iliyostaarabika, tabia ya mwili yenye uzoefu mkubwa wa maisha, tabia ya mwili

58. Taz. Luka 8:14.

iliyo njema kimaadili, naam, hata tabia ya mwili ya kidini, na hata hivyo inabaki kuwa tabia ya mwili.”⁵⁹

“Tabia ya mwili inabaki na dhambi! Je, tumejiandaa kwa makusudi kabisa kwamba katika hali yetu ya duniani tuna ‘tabia ya mwili’ ambayo bado ina hamu ya kuipinga sheria ya Mungu, na inapenda kujitoa kuwa chombo cha dhambi? Je, tuko tayari kwa hilo?”⁶⁰

Lakini hatupaswi kuuita uwepo tu wa tabia ya mwili na dalili zake za uhai kuwa tayari ni dhambi. Dhambi inatokea pale tunapoikubali tabia ya mwili, na kuiacha misukumoni na matendo ya tabia ya mwili yaendelee bila kuyafisha. Kadiri muda unavyopita tutautambua zaidi na zaidi ubaya kamili na usiobadilika wa tabia yetu ya mwili, bila sisi kuishi kwa kufuata tabia ya mwili. Tabia ya mwili ni kama mnyama mkali, kama pweza mwenye mikono mingi. Kadiri ufahamu wa kiroho unavyoingia katika maisha yetu, ndivyo tunavyozidi kuutambua wazi uharibifu kamili wa tabia yetu wenyewe ya mwili. Kujijua huku kunapaswa kuongezeka sambamba na kujua neema na upendo ambao kwao Kristo alikufa kwa ajili yetu. Anayekatishwa tamaa na ubaya na uovu wa tabia yake ya mwili bado hajaelewa kwamba hakuna kitu kinachoweza kutarajiwa kutoka kwa tabia ya mwili, na kwamba haiwezi kurekebisha.

Mungu ameamua kutoiondoa tabia ya mwili ndani yetu. Inaonekana kwamba uwepo na ukali wa tabia ya mwili ndani ya muumini ni wa lazima kwa ajili ya ukuaji wa kiroho:

- Inaufunua udhaifu wetu wa ndani.⁶¹
- Inaua kiburi chetu na majivuno yetu.
- Inatunyenyekeza tena na tena.
- Inatusukuma daima tumwite Mungu atusaidie.
- Inatuonyesha kwamba juhudi za kibinadamu hazifai kitu.
- Inatufundisha kumtegemea Bwana peke yake.
- Inatuongoza kumpenda Mwokozi aliyetuokoa kutoka katika dhambi.
- Inatuletea maisha ya toba ya kudumu.
- Inatufanya tukeshe dhidi ya mashambulizi ya dhambi.
- Inaamsha shauku ya mbinguni.

59. Ruth Paxson, *Life on the Highest Plane*, uk. 190.

60. Walter Nitsche, *Versagen und innere Zerrissenheit*, uk. 11.

61. <http://www.keepbelieving.com/sermon/2001-08-26-Full-Speed-Ahead-One-Step-at-a-Time-How-You-Can-Walk-in-the-Spirit-Every-Day/>

- Inatusukuma tutumie njia zote za neema ya Mungu.
- Inatutia moyo tujijengee mazoea matakatifu (au mema na ya kiroho).
- Inatusukuma tu tafute msaada wa kaka na dada zetu.

Tabia ya mwili inatufanya tuta fute masuluhisho kila siku, tena katika nuru ya yale ambayo Mungu anatuambia juu ya jambo hilo katika Neno lake. Hatupaswi kungoja muujiza wa ghafla. Mungu hayaondoi tu “kwa uchawi” matatizo yanayohusiana na tabia yetu ya mwili, kwa maana tunapaswa na tunaweza kutenda, kwa sababu ametupa kila tunachohitaji kwa ajili ya maisha ya ushindi.

Jambo hili tutalichunguza kwa kina hasa katika sura inayofuata. Katika kufanya hivyo kutakuwa na marudio zaidi ya mara moja. Hilo linahusu pia sura zinazofuata baada yake. Mwishowe sura zote zinashughulikia mada moja, lakini kwa mitazamo tofauti. Lakini kwa kuwa ni mada *moja* – kubadili upande kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo – tunapochambua mtazamo mmoja tutashughulika tena na mambo mbalimbali ambayo tumekwisha kuyashughulikia. Mtazamo mmoja unarudi kwenye mitazamo au pande nyingine. Upande mmoja hauwezi kuelezwa ukiwa umetengwa na pande nyingine.

12. Tabia ya mwili dhidi ya Roho

Kwa maana tabia ya mwili hutamani ikishindana na Roho, na Roho ikishindana na tabia ya mwili; kwa kuwa bizi zimepingana.

Wagalatia 5:17

Wagalatia walikuwa wameona kwa namna ya kuvutia kile ambacho Injili ilikileta: Walihesabiwa haki na kumpokea Roho, ambaye kwa ishara na miujiza alithibitisha kwamba Mungu mwenyewe ndiye chanzo cha ujumbe wa ajabu wa Injili. Lakini nini kilikuwa kimetokea? Wayahudi waliotaka kuwalazimisha watu desturi za Kiyahudi (Wayahudishaji), waliojitokeza kama walimu wa sheria, walimfuata Paulo nyuma, na wakajaribu kuiingiza sheria ya Musa katika makanisa yaliyoanzishwa karibuni. Waliieleza sheria kuwa ya lazima kwa ajili ya wokovu na kwa ajili ya maisha, na huenda hasa Wakristo wa Kiyahudi waliipokea hiyo kwa furaha. Hiyo ndiyo sababu ya Waraka kwa Wagalatia, ambamo Paulo anapinga jambo hili kwa nguvu kubwa: Misingi ya Injili inaguswa pale sheria inapochanganywa na Injili. Katika sheria na Injili dunia mbili zisizopatana zinagongana.

12.1 Tatizo lilikuwa nini?

Kwa kuirudisha sheria, Wagalatia walirudi nyuma kwenye wakati wa sheria, na hivyo pia kwenye maisha ya tabia ya mwili. Waliikimbilia sheria, wakidai kwamba ni ya lazima kwa ajili ya wokovu na kama kipimo cha maisha. Huenda walilitetea wazo hili hata mbele ya Paulo. Lakini mtume anawaeleza wazi kwamba kwa njia hii hawataokolewa. Zaidi ya hayo (na jambo hili linahusu mada yetu kuu), ilionekana kwamba hawakuweza kuishika sheria. Walitendeanza kama wanyama wakali wanang'oana macho na kumezana. Paulo anasema kwa kejeli kidogo kwamba wajihadhari wasije wakaliana wenyewe kwa wenyewe. Kwa njia hiyo anaufichua hadharani ukweli kwamba kuipenda kwao sheria na kudhani kwao kuwa waaminifu kwa sheria kulileta matokeo kinyume cha yaliyotarajiwa. Hakuna jema lililotokea. Wagalatia walikuwa wamesahau kwamba wakati wa sheria, na hivyo wa tabia ya mwili, ulikuwa umepita. Mfumo wa zamani ulikuwa umekomeshwa. Sasa enzi ya Roho na ya uhuru ilikuwa imeanza.

Tabia ya mwili (asili ya zamani ya Adamu iliyoanguka) inahitaji sheria pamoja na amri zake na makatazo yake. Lakini ilikuwa na inabaki kuwa isiyo na nguvu: Si sheria iliyoshindwa, bali mwanadamu. Paulo anaweka nini mkabala na hilo? Roho wa Mungu. Waraka huu ni utetezi wenye nguvu wa Roho wa Mungu kama badala ya Torati! Roho wa Mungu, ambaye Kristo amemtuma, anatosha kwa kila kitu! Kwa yeye tunaishi na kuenenda, asema Paulo. Kristo ndiye kiini, msingi wa kuhesabiwa haki kwetu; Roho ndiye yule ambaye kwa yeye tunaishi na kuivaa asili ya Kristo. Lakini lengo si kuishi bila sheria; sheria ya Kristo sasa, kwa Roho wa Mungu, inakuwa halisi katika maisha yetu ya kila siku.

12.2 Utendaji wa tabia ya mwili

Mfano wa wanyama wakali unatuonyesha kwa kiasi fulani jinsi tabia yetu ya mwili ilivyo. Tabia ya mwili inafanana na paka mkubwa mwindaji, anayetafuta mawindo na kutawala daima. Katika sarakasi paka wakubwa kama hao wanafugwa na mfugaji wao, lakini jambo hilo linafanikiwa tu kwa kusimama kwa uhakika na kwa kuwakazia macho daima ili kuwadhibiti. Mtazamo huu ni kielelezo kwetu pia. Tatalizungumzia zaidi baadaye.

Kwa sababu Wagalatia waliipenda sheria badala ya Roho, matendo ya tabia ya mwili yalijitokeza. Maisha yao pamoja yalitawaliwa na mwenendo wa tabia ya mwili (yaani wa dhambi). Katika mgogoro kati ya Roho na tabia ya mwili, Paulo hazungumzii kile kinachotokea *ndani yetu*, bali kile kinachotokea *kati yetu*. Mgogoro huu hauhusu kujiangalia ndani na kujitafakari – kile kinachotokea ndani yangu –, bali unahusu mwenendo unaoonekana na kuhisiwa na wengine: ama majivuno na wivu, ama utayari wa kuchukua mzigo wa mwingine (5:26-6:2). Chanzo cha la kwanza ni tabia ya mwili. Roho anataka mema kwa ajili ya mwingine, kama yalivyotimizwa kwa njia ya Yesu Kristo. Kwa hiyo Kristo anapaswa kuumbika ndani yetu kwa njia ya tunda la Roho, ambalo si kitu kingine ila kuonekana kwa asili yake. Matendo mafu ya tabia ya mwili, yanayoshuhudia juu ya Adamu aliyeandikiwa mauti, yanapaswa kuondolewa kabisa katika ushirika wa waumini. Jambo hilo linafanikiwa tu kwa kazi ya Roho. Tunda la kimungu halikui kwa juhudi zetu wenyewe, bali linaletwa na Mungu, ambaye peke yake anakuza.

Roho na tabia ya mwili wako katika mgogoro usio na mwisho. Inahusu kanuni mbili kuu, zinazowakilishwa kwa upande mmoja na asili ya dhambi, na kwa upande mwingine na Roho wa Mungu. Sisi sote tunahusika binafsi, kwa

sababu tabia ya mwili bado inakaa ndani yetu. Na Mungu mtakatifu anapambana nayo kwa kumtumia Roho wake Mtakatifu. Inashangaza! Nguvu kubwa namna hii lazima ihitajike – Mungu mwenyewe anashuka kwetu ili kuyaanza mapambano haya.

Mgogoro kati ya Roho na tabia ya mwili katika Waraka kwa Wagalatia haulengi kwanza kwamba mioyo miwili inapiga vifuaani mwetu. Haufundishi mgogoro usiokoma ndani yetu (unaofanana na ule unaoelezwa katika Warumi 7). Badala yake unahusu kwanza jinsi watu wa nyumbani mwa Mungu wanavyotendeanza. Hauhusu kile ninachokipitia nikiwa peke yangu, bali jinsi tulivyo tunapokuwa na ushirika pamoja. Bila shaka unahusu pia mgogoro ndani yetu, kwa sababu sisi wenyewe tuna tabia ya mwili ndani yetu, huku wakati huohuo Roho wa Mungu akikaa ndani yetu. Kwa kweli misukumo ya tabia ya mwili ipo pia tunapokuwa peke yetu.

Baada ya kuingia haraka hivi katika Waraka kwa Wagalatia, katika muktadha wa mada kuu ya kitabu, kwanza tunakusanya kutoka katika waraka huu yale ambayo tumekuwa kama Wakristo. Mgogoro kati ya Roho na tabia ya mwili Paulo anaushughulikia mwishoni mwa waraka tu.

12.3 Mkristo katika Waraka kwa Wagalatia

- Yesu alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu (1:4).
- tumeokolewa kutoka katika ulimwengu huu mbaya wa sasa (au zama hizi za sasa) (1:4)
- uhuru katika Kristo Yesu (2:4; 5:1)
- tumehesabiwa haki kwa imani katika Kristo (2:16-17)
- tumeifia sheria (2:19)
- tunaishi kwa ajili ya Mungu (2:19)
- tumesulubiwa pamoja na Kristo (2:19)
- Kristo anaishi ndani ya muumini (2:20)
- tunapendwa na Kristo (2:20)
- tumempokea Roho (3:2, 5)
- tumebarikiwa kwa imani (3:9)
- tumekombolewa kutoka katika laana ya sheria (3:13)
- tumeipokea ahadi ya Roho Mtakatifu (3:14)
- uzima si kwa sheria, bali kwa imani (3:21-22)
- wana wa Mungu kwa imani (3:26)

- Tumemvaa Kristo (3:27).
- Tuko katika Kristo (3:28; 5:6).
- Sisi ni wa Kristo (mali yake) (3:29; 5:24).
- tumekombolewa ili tufanywe wana (4:5-6)
- Roho wa Mwana yuko mioyoni mwetu (4:6).
- Mungu ni Baba yetu mpendwa (4:6).
- warithi kwa Mungu (4:7)
- Kristo anaumbika ndani yetu (4:19).
- tumezaliwa kwa kufuata Roho (kutoka kwa Roho) (4:29)
- tumeitwa na Mungu (5:8, 13)
- Tunaenenda kwa Roho (5:16, 25).
- Roho anatuongoza (5:18).
- Tunaishi kwa Roho (5:25).
- warithi wa ufalme wa Mungu (5:21)
- uzima wa milele (katika ufufuo) (6:8)
- watu wa nyumbani mwa imani (6:10)
- tumesulubiwa kwa ulimwengu (6:14)
- kiumbe kipya (6:15).

Huu ni muhtasari mkubwa wa kazi ya wokovu ya Mungu. Huu ndio ukweli wa wokovu (yale ambayo Mungu ameshatenda; kwa Kijerumani *Heilsindikati*) – yale ambayo “tayari sasa” hapa duniani ni mali yetu kwa imani. Baada ya kuijua kwa kina orodha hii ya wokovu, kutoka katika mtazamo huu tunashughulikia jinsi tunavyopaswa kuishughulikia tabia ya mwili na tamaa zake, na jinsi tunda la Roho linavyoweza kukua.

12.4 Sheria na tabia ya mwili – magurudumu mawili ya meno katika mashine moja

Ni kwa nini Paulo, katika waraka huu kwa Wagalatia, analishughulikia kwa namna halisi kiasi hiki suala la tamaa ya tabia ya mwili (kwa Kiyunani *sarx*; SUV: ‘mwili’) na shauku mbaya? Anaonyesha kwamba sheria haikuwasaidia kuishi maisha matakatifu. Kinyume chake, sheria iliyaleta tena maisha ya zamani ya Wagalatia. Sheria inaichochea dhambi na tamaa ya tabia ya mwili kwa makatazo yake na amri zake (taz. pia Warumi 7). Paulo anatoa uthibitisho mara moja: Wagalatia hawakuishika sheria iliyodai wampende jirani. Hata amri hii (ambayo si ya sheria ya Musa tu, bali pia ya Kikristo) iliwasumbua, kwa maana

walitendeana kwa namna isiyo ya urafiki hata kidogo (Wagalatia 5:15). Dai la kuwa waaminifu kwa sheria na hali halisi vilikuwa mbali sana kati yao. Tabia ya mwili na sheria vinakwenda pamoja, kwa sababu sheria inaelekezwa kwa mwanadamu wa asili ambaye hajazaliwa mara ya pili. Uhusiano huu, unaokatwa kwa mtu aliyekuja kuamini, Wagalatia waliurudisha tena. Je, kwa njia hii hawakuwa wakiufufua tena utu wa zamani? Lakini Paulo anawaonyesha jinsi upya wa uzima katika Roho unavyoonekana.

12.5 Mgogoro wa kale wa ulimwengu mzima na mgogoro wa sasa wa kibinafsi

Mwanzoni mwa historia ya wanadamu anguko lilitokea. Kwa sababu hiyo uadui umewekwa kati ya uzao wa mwanamke na uzao wa nyoka, yaani Ibilisi (Mwanzo 3:15). Kristo ndiye uzao wa mwanamke, naye atamponda nyoka kichwa, ingawa kwa maumivu. Uadui huu, ambao mwishowe ni pambano kati ya nuru na giza, ni wa ulimwengu mzima na upo kila mahali, lakini pia umefika *ndani* ya kila Mkristo. Kwa njia ya uzima mpya na kuingia kwa Roho moyoni mwa Mkristo, sasa kuna pale ncha mbili zinazopingana, ambazo haziwezi kamwe kufananishwa, wala mwelekeo wake hauwezi kamwe kuunganishwa kuwa mmoja – vita kati ya asili mbili. Majemadari wawili, yaani Roho na tabia ya mwili, wanakabiliana na kupigana. “Mkristo ni wakati mmoja jukwaa na kitu kinachogombaniwa, uwanja wa vita na zawadi ya vita, katika pambano kati ya tabia ya mwili na Roho.”⁶² Wapinzani hawa hawajui kusimamisha vita. Kamwe. Popote tulipo, tabia ya mwili ipo; tunaibeba pamoja nasi. Lakini Roho wa Mungu mwenye nguvu yuko ndani yetu pia. Yuko upande wetu daima ili kutusaidia katika mgogoro huu. Tuseme vizuri zaidi: Anataka kuyaongoza mapambano haya. Lakini Paulo hasisitizi vita vya kudumu, bali maisha ya kila siku kwa Roho. Mkristo anaweza kuwa na uhakika kwamba Roho atashinda. Mambo yasiyofuata kanuni hii, yaani makosa, yanathibitisha kanuni hiyo!

12.6 Ishini na enendeni kwa Roho!

Enendeni katika Roho (kwa Roho), wala hamtazitimiza kamwe tamaa za tabia ya mwili. Kwa maana tabia ya mwili butamani ikishindana na Roho, na Roho ikishindana na tabia ya mwili; kwa kuwa hizi zimepingana, bata hamwezi kufanya mnyotaka.

62. H. Schlier, *Galater*, uk. 181, imenukuliwa katika E. Mauerhofer, *Der Kampf zwischen Fleisch und Geist bei Paulus*.

Wagalatia 5:16-17

Badala ya kuishi kwa kufuata sheria, Wagalatia walipaswa kuenenda kwa Roho wa Mungu, ili wasiipe nafasi tabia ya mwili na matokeo yake. Kwa njia hiyo tu wapokeaji wa waraka huu wangeweza kutendeana kwa upendo.

Tabia ya mwili ni kitu kilicho hai kabisa. *Tamaa* na *shauku* ni nguvu kubwa; ndizo dalili za uhai wa tabia ya mwili. Tamaa ya tabia ya mwili inajumuisha kila shauku isiyo halali inayohusu kutimiza na kufuatilia malengo ya kujipenda nafsi. Hayo yanaweza kuwa mambo mengi – hata mambo ambayo huenda tusingeyashuku kamwe. Mtu, akiwa Mkristo, anaweza kulitenda jambo moja lilelile kwa Roho na pia kwa tabia ya mwili. Chanzo, msukumo na lengo ndivyo vinavyoamua kama mtu huyo analitenda jambo hilo katika Roho (yaani kwa nia ya kiroho) au katika tabia ya mwili (yaani kwa nia ya tabia ya mwili). Mmiliki wa zamani wa maisha yangu ya zamani, aliyenyang’anywa mamlaka, anawakilishwa na tabia ya mwili, yaani dhambi. Mmiliki wa zamani bado yupo, hata kama hana tena mamlaka wala haki. Bado yuko njiani pamoja nasi, maadamu bado hatujawa pamoja na Bwana na tunaishi katika mwili wetu wa duniani. *Tabia ya mwili* si kitu kimoja na mwili wa kibaiolojia, bali inautumia, kama vile nafsi na roho zinavyoutumia kuwa chombo. Matendo ya tabia ya mwili hayajumuishi tu matendo yanayofanywa kwa mikono na kwa miguu, bali pia mambo ya ndani yaliyo katika eneo la mawazo, hisia na mihemko (kiburi, ukaidi, dharau, kutokuwa na shukrani, chuki, mawazo machafu, uzinzi katika mawazo, tamaa mbaya au iliyopita kiasi ya kujipatia sifa, mambo ya uchawi na mengine mengi).

Tabia ya mwili inampinga Roho, na inataka kudai haki zake za zamani. Hapo zamani ilikuwa na nafasi ya pekee ya kuamua kila kitu, na imeweka mazoea ya dhambi katika fikira zetu na matendo yetu kama programu. Lakini sasa Roho amechukua umiliki na uongozi, ili ajipange dhidi ya tabia ya mwili na mazoea yake. Programu hii ya zamani haifutwi siku ya kuokolewa kwangu (yaani siku ya badiliko langu binafsi la wokovu na kuongoka kwangu). Badala yake, kwa Roho inapelekwa mahali inapostahili: kwenye mauti.

Kuna mgogoro ndani ya Mkristo unaotokea kati ya tabia yangu ya mwili na Roho Mtakatifu. Petro anauzungumzia anaposema kwamba tunapaswa kujiepusha na tamaa za tabia ya mwili, *zipiganazo na nafsi* (1 Petro 2:11). Yakobo anasema kwamba tamaa zinafanya vita katika viungo vyetu (Yakobo 4:1; taz. pia 1:13-15), zikitaka kulishwa na kutoshelezwa.

12.7 Kazi ya Mungu na kazi yetu – je, zinapingana?

Katika Agano Jipya mara nyingi tunahimizwa kutenda, ingawa wakati huohuo ni Mungu anayeleta jambo hilo. Ndivyo ilivyo hapa pia. Kwa hiyo kauli iliyo hapa (“Enendeni katika Roho”) ni agizo la wokovu (yale tunayoagizwa kutenda kwa sababu ya yale ambayo Mungu ameshatenda; kwa Kijerumani *Heilsimperativ*). Ni “namna ya kutenda na kutendewa”. Sisi ndio tunaoenenda (tunatenda), lakini tunapaswa kufanya hivyo kwa nguvu ya Roho (tunatendewa).

Tabia ya mwili na Roho zimepingana, *hata hamwezi kufanya mnayotaka*. Paulo anataka kusema nini kwa maneno haya? Je, kuna washiriki watatu katika mgogoro huu? Ni wazi: Kuna tabia ya mwili, kuna Roho wa Mungu, na kuna mimi, mtu mwenye wajibu, ninayeamua upande mmoja. Sentensi hii fupi “... hata hamwezi kufanya mnayotaka” ina angalau pande tatu:

1. Tumeitwa tupate uhuru (5:13), ili tusifanye kile ambacho tabia yetu ya mwili inakitaka.
2. Vita havipiganwi na sisi, bali na Roho.
3. Sisi (nafsi yetu, “mimi” wetu) tunasimama katikati ya mgogoro huu kama wahusika.

12.8 Mmeitwa mpate uhuru – lakini ni uhuru wa namna gani?

Neno kuu la mgogoro kati ya Roho na tabia ya mwili (5:1) – yaani ujumbe wa waraka huu – ni uhuru. Lakini katika pumzi ileile Paulo anaonya tusiutumie uhuru huu mbali na sheria ya Musa kuwa ruhusa kwa ajili ya tabia ya mwili. Kwa maana nje ya sheria ya Musa kuna sheria mpya inayotumika, yaani sheria ya Kristo (6:2)! Sheria mpya ni sheria ya Roho, ambayo kwayo Kristo anayatia alama maisha yetu, na matokeo yake yanaonekana katika matunda ya Roho. “Uhuru unatokea ndani ya sheria, si nje yake. Treni ina uhuru mkubwa kuliko wote lini? Inapojikwaa juu ya mawe na visiki? Bila shaka sivyo! Inapokubali ‘kulazimishwa’ kukaa juu ya reli, inakwenda vizuri bila kukwama, kwa maana ndivyo ilivyoundwa. Inahitaji ‘utaratibu’ na ‘nidhamu’ ya reli ili iweze kwenda vizuri na kwa kasi.”⁶³ Njia hii ya reli Paulo anaiita “kuongozwa” na “kuenenda” kwa Roho wa Mungu. Kwa sababu hiyo tunda la Roho, lenye sura nyingi, linakua, huku wakati huohuo matendo ya tabia ya mwili yakitoweka zaidi na

63. Jay E. Adams, *Grundlagen biblischer Lebensberatung*, uk. 256.

zaidi. Hiyo ndiyo njia mbadala ya Mungu badala ya sheria ya Musa, ingawa wakati huohuo tunaitimiza sheria ya Musa tunapolitimiza lile neno “mpendane” kwa Roho wa Mungu (5:14; taz. pia Warumi 8:3).

Hapa inahusu kuliacha eneo la sheria. Jambo hili limekwisha kutendeka kwetu pale Golgotha: Tumeifia sheria (Wagalatia 2:19; Warumi 7:6). Jambo hili likishatukia, hatusimami katika eneo lisilo la mtu yeyote, ambako hakuna sheria zinazotumika. Sisi ni mali ya Mungu – ni nchi *yake*. Nchi hii inagombaniwa kwa vita, kwa sababu lengo bado halijafikiwa. Mgogoro kati ya Roho na tabia ya mwili unamngoja kila mtu anayeingia katika uzima mpya. Tukiongozwa na Roho, hatuko chini ya sheria; njia hizi mbili za kuishi (sheria na Roho) haziwezi kwenda pamoja.

12.9 Roho anapigana kwa ajili yetu

Kwa kweli inaonekana kana kwamba katika mgogoro huu tuna nafasi ya kuwa watazamaji tu. Kwa sababu Roho na tabia ya mwili wanapigana ndani yetu, hatuwezi tena kufanya tunachotaka, kwa sababu hao wawili wanafanya wanachotaka! Tabia ya mwili inazaa matendo ya tabia ya mwili, na Roho anazaa tunda la Roho. Albrecht (tafsiri ya Biblia ya Kijerumani) inatafsiri hivi: “Kwa maana tabia ya mwili pamoja na tamaa yake inampinga Roho kwa uadui, na vivyo hivyo Roho

anaipinga tabia ya mwili. Wote wawili wanapigana wao kwa wao, wala hawavumili kwamba mtende kwa kufuata mapenzi yenu.” Somo ni kwamba katika pambano hili “hatufanyi tunachotaka”, hata kama kimekusudiwa kwa nia njema kiasi gani. Vita dhidi ya tabia ya mwili vinapiganwa na Roho. Lakini havitupiti kando, kana kwamba havituhusu. Hatuwezi kwenda likizo na kumwacha Roho apigane. Kinachomaanishwa ni kwamba vita dhidi ya tabia ya mwili ni sehemu ya uzoefu wetu wenyewe, lakini tukipigana kwa juhudi zetu wenyewe vinashindwa. Hatuna nguvu maadamu hatumwachii Mungu vita hivi. Kwa kweli tunayo nia ya kushinda, lakini hatuna njia za kufanya hivyo. Mgogoro huu unatokea ndani ya nafsi yangu, yaani moyoni mwangu, lakini huko jemadari mpya, Roho, ameshika uongozi.

12.10 Katikati ya vita

Turudie maneno haya kwa maneno ya Neue Genfer Übersetzung (NGÜ, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani):

“Ninataka kusema nini kwa haya? Mwacheni Robo wa Mungu auongoze mwenendo wenu, ndipo hamtazikubali tena tamaa za asili yenu wenyewe. Kwa maana asili ya kibinadamu pamoja na tamaa zake inampinga Robo wa Mungu, na Robo wa Mungu pamoja na tamaa yake anaipinga asili ya kibinadamu. Hao wawili wanashindana wao kwa wao, na kila upande unataka kuwazua msifanye kile ambacho upande ule mwingine unawasukuma kukifanya.”

Hakuna “mimi” asiyeegemea upande wowote anayeweza kuukwepa mgogoro huu kati ya tabia ya mwili na Roho. *Nafsi* yetu inapata nguvu ya kusukuma matendo yake ama kutoka kwa tabia ya mwili ama kutoka kwa Roho. Kamwe sisi si watazamaji wasiotenda kitu, bali tunasimama katikati kabisa ya mgogoro. Tunawajibika kwa yote tunayoyaamua, tunayoyafikiri na tunayoyatenda. Ninaposimama katikati ya pambano lenyewe, katika jaribu na kushambuliwa, ni lazima niamue waziwazi na kusimama upande mmoja. “Ingawa ... Roho Mtakatifu ameingia ndani yako, na humo kwa nafsi yake anamwakilisha Mungu Baba pamoja na Mungu Mwana, hata hivyo kamwe hatauvunja uhuru kamili wa mapenzi yako mwenyewe. Hatakuondolea uamuzi wako unaoufanya kwa wajibu wako mwenyewe. ... Hata hivyo, akitawala katika kila eneo la moyo wako, akiamua hivyo mwenendo wako, jambo hilo linatokea tu kwa uchaguzi wako mwenyewe ulio huru na kwa idhini yako ya furaha. Lakini haki hii ya kukubali au kukataa ndiyo inayokuinua wewe kama mwanadamu juu ya ulimwengu wa wanyama, na kukufanya kuwa kiumbe chenye maadili ambacho Mungu amekukusudia kuwa. Hiyo pia – na hiyo peke yake – ndiyo inayokuwezesha kumpenda Mungu kwa kumrudishia upendo, na hivyo kuujibu upendo wake. ‘Ndiyo’ hii ya furaha kwa Mungu katika kila dakika ya maisha yako inaujaza moyo wa Muumba furaha kubwa kuliko maajabu yote ya kususimua (ya kuvutia) ya mamilioni ya dunia, zilizorushwa kwa neno lake la uweza wote hadi katika ukomo usio na mwisho wa anga. Zote hizo hazina uwezo wa kumpenda, kwa sababu hazina uwezo wa kuchagua kwa hiari. Kwa hiyo fursa ya kuwa wewe mwenyewe, na kuwa mwanadamu, iko katika hili: kwamba unaruhusiwa kumjua Mungu, kumchagua na kumpenda. Hiyo ndiyo fursa yako binafsi kabisa.”⁶⁴

Uwepo wa Roho si jambo linalojiendesha lenyewe lenye uhakika wa kushinda uliowekwa ndani yake. Kauli mbiu ya maisha yetu inapaswa kuwa hii: kuishi

64. W. Ian Thomas, *Tote können nicht sterben*, uk. 115.

pamoja na Yesu, kukaa karibu naye, na kuliacha Neno lake likae ndani yetu kwa wingi. Kwa njia hiyo tutamchagua Roho na kuikataa tabia ya mwili.

Kazi ya Mungu na wajibu wetu kamwe havizuiani. Tukizungumza juu ya utendaji wa Mungu tu, huenda tukajiacha tuchukuliwe na hali ya kutotenda. Tukiutazama daima wajibu wetu na majukumu yetu, hatumtazami Kristo, bali dhambi tunayotaka kuishinda. Kwa mtazamo huu tutakuwa katika hatari ya kupigana kwa nguvu zetu wenyewe, na kubanwa na wasiwasi. Roho ndiye kanuni mpya ya maisha, na pia nguvu ya kuishi kwa kuifuata. Uongozi wake si kuonyesha njia tu; Roho ni mwenzetu wa safari, anatumtangulia.

12.11 Virusi na chanjo

Kuhusu jambo hili, mfano mmoja zaidi unaoonyesha nafasi ya mapenzi yangu, ya tabia ya mwili na ya Roho. Tuvilinganishe vijidudu vya magonjwa vilivyolala ndani ya mwili wangu na tabia yetu ya mwili. Mtu akiishi maisha yenye afya, ni mara chache atakapougua. Nikila vibaya, nisipovaa nguo za kutosha, hilo linaweza kuniletea mafua. Nikimeza dawa wakati huo (uamuzi huu ni lazima niufanye mimi), dawa hiyo itaanza ndani ya mwili wangu kupigana na mafua. Mapambano haya kweli yanatokea ndani ya mwili wangu, lakini si mimi ninayepigana. Lakini ninaweza kuyaanzisha mapambano haya kwa uamuzi wa makusudi wa kumeza dawa. Zaidi ya hapo ninaweza kuisaidia dawa ifanikiwe kwa kupumzika sana, kwa chakula kizuri na hewa safi.

12.12 Matendo ya tabia ya mwili ni nini?

Paulo haachi shaka yoyote juu ya kile anachokimaanisha kwa tabia ya mwili (kwa Kiyunani *sarx*; SUV: ‘mwili’) na matendo yake. Orodha yake ya matendo haya haijakamilika, kana kwamba hakuna dhambi nyingine zaidi ya hizi zilizotajwa hapa. Kwa maneno ya mwisho ya orodha hiyo, “na mambo mengine kama hayo”, Neno la Mungu halimpi kila msomaji nafasi tu ya kuiendeleza orodha hiyo, bali kwa njia isiyo ya moja kwa moja linamwagiza ayatambue matendo ya tabia yake mwenyewe ya mwili.

Matendo ya tabia ya mwili yanatofautiana, katika matokeo yake na pia katika jinsi yanavyopimwa. Si bure kwamba uasherati unatajwa kwanza. Lakini zikiwa “dhambi ndogo au kubwa”, zote zinatoka katika chemchemi ilcile mbaya. Tabia yetu ya mwili inaweza kutenda kila kimoja cha mambo yaliyotajwa hapa (katika matendo na pia katika nia). Kwa maana hiyo tabia ya mwili ni kama mbegu

ambamo dhambi za kila namna zimefichwa, ili siku moja ziweze kujitokeza. Kwamba Paulo, tofauti na anavyosema juu ya Roho, hazungumzi juu ya *tunda* la tabia ya mwili, inaonekana kuhusiana na matendo ya sheria, ambayo Wagalatia walitaka kuyategemea. Kwa maneno mengine: Tunaweza kuyatenda matendo ya tabia ya mwili kwa nguvu zetu wenyewe, lakini hatuwezi kuyazaa matunda ya Roho sisi wenyewe. Kwa hilo tunamhitaji Roho Mtakatifu. Basi, matendo ya tabia ya mwili ni dhahiri, nayo ni haya (5:19-21):

- **Uasherati** (kwa Kiyunani *porneia*) – zinaa, *kila* tendo la kingono nje ya ndoa
- **Uchafu** – upotovu, mambo machafu; mwenendo usio na kizuizi, yaani usio na haya, katika mambo ya kingono, iwe ndani au nje ya ndoa; uharibifu wa haiba nzima, unaotia sumu kila eneo la maisha
- **Ufisadi** – kukosa kiasi, kukosa kujizuia, kupumbaza akili na hisia
- **Ibada ya sanamu** – kuabudu kila kitu kinachomwondoa Mungu na mapenzi yake kutoka nafasi ya kwanza katika maisha ya mtu (ibada ya sanamu halisi, vilevile ibada ya sanamu ya kimawazo ya siku zetu); ubinafsi
- **Uchawi** (kwa Kiyunani *pharmakeia*) – uganga, ulozi, mambo ya siri ya giza, kuwasiliana na pepo, madawa ya kulevya
- **Uadui** – kujitenga na watu, ugomvi, chuki, hasira mbaya dhidi ya watu wengine
- **Ugomvi** – mafarakano, mabishano, roho ya ugomvi
- **Wivu** – husuda, mwenendo wa ubinafsi na mwingine wowote unaotafuta faida yake mwenyewe, shuku
- **Hasira** – ghadhabu, milipuko ya hasira, kuwashambulia wanaotuzunguka bila kujizuia, kung’ang’ania maoni yake mwenyewe kwa ukali
- **Fitina** – mabishano, hila
- **Faraka** – mtawanyiko, mafarakano, migawanyiko
- **Uzushi**⁶⁵ – mafundisho potofu, migawanyiko, madhehebu; kujenga makundi yanayoleta usumbufu
- **Husuda** – mazoea ya kutompendelea mwingine jema lolote
- **Uuaji** – chuki, mauaji (kwa kweli, si katika mawazo tu)
- **Ulevi** – kunywa pombe kupita kiasi, hali ya kulewa
- **Ulafi** – karamu za ulevi na ulafi, kula kupita kiasi, anasa
- **na mambo mengine kama hayo.**

65. Hivyo ndivyo yalivyo maneno ya tanbihi katika Elb 2003 (tafsiri ya Biblia ya Kijerumani). Katika maandiko makuu ya tafsiri hii ya Biblia hapa imeandikwa “madhehebu” (*Sekten*).

Hakuna wakati ujao katika ufalme wa Mungu kwa watu wanaotenda mambo haya, ambao kwao mambo kama hayo ni ya kawaida, wanaodumu ndani yake, na wasioziungama na kuziacha dhambi zao (5:21).

12.13 Tunda la Roho wa Mungu

Tunda lile tamu sana, ambalo Baba na Mwana wanalifurahia, na ambalo vilevile ni furaha kwa wale wanaobarikiwa nalo, linazaliwa ndani ya muumini na Roho wa Mungu. Siwezi kufanya tunda likue, kwa sababu Mungu ndiye anayekuza⁶⁶ (1 Wakorintho 3:6). Mimi mwenyewe ninapaswa kuandaa “mazingira” ambayo ndani yake ukuaji mzuri unawezekana. Ninaweza kujaribu kuandaa udongo mzuri; ninaweza kuzuia na kuondoa magugu ya tabia ya mwili; na ninaweza kuhakikisha kuna “umwagiliaji” wa kutosha kwa Neno la Mungu. Lakini katika hayo yote hatupaswi kuupuuza “muujiza” wenyewe: Zaidi ya ishara na miujiza yoyote, ni tendo la Mungu lisilo la kawaida wanadamu wanapobadilika kutoka kuwa wenye dhambi waliojaa chuki, hadi kuwa viumbe ambao upendo wa Mungu umemiminwa miyoni mwao, nao wenyewe wanapenda kama Mungu anavyopenda. Lakini tunda la Roho ni (5:22-23):

1. **Upendo** – upendo wa kimungu ulio tayari kujitoa dhabihu, hapa hasa ndani ya kanisa la Mungu; si hisia, bali ni uamuzi wa mapenzi. Bila upendo huu kwa Mungu na kwa wanadamu, hata katika maisha ya Kikristo kila kitu hakina thamani (1 Wakorintho 13). Tunapenda kwa sababu yeye alitupenda kwanza.
2. **Furaha** – furaha ya pamoja ya watu wa Mungu wanaoenenda katika Roho, hata katika makusanyiko yao; furaha ya kweli juu ya yale ambayo Mungu alitutendea sisi na wengine, anayoyatenda sasa na atakayoyatenda kufuatana na ahadi yake; furaha ya uzima katika Kristo
3. **Amani** – si kukosekana kwa ugomvi tu, bali upatanisho kati ya watu, kuishi pamoja kwa upendo wa moyo, umoja, ukamilifu
4. **Uvumilivu** – subira na moyo mkuu katika kuwashughulikia wengine; utayari wa kudumu wa kuwavumilia wanadamu wenzetu na hali; upendo katika upande wake wa kuvumilia, lakini wenye kudumu
5. **Utu wema** – mtazamo wa nia njema, ulio tayari kusaidia daima na wenye kuelewa, tabia ya upole, ukarimu; upande wa upendo unaotenda

66. Taz. pia Mathayo 6:28: “Fikirini maua ya mashambani, jinsi yanavyokua; *hayafanyi kazi*, wala hayasokoti” (msisitizo ni wa mwandishi).

6. **Fadhili** – wema wa moyo, unaofanana na utu wema; kumpa mwingine kilicho haki na chema
7. **Uaminifu (imani)** – kumtumaini Mungu; fadhila ya kuaminika, unyoofu, uaminifu; kumwiga Mungu, ambaye daima analishika neno lake na ni mwaminifu kwa ahadi zake
8. **Upole** – wema, nguvu na upole wa moyo kwa wakati mmoja (hakuna neno moja la Kijerumani linalofaa kabisa); kinyume cha ubinafsi na kudai kupita kiasi; unyenyekevu wa moyo kuhusu nafsi yake mwenyewe
9. **Kiasi** – kujitawala, nidhamu binafsi na kujidhibiti, utulivu wa ndani.

Tunda, yaani matunda, ni mengi na ya aina nyingi. “Orodha” hii pia, kama ile iliyotangulia, haijakamilika, bali inawakilisha mengine. William Barclay anasema ni vigumu katika orodha hii kupata maana kamili ya kila neno, na pia mipaka inayoyatenganisha.⁶⁷ Katika sifa hizi zote za kimaadili na fadhila hizi mtu anaweza kutambua kwamba ni karibu haiwezekani kwa mwanadamu kuziona katika maisha yake kwa kudumu, hata kwa kiasi fulani. Kwa kweli ni tunda la Mungu.

Paulo anaimaliza orodha yake kwa kuirudia ile hoja kuu inayopita katika waraka mzima: “*Juu ya mambo kama hayo hakuna sheria*” (mstari wa 23). Kwa maneno mengine: Fadhila hizi zikionekana kati yetu kwa sababu ya uwepo wa Roho, sheria haina kazi tena. Watu wanaopendana kwa Roho hawahitaji tena Torati iwaamuru: Usiue.

12.14 Tabia ya mwili ni ya kusulubiwa msalabani

Mkristo amechukua msimamo ulio wazi kabisa kuhusu tabia ya mwili. Yeye mwenyewe ameipigilia tabia ya mwili msalabani. Tunaamini na tunatenda kwa kufuata jambo hilo. Tabia yetu ya mwili haikustahili kitu kingine ila mauti msalabani. Ndivyo hasa Paulo anavyosema:

“Na hao walio wa Kristo wameisulubisha tabia ya mwili pamoja na shauku zake na tamaa zake.”

Wagalatia 5:24

Aliye wa Kristo amefanya hivyo mara moja tu kwa ajili ya wakati note: Tulipomwamini Kristo, tuliyahukumu maisha yetu ya zamani na kuyakataa.

67. William Barclay, *Fleisch oder Geist?*, Augsburg, 1968.

Tuliikubali hukumu ya kifo ya Mungu juu ya maisha yetu yasiyomcha Mungu, na juu ya kile kilichokuwa nguvu ya kusukuma maisha hayo yasiyomcha Mungu: tabia ya mwili. Kwa nini kusulubiwa? Kwa sababu Kristo, mahali petu, aliichukua juu yake msalabani hukumu ya kifo juu ya utu wetu wa zamani, kwa ajili yetu.

Tabia ya mwili inabeba ndani yake shauku na tamaa kama dawa yake ya uhai. Kwa hatua ya imani ya kumwendea Kristo tumezikataa. Jambo hilo linatuwekea wajibu, kwa maana kile ambacho mtu mwenyewe amekisulubisha na kukiua, kinapaswa kubaki katika mauti, wala kisionekekane tena katika maisha yetu. Lakini licha ya kusulubiwa, licha ya kuuawa, tabia ya mwili pamoja na matendo yake bado ipo. Bado iko ndani yetu bila kuweza kurekebisha. Jambo hili linalingana na neno kwa Warumi, kwamba tujihesabu kuwa wafu kwa dhambi (Warumi 6:11). Mungu alitutendea jambo fulani, ili iwezekane kuukwepa udikteta wa dhambi. Ndivyo ilivyo pia katika neno hili. Msalaba wa Yesu Kristo ndio mwisho wa tabia ya mwili, mwisho wa utu wa zamani, mwisho wa “mimi” wa zamani. Bila msalaba, na bila kulijua jambo hili, kuenenda katika Roho hakuwezekani.

Haisemwi kwamba tunapaswa kuisulubisha tabia yetu ya mwili kila siku. Jambo hilo linasemwa mara nyingi kwa nia njema. Lakini ukweli ni kwamba tunapaswa kuchukulia kwamba ilisulubiwa mara moja – pamoja na Kristo. Huo ndio mwanzo wa maisha mapya, katika hali bora kabisa iliyotolewa na Mungu mwenyewe. Sasa, baada ya tukio la msalaba, katika upya wa uzima, tunashughulika na *matendo* ya tabia ya mwili moja moja. Tabia ya mwili inapigana “vita vya msituni” kwa kuvizia. Mashambulizi haya tunapaswa “kuyafisha” kwa nguvu ya Roho Mtakatifu (Warumi 8:13; Wakolosai 3:5). Kufisha kunamaanisha kutoyaacha yapate uhai tena. Ninajikumbusha mauti ya Kristo kwa ajili ya utu wangu wa zamani, na kile kilichomgharimu kufa kwa ajili ya hilo. Kwa njia hiyo ninafikia tena na tena mtazamo na hukumu ya Mungu juu ya tabia ya mwili, na jambo hilo linanisaidia kuipinga kwa uthabiti.

12.15 Mtu ni nani baada ya kusulubiwa pamoja na Kristo?

Tunapoeleza kuwa watu ambao sisi wenyewe tumeisulubisha tabia ya mwili, huo ni upande *mmoja* tu wa sarafu. Upande mwingine Paulo anaueleza mwanzoni mwa waraka:

... nimesulubiwa pamoja na Kristo, lakini ninaishi, wala si mimi tena,⁶⁸ bali Kristo anaishi ndani yangu; na ubai nilio nao sasa katika mwili, ninao kwa imani, imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.

Wagalatia 2:19-20

Huenda haya ndiyo maelezo yanayofaa kuliko yote ya maana ya kuwa Mkristo. Maisha yetu ya zamani, yaani hali yetu ya kujiamulia wenyewe, ambamo sindano ya dira daima ilielekea kwetu wenyewe, yamesulubiwa pamoja na Kristo. Hiyo ndiyo iliyokuwa njia pekee ya kuwekwa huru kweli mbali na maisha ya zamani – na zaidi ya yote kwa namna ambayo jambo hilo lilitendeka kihalali mbele ya haki na utakatifu wa Mungu. Hakuna mtu anayetaka kupoteza maisha yake na kuacha kujiamulia mwenyewe, kwa sababu anaogopa hasara akiwaza kile kitachokuja baadaye. Hivyo ndivyo tabia ya mwili ilivyotuwekea “programu”, na “programu” hii bado inafanya kazi ndani yetu. Ni mara ngapi tunashikamana na kile tulicho na tulicho nacho! Hatutambui vya kutosha kile ambacho Mungu anakiweka mahali pa yale ya kale. Lakini neno hili haliachi shaka. “Kwa ukali kabisa: Nimekufa, ninaishi! Mfu katika mauti ya Kristo, hai katika uzima wa Kristo. Hili limesemwa kwa nguvu kiasi kwamba si rahisi kwa uwezo wetu wa kuelewa kulishika. Tunafikiri: Hili haliwezekani, kwa maana mtu anabaki kuwa yeye mwenyewe; wewe unabaki kuwa mtu yuleyule ulivyo, sivyo? Baadhi wametafuta suluhisho hapa kwa kumgawa mwanadamu katika sehemu tatu: roho, nafsi na mwili, ambapo mwili na nafsi lazima vife ili roho iweze kuishi. Lakini hatupaswi kuyatazama maneno ya Paulo kwa mtazamo wa Kimagharibi, bali tuyapokee kwa ajili ya kusudi yaliyokusudiwa, na tujaribu kuyaelewa kufuatana na lengo lake. Maisha katika Adamu yamekwisha, kwa kuwa sasa haki ya Mungu imefunuliwa katika Injili. Uzima wa Kristo unaanza kwa kila mtu anayeipokea Injili.”⁶⁹

Kwa kweli tunapaswa kuelewa mstari huu wa Biblia, ulio kiini cha maisha yetu, kwa urahisi kadiri iwezekanavyo. “Wewe utabaki daima kuwa wewe mwenyewe, wala si mtu mwingine yeyote. Mtu anayeamka asubuhi ni yuleyule hasa aliyekwenda kulala jioni iliyotangulia. Kwa hiyo ni lazima uukubali ukweli huu: Wewe mwenyewe ndiye mtu ambaye ni lazima uishi naye siku zako zote zilizobaki. Lakini pili, ni mapenzi ya Mungu! Hakutaka kamwe uwe mtu

68. Maneno “lakini ninaishi, wala si mimi tena” yanafuata maneno ya tanbihi ya Elb 2003 mahali hapa.

69. H. P. Medema, *Romeinen 7 enzovoorts*, uk. 80.

mwingine yeyote isipokuwa wewe mwenyewe. Lakini anataka sasa uwe kweli yule mtu aliyekukusudia kuwa ...

‘Mimi’ wangu (yuleyule anayetenda dhambi ndani yangu) amesulubiwa pamoja na Kristo. ‘Ninaishi (‘mimi’ yuleyule ambaye Kristo amenifanya kuwa), lakini si mimi tena, bali Kristo anaishi ndani yangu’ (Wagalatia 2:20) ... Hupotezi chochote cha haiba yako mwenyewe unapochukua mahali pako msalabani pamoja na Kristo kwa imani. Kinyume chake, haiba yako inabadilishwa. Unakuja tu chini ya uongozi mwingine, hata inasemwa juu yako: ‘Mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya’ (2 Wakorintho 5:17).’’⁷⁰

Mahali pa utu wa zamani na pa “mimi” wa zamani sasa anaingia mwingine, tena pamoja na wingi wa uzima wake. Huu ni uzima wa ushindi, uzima wa ufufuo, uzima wa kimungu. Kwa kweli ni Bwana Yesu Kristo mwenyewe anayeingia sasa katika maisha yangu, katika haiba yangu, yaani moyoni mwangu, ili akae huko milele. Huko ndiko kuwa Mkristo! Alama ya Ukristo ni msalaba mtupu, kaburi tupu, Kristo juu ya kiti cha enzi, na Kristo ndani yangu! Si badiliko la maisha nililowekewa kutoka nje; la, ni Kristo anayeishi ndani yangu na kutimiza yale yanayompendeza Mungu. Ni maisha mapya yanayotoka katika moyo uliofanywa upya. Ni Kristo mwenyewe anayetenda kazi, naye ndiye chemchemi ya nguvu isiyokauka kwa ajili ya maisha yangu mapya. Yeye si chemchemi tu kwa ajili ya “mambo ya kiroho” (kusoma Biblia, kuomba, kuhubiri Injili n.k.), bali ni chemchemi kwa ajili ya maisha yangu yote, hata kwa ajili ya kazi yangu, kwa ufupi kwa ajili ya kila sekunde ya maisha yangu. Sijifanyi tu kana kwamba ni hivyo – ni kweli halisi kwamba Kristo anaishi ndani yangu. Maisha haya yanatambulika kwa kumtumaini Mwana wa Mungu, ambaye kwa dhabihu yake kwa ajili yangu, na kwa ajili ya kila mtu binafsi, ndiye aliyeyawezesha yote.

12.16 Kujitwika msalaba kila siku

Kabla Yesu hajasulubiwa pale Golgotha, alikwisha kuzungumza juu ya msalaba – si juu ya msalaba wake tu, bali juu ya msalaba wa kila mmoja ambaye angemfuata. Katika Luka 9:23 (taz. pia Luka 14:27; Mathayo 10:38; 16:24; Marko 8:34) imeandikwa:

70. W. Ian Thomas, *Tote können nicht sterben*, uk. 106 na kuendelea.

“(Yesu) akawaambia wote, Mtu akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuata.”

Hapa Bwana Yesu anazungumza juu ya kujikana nafsi (jambo ambalo mara nyingi linaumiza). Anayemfuata yeye hajifuati mwenyewe, wala ubinafsi wake na malengo yake, bali anamfuata Bwana na Mwalimu wake. “*Mimi*” wangu ametolewa kwa mauti; hana maana tena. Kuuchukua msalaba huu kwa makusudi na kuukokota hadi mahali pa kunyongwa ni wajibu wa kila siku wa mwanafunzi. Bila shaka huu ni mfano. Inahusu kanuni ambayo Bwana anaiweka wazi kwa mfano huu mkali. Anayeyapoteza maisha yake (yaani msalabani pa kujikana nafsi na kujiachilia) atauona uzima wa kweli, uzima tele (Mathayo 10:39). Basi, maneno haya ya Yesu hayalingani kabisa na yale ambayo Paulo aliwaambia Wagalatia kuhusu kwamba wameisulubisha tabia ya mwili. Sababu mojawapo ni kwamba kwa Paulo inahusu mambo maovu ya tabia ya mwili. Lakini Yesu anaangalia pia mambo ambayo si lazima yawe maovu, bali kinyume chake. Kuna mambo ya kutosha yaliyo mema yenyewe, lakini ambayo, tukiyachunguza kwa makini, yanatuzuia tusimfuata Yesu kwa uthabiti.

Msalaba *wangu* (wa kibinafsi) si jambo la kinadharia, bali unanilenga mimi binafsi, sifa zangu za pekee na hali yangu. Ni yale maeneo ambamo tabia ya mwili bado inaonekana kwangu. Msalaba wa dada yangu na wa kaka yangu huenda unaonekana tofauti. Kujikana nafsi kwa namna hii kunagharimu sana kupita kiasi. Kuubeba msalaba pia ni tamasha la aibu kuliko zote. Anayeubeba msalaba havezi kutarajia heshima kutoka kwa wanadamu.

12.17 Kuishi na kuenenda kwa Roho: kuwa na kutokuwa

Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho.

Wagalatia 5:25

Msalaba umeyamaliza ya kale kwa ukamilifu wa Mungu. Tena tumezaliwa mara ya pili kwa njia ya Roho, kwa sababu tabia ya mwili ilikuwa imeharibika. Tumehuishwa, tumetoka katika mauti ya kiroho na kuingia katika uzima. Uzima huu ndio maisha mapya katika Kristo, huu ndio utu mpya. Hapa Roho Mtakatifu anaitwa chanzo na nguvu ya uzima huu mpya. Basi maneno haya mawili, kuishi na kuenenda, yanahusianaje? Yanatofautiana kwa nini? Kuishi ni mapigo ya moyo ya utu mpya – ukweli kwamba upo. Unakidhihirisha kiumbe

kipya, ambacho Kristo mwenyewe, aliye Mkombozi na Aliyefufuka, amekiumba. Sisi ni kazi yake bora. Ya kale yamepita, yamekuwa mapya.

Lakini aliyezaliwa mara ya pili si sanamu, bali ni *mtu* mpya aliye hai, aliyeumbwa kwa kufuata mfano wa Yesu Kristo. Mtu mpya anaenenda kwa kufuata kielelezo chake, yaani Kristo, aliye mwanzo na mwanzilishi wa kiumbe kipyaa. Kuenenda hakumaanishi tu *kuwa* (kuishi), bali pia *kutenda*. Uzima unalazimu mwendo na uchangamfu. Mwenendo maana yake ni kupiga hatua moja baada ya nyingine. Uzima unaotoka kwa Mungu daima huzaa matunda, yaani tunda la Roho. Gari linahitaji mafuta ili liweze kwenda. Tangi likiwa tupu, inabidi kulisukuma. Injini ya umeme inahitaji umeme, la sivyo haitamfaa mtu yeyote. Mkristo anamhitaji Roho Mtakatifu ili alizae tunda la Roho. “Kuongozwa na Roho kunamaanisha kwamba yeye anakaa ndani yetu na pamoja nasi, kama kiongozi mwenye nguvu, mwalimu mwenye hekima, mkufunzi mvumilivu. ‘Kuongoza’ huku si tukio la mara moja la kushangaza, bali ni mchakato unaoendelea mbele bila kukoma.”⁷¹ Kwa mara nyingine: kuishi peke yake hakutoshi, kama vile kuwepo tu kwa Roho kusivyotosha. Hatupaswi tu kumwita Roho kuwa wetu, bali tunapaswa pia kujiweka chini ya madai yake ya kutumiliki, kutuongoza na kutuelekeza. Moto huu tunapaswa kuuchochea tena na tena, na pia sisi kwa sisi, badala ya kumzima Roho.

12.18 Kuenenda kwa Roho – kunawezekanaje?

Huenda tumegundua kwamba Paulo anasema tunapaswa kuenenda kwa Roho, lakini haelezi kwa undani jinsi tunavyopaswa kufanya hivyo. Waraka mzima unafanana na “utetezi kwa ajili ya Roho”. Kwa hiyo sheria inaondolewa kabisa: “Kwa nafsi ambayo bado haijaelewa ukombozi wa kweli ni nini, ambao Mungu ametuandalia, dawa iliyo ya kawaida zaidi (na iliyo karibu zaidi) ni kujaribu kwa sheria. Hiyo si dawa, bali ni kinyume chake kabisa.”⁷² Kuitafuta sheria ili itusaidie ni kinyume kabisa cha kile ambacho kuenenda kwa Roho kunamaanisha. Inaonekana Paulo anachukulia tu kwamba kuishi kwa Roho ni uzofu halisi unaoweza kuhisiwa. Maandishi yake yenyewe yanatoa alama za kuongozwa na Roho:

- kutoifanya sheria hiyo (au sheria yoyote) kuwa kanuni ya maisha

71. H. P. Medema, *Romeinen 7 enzovoorts*, uk. 138.

72. F. W. Grant, *Numerical Bible*, Juzuu 6, uk. 313.

- Mtu huyo *anataka* kuenenda kwa Roho. Anayeenenda kwa Roho analikabili agizo hilo na uamuzi wa makusudi, unaorudiwa tena na tena, wa kumpa Roho utawala juu ya maisha yetu.
- kukubali kwa imani kwamba tabia yetu ya mwili ni mbaya, haifai kitu, na ilipaswa kusulubiwa pamoja na Kristo
- kuwa makini kuzaa matunda ya Roho kwa wengine
- kuwa makini kutoyaruhusu matendo ya tabia ya mwili
- Ninakiri na kuamini: Kristo na Roho wake wanaishi ndani yangu.
- kutoenenda kwa juhudi zetu wenyewe zinazojielekeza kwetu wenyewe, bali kwa kumtegemea Mungu, kumwomba na kumtazamia atupe uongozi wa Roho
- kutojikaza katika vita dhidi ya tabia ya mwili iliyo ndani yangu, bali kumkazia macho Kristo na yote yanayohusiana naye.

12.19 Kujikwaa na kuinuka

Ndugu zangu, mtu akighafilika katika kosa lo lote, ninyi mlio wa Roho mrejesheni upya mtu huyo kwa roho ya upole; ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe pia.

Wagalatia 6:1

“Kuja kwa Roho kunamaanisha kwamba ‘maambukizi ya kimungu’ yamelipuka ..., lakini si kwamba ukamilifu wa kimungu umewadia. Maisha yetu sasa yako chini ya uongozi wa yule ambaye hapo mwanzo aliivuvia sheria, ingawa jambo hili, bila shaka, halimaanishi kwamba watu walio miongoni mwa watu wa Mungu hawawezi ‘kughafilika katika kosa’.”⁷³ Si jambo la kweli kudhani kwamba tunaishi katika ushindi daima na peke yake. Mgogoro kati ya Roho na tabia ya mwili unatumia mfano wa vita, na kushindwa pia ni sehemu ya vita. Katika Kristo sisi ni washindi “tayari sasa”, lakini “bado” hatujafika kwenye lengo. Ushindi wa mwisho ni hakika kwetu, lakini katika mstari wa mbele wa vita adui wakati mwingine anaiteka ngome moja au nyingine. Hilo ndilo lililompata yule ambaye Paulo anamwita hapa mtu, ambaye amefanya kosa.

Wale walio na nia ya kiroho wanapaswa kumrejeshwa mtu kama huyo kwa upole. Ushirika ulio hai, wenye kuaminiana na wenye bidii wa waumini, kuishi pamoja na urafiki katika Bwana vina kazi muhimu katika mgogoro kati ya Roho

73. Gordon Fee, *Der Geist Gottes und die Gemeinde*, Metzingen, 2005, uk. 192.

na tabia ya mwili – katika kutiana moyo, na pia katika kurejeshwa na kuwarejesha wengine. Katika hilo wale walio na nia ya kiroho wanapaswa kujihadhari, wasiye wao pia wakaangukia jaribu lilelile; kwa maana ingawa wana mwelekeo wa kiroho, tabia ya mwili pamoja na tamaa zake zote, shauku zake na vishawishi vyake ni hatari ya kudumu ndani yao pia.

Hapa Paulo hazungumzii kosa fulani mahususi. Kwa makosa yale yote yasiyohesabika ya aina mbalimbali, madogo na makubwa, mpango uleule wa dharura wa Mungu wa kurejeshwa unatumika. Kosa ni uvunjaji wa sheria, hatua iliyokosewa, kujikwaa katika mbio za imani. Kosa linajumuisha dhambi, tendo la tabia ya mwili, kukubali jaribu.

Bila kujiinua tunaweza kusema, kama watu walio chini ya neema na wanaoishi chini ya neema, kwamba kushindwa kwa namna hiyo si kawaida katika maisha ya kawaida ya Mkristo. Hata hivyo tunapaswa kukiri kwa moyo wa unyenyekevu kwamba ndivyo tunavyoona katika uzoefu wetu wa kila siku. Yohana anasema kwamba tukidhani hatuna dhambi, tunajidanganya wenyewe. Tunapaswa kuichukulia dhambi katika maisha yetu kwa uzito mkubwa sana.

12.20 Kurejeshwa

Baada ya kosa mtu anahitaji kurudi kwenye njia sahihi. Kosa daima huleta hasara ya kiroho, ambayo ukubwa wake unategemea aina ya kosa na uzito wake. Hapa inahusu kanuni moja, yaani kwamba baada ya kosa mambo hayawezi kuendelea kana kwamba hakuna kilichotokea. Tunahitajika kutenda. Hatupaswi kuipita dhambi bila kujali, kana kwamba hakuna kilichotokea.

Kurejeshwa maana yake ni hii: Kristo na Roho wananiongoza haraka iwezekanavyo nisiifiche dhambi yangu, bali niiungame na kuifunua. Ninapaswa kuitambua dhambi niliyoitenda (kama mtoto wa nuru), kuijutia (yaani kuhuzunika kwa ajili yake) na kuiungama (yaani kuikiri), na kuwa na uhakika wa msamaha wa Mungu.

12.21 Msaidizi wetu mbinguni

Lazima kitu kitokee tunapokuwa tumetenda dhambi. Kristo, Mwombezi wetu mbinguni, katika hali hiyo anatenda kazi kwa ajili yetu kama Msaidizi:

Watoto wangu wadogo, nawaandikia hayo ili kwamba msitende dhambi. Na mtu akitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo, mwenye haki.

1 Yohana 2:1

Msaidizi wetu na Mwombezi wetu, aliye mwenye haki, ameshalimaliza swali la dhambi mara moja tu kwa ajili ya wote kwa dhabihu yake. Lakini sasa, dhambi inapojitokeza katika maisha yetu, baada ya kosa yeye anafanya kazi katika moyo wetu na dhamiri yetu. Msaidizi anatushughulikia *sizi*, si Baba, ambaye Kristo ameketi katika kiti chake cha enzi. Hahitaji kumtuliza Baba ili asitukasirikie. Dhambi si tatizo la Baba, bali ni tatizo letu. Yesu Kristo anataka kutuleta hadi tuitambue dhambi yetu, tutubu (yaani tuijutie) na tuiungame. Wakati huohuo anatushibitishia upendo wa Baba, ili tutambue kwamba tumekubaliwa bila masharti. Dhambi haiukati uhusiano wa uzima wa milele pamoja na Baba.

Agano Jipya haliwaagizi watoto wa Mungu waombe msamaha wanapokuwa wametenda dhambi. Wao *wamekwisha* kusamehewa dhambi zote, hata zile za wakati ujao, milele (Waefeso 1:7; 4:32; Wakolosai 1:14; 2:13; 3:13; Waebrania 10:18; 1 Yohana 2:12). Aidha, hii ndiyo tofauti kubwa na Agano la Kale, ambapo hata waumini, kama vile Daudi, waliomba msamaha. Baada ya msalaba jambo hili si la lazima tena. Hata hivyo: Tunaiungama dhambi na kuijutia, kwa sababu tunapaswa kuwa watakatifu, kama Baba yetu wa mbinguni alivyo mtakatifu. Kwa maana hii tunahitaji kutakaswa kwa maji ya Neno la Mungu: Neno linatuonyesha dhambi, na kisha tunapaswa kuiungama na, bila shaka, kuiacha: ***“Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atundolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote”*** (1 Yohana 1:9). Msamaha kamili tulipewa siku ya kuongoka kwa njia ya damu ya Yesu. Lakini kwa sababu bado tunaweza kutenda dhambi, sisi kama waumini tunahitaji kutakaswa kwa maji ya Neno la Mungu.

12.22 Itakuwaje tukiwa tumetenda dhambi?

Je, tunapaswa kuthibitisha kwamba hata hivyo tunaweza kufanya vizuri zaidi? Je, tunapaswa kuifuta hatia yetu kwa matendo ya kujiadhibu? Au je, kosa halina maana kubwa, kwa sababu dhambi zote tumekwisha kusamehewa?

Tunapaswa kuzitambua dhambi zetu, kuziungama na kuziacha. Hakuna njia ya kulikwepa hili, ni lazima: Kila tunapokuwa tumetenda dhambi – sisi waumini – na sisi sote hujikwaa mara nyingi na kwa namna nyingi (Yakobo 3:2), tunapaswa kuiungama dhambi hiyo. Kuungama kuna maana ya “kufunua”. Kuungama maana yake ni kukiita kitu jinsi kilivyo kweli. Kwa kutafsiri neno kwa neno, maana yake ni “kusema jambo lilelile”, yaani lile lile ambalo Mungu

anasema juu yake. Dhambi tunapaswa kuiita dhambi. Katika jambo hili hatupaswi kutoa udhuru wala kulipamba.

Kuungama dhambi kwa muumini hakuifuti hatia ya dhambi inayotupeleka jehanamu. Hatia ya dhambi zetu imefutwa milele kwa damu ya Yesu. Dhambi katika maisha ya muumini inaathiri uhusiano wa baba na mtoto unaofurahiwa kwa ufahamu, yaani ushirika na Mungu. Ushirika wa kivitendo unaonekana katika uzoefu pamoja na Baba na Mwana unaathiriwa, unasumbuliwa na kujeruhiwa na maisha ya tabia ya mwili. Lakini mtoto wa Baba anabaki kuwa mtoto hata kama wawili hao hawazungumzi tena na mtoto amekuwa asiyetii. Lakini ili kuwa na ushirika wa kweli, ulio hai na wakati huohuo wenye upendo, vizuizi vyote lazima viondolewe; na katika uhusiano wetu wa mbinguni wa baba na mtoto vizuizi hivyo vinapatikana upande wetu tu. Tunapaswa kugeuka na kujitupa tena na tena mikononi mwa Baba yetu wa mbinguni mwenye upendo.

Je, si rahisi kuiungama dhambi? La, si mara zote. Jambo hili lina sababu mbalimbali. Sababu inayotokea mara nyingi zaidi ni kwamba mwanzoni mara nyingi tunatenda kana kwamba dhambi hii haikuwa dhambi. Moyo wetu, kwa nguvu ya tabia ya mwili, unaweza kuwa na kiburi kiasi cha kutafuta kila udhuru unaowezekana unaotaka kuthibitisha kwamba si dhambi. Inashangaza jinsi mara nyingi tunavyochukua muda mrefu kufikia kuitambua dhambi.

Sababu nyingine ni kwamba dhambi tunazozitenda tena na tena hatuthubutu tena kuziungama. Kwa sababu tunaona aibu sana, tunataka kwanza kuthibitisha kwamba hata hivyo tunaweza kufanya vizuri zaidi. Lakini hilo linaibua swali la jinsi tunavyomwona Mungu. Hapo tunakuwa na wazo potofu kuhusu Mungu, ambalo kwa mujibu wake tunafanya kukubaliwa kwetu na yeye kutegemee matendo yetu. Kinyume chake, tumekubaliwa milele; Baba anatupenda wakati wote, kama anavyompenda Mwana wake mwenyewe. Upendo huu kwetu haupungui kwa sababu ya dhambi yetu, wala hauongezeki kwa sababu ya uaminifu wetu!

Jinsi kurejeshwa, kufanywa upya kiroho na kuponywa kunavyoendelea na kunavyoonekana katika uzoefu kwa undani, au kunachukua muda gani, daima kunahusiana pia na dhambi gani imetendwa na ilikuwa na historia gani kabla, na pia ikiwa ilitokea ghafla au imekwisha kuwa mazoea. Jambo muhimu ni kwamba uhusiano wetu na Baba na Mwana baada ya kuungama dhambi unakuwa tena safi na bila kusumbuliwa, hata kama inatubidi kubeba matokeo ya dhambi fulani.

12.23 Kuungama

Inavutia kwamba katika Agano Jipya kunazungumzwa kidogo tu kuhusu jinsi sisi waumini tunavyopaswa kushughulikia dhambi zinazopatikana katika maisha yetu. Dhambi tunazotendeanza sisi kwa sisi tunapaswa kuungamiana (Yakobo 5:16) na kusameheana (Waefeso 4:32; Wakolosai 3:13).

Huko Korintho kanisa lilikuwa na hatia, kwa sababu halikumweka chini ya nidhamu ya kanisa mwanamume mmoja aliyeishi katika uasherati. Katika muktadha huu kurejeshwa kulimaanisha huzuni, masikitiko na toba, kuitambua dhambi na kuiungama (2 Wakorintho 2:5-11; 7:9-11).

- Kuungama dhambi maana yake ni kuitaja dhambi kwa jina lake. Hatutoi maungamo ya jumla mwishoni mwa siku ili kwa hayo “kuzifunika” dhambi zote. Hebu tumfikirie mtoto anayekuja kwa baba yake na kusema: “Ninakuingamia mabaya yote niliyoyafanya leo.” Baba atasema nini? – Baba yetu wa mbinguni anataka kujua kwa uwazi kile tunachoungama.
- Hatupaswi hata kungoja hadi mwisho wa siku. Mara ninapotenda dhambi, ninaiungama dhambi hiyo mara moja. Hakika hatutaki kuiacha dhambi isimame kati yetu na Baba wa mbinguni hadi mwisho wa siku, au tuisahau tu!
- Katika mkutano mmoja wa Biblia mtu aliuliza kama dhambi tuliyoitenda bila kujua inaathiri ushirika na Baba. Jibu lilikuwa: “Ndiyo.” Lakini jibu hili si sahihi! Tunapaswa kutambua kwamba, zaidi sana kuliko tunavyodhani inawezekana, tunafanya bila kujua mambo yaliyo ya dhambi. Si ya kawaida wala hayakusudiwi, lakini yanatokea. Wakati mwingine pia tunakosa ufahamu kama jambo fulani ni dhambi. Kwa hiyo hatutaweza kamwe kuziungama dhambi zetu zote tunazotenda kama Wakristo, ingawa hiyo ndiyo shauku yetu ya dhati. Ushirika na Baba unaathiriwa pale ambapo hatuiungami dhambi tunayojua.

Hapa Paulo anasisitiza “uchungaji wa roho”, huduma ya kichungaji, ambayo utekelezaji wake umekabidhiwa wale walio na nia ya kiroho (na ambayo wale waliotenda dhambi wanapaswa kuikubali). Hii ni mada ambayo hatutaieleza zaidi hapa. Kurejeshwa ni lazima kwa kila kosa. Kwa kosa kubwa kurejeshwa kutaonekana tofauti na kwa kosa dogo. Wazo baya si kosa linalotutupa nje ya njia ya imani. Hata hivyo tunapaswa kuliungama.

12.24 Mkristo wa kiroho na Mkristo wa tabia ya mwili – je, wapo kweli?

Mkristo wa *kiroho* anaagizwa kumsaidia kusimama tena kwa “miguu” yake (ya kiroho) yule aliyeghafilika katika kosa na kujikwaa, au aliyeanguka katika jaribu. Kwanza: Ni nani aliye “wa Roho” (taz. Wagalatia 6:1)? Si kila mtu ambaye Roho Mtakatifu anakaa ndani yake, aliye na uzima kwa njia ya Roho, na kwa hiyo ni mtoto wa Mungu. Bali ni yule ambaye pia anaenenda kwa Roho na kuongozwa naye. Mtu wa kiroho si mwenye cheo katika kanisa, bali ni mtu aliyeumbwa na Roho: Kristo ni uzima wake, na tunda la Roho linaonekana. Mtu wa kiroho si mtu asiye na kasoro, bali ni mtu ambaye katika mgogoro kati ya Roho na tabia ya mwili anasimama upande wa Roho.

Mkristo aliyejikwaa, anayepaswa kupata msaada kutoka kwa wenzake wa kiroho wa nyumba ya imani, haitwi mtu wa tabia ya mwili anayetofautiana na ndugu zake wa kiroho. Kwa kosa moja mtu hawi moja kwa moja Mkristo wa tabia ya mwili. “Kosa” au “uvunjaji wa sheria” si jambo linaloyatambulisha maisha yangu yote. (Hivyo ndivyo ingekuwa kama ulimwengu wa mawazo yangu ungekuwa umekwisha kushindwa na jaribu tangu zamani, na matokeo yake kweli nikajikwaa.)

Wagalatia walikuwa wameanza katika Roho walipoamini. Lakini kwa kuwa walitaka kujiweka chini ya sheria, Paulo anawaonya wasijaribu kwa njia hiyo kukomaa na kuwa wakamilifu kwa nguvu ya tabia yao ya mwili iliyo ya dhambi na iliyoharibika. Ndani ya mfumo wa sheria tabia ya mwili inaamshwa, si Roho wa Mungu (Wagalatia 3:3). Na kweli matokeo kwa Wagalatia yalikuwa kwamba walitendeanza kama wanyama wakali. Kwa bahati mbaya Roho Mtakatifu hakuonekana sana.

Paulo anawaita Wakorintho watu wa tabia ya mwili (1 Wakorintho 3:1-3). Miaka kadhaa kabla walikuwa wameamini, lakini ukomavu wa kiroho haukuonekana sana. Hali ya Korintho tunaijua. Jumla ya mwenendo huu, uliotambulishwa na ugomvi na mafarakano, iliwafanya kuwa Wakristo wa tabia ya mwili.

Mkristo wa tabia ya mwili anajiruhusu kwa kiasi kikubwa au kidogo kuongozwa na tabia yake ya mwili (na mambo ya hisia, mambo ya ulimwengu huu, mawazo yake mwenyewe, fikira zake na nguvu zake). Hajaribu kwa kweli kupigana na vitendo au matendo ya tabia ya mwili. Jambo hilo linatokea tu kwa

kuungama dhambi (1 Yohana 1:9) na kujitoa upya (Warumi 6:13; 12:1-2), na pia kwa nguvu ya Roho Mtakatifu inayotenda kazi na kutubadilisha.

Lakini Mkristo ambaye ameamini kwa miongo mingi na hata hivyo anatambulishwa na ubinafsi ulio wazi, anajionyesha kuwa wa tabia ya mwili. Amezaliwa mara ya pili, kama ilivyokuwa kwa wengi katika kanisa la Korintho. Lakini licha ya kuzaliwa mara ya pili na kuwa na Roho Mtakatifu, mtu anaweza kuwa na nia ya tabia ya mwili kwa muda mrefu (au vipindi virefu), au hata maisha yake yote. Katika hukumu jambo hili litadhihirika, matendo yote ya tabia ya mwili yatakapoteketea, na mtu mwenyewe ataokolewa “kama kwa moto”, yaani kwa shida kubwa kabisa (1 Wakorintho 3:15).

Ukuaji wa kiroho una nafasi kubwa katika swali hili. Kuwa wa kiroho maana yake ni kukomaa na kuwa mtu mzima katika imani. “Sharti moja la hali ya kiroho”⁷⁴ ni muda. Kwa maana inahitaji muda kuwa kile kinachoitwa katika 1 Wakorintho 2:15 *mtu wa roboni*. Kama vile ukuaji wa mwili unavyohitaji muda wake, ndivyo pia kukua kiroho kunavyohitaji muda wake. Hakuna mtu anayekuwa wa kiroho mara moja anapozaliwa mara ya pili. Inahitaji muda hadi mtu awe mtu wa kiroho.”⁷⁵

12.25 Kiini cha mgogoro kati ya Roho na tabia ya mwili

Tuifikishe mwisho ile hoja kuu ya mgogoro kati ya Roho na tabia ya mwili: Roho na tabia ya mwili wanapingana kama maadui katika maisha yetu, katika maisha ya kila siku na katika mahusiano yetu sisi kwa sisi. Hivi ndivyo ilivyo hadi tutakapofika kwenye lengo. Hii si nadharia iliyopitwa na wakati, bali ni uzoefu wa maisha wa kila Mkristo. Roho na tabia ya mwili wanatambulika wazi kwa matunda yao. Wote wawili wanapigania uongozi katika maisha yetu. Sisi wenyewe tuko wakati wote katikati ya mgogoro huu: Kila kitu tunachofanya au tunachoacha kufanya kinapata chakula chake kutoka kwenye mojawapo ya vyanzo hivi viwili. Kwa maneno mengine: Kila mwendo wa mwili wetu au wa mawazo yetu unapata msukumo wake na nguvu zake kutoka kwenye mojawapo ya vyanzo hivyo viwili. Mwishowe sisi ndio tunaoamua. Tunasema Ndiyo au Hapana! “Nafasi ya pekee wanayoishika watu wenyewe katika vita hivi si ya kukaa tu wala si ya kutokuwa na upande. Wanapaswa kufanya maamuzi

74. “Hali ya kiroho” (kwa Kijerumani *Spiritualität*) haipaswi kueleweka hapa kwa maana ya “udini wa kisasa”. Bali inahusu tu “ukomavu wa kiroho”, “nia ya kiroho” au “asili ya kiroho”. Kwa kuwa ni nukuu, neno husika katika maandishi makuu halikubadilishwa.

75. Arnold G. Fruchtenbaum, *Gesetz und Gesetzlichkeit*, Hünfeld, 2010, uk. 109.

yanayoamua mwendo wa vita hivi. Kuenenda katika Roho kunaleta uamuzi mzito, lakini si uamuzi unaohusisha juhudi kubwa ya mapenzi ili kushinda upinzani mkubwa mno na kutimiza jambo fulani. Bali Wakristo wanaitwa kujikabidhi kwa Roho na kwa utendaji wa Mungu, na kufuata tu uongozi wake.”⁷⁶

Mpango mpya wa maisha ni huu: Roho wa Mungu anatembeza ndani yetu yale yanayompendeza Mungu. Kipimo cha jambo hili si sheria ya Musa tena, bali ni Kristo, au sheria yake. Sasa tuko huru kumpendeza Kristo, si kujipendelea wenyewe. Kuenenda kwa Roho katika nguvu yake maana yake ni kupanda kwa ajili ya wakati ujao, na siku moja kuvuna kwa ajili ya hilo uzima wa milele (Wagalatia 6:8).

“Kuutumia ushindi wa Kristo na kuufaidi kikamilifu kunahitaji zaidi ya tendo moja tu la imani. Kunahitaji mtazamo mzima wa imani. Huko ni kumtegemea Mungu daima. Siku kwa siku, saa kwa saa, dakika kwa dakika. Na kumtegemea kwako sasa hivi hakutatosha kwa ajili ya dakika inayofuata. ‘Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za tabia ya mwili.’”⁷⁷

Tabia ya mwili inavuta chini, kuelekea kutafuta utoshlevu na kuridhika hapa na sasa; daima inaelekea dhambi. Roho anavuta juu, kuelekea kwa Kristo. Na tukubali kuvutwa juu! Ndege isiyo na injini (ndege ya kuteleza angani) haiwezi kuruka yenyewe; inaweza tu kujiongoza na kutumia upepo. Inapaswa kuvutwa juu. Basi na tuyatafakari yaliyo juu, aliko Kristo!

76. Charles B. Cousar, *Galatians*, uk. 138.

77. W. Ian Thomas, *Tote können nicht sterben*, uk. 111.

13. Utu mpya na utu wa zamani: Ya kale yamepita, yamekuwa mapya

Paulo anazungumza kuhusu *utu mpya* mara tatu tu: mara moja katika Waraka kwa Wakolosai, mara mbili katika Waraka kwa Waefeso. *Utu mpya* ni muhtasari wa yote ambayo Mungu ameyatimiza kwa njia ya Kristo. Kazi ya Mungu ya wokovu inaumba *mtu mmoja* mpya kwa kufuata mfano wa Mwana wa Adamu aliyetukuzwa, na wakati huohuo watu *wengi* wapya!

Watu hawa hawataki tu kuwa tofauti kwa kujizoeza kanuni mpya za mwenendo – la, wao kweli ni kiumbe kipya. Kama vile Mungu alivyomwumba mwanadamu wa kwanza, vivyo hivyo kuumbwa kwa utu mpya ni halisi! Badiliko hili kubwa kabisa, kubadilishana huku kwa kale na kupata kipya, kunatokea kutoka ndani; ni badiliko la moyo, ambalo kutoka kwake kunachipuka kitu kipya kabisa, yaani uzima wa Mungu mwenyewe.

Utu mpya unadhihirisha kile ambacho mwenye dhambi aliyekombolewa amekuwa sasa katika Kristo. Nyaraka zote mbili za Paulo zinazotumia neno hili zinaeleza pande mbalimbali za nafasi yetu mpya ya wokovu *katika Kristo*. Mtu angeweza kuziita jumla ya pande hizi nyingi za wokovu tusizostahili kuwa *utu mpya*. Maandiko ambamo neno *utu mpya* linatajwa ni haya yafuatayo:

“... ili afanye hao wawili kuwa mtu mmoja mpya ndani ya nafsi yake, akifanya amani.”

Waefeso 2:15

“... kwamba, kwa habari ya mwenendo wenu wa kwanza, mmeuvua utu wa zamani, unaobaribika kwa kufuata tamaa zenye kudanganya, lakini mnafanywa upya katika (au: kwa) robo ya nia yenu (au: ya fikira zenu) na mmevaa utu mpya, uliumbwa kwa kufuata mfano wa Mungu katika baki na utakatifu wa kweli.”

Waefeso 4:22-24

“Msiambiane uongo, kwa kuwa mmeuvua utu wa zamani pamoja na matendo yake, na mmevaa utu mpya, unaofanywa upya upate ufabamu kwa kufuata mfano wa yeye aliyeuumba; hapo hapana Myunani wala Myabudi, kutabiriwa wala kutokutabiriwa, msbenzi, Msakithe⁷⁸, mtumwa, mtu huru; bali Kristo ni yote, na katika yote.”

78. Yaani mtu wa kabila la wahamaji wapanda farasi waliokaa karibu na Bahari Nyeusi.

Wakolosai 3:9-11

Kabla hatujayachunguza maneno haya kwa makini, tukusanye, kama tulivyofanya katika Waraka kwa Wagalatia, pande nyingi za wokovu katika nyaraka hizi mbili pia:

13.1 Utu mpya katika Waraka kwa Waefeso

- watakatifu (1:1, 4)
- wamebarikiwa (1:3)
- wamechaguliwa (1:4)
- watu wasio na hatia (1:4)
- kufanywa wana wa Mungu (1:5)
- wamepewa neema (1:6)
- wametiwa muhuri (1:13)
- wamechuishwa (2:5)
- wameketishwa pamoja naye katika ulimwengu wa roho, yaani katika ulimwengu wa mbinguni (2:6)
- wameokolewa (2:8)
- Sisi ni *kazi yake* (kitu alichokiumba, viumbe vyake), tuliombwa katika Kristo Yesu (2:10).
- Tumeletwa karibu, sisi tuliokuwa mbali (2:13).
- Tumeumbwa kuwa *mtu mmoja mpya* (Wayahudi na watu wa mataifa wameunganishwa katika Kristo) (2:15).
- wamepatanishwa na Mungu (2:16)
- wana njia ya kumkaribia Baba (2:18)
- wenyeji pamoja na watakatifu (2:19)
- watu wa nyumbani mwa Mungu (2:19)
- warithi pamoja (3:6)
- viungo vya mwili mmoja pamoja (3:6)
- washiriki pamoja wa ahadi (3:6)
- wameimarishwa kwa Roho wa Mungu katika *utu wa ndani* (3:16)
- Kristo anakaa ndani ya moyo wake (3:17).
- wamejazwa hata kufikia utimilifu wote wa Mungu (3:19)
- mtoto wa nuru (5:8).

13.2 Utu mpya katika Waraka kwa Wakolosai

- watakatifu (1:2, 22)
- wamestahilishwa kupata urithi katika nuru (1:12)
- wameokolewa kutoka katika nguvu za giza (1:13)
- wamehamishwa kuingia katika ufalme wa Mwana wa pendo lake (1:13)
- wana ukombozi ndani yake (1:14)
- msamaha wa dhambi (1:14)
- wamepatanishwa (1:22)
- watu wasio na hatia (1:22)
- watu wasio na lawama (1:22)
- *Kristo ndani yetu*, tumaini la utukufu (1:27)
- *wakamilifu katika Kristo* (1:28)
- *wametimilika – wameletwa kwenye utimilifu – ndani yake* (2:10)
- wametahiriwa (kiroho) katika Kristo (2:11)
- wamefufuliwa pamoja naye (2:13; 3:1)
- wamekufa pamoja na Kristo (2:20; 3:3)
- *Kristo ndiye uzima wetu* (3:4).
- Wateule wa Mungu (3:12).

“Orodha ya wokovu” hii yenye kuvutia inamulika kwa nuru angavu jinsi utu mpya ulivyo katika Kristo.

13.3 Utu wa zamani katika Waraka kwa Waefeso na kwa Wakolosai

Mtu akitaka kueleza *utu wa zamani* ni nani na ni nini, nyaraka hizi zinatoa mwanga pia juu ya jambo hilo:

Waefeso

- wafu kwa sababu ya makosa na dhambi (Waefeso 2:1; taz. 5:6)
- wanaoendeshwa na kudanganywa na mfalme wa uweza wa anga (2:2)
- wana wa kuasi (2:2)
- wanaoamuliwa na tamaa za tabia ya mwili (2:3)
- watoto wa hasira kwa asili (2:3)
- bila Kristo (2:12)
- wametengwa na jamii ya Israeli (2:12)
- wageni wa yale maagano ya ahadi (2:12)

- bila tumaini (2:12)
- bila Mungu duniani (2:12)
- wanaoishi katika ubatili wa nia (4:17)
- wametiwa giza katika akili (4:18)
- wametengwa na uzima wa Mungu (4:18)
- wenye mioyo migumu (4:18)
- wasio na hisia njema (4:19)
- wasio na urithi katika ufalme wa Kristo na wa Mungu (5:5)
- (kimaadili) giza kabisa (5:8).

Wakolosai

- walio katika nguvu za giza (1:13)
- wametengwa (na Mungu na hali ya utu ambayo Mungu ameikusudia) (1:21)
- adui wa Mungu katika nia (1:21)
- wasiopatanishwa (1:22)
- wana wa kuasi (3:6).

Kwa hiyo tofauti kati ya utu wa zamani na utu mpya zimeelezwa waziwazi. Utu wa zamani ni mwenendo wa zamani wa maisha, kabla ya kugeuka kabisa kwa wokovu, na kabla Mungu, kwa tendo lake la uumbaji katika kazi ya ukombozi, hajaumba utu mpya. Sasa utu mpya haudhihirishi tu mwenendo mpya wa maisha, au mwenendo mpya au bora zaidi kinyume na maisha ya zamani. Wapo watu wasio na uhusiano wowote na Yesu ambao, kwa nidhamu kali, wanaweza pia kuyabadilisha maisha yao kuwa bora zaidi. Hata wanaishi maisha mazuri zaidi kimaadili kuliko baadhi ya Wakristo walio “utu mpya”. Lakini mtu aliye katika tabia ya mwili, ingawa anaweza kuwa na mwenendo mzuri kimaadili, maadamu yuko katika tabia ya mwili, huenda akawapendeza wanadamu, lakini hawezi kumpendeza Mungu. Hapa tunashughulika na kiwango kingine cha badiliko, si tu na mwenendo. Wala haihusu marekebisho ya mtu, bali kuumbwa upya kwa kweli, yaani kuumbwa kwa uzima mpya ndani ya mtu. Kitu hiki kipya, yaani uzima mpya, kwa uhalisi ni Mtu: Kristo (1 Yohana 5:11-12; Wakolosai 3:4, 11). Kwa bahati mbaya, kwa mtazamo wa Mungu hakuna kitu katika utu wa zamani kilichoweza kutumika tena.

13.4 Historia ya kuumbwa kwa utu mpya

Utu mpya umeumbwa kwa kufuata vipimo vya asili ya Mungu, yaani katika haki, utakatifu na kweli. Kwa kweli kumetokea utu mpya, wala si tu mtindo mpya wa mwenendo. Mambo haya mawili yameshikamana bila kutenganishwa: Utu mpya pia una mwenendo mpya wa kimaadili. Jambo hili linawezekana tu ikiwa mtu amefanywa upya pia kwa upande wa maadili. Hilo linagusa moyo wake, dhamiri yake, hisia zake, roho yake, nia yake na nafsi yake, ambavyo vyote vinahusiana na maadili na kuyaamua.

Tunaposoma maneno haya ya Maandiko tunafikiria historia ya kuumbwa kwa mwanadamu wa kwanza, kwa sababu hapa kuna angalau mfanano mmoja. Adamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu na kwa sura yake (Mwanzo 1:26-28). “BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai” (Mwanzo 2:7). Tendo hili la uumbaji linamfanya mwanadamu, tofauti na mnyama, kuwa kiumbe chenye roho, nafsi na mwili. Kuvitaja vipengele hivi vitatu hakukusudii kuibua swali la elimu ya asili ya mwanadamu, bali kuonyesha tu kwamba mwanadamu, kama mbeba mfano wa Mungu, ana roho pia. Kwa hiyo anaweza kuwasiliana na Mungu, kumwamini na kumwomba.

Utu mpya katika Kristo nao unapata kinacholingana nao, au kielelezo chake, katika yule aliyeuumba. Ni nani aliyeuumba utu mpya? Mungu aliuumba. Mungu peke yake ndiye anayeweza kuumba kitu kipya. Lakini kuna tofauti pia na historia ya mwanzo. Kuumbwa upya kwa mwanadamu kulikuwa lazima kwa sababu ya hali ya mwanadamu ya kuwa mwenye dhambi kabisa na kuharibika kwake kimaadili. Kwa hiyo utu mpya sasa unatambulishwa na kinyume kabisa: na haki, utakatifu na kweli, kama vilivyoonekana pia katika maisha ya Yesu kama mwanadamu duniani. Jambo hili lina maana ya pekee kwa maisha yetu ya kila siku, ambapo inahusu ukweli kwamba katika sayari hii watu wa utu wa zamani na wa utu mpya bado wanaishi pamoja.

Basi Mungu alimpulizia Adamu puani pumzi ya uhai. Kwa njia hiyo mwili uliuiumbwa kwa udongo ukawa kiumbe hai, mtu. Roho wa Mungu naye alikuwa na sehemu katika tukio hili. Kwa hiyo ilikuwa pumzi ya Mungu iliyomfanya Adamu kuwa mtu, kiumbe chenye roho. Sasa katika kuumbwa upya kwa mwanadamu ni hivi: Uzima wa Kristo, kwa kulinganisha na kuumbwa kwa Adamu, unapuliziwa ndani yetu kwa namna fulani (taz. pia Yohana 20:22).

Ndani yetu uzima huu unaungana na haiba yetu, na ‘mimi’ wetu. Kwa hiyo inaweza kusemwa juu yetu kwamba sisi ni watu wapya.

Utu mpya unasimama kama kishika nafasi kwa kila mtu binafsi. Kwa maneno mengine: Utu mpya ni Hans-Jörg mpya, Christine mpya – katika Kristo. Kilicho cha msingi katika utu huu mpya ni Kristo anayeishi ndani yetu na ambaye sisi tunaishi ndani yake. Yeye ndiye kitu kipya halisi. Uzima wa Kristo unapiga ndani yetu! Mfano wa Kristo unaumbika tu kwa njia ya Kristo anayekaa ndani yetu! Hakuna kitu kingine (wala sheria, kanuni, maazimio, wala juhudi au malezi) kinachoweza kuchukua nafasi ya Kristo huyu anayeishi ndani yetu.

Katika Yesu sifa hizi tatu za asili zilizotajwa (haki, utakatifu na kweli) zilikuwepo kikamilifu. Msalabani ndipo alipowezesha kwanza kuumbwa kwa utu mpya, kwa sababu msalabani alichukua matokeo yote, hesabu yote ya utu wa zamani (Warumi 6:6). Ni hapo tu ndipo njia ilipofunguliwa kwa ajili ya kitu kipya kabisa. Sasa Kristo mwenyewe ndiye sura ambayo kwa kufuata kwake utu mpya umeumbwa. Kristo ndiye sura ya asili *na* pia nakala yake; nakala, kwa kuwa sasa yeye mwenyewe anakaa ndani yangu na ndiye uzima huu mpya. “Na kama vile tulivyoivaa sura yake yeye aliye wa udongo, vivyo hivyo tutaivaa na sura yake yeye aliye wa mbinguni” (1 Wakorintho 15:49). Hili ni neno *moja* tu la Biblia kati ya mengine mengi yanayoshuhudia kwamba ni mpango wa Mungu kutubadilisha tufanane na sura ya Yesu (kwa mfano Warumi 8:29; 2 Wakorintho 3:18; 1 Yohana 3:2). Sura ya yeye aliye wa mbinguni mwishowe inajumuisha mwili pia, lakini mchakato wa kubadilishwa kufanana na sura ya Yesu umeanza tu siku ya kuumbwa (au kuzaliwa) kwa utu mpya. Na njia ya kufika huko inapitia kwa Kristo mwenyewe. Kristo ndani yetu ndiye uzima mpya, na kwa maana hii ndiye “utu mpya”.

13.5 Wengi ni mtu mmoja mpya

Neno *utu mpya* linatokea kwa mara ya kwanza katika Waraka kwa Waefeso katika 2:15: “... ili afanye hao wawili kuwa mtu mmoja mpya ndani ya nafsi yake, akifanya amani.” Hapa inahusu kuunganishwa kwa Wayahudi na watu wa mataifa kuwa *mtu mmoja mpya*. Hapa Kristo mwenyewe ndiye Muumba wa utu mpya. Hapa kanisa la ulimwengu mzima, kama hekalu la Mungu na makao ya Mungu katika Roho, liko katikati, na kwa hiyo upande ule unaletwa mbele unaosisitiza umoja na ushirika kuwa sifa ya msingi ya hali mpya ya utu. Hapa inahusu kile ambacho sasa ni cha Wakristo wote kwa pamoja. Na kwa maana hii

pia, mwili huu mpya wa pamoja mwishowe ni Kristo mwenyewe: 1 Wakorintho 12:12: "... ndivyo alivyo Kristo": Kristo ni mwili na wakati huohuo ni kichwa.

Utu mpya daima unatajwa kwa umoja. Kwa maana hii inahusu pia *jumuiya mpya ya wanadamu*, ambayo Kristo ndiye kichwa chake na mwanzo wake (Wakolosai 1:17-18). Jumuiya hii inasimama kinyume na jumuiya ya wanadamu ambayo kichwa chake ni Adamu aliyeanguka (Warumi 5:12-21). Waumini wote wanahitajika ili kuakisi katika mwenendo wao wa maisha asili kamilifu ya Kristo, yaani asili ya utu mpya.

"Mkazo wa kibinafsi katika kazi ya Mungu ya uumbaji ya wokovu unaonekana katika Waefeso 2:10, ambapo Paulo anamrejelea kila mtu kuwa 'ameumbwa katika Kristo Yesu'. Kuhamia kwenye mtazamo wa kijumuiya zaidi kunakuja katika 2:11-22. Ulinganisho wa mfano kati ya Adamu na Kristo uko pia nyuma ya sehemu hii. Lakini mkazo katika Waefeso 2:15 hauko sana kwenye nafasi ya mtu binafsi mbele za Mungu na 'kuwa kwake katika Kristo' kinyume na 'kuwa katika Adamu', bali zaidi kwenye mahusiano mapya yaliyopo kati ya watu kwa wale walio 'katika Kristo'. Wayahudi na watu wa mataifa wamepatanishwa, na kwa pamoja katika Kristo wanaunda 'mtu mmoja mpya'. 'Mtu mpya' ni jamii mpya, ambamo wote wana njia huru na sawa ya kumkaribia Mungu, na wameketishwa katika ulimwengu wa mbinguni (yaani katika maeneo ya mbinguni) (2:5-6). Kwa mujibu wa mpango wa Mungu wa 'mtu mpya' hakuna mafarakano wala uadui kati ya viungo vyake, bali amani tu (2:16)."⁷⁹

Utu mpya hauna uhusiano tena na asili yetu ya kikabila, na hali yetu ya kijamii na ya kidini, wala na faida na hasara zote na matokeo yaliyohusiana nazo zamani. Mahusiano na mafungamano hayo yote yamekoma. Yametokea mapya – ndani ya nyumba ya Mungu, ndani ya kanisa, ndani ya mwili wa Kristo. Kwa namna fulani tumepata nyumbani mpya katika utu huu mpya.

Sasa tunavutiwa pia na upande wa kibinafsi wa utu mpya, yaani kile ambacho sisi – kila mmoja binafsi, kila mtu peke yake – tumekuwa.

13.6 Kila mtu binafsi anakuwa utu mpya

"Mfano wa kwanza", kielelezo cha utu mpya, ni mwanadamu Kristo Yesu. Yeye ndiye kipimo cha mambo yote. Hata hivyo yeye si mtu wa kiwango kimoja anayesawazisha, kufananisha au kufuta sifa zote za kibinafsi zinazounda haiba ya kila mtu. Hata kama upande ule tuliouelezea sasa hivi, unaosisitiza ushirika na

79. Greg Herrick, *Old Man and New Man in Paul*, 1999, uk. 5.

umoja, huenda ukaonekana hivyo, utu mpya unaundwa na viumbe vipya vingi (taz. 2 Wakorintho 5:17). Ni ushahidi wa uweza wote wa Mungu, lakini pia wa hekima yake na ufundi wake, kwamba uumbaji wake unafurika kwa wingi wa aina mbalimbali na upekee wa kila kitu. Kwa hiyo inasemekana kwamba hakuna jani linalofanana kabisa na jani jingine, na hata chembe ya theluji, kwa muundo wake wa fuwele, haifanani na nyingine. Ndivyo ilivyo pia kwa mwanadamu. Kwa nje na pia kwa haiba yake, hakuna mtu anayefanana kwa asilimia 100 na mtu mwingine yeyote.

Vivyo hivyo haiba ya kila mtu binafsi inabaki anapozaliwa mara ya pili. Mtu anapoamini, kwa nje (katika mwenendo wake) mwanzoni karibu hakuna kinachobadilika. Lakini ndani yake kinaanza kitu kikubwa mno: Mbegu ya Neno la Mungu inapandwa, kwa namna fulani DNA ya Mungu, ambayo kwa njia yake anazaliwa mara ya pili (1 Petro 1:3, 23).

Mtu yuleyule sasa ana maisha yaliyobadilishwa: *“Wala si mimi ninayeishi tena, bali Kristo ndiye anayeishi ndani yangu; na ubai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ... ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu”* (Wagalatia 2:20). Hapa *mimi* wa zamani, asiyeishi tena, analingana na utu wa zamani. Lakini sasa bado kuna “mimi”, la siyyo mtu huyo asingekuwepo tena. “Mimi” huyu sasa ndiye utu mpya, “mimi” mpya, mimi katika Kristo, ambaye sasa anaishi ndani yangu (katika utu wangu wa ndani). Kwa hiyo *“Mimi ninaishi, na Kristo anaishi ndani yangu”* kunasimama kwa ajili ya utu mpya, ambao wakati huohuo ni mtu yuleyule aliyekuwa hapo awali, lakini sasa ameamuliwa na Kristo mwenyewe na amejazwa na Kristo mwenyewe.

“Uzima mpya ulikuwa wa lazima kabisa. Kwa habari ya kile *nilicho* mimi, juhudi zote, ulazima wote wa kujitahidi, umefikia mwisho. Siwezi kuipa nafsi yangu utauwa. Kwa ‘mtu aliye katika Kristo’ (2 Wakorintho 12:2), tabia ya mwili na dhambi hazipo tena (katika kiumbe kipya nilicho katika Kristo). Zaidi ya hayo – kwa maana halisi kabisa: ‘Mimi’ (kwa maana ya utu wa zamani) sipo tena – ‘nimesulubiwa pamoja na Kristo, nimekufa; hata hivyo ninaishi, lakini si mimi, bali Kristo anaishi ndani yangu.’ Au kwa usahihi zaidi: ‘Ninaishi, lakini si mimi tena.’ Huyu ‘mimi, si mimi tena’ ndiye siri na nguvu ya kuitekeleza imani ya Kikristo katika maisha. *Ninaishi*, kwa sababu bila shaka mtu (mtu binafsi, yaani kila mtu mmoja mmoja) anabaki yuleyule. Haihusu fumbo la Plato, wala kumezwa kwa mtindo wa imani ya kwamba kila kitu ni Mungu katika bahari ya kuwepo. Furaha inayoujaza moyo wangu, na nuru inayoyaangaza maisha *yangu*,

ni *yangu*. Ni *yangu* kabisa. La, tangu sasa ninaishi uzima wa milele wa kweli, unaoweza kweli kuitwa hivyo. Kwa mara ya kwanza, kama mtume anavyosema, nina ‘uzima ulio kweli kweli’ (1 Timotheo 6:19).

Amani *yake*, furaha *yake*, uzima *wake* na Roho *wake* sasa ni *vyangu*; juhudi *zake*, malengo *yake*, mambo *anayoyajali* sasa ni *yangu*; upendo wa Baba sasa ni *wangu*; kukataliwa *kwake* sasa na utukufu *wake* ujao vilevile; na haya yote katika nguvu ya upendo ambao kwao yeye, kwa gharama *yake* mwenyewe na kwa malipo *yake* mwenyewe, amenifanya huru kabisa.”⁸⁰

Utu mpya (yaani Kristo ndani *yangu*) ni matokeo na tunda la mateso ya Mwokozi wetu, aliyejitoa yeye binafsi kuwa dhabihu. Kiumbe hiki kipya kimetambulishwa milele na upendo wa Yesu!

13.7 Utu mpya ni nini?

Katika Wakolosai 3:11 haya ndiyo maelezo halisi ya jinsi utu mpya ulivyo:

Kristo (ni) yote, na katika yote.

Kwanza, Kristo ndiye kielelezo cha utu mpya – katika kuumbwa kwake na pia kwa ajili ya mwenendo wa maisha; yeye ndiye mazingira *yake* ya kuishi na tumaini lake. Lakini Kristo yuko pia *ndani* yetu. Huo ndio utu mpya. Na huo ndio pia ujumbe wa Waraka kwa Wakolosai: *Kristo ndani yenu*, tumaini la utukufu (1:27). *Kristo ndiye uzima wetu* (3:4).

Sasa, mtu akimwita Kristo mwenyewe kuwa utu mpya, hawezi kuzungumzia uumbaji. Kristo hakuumbwa; yeye ni wa milele, kwa sababu yeye ni Mungu. Kitu kingine kilipaswa kuumbwa, kwa sababu kilikuwa hakijawepo kabla: Mtu anakuwa kiumbe kipya kwa kupokea uzima wa Kristo na kushiriki asili *yake*. Uzima *wake* unapandwa ndani kabisa *yangu*. Ndani ya haiba *yangu* binafsi uzima wa Kristo unazamishwa kwa namna fulani, kama vile Mungu alivyompulizia Adamu puani pumzi ya uhai. Kwa njia hii “tumeletwa kwenye utimilifu” (Wakolosai 2:10; ER, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani), yaani tumekamilishwa. Uzima wa Kristo sasa umeujaza au kuutimiza uwepo wetu wote, kama tulivyojaliwa zamani. “All of HIM in all of me” – “YEYE wote ndani *yangu* mimi wote”⁸¹. Kwa njia hii, bila shaka, sitakuwa Kristo mpya, bali mtu mpya, Hans-Jörg mpya. Mtu anaweza kusema “mpya” kwa sababu maisha

80. F. W. Grant, *Deliverance: What is it?*

81. W. Ian Thomas, *The Indwelling Life of Christ*.

yake sasa yanajazwa na Kristo, kwa kuwa uzima huu mpya unaushika uwepo wake wote wa ndani (utu wa ndani, moyo, nia, dhamiri, nafsi). Jambo hili kwanza kabisa halihusu hisia, bali ni jambo halisi la wokovu ambalo Mungu amelitenda na kulitimiza!

“Utu wa zamani ulikuwa Adamu, au afadhali, sisi katika muungano na Adamu. Utu mpya ni Kristo, au kwa usahihi zaidi: sisi wenyewe tulioungana na Kristo.”⁸²

Arthur C. Custance⁸³ analieleza tendo hili la kuumbwa upya kuwa kufanyika mwili (kupata mwili) kwa Kristo ndani ya muumini. Kama vile Mwana wa milele alivyochukua nyama na damu alipofanyika mwanadamu, ndivyo sasa Kristo Yesu, aliye mwanadamu wa kweli, anavyozaliwa ndani yetu kwa maana ya kiroho (isiyo ya kawaida), ili tangu hapo akue na kuumbika katika maisha yetu (taz. pia Wagalatia 4:19). Kwa njia hii kila mtu, anapozaliwa mara ya pili, anapata “Krismasi yake binafsi”. Na ni kwa upande huu tu ndipo kufanyika mwanadamu kwa Yesu mwishowe kuna maana kwake.

“Muumini katika Kristo Yesu anakuwa mmiliki wa mali ambayo hakuwahi kuwa nayo kabla – anakuwa mshirika wa asili ya Mungu. Uzima wa milele wa Mungu asiyeumbwa umepandwa katika sehemu ya ndani kabisa ya haiba yake ya kibinadamu, na asili yake yote na hali yake yote ya kuwa vinapitiwa na nguvu ya kimungu ya uzima mpya. Kuzaliwa upya ni kupewa asili mpya, inayojumuisha akili, hisia na mapenzi, inayozaa ndani ya mtu uzima mpya kabisa na kumwezesha kuishi katika ulimwengu mpya kabisa.”⁸⁴

13.8 Kiumbe kipya

Mahali hapa tunajikumbusha tena kwamba kwa kweli na kwa uhalisi (kiroho) kitu kipya kimetokea na sasa kipo ndani ya muumini. Sambamba na neno “utu mpya” kuna maneno mengine yanayohusiana:

“Sisi tu *kazi yake* (kazi bora, kitu alichokiumba), tuliumbwa katika Kristo Yesu” (Waefeso 2:10). Huu ni zaidi upande wa kibinafsi. Unaonyesha kwamba, kama vile Mungu alivyoweka upendo wake, hekima yake na uweza wake wa kimungu katika uumbaji wa kwanza, ndivyo ilivyo pia kwa kiumbe kipya. Huko upendo wake unaonekana kwa uwazi zaidi, kwa maana haukuhitajika uweza

82. C. K. Barrett, ananukuliwa na H. P. Medema, *Romeinen 7 engovoorts*, uk. 79.

83. Arthur C. Custance, *Man in Adam and in Christ*, uk. 273.

84. Ruth Paxson, *Life on the Highest Plane*, uk. 192.

wake, bali upendo wake usio na mwisho. Kwa maana kifo cha Mwana wake (kinachoonyesha kwa mfano wa punje ya ngano iliyopandwa, mbegu ya uzima mpya) ndicho kinachozaa tunda jipya.

“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa *kiumbe kipya*, ya kale yamepita, tazama, *yamekuwa mapya*” (au “yote yamekuwa mapya” [Elb, tafsiri ya Biblia ya Kijerumani]; 2 Wakorintho 5:17). Kweli ya kale yamepita, hata kama leo bado tuna asili ya zamani ndani yetu. Msalaba ni mwisho wa utu wa zamani. Kwa Mungu sisi tayari sasa ni wakamilifu “katika Kristo”; ya kale hayaoni tena.

“Kwa maana kutahiriwa si kitu, wala kutokutahiriwa, bali *kiumbe kipya*. Na wote watakaoenenda kwa kanuni hii ...” (Wagalatia 6:15-16; Schl 2000). Kiumbe kipya kinaleta maisha mengine, yasiyoelekezwa kwa uumbaji wa zamani wala kwa sheria ya Musa. Bali uumbaji huu unatupa uwezo kutoka ndani, na kutuonyesha jinsi tunavyopaswa kuishi: Kama tulivyompokea Kristo, Bwana, ndivyo tunavyopaswa kuenenda ndani yake (taz. Wakolosai 2:6).

Kristo ni mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote (pia vya uumbaji mpya; Wakolosai 1:15); yeye ndiye mwanzo wake na mwanzilishi wake (Wakolosai 1:18; Ufunuo 3:14), kama mzaliwa wa kwanza katika wafu. Kwa hiyo kiumbe kipya kinatokana waziwazi na Kristo, kwa maana ni matokeo ya ukweli kwamba mauti imeshindwa. Kinaanzia upande wa pili wa mauti, katika nguvu ya uzima wake usio na ukomo (Waebrania 7:16). Kwa hiyo utu mpya katika Kristo, hata upande wa pili wa mauti, hauwezi kuharibiwa, hauwezi kupotea, hauzi, na ni wa milele.

13.9 Ni nini kiliumbwa upya?

Katika mistari hii haisemwi ni nini hasa kiliumbwa upya. Haiumbwi “mtu wa pili sambamba” ndani ya mtu, hata kwamba ndani ya mtu mmoja sasa kungekuwa na haiba mbili. Katika kugeuka kwa wokovu kwa kila mtu, historia, au uwepo wote wa utu wa zamani, umekomeshwa msalabani pale Golgotha. Utu wa zamani na utu mpya haviendelei kuwepo kando kwa kando. **Utu mpya umechukua nafasi ya utu wa zamani.** Utu mpya ni muhtasari wa kile ambacho sasa tumekuwa katika Kristo – binafsi na pia kwa pamoja.

Kuumbwa upya kwa sasa kumewekewa mpaka katika utu wa ndani wa mtu (ingawa kunaonekana katika mwenendo wa maisha). Kwa hiyo kunazungumzwa juu ya “utu wa ndani” (Waefeso 3:16; Warumi 7:22; 2 Wakorintho 4:16; taz. 1 Petro 3:4), unaolingana na uzima mpya na utu mpya. Mwili utapata sehemu katika kiumbe kipya katika kubadilishwa au kufufuliwa kunakokuja tu.

Mwishowe hakuna kitu kitakachoachwa nje ya kuumbwa upya huku, kwa maana katika ufufuo tutakuwa wakamilifu kabisa, na katika pande zote za utu ambao Mungu ameukusudia. Hapo tutafanana na Bwana Yesu kwa upande wa mwili, wa nafsi na wa roho; lakini wakati huo si kama watu wa udongo, bali kama yeye, kama watu wa mbinguni.

Kwa muhtasari tunaweza kusema kwamba sisi – kwa habari ya haiba yetu – kwa upande mmoja tumebaki walewale, na hata hivyo wakati huohuo tumekuwa wapya kabisa. Mungu anataka tuwe haiba jinsi tulivyo (yaani jinsi tulivyojaliwa kama viumbe vyake, na kama watu walio na utambulisho wao wenyewe). Lakini anatukubali tu “katika Kristo”, yaani tu kama watu waliohamishiwa ndani ya Kristo. Na kwa ajili ya hilo ameshughulika, kwa kuwa yeye mwenyewe ametuweka ndani ya Kristo (1 Wakorintho 1:30). Kwa njia hiyo pia “ametupandikiza” ndani ya kazi yote ya wokovu ya Yesu. Mauti ya Kristo, kuzikwa kwake, ufufuo wake, kupaa kwake mbinguni na kutukuzwa kwake vinatuhusu sisi, kwa maana tumeketishwa pamoja naye katika ulimwengu wa roho, mbinguni (Waefeso 2:6).

13.10 Je, utu mpya unahitaji kufanywa upya?

Nyaraka zote mbili (kwa Waefeso na kwa Wakolosai) zinasisitiza kwamba utu mpya unafanywa upya daima. Je, kuna hatari kwamba utazeeka na kukosa nguvu, au hata kufa?

Kuhusu jambo hili, kwanza neno la msingi: Hakuna kitu, hakuna kiumbe, kinachojitegemea chenyewe na kuwepo kwa nguvu yake chenyewe. Kila kitu kilichoumbwa na kilicho hai (hata kiumbe kipya) kinachukuliwa na kudumishwa na Muumba (Wakolosai 1:17; Waebrania 1:3; Nehemia 9:6). Kwamba moyo wangu unapiga (kila siku hadi mara 80,000) ni kwa sababu ya nguvu ya Mungu inayodumisha uumbaji. Kilichoumbwa kinamtegemea yeye! Ndivyo ilivyo pia kwa utu mpya. Unahuishwa na Muumba wake, Kristo.

Utu wa ndani unapaswa kufanywa upya na kuhuishwa daima. Maisha ya kiroho ya Mkristo yanapaswa kulishwa bila kukoma. Mkristo anapaswa kuongezeka nguvu daima kwa njia ya Roho wa Mungu. Nguvu hiyo inatenda kazi “ndani ya utu wa ndani” (hivyo ndivyo Waefeso 3:16 linavyosema neno kwa neno). Kufanywa upya na kuhuishwa huku kwa kudumu ni lazima, kwa sababu Mkristo bado yuko katika mwili unaokufa na ulio dhaifu, na bado ana mabaki ya maisha ya zamani (asili ya zamani), na mara nyingi fikira zake bado zinaathiriwa

nayo. Tunaishi katika “tayari sasa” na katika “bado”. Kufanywa upya ni lazima, kwa sababu Mkristo anakabiliwa na shida na dhiki za uumbaji ulioanguka, na yuko katika ulimwengu wenye uadui unaoshawishi. Na si kwa uchache, kufanywa upya na kuhuishwa ni lazima kwa sababu adui wa roho za watu, mdanganyifu na mwuaji tangu mwanzo, anampinga muumini.

Mkristo yuko katikati ya mivutano. Kuwa kwetu Wakristo kunashambuliwa kila siku katika pande mbalimbali za vita. Mashambulizi haya yana lengo moja: Yanataka kutushawishi tuyafananishe maisha yetu na ulimwengu, na kuishi kama utu wa zamani unavyoishi, yaani kwa ajili ya nafsi yake, bila kujali imani wala utii. Maadui wanaweza kutambuliwa kwa usahihi kwa msaada wa Biblia: Ndani yangu iko tabia ya mwili, asili ya zamani. Nje yangu kuna ulimwengu (watu na ulimwengu wao) usiomjali Mungu. Na tena yuko yule adui mkuu anayeitwa Ibilisi na Shetani. Kufanywa upya hakutakuwa lazima tena mbinguni, kwa sababu maadui hawa hawatakuwepo tena: Tabia ya mwili itafikia mwisho pamoja na mwili wetu unaokufa, ulimwengu unapita pamoja na tamaa zake, na Ibilisi atakanyagwa chini ya miguu yetu.

“Neno ‘mpya’ katika usemi ‘*na mmevaa utu mpya*’ kwa Kiyunani ni *neos*; halielekezi tu kwenye maisha mengine, bali kwenye maisha ya aina mpya kabisa, yaani kwamba ‘aina hii ya utu’ inaonyeshwa katika ujana na ubichi wake, huku mchakato hai wa ukuaji ukichukuliwa kuwepo. Inahusu uzima mchanga wenye nguvu, unaoumbika kwa kukua na kuongezeka katika maisha ya kawaida. Mchakato wa ukuaji unaelezwa kuwa kufanywa upya kwa kudumu, ambamo Roho Mtakatifu anaupa utu huu mpya (Tito 3:5) namna mpya kabisa ya kufikiri na alama (mpya), wala hampi utu wa zamani dawa ya kuurudishia ujana. Alama hizi zinapatana na mfano wa yeye aliyeuumba, yaani na Mungu mwenyewe na Kristo: Kwa maana Mungu (Waefeso 2:10) na Kristo (2:15) wote wawili wanahusika na utu mpya. Wanataka watu ambao kwa pamoja wanaunda ‘aina hii mpya ya utu’ waifahamu zaidi kazi hii ya uumbaji – ni kufanywa upya ‘upate ufahamu’. Jambo la msingi ni ukweli kwamba Kristo, anayekaa ndani ya waumini, ni kila kitu kwao: ‘Utu mpya’ ni Kristo, jinsi anavyoumbika ndani ya waumini katika utajiri kamili wa nafsi yake, au kwa ufupi: Kristo ndani ya waumini.”⁸⁵

Ufahamu na fikira vinafanywa upya. Mtu anapoamini, bado ana ndani yake mitindo ya zamani ya kufikiri na ya mwenendo iliyo ya dhambi. Katika tabia

85. G. H. Kramer, *Christus ons leven*, uk. 117.

yake ya mwili mambo hayo yanabaki. Lakini kinyume chake kuna utendaji wa Roho wa Mungu, nao unaanza katika kituo chetu cha uongozi – mahali pale ambapo maamuzi yanafanywa. Utu wa nje unachakaa katika msuguanu wa maisha ya kila siku. Lakini Neno la Mungu linatuhakikishia kwamba utu wetu wa ndani (yaani utu mpya) unafanywa upya siku kwa siku (2 Wakorintho 4:16). Mtu anapata kufanywa upya kwa kuutazama umilele, au kwa kumtazama Kristo mwenyewe, ambaye utukufu wake unaakisiwa juu yetu (2 Wakorintho 3:18) na kututia nguvu (Wakolosai 1:11).

13.11 Utu mpya: tumeuvaa kama vazi

Utu mpya unafanana na vazi analolivaa mtu. Tendo lililo kinyume chake linahusu utu wa zamani, ambao mtu ameuvua kama vazi. “Picha ya ‘kuvaa’ na ‘kuvua’ inahusiana na kubadilisha mavazi, na inarejelea badiliko la tabia katika nuru ya badiliko la utambulisho, kwa kuwa mtu huyo amebadilisha eneo la maisha la zamani (bila Mungu) kwa eneo jipya la maisha (pamoja na Mungu).”⁸⁶ Kuvua na kuvaa kulitokea wakati wa kugeuka kwetu kwa wokovu, Kristo alipoingia katika maisha yetu.

Utu wa zamani kwa kila namna ni jambo lililopita – au sivyo? Mistari yote mitatu ya Biblia inayoutaja utu wa zamani inaeleza mwisho wake: ama kama “umesulubiwa”, ama kama “umevuliwa”. Yote yanaashiria tendo la mara moja lililokamilika. Kuvua vazi kunatokea mara moja, lakini kufanywa upya kunaendelea daima. Kunawezesha vazi hili jipya libaki jipya pia, lisichakae wala lisichafuke.

Mavazi humtambulisha mtu. Vazi ni kile kinachoonekana kwa mtu. Na hilo ndilo Paulo anataka kusema hapa: Inapaswa kuonekana wazi kwamba utu mpya haukuwa tu wazo la busara au nadharia, bali nguvu ya Mungu inayoumba uzima na kufanya upya imezaa kazi bora kabisa ya kweli. Ushahidi wa hili ni kwamba utu mpya unaonekana katika maisha ya kila siku. Sasa unayaelekeza maisha yake kwa Mkombozi wake na Muumba wake. Unamvaa Bwana Yesu Kristo (Warumi 13:14). Kwa hiyo inahusu utu mpya kuonekana zaidi na zaidi; Kristo (asili yake, upendo wake) anapaswa kuiondoa asili ya ubinafsi ya utu wa zamani iliyokuwepo hadi sasa.

Njia ya utu mpya imezungukwa na vibao vya Mungu vinavyoonyesha njia, vinavyotuonyesha uzima mpya unajidhihirisha kwa namna gani na si kwa namna

86. Greg Herrick, *Old Man and New Man in Paul*, 1999, uk. 7.

gani. Mkazo mkubwa uko kwenye kubadilishwa kwa mwenendo wa maisha. Mtu anayeamini habadilishi maisha yake ghafla kutoka ya kale kwenda mapya. Kama ingekuwa hivyo, kusingehitajika kufanywa upya, wala hata amri za Agano Jipya zinazoonyesha jinsi maisha ya utu mpya yanavyoonekana.

Hatuhitaji *kufanyika* watu wapya, kwa mfano kwa juhudi za kujikaza na za kung'ang'ania zinazolenga maisha yanayofanana na ya Kristo. La! Inahusu sisi kutekeleza katika maisha kile ambacho tayari *tulicho* katika Kristo: wenye haki, watakatifu na wa kweli.

Fursa ya kuwa utu mpya inatulazimu pia kuishi hivyo. Tunapaswa kuwa kile tulicho! *Kuna* watu wapya na wakati huohuo *kufanyika* watu wapya – hilo linasikika kama kitendawili kinachojipinga, lakini sivyo. Kimoja ni *ukweli* wa wokovu (yale ambayo Mungu ameshatenda; kwa Kijerumani *Heilsindikatin*) – kile tulicho mbele za Mungu bila kupingika. Kingine ni *agizo* la wokovu (yale tunayoagizwa kutenda kwa sababu hiyo; *Heilsimperatin*), linalotuagiza tuishi ipasavyo kutokana na hali hii ya kuwa. Hakuna upande wowote kati ya hizi mbili unaopaswa kuwekwa kinyume na mwingine wala kuondolewa katika uwiano. Anayeisitiza nafasi yetu, yaani ukweli wa wokovu, kuliko utekelezaji wa kivitendo, anayavuruga mambo kutoka katika uwiano. Maandiko mara nyingi yanazungumzia pande zote mbili kwa pumzi moja, ili kutuonyesha wazi kwamba hatupaswi kuzikatakata (mara nyingi kama kisingizio au udhuru) kwa mazoezi magumu ya kitheolojia. Kwa Agano Jipya nafasi yetu ya wokovu hakika ni muhimu sawasawa na matokeo yake katika maisha ya kila siku. Jambo hili la mwisho ndilo linalomaanishwa na agizo la wokovu: kujitahidi kwa bidii yote kuishi jinsi Mungu anavyotaka, na jinsi alivyowezesha pia.

13.12 Muhtasari – picha moja

Picha na ulinganisho na kweli za Biblia vinaweza kusaidia sana. Biblia yenyewe (zaidi ya yote Bwana Yesu) inatumia picha na mifano ili kufanya kweli za kiroho zieleweke. Lakini picha pia zina mipaka yake. Zinataka kufanya pande fulani zieleweke wazi, lakini hilo pia linamaanisha kwamba si kila upande uliopo katika picha kama hiyo unapatana na kweli ambayo picha hiyo inapaswa kuifafanua. Kile kinachotajwa katika picha au katika ulinganisho ndicho chenye maana. Kile kisichotajwa wala kuzungumziwa, kinyume chake, hakina umuhimu.


13.12.1 Mti wa zamani


Biblia mara kadhaa inamlinganisha mwanadamu na mti. Mfano maarufu ni mfalme mkuu Nebukadnezar. Analinganishwa na mti mkubwa wenye nguvu. Kwa kuwa alijivuna kwa sababu ya ukubwa wake na uweza wake, Mungu aliamua kuukata mti huo. Shina pamoja na mizizi yake tu lilipaswa kubaki: Kwa maana mfalme hakufa, bali kwa muda fulani alipewa moyo wa mnyama, kisha akawa mfalme tena (Danieli 4; taz. pia Waamuzi 9:7-15). Kwa hiyo mti huu, kwa lugha ya picha, ulikatwa kwa shoka na Mungu mwenyewe. Hii ni picha ya mtu anayeishi bila Mungu, mzao wa Adamu. Yesu anasema kwamba hakuna mti mbaya uzaao matunda mazuri (Luka 6:43). Kwa maneno mengine: Watu walio katika tabia ya mwili hawawezi kumpendeza Mungu. Utu wa zamani ni mti usiozaa matunda mazuri. Jambo hili linahusu wanadamu wote kwa jumla, sawasawa na kila mtu mmoja mmoja (Zaburi 37:35). Mti mbaya kiasi hicho, linapokuja suala la matunda yake, haustahili kitu kingine ila kukatwa na kutupwa motoni (Luka 3:9). Hilo ndilo lililotokea kwa utu wetu wa zamani: Ulihukumiwa msalabani, na hukumu ya kifo ikatekelezwa. Kwa namna fulani uliteketea katika hukumu ya utakatifu wa Mungu. Kwa njia hiyo maisha yetu ya zamani yalikomeshwa. Si sisi wenyewe tuliyakomesha, yeye ndiye aliyeyakomesha. Ni Kristo aliyekufa *badala yetu*. Kama tungekufa sisi kihalisi, mzizi nao ungekuwa umeng'olewa. Katika picha yetu mzizi unawakilisha mtu mwenyewe. Unawakilisha kile nilicho kama mwanadamu, kama kiumbe cha Mungu.

13.12.2 Mti mpya

Basi lengo la Mungu ni nini? Mungu anataka niwe mti uliopandwa kando ya vijito vya maji. Ndivyo inavyosemwa juu ya mwenye haki katika Zaburi 1 (taz. Zaburi 92:12; Yeremia 17:8). Ninapaswa kuwa mti mzuri unaozaa matunda mazuri (Mathayo 7:17), tunda la Roho (Wagalatia 5:22-23). Kwa ajili ya hilo unahitajika mti mpya. Mti huu lazima upandwe na ukue. Na ili siku moja uwe mti wenye nguvu, wenye mizizi imara na matunda mazuri, unahitaji kutunzwa na zaidi ya yote maji. Picha yetu inaruhusu upande mwingine pia: Tumezaliwa mara ya pili kwa mbegu isiyoharibika ya Neno la Mungu (1 Petro 1:23). Mbegu hii ni mbegu ya Mungu (1 Yohana 3:9), ambayo ndani ya mtu baada ya

kuongoka kwake (kwa lugha ya picha) inaota na kukua, hadi inakuwa mti wenye nguvu. Mbegu hii ni Kristo mwenyewe (Wagalatia 3:16). Kwa hiyo tunao ulinganisho na ukweli kwamba Kristo mwenyewe ndiye *utu mpya*, uzima wake ndani yetu (Wakolosai 3:4, 11). Uwezo wote wa ukuaji wa utu mpya umo wote kamili ndani ya mbegu hii, hata ikiwa ndogo kiasi gani. Utu huu sasa unapaswa kuchanua, kukua, kuongezeka, kuenea. Hili halitokei kwa dakika moja, bali tu kwa ukuaji unaoendelea na kufanywa upya kwa kudumu. Mungu peke yake ndiye anayetoa ukuaji, kufanywa upya na nguvu. Katika muktadha mwingine Agano Jipya linazungumzia mzeituni (Warumi 11:16-24), ambamo chipukizi jingine linapandikizwa, ili liendelee kukua juu ya mti wa zamani. Hebu tulifikirie kisiki cha mti, tulichokilinganisha na sisi wenyewe kama watu. Sasa ndani ya kisiki hiki chipukizi jipya, yaani mbegu ya Neno (Kristo mwenyewe), linapandikizwa, ili liweze kukua na kuwa mti mpya. Mtaalamu analiita tendo hili “kupandikiza”.





13.12.3 Mzizi wa zamani ambao bado uko hai

Mzizi wa zamani (kisiki cha mizizi cha mti wa zamani uliokatwa) bado upo. Tena bado uko hai. Katika picha yetu huu si utu wa zamani, bali ni tabia yetu ya mwili – asili ya Adamu ya zamani, iliyoharibika na yenye dhambi. Ndiyo iliyoyatambulisha maisha yetu ya zamani, yaani maisha ya utu wa zamani. Hata kwa hatari ya kwamba kurudia kweli hizi kunaweza kuchosha, na isemwe tena: Utu wa zamani si tabia ya mwili. Bali utu wa zamani unawakilisha kuwepo kwangu bila Mungu, kabla sijaamini. Tabia ya mwili, kinyume chake, ni asili na hali ya utu wa zamani. Hii bado ipo. Maadamu tunaishi, mzizi huu wa zamani utapatikana ndani yetu. Sasa mzizi huu una sifa ya kuchipuka tena (Ayubu 14:7-9). Kutoka katika kisiki hiki cha mizizi yanachipuka machipukizi madogo – matunda mabaya, matendo na mazoea ya mwili na ya tabia ya mwili. Wakati Mungu anashughulikia ukuaji wa mti mpya, sisi tunapewa agizo la kuvifisha

viungo vilivyo katika nchi, yaani viungo vya tabia ya mwili yenye dhambi (Wakolosai 3:5; Warumi 8:13). Jambo hili linapaswa kutokea kwa imani na kwa Roho. Tunapaswa kuyaondoa machipukizi haya kama magugu, kukata matawi, au (kama tayari yamekwisha kuwa vigogo vidogo vya miti) kuyakata kwa shoka la nguvu ya Mungu. Kazi ya “mtunza bustani”, anayeshughulikia magugu kwa uthabiti, iko ndani ya eneo la wajibu wetu. Katika kazi hii hatuachwi peke yetu: Kwa njia ya Roho Mtakatifu wa Mungu tunaishi na kuenenda (Warumi 8:13; Wagalatia 5:18)!

13.13 Kwa imani peke yake

Jambo hili linatoka tu katika imani na kwa njia ya imani katika Mwana wa Mungu, ambaye (kama Paulo anavyosema) “alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu” (Wagalatia 2:20). Imani ni kumtegemea Mungu. Inajumuisha mtazamo unaotazamia kila kitu kutoka kwa Kristo wala hautazamii chochote kutoka kwa nafsi yake mwenyewe. Kufisha kunakoelezwa kwa mfano katika Warumi 8:13 na katika Wakolosai 3:5 mwishowe kunatokea *kwa imani*. Kunajumuisha kuiambia dhambi Hapana, na wakati huohuo kumwambia Kristo Ndiyo (Warumi 6:13, 19). Mwenye haki ataishi (kila siku) kwa *imani* yake (Warumi 1:17). Tunamkaribia Mungu kwa imani (Warumi 5:2), tunasimama kwa imani (Warumi 11:20; 2 Wakorintho 1:24). Ninamwacha Kristo akae moyoni mwangu kwa imani (Waefeso 3:17). Ninasimama na kuimarishwa kwa imani (1 Petro 5:9). Imani hii ninapaswa kuitumia leo. Huo ndio ufunguo. Imani si hisia. Kwa imani, kile ambacho Mungu anasema ni kweli kabisa na kina nguvu: Hilo halihusu tu wokovu wangu wa milele, bali pia maisha yangu ya kila siku. Kwa maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu!

13.13.1 Mtunza bustani mvivu

Mithali 24:30-32 inasema: “Nilipita karibu na shamba la mtu mvivu, na karibu na shamba la mizabibu la mtu asiye na akili. Na tazama, lote lilikuwa limejaa miiba, uso wake ulikuwa umefunikwa na magugu, na ukuta wake wa mawe ulikuwa umebomoka. Nikatazama, nikautia moyo wangu juu yake; nikaona, nikapokea mafundisho.”

Mara nyingi chini kabisa ya kipandikizi bora (hilo ndilo jina la chipukizi hili jipya na bora) machipukizi ya zamani yanaota tena. Haya lazima yakatwe bila

kukosa, kwa maana yanalinyang'anya chipukizi jipya maji, na kadiri linavyoendelea kukua, pia mwanga.

Mtunza bustani asipotimiza wajibu wake, kuna tatizo. Nguvu ya tabia ya mwili inayojisukuma yenyewe haipaswi kudharauliwa. Mtu akiilisha tabia ya mwili na kuihurumia, badala ya kuitoa kwa mauti daima au tena na tena, machipukizi ya zamani yataota mahali pengi. Jambo hili lina athari mbaya kwa ukuaji wa mti mpya. Ukuaji wake unazuiliwa, mizizi haiendelei kukua ndani ya Kristo, hata mti haupati chakula tena. Ni karibu kana kwamba Paulo naye alikuwa na picha hiyohiyo mbele ya macho yake (Wakolosai 2:7).

Maisha ya tabia ya mwili yenye ubinafsi yanafanana na mti uliokauka, uliozungukwa na machipukizi mengi ya mzizi wa zamani, yanayoweza kukua juu kiasi kwamba mti ule uliokuwa mpya hauonekani tena. Maji yaliyokusudiwa kwa ajili ya mti huu mpya yanatiririka kwenda kwenye machipukizi mengi ya mzizi wa mti wa zamani. Mti unaweza kuugua, matawi mazima yanaweza kukauka, na matunda yake yanaweza kuwa machache au madogo.

Muda fulani uliopita nilishangaa tulipokuwa tukiokota na kuchuma matofaa ambayo tunayapeleka yakamuliwe juisi: Katika mti mmoja nilikuta aina mbili tofauti za matofaa. Hayo yalikuwa matokeo ya kupandikiza. Mmiliki wa zamani alitaka kuwa na aina mbili za matofaa katika mti mmoja. Mara moja nilifikiria maisha ya Kikristo: Huko pia zinapatikana aina mbili tofauti za matunda – matunda ambayo Roho anayakuza, lakini pia matunda yanayozaliwa na tabia ya mwili.

13.14 Wakati ujao wa utu mpya

Hadi sasa tumeuona utu mpya katikati ya mivutano ya ulimwengu unaopita. Mtazamo mfupi wa wakati wake ujao haupaswi kukosekana. Utu mpya tayari unapepewa na pumzi ya uumbaji mpya ujao, kama unavyoelezwa katika Ufunuo 21. Ndani yetu uumbaji huu mpya tayari umeanza. Sisi ni kama malimbuko ya uumbaji mpya wa Mungu (Yakobo 1:18). Katika Kristo tayari tumeketishwa katika ulimwengu wa roho (katika ulimwengu wa mbinguni) (Waefeso 2:6). Ndivyo nafasi yetu inavyoelezwa na Neno la Mungu. Kama watu *mapya* tutaishi katika uumbaji *mpya*, siku moja pia tukiwa na mwili mpya, utakaolingana na ubora uleule wa uumbaji mpya, kama ilivyo sasa kwa habari ya *utu wetu wa ndani* (1 Wakorintho 15:35-57). Wakati ujao wa utu mpya unashangaza hata kukata pumzi, na ni wenye utukufu kupita kiasi kama Muumba wake mwenyewe: Yeye

aliye uzima wetu atakapofunuliwa, ndipo sisi nasi tutakapofunuliwa pamoja naye katika utukufu mbele ya ulimwengu wote (Wakolosai 3:1-4)!

Lakini tuisahau upande wa kijumuiya au wa ushirika, ambao huenda ndio hata muhimu zaidi. Ubinadamu mpya, ambao Kristo ndiye mwanzo wake na kichwa chake, utakuwa ndio wakazi wa mbingu mpya na nchi mpya. Kristo ni yote, na ndani ya *wote*!

Uhalisi wa wokovu wa utu mpya unadhihirishwa na kanisa la Agano Jipya, lililotokea siku ya Pentekoste tu. Kanisa hilo (likiwa na waumini wote) litakuwa utu huu mpya, ambao Kristo ameuumba na ambao yeye ni kichwa chake. *Mtu huyu mmoja*, anayeundwa na viungo vyote vya mwili, atakuwa kwa nyakati zote – hata milele na milele – kwa sifa ya utukufu, ya neema na ya upendo wa Mungu, au wa Kristo.

Utu wa zamani unaharibiwa na tamaa; kwa sababu ya mauti ya kiroho unaelekea mauti ya mwili, ambayo mwishowe inaongoza kwenye mauti ya milele. Hauboreki; uko chini ya uharibifu na unaangamia. Utu mpya unafanywa upya kwa njia ya uhusiano wa uzima na Muumba wake, hadi uzima wa milele, au ukamilifu katika ufufuo, utakapoanza.

13.14.1 Kuishi maisha ya wakati ujao tayari sasa

Wakati ujao wa utu mpya si mada isiyoshikika, wala iliyotengwa na uhalisi wa maisha yetu. Wakati ujao huu kwa upande mmoja unajumuisha tumaini letu, lakini tayari sasa unajumuisha pia kile kinachoyaamua maisha yetu. Mtu angeweza kusema hivi: Tunaishi kwa kuanzia kwenye lengo, tukimtazama Yesu na yale aliyoyaumba na atakayoyatenda. Ikiwa uzima wa uumbaji mpya tayari unapiga ndani yetu, basi maana yake si kitu kingine ila kwamba tayari sasa tunaishi maisha ya wakati ujao.

Tunda la Roho Mtakatifu, maisha ya Yesu mwenyewe yasiyo na mfano na yaliyo kielelezo, amri zake za upendo, na kwa jumla amri zote za Agano Jipya zinatuonyesha jinsi maisha katika uumbaji mpya yatakavyokuwa kwa upande wa maadili. Katika uumbaji mpya wa Mungu kila kitu kitajazwa na upendo wa Mungu – upendo uleule ambao sisi tayari sasa tunapaswa kuutekeleza katika maisha yetu.

Makanisa yetu ni vituo vya mbele na vituo vya ulinzi vya ulimwengu mpya wa Mungu. Hapa wale wasiomjua Mungu wala ukombozi katika Kristo wanapaswa

kukutana na “utu mpya”, au na uumbaji mpya. Kwetu sisi lazima kuonekane kile ambacho Mungu hivi karibuni atakuwa nacho kila mahali katika ulimwengu wake mpya kama jambo la kawaida, na wakati huohuo lenye utukufu wa ajabu.

Tukiutazama hivyo ulimwengu mpya wa Mungu na kuufikiria ukweli kwamba tayari umeanza ndani yetu, tunaishi maisha ya wakati ujo si kwa kulazimishwa wala chini ya shuruti, wala kwa nia za kisheria. Mwenendo mpya wa maisha unapaswa kuwa jambo la kawaida kwetu, kama itakavyokuwa hivi karibuni katika utukufu wa milele wa Mungu.

Hapo, tofauti na leo, hakutakuwa tena na maadui wala vizuizi vinavyoweza kuzuia uzima mpya. Kwa hiyo leo kuwa kama Yesu alivyokuwa kunahusisha maamuzi ya mapenzi, juhudi na kujitoa. Lakini sisi hatulazimiki kujitegemea wenyewe (kama, kwa mfano, mtu asiyeamini anayetaka kuiboresha tabia yake kimaadili); bali tunayo neema ya Mungu na Roho wake mwema upande wetu.

13.15 Wito

Neema inatufundisha, naam, inatulea (Tito 2:11-12), ili utu mpya kweli upate nafasi katika maisha yetu ya kila siku. Si sheria, bali neema inayotulea, kwa kutukumbusha kwanza tena na tena kile tulicho tayari katika Kristo, na ambacho hatuhitaji bado kufanyika. Neema inatuweka katika utajiri wa Kristo usio na kipimo na kutujaza kwa huo, kwa maana ni kutokana na neema tu ndipo maisha yaliyobadilika yanawezekana.

Tumeuvua utu wa zamani pamoja na mwenendo wake wa zamani wa maisha. Lakini nia, asili au hali ya utu huu wa zamani bado iko ndani yetu maadamu tuko katika mwili wetu. Dhidi ya kuibuka kwa mwelekeo wa zamani wa maisha kunasimama kufanywa upya kwa fikira zetu daima.

Kristo ndani yetu: Huo ndio uhalisi wa maisha wa utu mpya. Ian Thomas aliufananisha na glavu, ambayo bila mkono ulio hai ni kitu kilichokufa. Ndivyo tulivyo sisi – hatuwezi kitu kabisa bila Kristo na nje ya Kristo. Lakini mkono ulio hai unapoingia ndani ya glavu, basi inaweza kufanya kila kitu! Kwa hiyo tunaweza kutegemea na kuamini kwamba tunaweza kuyafanya mambo yote katika yeye atutiaye nguvu!

14. Kuzaliwa mara ya pili kwa uzima mpya

Katika kilele chetu cha mwisho cha mlima tunafika kwenye jambo ambalo huenda ndilo linalojulikana zaidi katika mada hii. Inahusu kuzaliwa mara ya pili, kupokea uzima mpya na wa milele. Kwa njia hiyo tunafika kwenye kile tunachoweza kujifunza kutoka kwa mtume Yohana kuhusu nguvu inayobadilisha ya Injili, inayoumba mambo mapya. Tumewekwa huru mbali na nguvu ya dhambi, tumepewa Roho Mtakatifu, tumefanywa kuwa watu wapya. Hiyo ilikuwa hasa mada ya Paulo. Lakini ilitubidi pia kuzaliwa mara ya pili, kwa sababu maisha yetu ya zamani, kwa sababu ya dhambi, yalionekana kuwa hayafai, na kwa hiyo hatukuwa na uzima wa kweli, yaani tulikuwa wafu kiroho.

Lakini kwanza tutaliangalia neno ambalo tumelitumia mara kadhaa tayari: “*asili mpya na asili ya zamani*”. Ingawa maneno haya hayapatikani hivyo katika Biblia, jambo yanalolisimamia linapatikana humo. Kile tunachokiita “*asili mpya*”, kinyume na “*asili ya zamani*” (yaani *tabia ya mvili*), si kitu kingine ila “*asili ya Mungu*”. Petro anaandika katika waraka wake wa pili, sura ya 1:4:

“... ili kwa hizo (abadi) mpate kuwa washirika wa asili ya Mungu.”

Daima inasaidia kuutazama muktadha ambamo maneno haya yamefungamana. Mahali hapa muktadha ni huu:

Mkristo amepokea kila kitu kutoka kwa Mungu ili aweze kuishi kwa ajili yake. Kwanza uzima wenyewe. Huo unaweza kuitwa uzima wa utu mpya. Kuutekeleza uzima huu wa Mungu katika maisha ya kila siku maana yake ni “utauwa” (kicho kilicho sahihi; maisha yanayopatana na Mungu), yaani maisha kwa utukufu wa Mungu. Kwa Neno lake Mungu ametuonyesha utukufu wake mwenyewe, uliotushika na kuleta uamuzi kamili wa kumweka yeye mwenyewe mbele ya macho yetu kuwa lengo la maisha yetu na la safari yetu ya maisha. Safari hii inapita katika ulimwengu – si tu katika uumbaji wa Mungu, bali pia katika ulimwengu uliobadilishwa na kuharibiwa na wanadamu, yaani jamii tunamoishi. Kama wapokeaji na washirika wa asili ya Mungu tumeukimbia uharibifu ulioko duniani. Tukiwa na asili ya Mungu sasa tunaweza kuishi tofauti na ulimwengu, ulio na alama ya tamaa. Hapa pia inakuwa wazi asili hii ya Mungu ni nini na si nini. Haihusu utukufu wa nje wa Mungu, bali asili ya Mungu ya kimaadili. Ni

uzima wa kiroho unaopita uwezo wa asili, unaobeba ndani yake sifa za Mungu za kimaadili, ambazo Petro hapa anazilinganisha kinyume na mwenendo wa ulimwengu uliopotea.

Asili hii inajidhihirisha kwa uhalisi katika mchakato wenye nguvu na mwendo, ambamo aliyezaliwa mara ya pili anajitahidi kwa bidii yote na kuzaa matunda ya kiroho. Kwa njia hii anafanya imara kuitwa kwake na kuteuliwa kwake na Mungu. Ndivyo anavyothibitisha katika maisha yake kazi ya Mungu ya wokovu ndani yake. “Kuwa washirika wa asili ya Mungu” hakumaanishi tu *kumiliki* kitu, bali vilevile pia *kufanyika* kitu: Inahusu kufanana na Mungu, na kwa hiyo kuwa wafuasi wa mfano wake.

Ushahidi kwamba asili, au hali, ya Mungu inaweza kweli kuingia ndani ya mtu na kuyatambulisha maisha ya mtu, ni Yesu mwenyewe. Ndani yake kuna uzima wa Mungu; yeye mwenyewe ndiye uzima wa milele. Alifanyika mwanadamu ili uzima huu ufikike kwetu sisi wanadamu na tuweze kuuonja katika uzoefu. Kwa hiyo Yohana anaweza kusema: “Jambo lililo kweli ndani yake na ndani yenu” (1 Yohana 2:8).

14.1 Asili ni nini hasa?

Asili maana yake ni hali au umbile la asili linalokitambulisha kitu tangu mwanzo, au kiumbe hai tangu kuzaliwa. Asili ya mnyama ni tofauti na asili ya mwanadamu (Yakobo 3:6-7). Katika muktadha wetu asili inajumuisha kitu ambacho mtu amekipokea – tofauti na kile ambacho mtu amekizalisha mwenyewe. Neno *asili* (kwa Kiyunani *physis*) linamaanisha “kule kuwa kumetokea”⁸⁷; kitenzi chake kinamaanisha *kuzaa*, *kukuza*, *kuchipua* na *kukua* (hasa kwa mimea); nomino yake inamaanisha pia *chanzo* na *kuzalima*.

Sisi wanadamu *kwa asili*, yaani tangu kuzaliwa na kwa hali yetu na asili yetu, ni watoto wa hasira (Waefeso 2:3; Wagalatia 2:15). Katika maumbile kuna kanuni kwamba kila aina inazaa wazao wake yenyewe. Ndivyo ilivyo pia kwa mwanadamu: Inahusu mwili, yaani utu wa nje, sawasawa na moyo wake, yaani utu wa ndani. Hata leo katika karne ya 21 mwanadamu bado anaidhihirisha asili ya Adamu (mwanadamu wa kwanza aliyeumbwa), lakini pia kile ambacho Adamu alikuwa kwa sababu ya anguko lake. Tunatofautisha kati ya asili ya mwanadamu inayotajwa na Yakobo (yaani kile tulichofanyika kuwa kama viumbe vya Mungu kwa mfano wake) na hali ya dhambi tuliyoirithi kutoka kwa

87. Kittel, *Theologisches Wörterbuch zum Neuen Testament* (kwa Kiyunani *phyein*).

Adamu (baada ya anguko). Kwa maneno mengine: “Tunapaswa kutofautisha kati ya asili ya mwanadamu na asili yetu kama wanadamu walioanguka.”⁸⁸ Sisi ni wanadamu na tutakuwa hivyo daima, badiliko lolote tunalolipata kwa kuzaliwa upya kwa habari ya roho na nafsi, na badiliko lolote linalongoja mwili wetu wakati ule Bwana atakapokuja kutuita kwake. Kamwe hatutapoteza utambulisho wetu wa asili ambao Mungu alituumba nao hapo kwanza (kwa kuzaliwa). Sisi ni watu walewale, na tutabaki hivyo – watu binafsi walewale. Kwa hiyo tunapaswa kutofautisha kati ya maneno kama ‘asili yetu ya kibinadamu’, ‘asili yetu iliyoanguka’, ‘asili yetu mpya’. Anguko halikuuondoa (asili ya) ubinadamu wetu; kwa upande mwingine kuzaliwa kwetu upya hakuuondoi ubinadamu wetu. Kilicho cha asili kwa ubinadamu hatutakipoteza kamwe, na upekee wetu kama watu binafsi hautabadilishwa kamwe.”⁸⁹

Asili ya Adamu iliyoanguka inaeleza kwa ufupi uhalisi wa kibinadamu ambao hauamuliwi tena na roho ya mwanadamu na uhusiano wake na Mungu (tofauti na mnyama, ambaye hana roho), bali na nafsi na mwili. Roho ya mwanadamu ndiyo makao ya ufahamu wake wa Mungu na uwezo wake wa msingi wa kutambua kuwepo kwa Muumba, na pia uwezo wake wa kumwamini, kumwomba, kumtafuta na kumheshimu. Lakini kazi hii imepata madhara makubwa kwa sababu ya dhambi. Roho haijazimwa, lakini kazi yake haielekezwi tena kwa Mungu aliye hai. Paulo anaeleza matokeo yake hivi: “Mwanadamu wa *asili* (kwa Kiyunani *psychikos*, yaani hasa *wa nafsi*) ... hayapokei mambo ya Roho wa Mungu” (1 Wakorintho 2:14). Anguko limegusa pande zote za uhalisi wa kibinadamu. “Uhusiano (na Muumba katika) upendo, heshima na kumtegemea, uliomweka karibu na Mungu, umevunjika; anafanana na nyumba ambayo paa lake limeporomoka na kuanguka chini. Akiitwa kwa jina la upande wa chini kabisa ambao roho na nafsi zimeshuka hadi kwake, yeye ni ‘tabia ya mwili’. Kwa hiyo ‘tabia ya mwili’ ndilo jina la Kimaandiko la asili yake ya zamani au iliyoanguka.”⁹⁰

14.2 Washirika wa asili ya Mungu

Tukiwa na *asili ya zamani* tulikuwa mali ya ulimwengu, ambamo hatawali Kristo, bali Shetani. Lakini kwa kupokea uzima mpya tumeukimbia uharibifu wa

88. Tofauti hii inaweza kuonyeshwa vizuri sana kwa mfano wa Yesu mwenyewe: Alichukua asili ya kibinadamu alipofanyika mwili (kupata mwili), lakini si asili ya zamani, yaani ile yenye dhambi.

89. F. W. Grant, *The two Natures*, uk. 5.

90. *Ibid.*, uk. 7.

ulimwengu na unajisi wake (2 Petro 1:4; 2:18, 20). Kwa mwili bado tuko ulimwenguni. Kwa hiyo tunaishi katika ulimwengu miwili wakati mmoja (Waefeso 2:6; Wakolosai 2:20; 3:1-5). Tukiwa na uzima wa Mungu tu mali ya ulimwengu mpya wa Mungu, wa uumbaji wake mpya, uliombwa ndani ya Kristo na kwa njia ya Kristo.

Maisha yetu ya kujiamulia wenyewe yamefikia mwisho; “kampuni yetu ya Mimi” imefilisika; biashara ya maisha yetu, au ya ulimwengu wa nafsi zetu, imeanguka kabisa. Shauri la ufili lilimalizwa pale Golgotha. Madeni yamelipwa na Kristo. Lakini sasa sisi ni washirika katika uzima wa Mungu; sasa tuna “hisa salama”, sisi ni “wanahisa”, kwa sababu tunashiriki uzima wa Mungu. Kwa “hisa” hizi kuna mwanzo mpya wa kweli, kwa sababu Mungu mwenyewe ndiye chanzo chake.

14.3 Uzima wa milele ni uzima wa Kristo

Kihalisi tumepewa sehemu katika uzima wa Mungu, sehemu katika uzima wake wa milele. Mwishowe hili si kitu kingine ila ukweli kwamba Kristo mwenyewe, kama Mtu, ndiye uzima wetu mpya (kwa hilo unaelezwa tu upande mwingine wa jambo lililile). Kama vile yeye mwenyewe alivyo utu mpya ambao tuliumbwa kuwa, ndivyo anavyodhihirisha uzima wetu mpya.

Ukweli kwamba tuna uzima wa Mungu hautuinui kufikia nafasi ya miungu. Vivyo hivyo hatugeuki kuwa Kristo, Kristo anapokuwa uzima wetu. Tunabaki viumbe, wanadamu kwa mfano wa Mungu, ambao kwa sababu ya uzima huu sasa wanaweza kuwa tena katika ushirika na Mungu. Tuna uzima “*katika Kristo*”, aliye chanzo chake na ambaye tunamtegemea. Hatuna uzima huu tukiwa tumetengwa naye.

14.4 Tunakuwaje washirika wa uzima wa Mungu?

Neno *asili* linahusiana na kuzaliwa na kukua, na linaelekeza mawazo yetu kwenye jambo ambalo Yesu alimfafanulia mwalimu wa sheria Nikodemo: *kuzaliwa mara ya pili*.

Kwa kiini chake inahusu kuzaliwa mara ya pili, ambako kwa njia yake tunakuwa washirika wa asili ya Mungu. *Kuzaliwa mara ya pili* ni neno la Biblia lisilo na uhusiano wowote na dini za Mashariki ya Mbali, na “mzunguko wa milele wa kutokea na kutoweka” (kama, kwa mfano, katika Ubudha), wala na mtazamo wowote wa ulimwengu wa aina yoyote ile. Kuzaliwa mara ya pili

kunazungumziwa na waandishi kadhaa wa Agano Jipya, lakini kunaielezwa kwa kirefu zaidi na mtume Yohana. Ingawa kuhama kwetu kutoka kwa Adamu hadi kwa Kristo kuna pande mbalimbali, upande wa kuzaliwa mara ya pili unaelezwa hasa na Yohana. Kuzaliwa mara ya pili kunaumba uzima mpya ulio tofauti. Uzima huo unatofautiana na ule uzima tuliourithi kwa asili (kutoka kwa Adamu).

Waandishi wote wa Agano Jipya wametoa michango yao kuhusu jinsi mtu anavyopata uzima mpya na jinsi unavyojidhihirisha katika maisha ya kila siku. Wote wanakubaliana kwamba kuwa Mkristo kunamaanisha badiliko la mtu, ambalo mtu mwenyewe hawezi kulileta, bali linakuja kutoka juu, kutoka kwa Mungu mwenyewe. Kwa hilo tayari tuko katikati ya mada yetu. “Kutoka juu” ndilo hasa neno ambalo Yesu analitumia kuhusiana na kuzaliwa upya.

14.5 Kuzaliwa mara ya pili – kuzaliwa na Mungu

Nikodemo alitaka kuzungumza na Yesu kuhusu maswali ya kitheolojia. Lakini Bwana Yesu hakuwa na muda kwa ajili ya hilo. Kwake ulazima wa kuzaliwa upya ulikuwa muhimu zaidi. Kwa hiyo Bwana Yesu anasema katika sentensi moja kwamba kile alichomo mwanadamu kwa sababu ya kuzaliwa kwake (kwa asili) hakiwezi kuuona ufalme wa Mungu, sembuse kumpa njia ya kuingia (Yohana 3:1-36). Ulazima wa kuzaliwa upya hauachi chochote chema katika kile tulicho kwa asili. Hili linamhusu pia Nikodemo, mwalimu wa Israeli. Yesu anamwambia kwamba kuzaliwa huku hakutokei kwa kuzaa kwa kibinadamu, bali “kwa maji na kwa Roho”. Si kuzaliana kwa kawaida, bali ni utendaji kutoka juu, kutoka kwa Mungu. Watoto wa Mungu hawazaliwi kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu (Yohana 1:13). Mtu anakuwa mtoto wa Mungu tu kwa kuzaliwa mara ya pili! Mtu angeweza kuzaliwa mara mamia na baba wa kimwili na mama yake, na matokeo yangukuwa yaleyale daima: Kilichozaliwa kwa tabia ya mwili ni tabia ya mwili. Ikiwa mtu anapaswa kuzaliwa upya, basi chanzo chake lazima kitafutwe mahali pengine kabisa. Lakini kuzaliwa huku kwa ajabu kunaletwaje? Kunatokea kihalisi kwa maji na kwa Roho, kama Bwana Yesu anavyosema (Yohana 3:5).

14.5.1 Kuzaliwa kwa maji

Hapa haihusu kuzaliwa kihalisi, wala vifaa vinavyotumika wakati wa kuzaliwa. Kwa hiyo maji lazima yawe na maana ya mfano. Maji yanaashiria nini? Maji ni

mfano wa Neno la Mungu, kama Paulo anavyowaandikia Waefeso: "... kwa kuoshwa kwa maji katika neno" (5:26). Neno la Mungu ni chombo halisi katika kuzaliwa mara ya pili:

"Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa kwa neno la kweli."

Yakobo 1:18

"... kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu ibaribikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo bata milele." (taq. pia 1:3)

1 Petro 1:23

"Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia."

Yohana 15:3

Maji ni Neno la Mungu na nguvu yake ya kutakasa. Linahuishwa na Roho wa Mungu na linamtendea kazi mwenye dhambi. Neno la Mungu linalohubiriwa, linaloshuhudiwa au linalosomwa linaifunua dhambi na kuongoza kwenye toba na imani. Kumpokea na kumkubali Yesu Kristo kwa imani kunaleta kuzaliwa mara ya pili (Yohana 1:12). Imani ni matokeo ya kuhubiriwa kwa Neno la Mungu (Warumi 10:17). Kama mbegu ya Mungu, Neno hilo linazaa uzima mpya.

Neno, ile mbegu isiyoharibika, linaleta angalau mambo mawili: Linazaa uzima ambao, kama Neno lenyewe, hauharibiki (yaani ni wa milele). Na linazaa uzima ulio na sifa zilezile hasa ambazo Neno la Mungu linazo. Neno la Mungu ni DNA ya uzima mpya. Mbegu ina habari zote kuhusu jinsi mmea au kiumbe hai kilichozaliwa kitakavyokuwa. Ndivyo Neno la Mungu lilivyo ramani, "msimbo wote wa kijeni" wa uzima mpya. Neno hili, tunaloweza kulisoma, linaonyesha jinsi uzima huu unavyotekelezwa na kujidhihirisha. Kwa maana hii Yakobo anasema kwamba tumezaliwa kwa neno la kweli, na kwamba neno hili wakati huohuo ni mbegu iliyopandwa ndani yetu ili iweze kukua (Yakobo 1:18, 21). Asili ya mbegu inaamua umbo la uzima. Asili ya Mungu ndani yake yenyewe ni kamilifu au kamili (kama ilivyo pia kwa mbegu husika), lakini ndani yetu inaweza na inapaswa kuumbika na kuongezeka.

Kabla hatujafika kwenye chombo cha pili, baada ya mawazo yaliyotangulia, inatosha kusema kwamba hapa hauzungumziwi ubatizo wa maji. Maji ya ubatizo wa maji hayazai utu mpya wala hayatufanyi kuwa watoto wa Mungu. Bali ubatizo wa maji unatuunganisha na Kristo *kwa nje* (katika ushuhuda wetu wa imani).

14.5.2 Kuzaliwa kwa Roho

Si roho ya mwanadamu inayozaliwa mara ya pili. Vivyo hivyo si roho hiyo inayoleta kuzaliwa upya. Bali ni Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa njia yake kuzaliwa mara ya pili kunaanzishwa na kukamilishwa.

Kilichozaliwa kwa Roho ni roho. Ni kweli kwamba zawadi ya kuzaliwa mara ya pili haihusu uzima mpya kwa upande wa mwili au wa kibiolojia. Ni uzima wa kiroho, kinyume na hali ya asili ya mtu ambaye hajakombolewa. Lakini pia unapatana na Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, kwa sababu ni uzima wa Mungu. Uzima mpya unalingana na asili ya Roho Mtakatifu; kwa maana tumekuwa washirika wa asili ya Mungu (wa uzima wa Mungu).

Licha ya elimu yake, Nikodemo analemewa. Angeweza kujua kutoka katika Agano la Kale kile ambacho “maji na Roho” vinaleta, vyote viwili vinapomtendea mwanadamu kazi kwa utendaji wa Mungu!

14.5.3 Unabii wa Ezekieli: mioyo mpya na roho mpya

Ni Ezekieli ambaye hakuzungumzia *kuzaliwa mara ya pili* kwa maana ya neno lenyewe, lakini kwa hakika alimaanisha tukio lilelile, ambamo maji na Roho vingetumika. Mungu atafanya mambo yafuatayo (Ezekieli 11:19; 36:25-27):

- kuwanyunyizia Waisraeli maji safi ili kuwatakaswa
- kuwapa moyo mpya na roho mpya
- kuwapa moyo wa nyama badala ya moyo wa jiwe
- Roho wa Mungu atatiwa ndani yao, ili waishi katika amri za Mungu.

Hapa vimetajwa vipengele muhimu vya wokovu wa Mungu katika kuzaliwa mara ya pili. Kwanza ni kutakaswa, kunakomaliza mambo yaliyopita. Mahali pa maisha ya zamani, ambayo yalihitaji kutakaswa, sasa vinakuja moyo mpya na roho mpya.

Neno “moyo” hasa, na pia neno “roho” (kwa maana ya “roho ya mwanadamu”), yote yanamaanisha sehemu ya ndani kabisa ya mtu husika (Mithali 4:23). Inahusu kiini cha haiba ya mwanadamu, kinachopaswa kubadilishwa kabisa. Kwa badiliko hili mwanadamu hawi mtu asiye na mapenzi, bali kwa njia hiyo anawezeshwa kuyatenda mapenzi ya Mungu. Moyo wa jiwe ni moyo mgumu – moyo uliokufa, usioweza wala usiotaka kuishi kumwelekea

Mungu. Mapenzi ya mtu yanapofanywa upya, anahitaji nguvu ili aweze pia kuyatenda mapenzi ya Mungu. Anapokea Roho wa Mungu, ambaye kwa njia yake anawezeshwa kweli kuishi kwa kufuata amri za Mungu.

Hapa pia inaonekana wazi kwamba mwanadamu anabadilishwa kutoka ndani, wala si kwa amri anazowekewa kutoka nje, zinazoleta tu badiliko la nje la mwenendo. Watu wanaweza kubadilisha mwenendo wao kwa nidhamu kali, lakini Mkristo anaenenda tofauti kwa sababu amepokea moyo mpya na Roho wa Mungu. Utii mpya kwake ni jambo la moyo. Katika hilo nidhamu pia ni muhimu, lakini si ya kuamua.

Kilichozaliwa kwa Roho ni roho! Hivyo tayari Ezekieli anatofautisha kati ya “roho mpya”, inayolingana na uzima mpya, na Roho Mtakatifu kama Nafsi, anayekaa ndani ya aliyezaliwa mara ya pili. Ingawa Yesu hazungumzi moja kwa moja na Nikodemo kuhusu kipawa cha Roho Mtakatifu, hata hivyo jambo hilo limejumuishwa hapa. Yohana anamtaja Roho mara kadhaa kuwa mali yetu (Yohana 7:39; 14:17, 26; 15:26; 16:13).

Paulo anayachukua maneno ya Ezekieli na kueleza kwamba yanatuhusu sisi pia: Roho wa Mungu anaandika juu ya mioyo yetu, ambayo, tofauti na zile mbao za mawe za sheria, si ya jiwe, bali ya nyama. Hili linamaanisha kwamba mioyo yetu nayo imebadilishwa kabisa. “Kazi” hii ya Mungu katika moyo wetu inaonyesha kwa mara nyingine kile ambacho Mungu anafanya ili kutubadilisha zaidi na zaidi tufanane na mfano wa Mwana wake. Kuandika kwake juu ya mioyo yetu kuna lengo moja: Tunapaswa kubadilishwa kwa upande wa maadili tufanane na mfano ulcule wa Kristo aliyetukuzwa katika kiti cha enzi cha Mungu – nayo ni kwa njia ya Roho (2 Wakorintho 3:3, 18).

14.6 Tumeokolewa kutoka mautini hadi uzimani: tumehuishwa

Kuzaliwa upya ni lazima si kwa sababu hatuna uzima, bali kwa sababu tunakosa uzima *ulio sabihi*. Kilichozaliwa kwa tabia ya mwili ni tabia ya mwili, na kwa hiyo hakifai kitu. Tunapaswa kuzaliwa kwa Roho. Ni kwa njia hii tu tunaingia katika ufalme wa Mungu na kuyamiliki mambo ya mbinguni.

Lakini kwa mantiki, matokeo ya kuzaliwa ni pia uzima ambao haukuwepo kabla. Kwa hiyo Bwana Yesu anasema kwamba tayari sasa atawaleta watu kutoka mautini hadi uzimani. Hapa na leo (si tu wakati ujao) atafanya hivyo: “Saa inakuja, na sasa ipo, ambayo wafu wataisikia sauti ya Mwana wa Mungu, nao waisikiao watakuwa hai” (Yohana 5:25). Kama vile Neno la Mungu lilivyo

mbegu ya kuzaliwa mara ya pili, ndivyo hapa Neno (sauti ya Mwana) linalohuisha. Kwa asili mwanadamu si tu mwenye dhambi (yaani kiumbe kinachotawaliwa na tabia ya mwili, kisichofaa kitu). Yeye pia ni mfu anayehitaji uzima. Kwa asili amekufa katika dhambi zake (Waefeso 2:1; Wakolosai 2:13 na kwingineko). Mauti daima maana yake ni kutenganishwa kwa mambo ambayo kwa asili yao ni ya kuwa pamoja. Kwa hiyo mwanadamu kwa upande wa kibiolojia na wa akili yuko hai kabisa, lakini *kwa maana ya kiroho*, kwa habari ya uhusiano wake na Mungu, amekufa. Uhusiano huu, pamoja na yote yanayohusiana nao, haupo. Kwa njia ya kufufuliwa *kiroho* (au kuhuishwa, ambako mwishowe kunajumuisha upande mwingine wa kuzaliwa mara ya pili) mwenye dhambi aliyekufa kiroho anapokea uzima wa milele. Kutengwa kwake na uzima wa Mungu (Wakolosai 1:21; taz. Waefeso 4:18) kunaondolewa kwa njia hiyo. Kwa uzima huu uhusiano na Mungu haurudishwi tu na kufikishwa katika hali ya uhusiano wa Adamu na Mungu kabla ya anguko lake. Bali kwa njia hiyo unafungwa uhusiano unaotufanya kuwa watoto na wana wa Mungu. Tumepita kutoka mautini kuingia uzimani! “Roho ndiye atiaye uzima; tabia ya mwili haifai kitu. Maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima” (Yohana 6:63), asema Bwana Yesu.

14.7 Siri ya kutokea na kukua

Inasaidia kusema jambo kwa ujumla kuhusu tendo la kuzaliwa upya. Biblia haisemi ni katika sehemu gani ya mwanadamu uzima wa milele unakaa Mungu anapompa mwanadamu. Wengine wanasema kwamba uko katika roho yetu, wengine wanasisitiza nafsi. Inavutia kuyapangia matukio ya wokovu yanayotokea ndani ya mwanadamu kila kipengele kimoja cha hali ya kibinadamu. Lakini Biblia si kitabu cha elimu ya mwanadamu, wala ya utu wa zamani wala ya utu mpya.⁹¹ Katika kuzaliwa mara ya pili tunashughulika na siri iliyofunuliwa kwa sehemu, lakini kwa sehemu fulani pia imefichwa, jambo linalotokana na utata wa asili ya mwanadamu. Hili linaonyesha kwa mara nyingine mipaka ya ufahamu wetu, lakini haliondoi chochote katika ukweli kwamba kweli tunao uzima wa milele (wa kiroho) wa Mungu kuwa uzima wetu wenyewe. Bwana Yesu mwenyewe analinganisha tendo la kuzaliwa upya, linaloletwa na Roho, na upepo: Mvumo wake mtu anaweza kuusikia (yaani mtu anaweza kuona matokeo

91. Hans-Jörg Ronsdorf, *Hata Hiiyo, Wajifu Wako Hai* (Und die Toten leben doch), sura ya 3 (Mtazamo wa Biblia kuhusu mwanadamu), uk. 147 na kuendelea.

yake ndani ya mtu husika ambaye Roho anamtendea kazi). Lakini hawezi kuona unakotoka wala unakokwenda (Yohana 3:8). Kuzaliwa mara ya pili kwetu ni tukio lililofichika, lisiloweza kuonekana wala kwa ufahamu wetu wala kwa teknolojia.

Hata mchakato wa ukuaji wa uzima mpya haelezwi kwa undani, bali unachukuliwa kuwa upo. Karibu waandishi wote wa Agano Jipya wanathibitisha kwamba kuna ukuaji na kufanywa upya (kwa kudumu), mwendo, na pia maendeleo na ukomavu unaoongezeka katika imani (Yohana 3:30; Waefeso 4:13; 1 Petro 2:2; 2 Petro 3:18; Wakolosai 1:10; 3:10; 1 Yohana 2:12-17; Wagalatia 4:19; Warumi 12:2; 2 Wakorintho 3:18; 4:16; Waefeso 4:23). Hili linaelezwa kwa kiasi kikubwa kwa kanuni. Katika hilo daima inahusu tukio ambalo kwa upande mmoja linaanzishwa na kuendelezwa na Mungu mwenyewe, lakini kwa upande mwingine linaweza kutekelezwa tu kwa mchango wetu, kukubali kwetu na uamuzi wetu, na pia kwa nidhamu yetu na uthabiti wetu katika kuzifuata amri za Kristo (Luka 8:15; 2 Petro 1:8; Yakobo 3:18; Tito 3:14). Mchakato wa kubadilishwa daima unatokea kwa kufuata kanuni zilizotajwa. Lakini ndani ya mamilioni mengi ya Wakristo unaendelea (kwa sababu ya tofauti za Wakristo hawa katika umbile lao la asili, hali yao ya maisha na pia uthabiti wa uamuzi wao) kwa kasi na nguvu tofauti. Mtunza bustani wa kimungu anashughulikia kwa upendo kila mmea mmoja mmoja (Waebrania 12:11; Yohana 15:2) – kwa wote akiwa na lengo moja kuu, kwamba wafananishwe na mfano wa Mwana wake (Warumi 8:29). Ikiwa hili ndilo lengo kuu la *Mungu*, basi lazima liwe pia shauku yetu kuu. Ushirika huu na Mungu, au makubaliano haya ya kuwa na lengo lilelile, utarahisisha mambo mengi katika maisha yetu na kutupa mwelekeo mkubwa zaidi kuelekea lengo. Kwa njia hiyo tutapata mtazamo tofauti kabisa – yaani wa kimungu – juu ya hali yetu ya maisha ya kila siku.

Ni hekima ya Mungu peke yake inayoleta *kutokea* kwa uzima mpya na pia *ukuaji* wake. Jambo la kuamua ni matokeo, ambayo kwayo utendaji wa Mungu unatambulika, yaani tunda jema la Roho katika maisha yaliyobadilika ya Wakristo.

14.8 Ukuaji – uzima unakua

Ukuaji ni jambo la muhimu kabisa. Uzima wa Mungu wenyewe ni kamili, lakini unapowekwa ndani ya mtu, unapaswa kukua. Unapaswa pia kumwenea mtu wote kwa vitendo. Uzima mpya unabadilisha mwenendo wa mtu, ufahamu wake

au hali yake, zaidi na zaidi kutoka katika maisha ya zamani kuelekea maisha mapya (yaani asili ya Yesu Kristo inaumbika zaidi na zaidi ndani yake; Wagalatia 4:19; 2 Wakorintho 3:18).

Hebu tuyatazame maumbile ya porini. Huko hakuna mashamba ya ngano. Yanapatikana tu mahali ambapo watu wameyaandaa na kupanda mbegu inayofaa. Vivyo hivyo katika maisha yetu ya zamani tulizaa tu miiba na michongoma (Waefeso 5:11). Lakini sasa mbegu ya Neno inatawanywa; na nafaka njema inakua, tunda kwa ajili ya Mungu (Mathayo 13:23; Warumi 6:22; 7:4). Mbegu inaota katika “udongo wa moyo” wenye rutuba. Ndivyo uzima mpya utokao kwa Mungu unavyombadilisha mtu. Matokeo ya kile kilichotokea ndani, na kinachoendelea kutokea tangu hapo, yanaweza kuonekana katika mwenendo wa mtu aliyezaliwa mara ya pili: Sasa ameelekezwa kwa yule aliyemzaa.

Ndani ya mtu ambaye mbegu inapandwa ndani yake bado kuna uovu, kama vile katika shamba la ngano mtu anaweza bado kuona michongoma na miiba, kwa kiasi kikubwa au kidogo. Lakini uzima mpya, tunda jipya, pia ni maisha ya ushindi (1 Yohana 5:4). Ndani yake mabadiliko ya aliyezaliwa upya yanaweza kuchanua: Sasa amekuwa mfuasi wa mfano wa Mungu, aliyempa uzima. Wakati udongo mzuri unazaa tunda jema, sisi katika shamba la maisha yetu tunaondoa kile kisicho tunda jema: miiba ya tabia zetu za zamani zenye dhambi, na michongoma yenye mizizi mirefu na yenye kina, inayowakilisha mazoea ya zamani yaliyo sugu. Baadhi ya magugu yanahitaji nidhamu kali na uvumilivu hadi yakome kuleta madhara, lakini juhudi hizi zinalipa tukijikabidhi kwa lengo ambalo Mungu analo kwa ajili yetu. Mawe yaliyotapakaa katika shamba la maisha yetu ni mizigo na uzito usio wa lazima; wakati mwingine ni dhambi zinazotuzinga kwa urahisi, zinazopunguza kasi ya ukuaji wetu na maendeleo yetu na kuyazuia (Isaya 5:1-7; Waebrania 12:1).

Inashangaza jinsi ukuaji unavyochukua nafasi kubwa katika Biblia, na jinsi unavyotumiwa mara nyingi kwa mwanadamu. Israeli lilikuwa shamba la mizabibu la BWANA, nalo lilipaswa kuzaa matunda mazuri. Mungu mwenyewe ndiye mtunza shamba la mizabibu.

Ni muhimu kulilinda vema shamba la mizabibu la maisha yetu, au “shamba letu wenyewe la mizabibu” (Wimbo Ulio Bora 1:6). Kristo ndiye mzabibu, na sisi ni matawi yake, ili tumzalie Baba matunda (Yohana 15:1-8).

Ukuaji wa kiroho ni mchakato wa kawaida, kama unavyotokea katika maumbile na pia katika asili yetu ya kibinadamu. Ukuaji huu unahitaji muda na mazingira yote yanayohitajika. Ukuaji hautokei kwa kuruka hatua, wala hakuna njia za mkato – kwa mambo au uzoefu wa aina yoyote ile. “Hakuna mahali popote katika Maandiko panapofundishwa kwamba kuna kuruka ghafla kutoka hali ya tabia ya mwili hadi hali ya kiroho, au kutoka maisha ya kutojali kiasi hadi maisha ya kujitoa kwa Kristo. Kinyume chake, ukuaji katika utauwa unaonyeshwa kuwa ukuaji unaopaswa kuwa wa kawaida na wa asili kama ukuaji wa kawaida wa mtu kutoka utoto hadi kuwa mtu mzima aliyekomaa.”⁹²

Kwa nyumba za kuoteshea mimea (nyumba za kioo) mtu anaweza kuziepuka kanuni za majira ya mwaka na kuvuna mimea mingi na aina nyingi za mboga katika kila majira. Lakini sote tunajua kwamba katika nyumba ya kuoteshea mtu hawezi kamwe kukuza mimea yenye ubora ule unaofikiwa na mimea ya shambani wazi. Hilo linahusu pia ladha ya matunda ya mimea inayopandwa katika nyumba ya kuoteshea. Vivyo hivyo tunda la kiroho hukua vizuri zaidi katika maisha ya kila siku. Katika maumbile ya wazi, ambapo linakabiliwa na upepo na hali ya hewa, joto na baridi, ukame na mvua, tunda lina mazingira bora kabisa ya kukua. Hatutaki kuwa “Wakristo wa nyumba ya kuoteshea”.

14.9 Kutunza

“Kutunza” (kulima) maana yake, kwa mfano, ni kuandaa shamba la ngano mahali ambapo hapo awali palikuwa msitu au nyika. Kuhusiana na “kuzaa matunda” Paulo anasema (Wafilipi 2:12-13):

*“Utimizezi wokovu wenu wenyewe
kwa kuogopa na kutetemeka;
kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu
kutaka kwenu
na kutenda kwenu,
kwa kuliitimiza kusudi lake jema.”*

Huenda hakuna neno jingine la Biblia linaloonyesha kwa ufupi na kwa wazi namna hii wajibu wetu wa kutenda, na wakati huohuo utendaji wa Mungu katika matendo yetu. Wakati sisi “tunatimiza”, wakati huohuo Mungu yuko kazini. Wokovu unatulazimu kutenda: Kwa maana tunapaswa kutoa ushahidi wa

92. Henry Allen Ironside, *Heiligung – Zerrbild und Wirklichkeit*, uk. 153.

wokovu tuliopata – naam, kuutimiza. Neno hili la Biblia lina mvutano mkubwa kati ya wajibu wetu na utendaji wa Mungu. Lakini hatupaswi kuuondoa mvutano huu kwa urahisi, tukidhani kwamba wokovu unapaswa kutazamwa kando na utendaji wetu, na kwamba hauhusiani na juhudi zetu wenyewe. Na tulichukue Neno la Mungu jinsi lilivyo! Hata kwa kuogopa na kutetemeka (yaani tukijua kwamba tunaweza kukosea) tunapaswa kuuishi wokovu na kulichukulia kwa uzito “agizo la wokovu” (yale tunayoagizwa kutenda kwa sababu ya wokovu; kwa Kijerumani *Heilsimperativ*) linalotajwa mara nyingi. Siku tutakapofika kwenye lengo, tutatambua kwamba katika juhudi zetu zote, ni Mungu kwa neema yake aliyetimiza kila kitu.

Lakini mstari huu unahusianaje na ukuaji wa kiroho? Neno “timizeni” katika lugha ya Kiyunani lilitumika pia kwa kilimo, au kwa kulima shamba. Hili linatuthibitishia: Mungu amepanda Neno lake mioyoni mwetu, uzima mpya tumepewa. Sasa tunapaswa kulitunza na kulilima shamba hili la uzima mpya: Katika hilo tunapaswa kuondoa kila kinachosumbua na kuandaa kila kinachostawisha ukuaji. Zaidi ya hayo tunapaswa kuhakikisha kwamba mavuno mazuri yanaweza kukusanywa. Maisha yetu yanafanana na shamba, jambo ambalo bila shaka linamaanishwa kwa lugha ya picha. Tena kazi hii ya mkulima ni kazi ya Mungu mwenyewe. Kwa kumtumaini Mungu, anayetenda kila kitu na anayetaka kutenda, tunakitunza kile ambacho Mungu ameumba ndani yetu.

Mambo ya ulimwengu yanaufanya udongo wa moyo kuwa mgumu na usiopokea maneno ya Mungu. Udongo ambao hadi sasa ni mgumu unapaswa kulainishwa kwa taabu, ili uweze kupokea maji na kuzaa matunda tena. Pia magugu ya mawazo mabaya na machafu yanapaswa kuondolewa daima. Mimea michanga ni rahisi kuondoa kuliko ile ya zamani yenye mizizi mirefu. Kwa hiyo na tupambane nayo mara moja na daima!⁹³

14.10 Burudani au wajibu?

Mtu anayelima bustani kama burudani anashughulikia magugu kwa sababu kuwa na bustani nzuri ndiyo burudani yake. Halazimiki kufanya hivyo, hakuna anayemlazimisha. Tukiitumia picha ya mtunza bustani au ya mkulima kwa utakaso wetu, basi si jambo la hiari tunaloweza kulifanya au pia kulipuuza. Kuamua kuishi maisha ya utakaso na ya ukuaji wa kiroho si jambo la kundi la pekee la Wakristo wanaotaka kwenda kwenye umisionari au kuwa wahubiri. Bali

93. C. G. Willis, *Betrachtungen über den Brief an die Philipper*, uk. 184.

wokovu unatulazimu kuufuatia utakatifu, ambao bila huo hakuna mtu atakayemwona Bwana. Hata ikisikika ngeni kwa mtu mmoja au mwingine: Bila utakatifu katika maisha yetu hatutamwona Bwana mwishoni (Waebrania 12:14)!

“Kwa maana nchi inayoinywa mvua iinyeshayo juu yake mara kwa mara, na kuzaa mimea yenye manufaa kwa wale ambao kwa ajili yao inalimwa, inapokea baraka kutoka kwa Mungu; bali ikizaa miiba na michongoma, haikubaliki, na karibu kulaaniwa, na mwisho wake ni kuteketezwa” (Waebrania 6:7-8).

14.11 Ukweli wa wokovu katika maandiko ya Yohana

Uzima wa Mungu (uzima wa milele) ndio mada ya Yohana. Vivyo hivyo anashughulikia kuzaliwa upya, ambako kwa njia yake tunaupokea uzima huu. Katika nyaraka zake tatu tunataka kukusanya kile tulichofanyika kuwa kama watoto wa Mungu na kile tulichopewa. Kwake *ukweli* wa wokovu (yale ambayo Mungu ameshatenda; kwa Kijerumani *Heilsindikativ*) maana yake ni haya yafuatayo (angalieni mifanano mingi na Paulo):

- ushirika na Baba na Mwana wake Yesu Kristo (1 Yohana 1:3)
- furaha kamili (1:4)
- Tunaenenda nuruni (1:7; 2:9-11).
- Yeye, Mwana wa Mungu, aliutoa uhai wake kwa ajili yetu (3:16).
- Damu ya Yesu Kristo inatusafisha dhambi yote (1:7).
- Yeye ndiye dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu (2:2; 4:10).
- Dhambi zetu zimesamehewa (2:12).
- Dhambi zetu zimeondolewa (3:5).
- msamaha wa kudumu (baada ya kuungama) na kutakaswa na udhalimu (1:9)
- Tunaye Mwombezi (Msaidizi) kwa Baba tunapokuwa tumetenda dhambi (2:1).
- Ndani yetu kweli upendo wa Mungu umekamilishwa (2:5; 4:12, 17).
- Upendo wa Baba tumepewa (3:1).
- Mungu anatupenda (4:16).
- Tuko *ndani yake* (2:5).
- Tuko ndani yake aliye wa kweli, ndani ya Mwana wake Yesu Kristo (5:20).
- Lililo kweli ndani yake ni kweli vilevile ndani yetu, yaani uzima wa Mungu (2:8).
- Tunadumu hata milele (2:17).
- Tunaye Roho Mtakatifu, mafuta kutoka kwake aliye Mtakatifu (2:20, 27).

- Ametupa Roho wake (3:24; 4:13).
- Tuko ndani ya Baba na ndani ya Mwana (2:24).
- ahadi yake kwetu: uzima wa milele (2:25)
- Mungu ametupa uzima wa milele; uzima huu umo katika Mwana wake (5:11, 13).
- Tunaye Mwana, na pamoja naye uzima (5:12).
- Uzima wa milele unadumu (yaani unakaa) ndani yetu (3:15).
- Tumezaliwa na Mungu (2:29; 3:9; 4:4, 6-7; 5:1, 3, 18-19; 3 Yohana 11).
- Sisi ni watoto wa Mungu (3:1).
- Mbegu ya Mungu iko ndani yetu (3:9).
- Tutaфанana na Mwana wa Mungu (3:2).
- Tutamwona Mwana wa Mungu kama alivyo (3:2).
- Tumepita kutoka mautini kuingia uzimani (3:14).
- Tuko ndani yake, naye yuko ndani yetu (3:24; 4:4).
- Tuna uzima kwa njia ya Mwana (4:9).
- Tuna ujasiri katika siku ya hukumu (4:17).
- Hofu imeondolewa kwetu kwa upendo kamili wa Mungu (4:18).
- Tunaomba kwa uhakika na sawasawa na mapenzi yake (5:14-15).
- Sisi ni wateule (2 Yohana 13).
- Kweli ya Mungu inakaa (kama Roho wa Mungu pia) ndani yetu na pamoja nasi hata milele (2 Yohana 2).

14.12 Agizo la wokovu katika maandiko ya Yohana

Mahali zilipo baraka na fursa, pana pia wajibu na majukumu. Ufahamu huu si mpya, lakini mkusanyiko huu unatugusa:

- kuzishika amri zake (2:3-4; 3:22; 5:2-3; 2 Yohana 5)
- kulishika neno lake (2:5)
- imetupasa kuenenda kama yeye alivyoenenda (2:6; taz. 4:17)
- kumpenda ndugu (2:10; 3:10, 14; 2 Yohana 5)
- kutoupenda ulimwengu (2:15)
- kuushinda ulimwengu kwa imani (5:4)
- kumkiri Mwana (2:23)
- kukaa ndani yake (2:28)
- kutenda haki (2:29)
- kujitakasa, kama yeye, Mwana wa Mungu, alivyo mtakatifu (3:3)

- kutotenda dhambi (3:6, 9; 5:18)
- kuutoa uhai wetu kwa ajili ya ndugu na kuwafungulia mioyo yetu (3:16-17)
- kupendana kwa tendo na kweli (3:18; 4:7; 4:11)
- kukaa katika pendo (4:16)
- kuyatenda yampendezayo Mungu (3:22)
- Tunapenda kwa sababu yeye alitupenda kwanza (4:19).
- kuenenda katika kweli (2 Yohana 4; 3 Yohana 4)
- kujiangalia ili tusipoteze yale tuliyoyatenda (2 Yohana 8)
- kukaa katika mafundisho ya Kristo (2 Yohana 9)
- kuishika kweli (3 Yohana 3)
- kuwapokea watumishi wa Mungu wakae (3 Yohana 5-8)
- kutenda mema na kuliiga lililo jema (3 Yohana 11).

14.13 Uzima wa milele – ubora na urefu

Uzima mpya una kipimo kinachofunika kila kitu kilichokuwepo hadi sasa, na kila kitu ambacho wanadamu walidhani kinawezekana. Uzima wa milele si tu kuwepo kusiko na mwisho. Hilo kila mtu analo, hata yule ambaye hajazaliwa mara ya pili. Bali kwa njia ya kuzaliwa mara ya pili tunapata kuwepo kunakotuwzesha siku moja kuwa mbinguni, na kwa hiyo kuwa pale ambapo uzima wa milele “uko nyumbani”. Lakini katika ujumbe wa Yohana inahusu wingi wa uzima huu wenye alama ya mbinguni, ambao tunaubeba ndani yetu si wakati huo tu, bali tayari sasa, tungali duniani. Wingi, utajiri na yaliyomo ya uzima huu sasa yanapatikana ndani yetu. Kwa hiyo si kuwepo tu kulikotokea, bali utu mpya pamoja na yote yanayomfanya mtu kuwa mtu: mapenzi, upendo, ufahamu na mengi zaidi. Kwa uzima huu tumepata kumjua Baba (Yohana 17:3). Tumeingia katika uhusiano ulio hai, wa karibu na wenye alama ya upendo, na katika ushirika na Baba na Mwana. Jambo hili lisingewezekana kamwe kama tusingekuwa na uzima uleule walio nao Baba na Mwana.

14.14 Dalili za uzima

Yule aliyeweza kuwepo wakati watoto wake walipozaliwa anajua ninachomaanisha. Wote wanangoja kwa hamu sauti za kwanza za mtoto. Mtoto anapolia, muujiza wa kuzaliwa umetimia. Katika maisha ya kiroho pia kuna dalili kama hizo za uzima. Muda mfupi baada ya kuzungumzia kuzaliwa mara ya pili (1 Petro 1:23), Petro anasema kwamba, kama watoto wachanga waliozaliwa sasa,

tunapaswa kuyatamani maziwa ya Neno la Mungu yasiyoghoshiwa (1 Petro 2:2). Kwa maneno mengine: Mtu aliyezaliwa mara ya pili ana njaa ya Neno la Mungu, au anavutiwa nalo. Hawezi tena kuishi bila Neno la Mungu, kwa sababu kwake ni kama chakula. Dalili nyingine za uzima, ambazo tumekwisha kuziorodhesha chini ya maagizo ya wokovu, ni hizi:

- Aliyezaliwa na Mungu anatenda haki (1 Yohana 2:29).
- Aliyezaliwa na Mungu anampenda Mungu na kumjua (1 Yohana 4:7).
- Aliyezaliwa na Mungu anaamini kwamba Yesu ndiye Kristo (1 Yohana 5:1).
- Aliyezaliwa na Mungu anawapenda ndugu katika imani (1 Yohana 5:1).
- Aliyezaliwa na Mungu anaushinda ulimwengu (1 Yohana 5:4).

Alama moja ya uzima mpya tutaichunguza kwa undani zaidi (1 Yohana 3:6, 9; 5:18):

“Kila akaaye ndani yake

batendi dhambi;

kila atendaye dhambi

bakumwona

wala bakumtambua.”

“Kila mtu aliyezaliwa na Mungu

batendi dhambi,

kwa sababu mbegu yake inakaa ndani yake;

wala hawezi kutenda dhambi,

kwa kuwa amezaliwa na Mungu.”

“Twajua

ya kwamba kila mtu

aliyezaliwa na Mungu

batendi dhambi.”

14.15 Aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi

Hii ni dalili ya uzima ambayo kwa mtazamo wa kwanza inatushtua, na huenda pia ikatuhuzunisha. Je, Yohana anataka kusema kwamba Mkristo hawezi kutenda dhambi tena kamwe? Kama angemaanisha hivyo, angekuwa amejipinga mwenyewe; kwa maana katika sura ya 2:1 anaandika:

“Watoto wangu wadogo, nawaandikia hayo

ili kwamba msitende dhambi.

*Na mtu akitenda dhambi –
tunaye Mwombezi kwa Baba,
Yesu Kristo, mwenye haki.”*

Hata kabla ya hapo anasema:

*“Tukisema kwamba hatuna dhambi,
twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu.
Tukiziungama dhambi zetu,
yeye ni mwaminifu na wa haki
hata atuondolee dhambi zetu,
na kutusafisha na udhalimu wote.”*
1 Yohana 1:8-9

Yohana anapoagiza tusitende dhambi, ni wazi kwamba bado kuna uwezekano kwamba mtu huyo anaweza kutenda dhambi, na kwamba hajawa asiye na dhambi. Kwa bahati mbaya uzoefu wetu wa kila siku pia ni ushahidi usiopingika kwamba ndivyo ilivyo. Lakini kiwango au kipimo cha Yohana ni wazi kwamba (hata kidogo) *hatupaswi* kutenda dhambi; hasemi, kama ambavyo huenda sisi tungenesema: “Jaribu kutenda dhambi kidogo iwezekanavyo!” Bali Yohana anakitoa kiwango cha maisha yetu kutoka katika kile ambacho Yesu mwenyewe alisema kuhusu Mungu, kwamba “Mungu ni nuru (mtakatifu kabisa na mwenye haki kabisa), wala ndani yake hamna giza (dhambi) hata kidogo” (1 Yohana 1:5). Anaposema mwanzoni: “Mtu akitenda dhambi ...”, inakuwa wazi kwamba hapa hazungumzii kawaida, bali jambo lisilo la kawaida. Hatuhitaji kufanya mazoezi magumu ili kuyapatanisha maneno haya na yale yanayosema kwamba aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, au (kwa kusema wazi zaidi) *hawezi* kutenda dhambi. Maneno haya yanayoonekana kupingana kiasi hicho lazima yapatane.

Hapa Yohana anatuona kama wale waliopewa nguvu na asili ya uzima mpya. Machoni pake hapa sisi ni wale walio na uzima huu, uliotoka kwa mbegu ya Mungu ya Neno. Na jambo hilo kwa lazima lina matokeo haya: Mkristo hatendi dhambi kwa kudumu (hii ndiyo ingekuwa maana ya muundo wa kisarufi wa kuendelea) wala kwa mazoea. Kwa kusema kama Paulo, amewekwa huru mbali na nguvu ya dhambi. “Ingawa muumini wakati mwingine anatenda dhambi, hata hivyo kanuni inayotawala maisha yake si dhambi, bali kinyume cha dhambi. Sisi ni watoto wa Mungu, na dhambi kwetu ni jambo lisilo la kawaida na lisilo la

asili.”⁹⁴ Mkristo anampenda Mungu na amri zake. Ni sehemu ya asili yake kwamba anaichukia dhambi. Anaishi na kuenenda kwa Roho, ili asizitimize tamaa za tabia ya mwili (Wagalatia 5:16, 25).

Wengine wanaeleza jambo hili hivi: Yohana anamaanisha uzima mpya peke yake (uzima wa Kristo ndani yake), ambao hauwezi kutenda dhambi. Maelezo haya ni sahihi kwa kiasi fulani tu. Bila shaka uzima huu hauwezi kutenda dhambi. Lakini hapa haihusu utendaji wa uzima mpya, bali mwenendo wa yule *mtu* aliyezaliwa na Mungu. Uzima mpya wenyewe *hautendi* chochote. Bali *mtu* husika *anatenda* kitu kwa kupatana na uzima wake, na asili yake. *Mtu anatenda* kitu kwa uwajibikaji kamili na kwa uamuzi wake mwenyewe, huku uzima wake, au asili yake, ikiamua chanzo cha tendo – yaani chemchemi ambayo *mtu* huyo anachota kutoka kwayo. Mbegu ndiyo ambayo kwa njia yake *mtu* husika amezaliwa upya, na mbegu hii wakati huohuo ni uzima mpya. Sasa Yohana anamwona *mtu* aliyezaliwa mara ya pili kama yule anayeishi uzima huu, au anayeamuliwa na kutambulishwa na uzima huu. Katika uzima huu dhambi haifai; ni kitu kigeni. “Waraka wa Yohana una tofauti kali. Zaidi ya hayo una kauli nyingi za kidhahania. Ndivyo ilivyo kwa dhambi na haki. Daima kinaonyeshwa kile kinachoitambulisha hali ya jambo fulani. Kwa hiyo muumini kwa asili yake ni mwenye haki: Anatenda haki wala hatendi dhambi. Lakini hilo linamaanisha kwamba tabia ya maisha yake ni njema: Anaishi kwa haki, na kwa hiyo haishi maisha ya dhambi. Kwa asiyeamini kinyume chake ndicho kilicho kweli.”⁹⁵

Yohana hazungumzii hali bora jinsi ambavyo *ingeweza* kuwa, bali jinsi *ilivyo*. Wakati mwingine *mtu* anaweza kupata hisia kwamba anaipita tu tofauti kati ya *nafasi* na *hali* ya kivitendo (msaada wa kuelewa ambao tumeutumia hasa katika mafundisho ya Paulo kuhusu wokovu). Kwa hiyo kauli hii si kweli tu “kinadharia”, kwa mujibu wa nafasi yetu au kwa uhalisi usiotegemea hisia, bali inaeleza kweli kile tulicho pia kwa vitendo katika maisha yetu ya kila siku (agizo la wokovu, kwa Kijerumani *Heilsimperativ*: yale tunayoagizwa kutenda). Inapita kile ambacho tumekuwa kwa neema katika nafasi yetu (ukweli wa wokovu, *Heilsindikativ*: yale ambayo Mungu ameshatenda).

94. Alfred Plummer, katika John R. W. Stott, *The Letters of John*, uk. 138.

95. Ibid., uk. 137.

14.15.1 Hatua nne za historia ya wokovu: mwanadamu na dhambi

Augustine wa Hippo (354 – 430), katika mabishano yake na Pelagius⁹⁶, alifanya mpangilio ufuatao kwa kutumia maneno matatu ya Kilatini: *posse* (kwa maana ya “kuweza, kumudu, kuwa na uwezo”), *peccare* (kwa maana ya “kutenda dhambi, kukosa, kukosea”) na *non* (kwa maana ya “si”).

14.15.2 Kutotenda dhambi tena: inawezekana au haiwezekani?

Ni wazi: Yohana anaujua ukweli kwamba muumini “anaweza kutenda dhambi”. Haukatai. Kutenda dhambi si kawaida katika maisha ya Mkristo. Kilicho cha kawaida ni kwamba Mkristo hatendi dhambi, kwa sababu uweza wa Mungu umempa kila kitu kinachohusu maisha ya kumcha Mungu, kwa njia ya kumjua Mungu (2 Petro 1:3). “Mkristo wa kweli si mtu aliyepoteza uwezo wa kutenda dhambi, bali aliyepoteza nia na utayari wa kufanya hivyo.”⁹⁷

Yohana hakuzungumza kwamba kunaweza kuwepo hali ya kutokuwa na dhambi na ukamilifu usio na kasoro (vinginevyo angejipinga mwenyewe waziwazi). Kutokuwa na dhambi kwenyewe hakuwezekani, kwa sababu tu dhambi inakaa ndani yetu na imefungamana bila kutenganishwa na mwili wetu na maisha yetu ya duniani. Kutotenda dhambi tena ni jambo la kutamaniwa leo (taz. maneno ya Yohana: “... ili kwamba msitende dhambi”), lakini

96. Mtawa wa Uingereza ambaye, akiwa mtu wa wakati mmoja na Augustine, aliyakataa mafundisho yake kuhusu neema na wokovu, na badala yake akasisitiza uhuru wa mapenzi ya mwanadamu.

97. William MacDonald, *Der vergessene Befehl – Seid heilig*, uk. 45.

linawezekana tu katika utukufu, tutakapofanana naye kabisa, yeye aliye Bwana wetu.

1. Mwanadamu kabla ya anguko	2. Mwanadamu aliyeanguka	3. Mwanadamu aliyezaliwa mara ya pili	4. Mwanadamu katika ukamilisho
Posse peccare	Non posse Non peccare	Posse non peccare	Non posse peccare
Aliweza kutenda dhambi (lakini pia kuipeuka).	Hawezi kutotenda dhambi; hana uwezo wa kutotenda dhambi.	Anaweza kutotenda dhambi (lakini pia kutenda dhambi).	Hawezi kutenda dhambi tena.
Kwa sababu ya hiari yake, mwanadamu aliweza kuamua kuiheshimu amri ya Mungu au kuivunja.	Yuko katika tabia ya mwili, amezwa chini ya dhambi. Si kila tendo la mwanadamu aliyeanguka ni dhambi, lakini hawezi kuishi bila dhambi.	Kwa upande wa kiroho, uzima mpya na uzima wa zamani viko ndani yake. Kulazimishwa kutenda dhambi kumevunjwa. Amewezeshwa kutotenda dhambi, lakini bado anaweza kutenda dhambi.	Dhambi na tabia ya mwili, yaani asili ya zamani, ndani ya Mkristo vilikuwa vimefungwa na maisha yake ya kimwili ya duniani ya uumbaji wa zamani, ambayo katika ukamilisho yamekoma na nafasi yake inachukuliwa na mwili wa utukufu, na kuwa karibu na Kristo daima.

Je, sasa tunapaswa kuvunjika moyo kwa sababu ya uzoefu wetu – tukijua kwamba hatuwezi kamwe kulifikia lengo hili? Au je, kuna sababu katika Maandiko inayotuthibitishia kwamba *hatutaweza* kuwa bila dhambi? Kauli kama hiyo ingetushangaza sana. Mtu angewezaje kumtia Mkristo moyo asitende dhambi kwa upande mmoja, na wakati huohuo kumwonyesha wazi kwamba jambo hilo halitafanikiwa kamwe? Hilo haliendani, na lingekuwa jambo lisilo la busara kabisa kwa upande wa malezi. Kiwango cha maisha yetu daima ni ukamilifu wa Mungu, kamwe si chini ya hapo.

Lakini mtu akidhani kwa dhati kabisa kwamba amefikia hali ya ukamilifu (maisha bila dhambi), huenda amepoteza kuiona na kuihisi asili ya dhambi na uhalisi wenyewe. Dhamiri yake haina tena usikivu kwa jambo hilo. Hata katika mambo mengi mema tunayoyatenda, mara nyingi bado kivuli cha dhambi kinaonekana. Anayedai kwamba hatendi dhambi tena anapaswa kuleta ushahidi na “mashahidi” wa kutokuwa kwake na dhambi: mume wake au mke wake, watoto wake na watu wengine wa karibu yake. Ninamjua mmoja tu ambaye hili

linamhusu: Yesu. Mahali hapa ninaongeza sentensi inayotumika mara nyingi, iliyo kweli kwa kila namna: “Wakristo wanaweza kukatisha tamaa, Kristo hakatishi tamaa kamwe.” Haipaswi kutumika kama udhuru, bali kama kutia moyo.

14.16 Ukamilifu – ni nini?

Agano Jipya mara nyingi linazungumzia ukamilifu, hata linapohusu maisha yetu ya imani. Kwa hilo haimaanishwi ukamilifu usio na kasoro wala kutokuwa na dhambi. Kwa uelewa wetu wa utakaso ni muhimu kuuelewa ukamilifu huu ipasavyo. Tunaweza kutofautisha angalau maana tatu za neno hili katika mistari ya Maandiko ambamo linatokea:

14.16.1 Ukamilifu wa nafasi yetu ya wokovu

“Kwa maana kwa toleo *moja* amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa” (Waebrania 10:14). Kwa dhabihu ya Yesu iliyo kamili na inayotosha kwa yote tumewekwa huru mbali na dhambi zetu milele. Huu ni wokovu usiobadilika, usio na kasoro, na ulio kamili kwa mtazamo wa Mungu. Tumeoshwa, tumetakaswa, tumehesabiwa haki (1 Wakorintho 6:11). Katika uumbaji mpya wa Mungu (2 Wakorintho 5:17) sisi ni wakamilifu (1 Wakorintho 2:6; Wafilipi 3:15). Katika Kristo tumeletwa kwenye utimilifu, au tumekamilishwa (Wakolosai 2:10).

Ukamilifu huu unajumuisha karama ya neema na kazi ya Mungu ya wokovu. “Ukamilifu huu tuliopewa haupaswi kuchanganywa na kutokuwa na dhambi kabisa wala na ukamilifu wa kimaadili; lakini hakuna ukuaji kuelekea ukamilifu wa kimaadili na ukomavu, ikiwa ukamilifu wa msingi haupo.”⁹⁸

14.16.2 Ukamilifu (ukomavu) katika maisha yetu: kukua kuwa watu wazima

Wakati maana ya kwanza kweli inamaanisha ukamilifu usio na doa na usiobadilika, Agano Jipya linalitumia neno hili pia kwa jambo lililotokea na lililo katika ukuaji, au katika maendeleo. Lina ukamilifu (kwa Kiyunani: ukomavu) kuwa lengo lake, yaani ukomavu wa kuwa mtu mzima kiroho. Maana hii ya neno *kamili* inapatikana katika 1 Wakorintho 14:20. Hapo inasemwa kwamba

98. Erich Mauerhofer, *Der Kampf zwischen Fleisch und Geist bei Paulus*, uk. 124.

Wakorintho katika mikutano yao, kwa habari ya akili zao, hawapaswi kuwa watoto, bali wakamilifu, yaani watu wazima, waliokomaa. Kanisa lote linapaswa kufikia umoja wa imani na wa kumjua Mwana wa Mungu, hata kufikia kuwa mtu mzima (mkamilifu au aliyekomaa), hata kufikia kimo cha cheo cha utimilifu wa Kristo (taz. Waefeso 4:13). Kwa hiyo chakula *keigumu* cha mafundisho ya Biblia kimekusudiwa kwa watu wazima (wakamilifu, waliokomaa), ambao kwa sababu ya kuzoea wamezoezwa akili zao – kupambanua mema na mabaya pia (taz. Waebrania 5:14).

Yesu anapotuagiza tuwe wakamilifu, kama Baba yetu wa mbinguni alivyo mkamilifu (Mathayo 5:48), jambo hili linaonyesha mambo mawili: Kwa upande mmoja linaonyesha ukamilifu wa Mungu, na kwa upande mwingine mchakato katika maisha yetu wa kuwa kama Baba yetu, kwa sababu sisi ni wafuasi wa mfano wake.

14.16.3 Ukamilifu wa mtu kwa ujumla wake katika ukamilisho ujao

Imani yetu ina lengo moja: kuwa kwake na pamoja na Kristo na kufanana naye kabisa. Ni nini kingine kinachoweza kuitwa kamilifu au kilichokamilishwa, tutakapofanana naye? Kuwa kitu kimoja kabisa na Kristo, hata katika ufufuo wake, ndiko alikokufuatia Paulo, lakini alikuwa bado hajakufikia: “Si kwamba nimekwisha kufikilia (ufufuo wa wafu, na kwa hiyo ukombozi wa mwili pia), au kwamba nimekwisha kuwa mkamilifu (kufikia ukamilifu, yaani kufikishwa kwenye lengo)” (Wafilipi 3:12). Siku ya kubadilishwa kwetu au ya kufufuliwa kwetu itatufanya wakamilifu (itatufikisha kwenye lengo, itatukamilisha) katika roho, nafsi na mwili (taz. Wakolosai 1:28).

14.17 Wajibu kwa ajili ya matendo yetu, si kwa ajili ya hali yetu ya kuwa

Wakati mwingine tunasema juu ya mtu: “Ametenda kwa kufuata asili yake.” Kwa hilo tunamaanisha kwamba yeye mwenyewe hakuamua kama atatenda na atatenda nini, kwa sababu alisukumwa na asili yake. Siku ya hukumu watu hawatahukumiwa kwa kile walichokuwa kwa asili, bali kwa kile walichokitenda kwa uwajibikaji wao wenyewe na kwa makusudi kabisa (Warumi 2). Hili linamhusu pia muumini. Anapotenda dhambi, hawezi kujitetea kwa kusema kwamba ilikuwa asili yake ya zamani, “mimi” wake wa zamani au tabia ya mwili.

Daima tutalazimika kuamua kama tunataka kuenenda kwa Roho au kwa tabia ya mwili. Kuishi kwa Roho wa Mungu kunaweza na kunapaswa kuwa mazoea ya kawaida kwetu. Hiyo ndiyo nia ya Mungu na lengo lake kwetu. Si lazima iwe vita vya kudumu, vya kujikaza na vinavyochosha, kuamua daima kwa ajili ya lililo jema. Tunapaswa kuukubali kwa imani ukweli kwamba sisi ni watu wapya – wenye moyo mpya, wenye uzima mpya na wenye roho iliyofanywa upya. Tukiufahamu uwepo huu mpya tunaweza pia kuishi kwa kufuata hivyo. Kipepeo zamani alikuwa kiwavi, mpaka kwa muujiza wa metamofosisi akapata badiliko kamili. Ingawa ni mdudu yuleyule, hakuna mfanano wowote kati ya maumbo haya mawili ya kuwepo. Kipepeo anaruka kutoka ua moja hadi ua jingine. Kama asingekuwa “kile alichofanyika kuwa” na bado akajiona kama kiwavi, hilo lingeshangaza sana. Kipepeo anayefikiri kwamba yeye ni kiwavi! Ni ulinganisho wa kuchekesha, lakini wakati huohuo wa kuzingatiwa kwa uzito, kwa sababu Wakristo wengi katika maisha yao wanatoa picha hiyohiyo. Tusienende kama kiwavi anayejishibisha kupita kiasi kwa mambo ya “duniani”, bali kama vipepeo wanaoruka na kuishi kwa “baraka za mbinguni”! Tunaweza na tunapaswa kuishi utambulisho wetu mpya: Ninaishi, lakini si mimi tena! Kristo anaishi ndani yangu (taz. Wagalatia 2:20).

14.18 Asili mpya na asili ya zamani ziko ndani yetu wakati mmoja

Ni siri kwetu, na itabaki kuwa siri, kwamba asili ya zamani na asili mpya ziko ndani yetu wakati mmoja, na kwamba (kwa lugha ya Biblia) Kristo na dhambi wanakaa ndani yetu wakati huohuo. Hata hivyo Maandiko yanafundisha jambo hili, na uzoefu wetu pia unalithibitisha. Kusudi la Mungu linaweza kuwa nini, kwa kuuacha uovu ndani yetu hadi siku ya ukombozi? Uovu haupaswi kutendwa, lakini tunapaswa kuutambua, ili katika muda huu mfupi tuelewe zaidi na zaidi uovu ulivyo hasa, na maana yake kwa Kristo kufanywa kuwa dhambi.

Baada ya kujifunza maneno ya Maandiko yanayohusika, fundisho linalosema kwamba Mkristo ana asili moja tu (yaani ile mpya peke yake) lazima likataliwe waziwazi. Kama tulivyo wakamilifu katika Kristo, ndivyo ilivyo potovu tabia ya mwili ambayo bado tunayo. Imefungamana na kuwepo kwetu katika mwili bila kuweza kutenganishwa (ndiyo sababu inaitwa “*Fleisch*” – kwa Kiyunani *sarx*, yaani mwili au nyama. Neno hilohilo linatumika kwa kuwepo kwetu duniani katika mwili, na pia kwa hali ya zamani ya dhambi, yaani asili ya zamani, inayoishi katika mwili huo, katika nyama hiyo). Ni kwa kifo cha mwili tu, au kwa

kubadilishwa kwa waumini wote wakati wa unyakuo, ndipo mwisho kamili wa tabia ya mwili yenye dhambi unamfikia kila Mkristo.

14.19 Hitimisho

Kuzaliwa *upya* na *kutoka juu* ni tukio kubwa mno, kwa sababu hekima yote, ufundi wote na nguvu zote za mwanadamu haviwezi kulileta jambo hili, wala haviwezi kuleta badiliko linaloonekana baadaye.

Mbingu zinachangamka kwa furaha mwenye dhambi anapotubu – kama ilivyo kwa mama na baba, mtoto anapozaliwa na “wanaposikia” dalili za kwanza za uhai. Mtoto mchanga anahitaji utunzaji na uangalizi mwingi hadi aweze kujitegemea. Ndivyo ilivyo pia kwa namna inayofanana katika maisha ya kiroho. Uumbaji mara nyingi ni picha ya mambo halisi ya kiroho, nayo hutusaidia kuzielewa vizuri zaidi kweli za kiroho. Watoto wanakuwa vijana, na siku moja vijana hao wanakua kuwa akina baba katika Kristo (1 Yohana 2:13-14).

Tunapozungumza leo juu ya “asili mpya”, kwa kweli tunamaanisha “uzima mpya, yaani uzima wa milele uliotolewa na Mungu”, ambao wakati huohuo Bwana Yesu mwenyewe anauonyesha katika nafsi yake. Uzima huu kwa lazima una namna fulani, uhalisi fulani, yaani asili maalumu. Hiyo inamaanisha kwamba uzima huu hauelezi tu kuwepo (yaani hali ya kuwa), bali pia unashuhudia ni mkono wa nani unaoutambulisha, na jinsi unavyojionyesha katika mambo ya kimaadili. Tena nakumbusha: Usemi “asili ya Mungu” (tabia ya uungu) unatajwa mara moja tu katika Agano Jipya. Hapo unaonyesha jinsi asili ya Mungu na sifa zake zinavyojifunua ndani yetu na kuonekana katika maisha yetu.

Tulianza na Paulo, na sasa, pamoja na Yohana, Petro na Yakobo, tumepanda milima yote. Tumepata mandhari nyingi za kuvutia na kuona mambo mengi kwa ndani, yaliyotonyesha ukuu wa Mungu katika asili yake na katika wokovu wake. Kumjua Mungu – asili yake na matendo yake – kunataka kuijaza mioyo yetu.

Maisha ya waliozaliwa mara ya pili si kuwepo tu, si hali ya kuwa tu na kungoja mbingu, bali zaidi ya yote ni maisha yatokayo katika wingi. Mungu anapenda kutoa, tena kwa ukarimu, na hatupaswi kulitambua hilo tu tutakapokuwa mbinguni.

15. Hulka na tabia

Ukristo wa kweli unaanza na kufanywa upya kabisa. Juu ya msingi huo linafuata badiliko la kudumu, tukifanana zaidi na zaidi na Kristo. Je, hulka yangu ina mvuto gani juu ya maisha yangu ya imani na ya kushinda?

Wikipedia, kamusi elezo huru kwenye intaneti, inatoa maelezo haya mafupi: “Hulka inaeleza namna kiumbe hai kinavyotenda na kujibu, yaani mtindo wake wa tabia. Mtindo huu umezama kwa kina, nao unaundwa na majibu ya kihisia, ya kimwendo na ya umakini, pamoja na uwezo wa kujidhibiti. Neno hili linaeleza sifa za mwenendo zinazodumu kiasi, na kwa hiyo za kawaida kwa mtu, kama uvumilivu, kiwango cha kuchochewa, hali ya moyo, na kasi.”⁹⁹

“Nadharia ya hulka, iliyo na umri wa karibu miaka 2,500, inawapanga watu kwa kufuata asili yao ya msingi, na kwa mtazamo wa kisayansi leo ni nadharia iliyopitwa na wakati ... Chanzo chake ni nadharia ya maji ya mwili (nadharia ya maji manne), inayohusishwa na Hippokrates wa Kos (tabibu Mgiriki, 460 – 375 KK) ... Galenus wa Pergamo ndiye aliyeiunganisha nadharia ya maji manne na nadharia ya hulka nne; aliyapa maji manne ya mwili (‘humores’) kila moja hulka yake. Kwa kadiri moja ya maji hayo manne linavyotawala, ndivyo hulka inayohusiana nalo inavyojitokeza hasa ... :

- Damu (‘Sanguis’): Sanguini (mchangamfu, mtendaji)
- Kamasi (‘Phlegma’): Flegmatiki (mtulivu, mzito)
- Nyongo nyeusi (‘Melas Cholé’): Melankoli (mwenye huzuni, mtafakari)
- Nyongo ya manjano (‘Cholé’): Koleriki (mwepesi wa kukasirika na wa kusisimka).¹⁰⁰

15.1 Biblia na nadharia ya hulka

Kwanza ni lazima tuseme kwamba nadharia ya hulka ina asili ya kipagani. Pili, ni ukweli kwamba kisayansi imepitwa na wakati. Mambo haya mawili yanahusiana na ukweli kwamba nadharia hii haipatikani katika Biblia, wala haiwezi kutolewa kutoka humo. Biblia inainyamazia tu nadharia hii, ingawa ilikuwepo tayari wakati sehemu yake ya pili (Agano Jipya) ilipoandikwa.

99. Inapatikana mtandaoni: <http://de.wikipedia.org/wiki/Temperament>.

100. Inapatikana mtandaoni: <http://de.wikipedia.org/wiki/Temperamentenlehre>.

Hata hivyo hatutaki kumtupa mtoto pamoja na maji ya kuogea. Hulka ni jambo halisi, na kwa hiyo kuitazama hulka (yetu wenyewe) kunaweza kuwa na faida. Hata kama nadharia hii imepitwa na wakati, kila mwanadamu ana hulka, ambayo mara nyingi inalingana kwa kiasi fulani na mojawapo ya zile nne zilizotajwa, au na mchanganyiko wake.

Hata baada ya kuzaliwa kwangu mara ya pili, mimi ninabaki mtu yuleyule niliyekuwa hapo awali. Lakini nimepewa uzima mpya wa kiroho, ulio na asili na uhalisi wa Kristo. Uzima huu unapaswa kuitengeneza haiba yangu. Hata zile zinazoitwa pande zenye nguvu za hulka yangu hazina thamani bila Kristo. Ni haiba zilizojazwa na yeye tu zinazolingana na kipimo cha Mungu kwa ajili ya uzima mpya: Kristo ndiye kanuni na kipimo cha kiumbe kipya tulichofanyika. Tena, asili ya Kristo inaonekana katika tunda la Roho. Hicho ndicho kipimo chetu cha kujenga haiba yetu. Kuchunguza hulka kuna haki yake, ilimradi kunabaki chini ya lengo halisi la kuwa kwetu Wakristo.

Ni vizuri kuzitazama nguvu na udhaifu wa hulka mbalimbali. Tunashughulika nazo kila siku; ni sehemu ya maisha yetu, na kwa hiyo pia ya maisha yetu ya imani. Tunajua kwamba hatuwezi kubadilisha tu muundo wetu (yaani kile tulichorithi kutoka kwa wazazi wetu). Ni muhimu sana kutambua jinsi tulivyoungwa, kwa maana kwa njia hiyo yanafunuliwa pia mambo mabaya na mienendo inayoweza kuzuia na kukwamisha ukuaji wetu wa kufanana na Kristo. Mwenendo wa uvivu wa Flegmatiki mara nyingi ni kizuizi kwa maisha ya imani yenye bidii. Vivyo hivyo kutenda na kuhukumu kwa haraka kwa Koleriki. Tunapaswa kuzitambua pande hizo mbaya ili tuweze kuchukua hatua dhidi yake. Kwa ajili hiyo kipimo (test) kinaweza kusaidia kweli.

Kujishughulisha kupita kiasi na hulka, kwa kuangalia maisha yetu ya kiroho na vipawa vyetu, kunaelekeza uangalifu sana kwetu wenyewe. Kuna maagizo kadhaa ya kujichunguza sisi wenyewe na kazi yetu, lakini kanuni karibu siku zote ni kwamba tumtazame Kristo. Jambo hilo ndilo linaloleta badiliko, ambalo bila shaka sisi pia tunashiriki ndani yake.

W. J. Ouwenel: “Wao (Ole Hallesby, Tim LaHaye na Henry Brandt) wameonyesha jinsi maisha yanavyokuwa kwa hulka nne, moyo unapomwacha Mungu na kujitoa kwa dhambi; hapo pande mbaya za hulka hushinda. Lakini moyo unapomwelekea Mungu na kujikabidhi kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, pande zenye nguvu zinaweza kukuzwa katika haiba. Na Kristo anapata sura ndani ya mtu: kwa Sanguini katika uchangamfu wa moyo, unyoofu, uhai, upole

na matumaini; kwa Koleriki katika uongozi, uthabiti, roho ya ushirikiano, azimio na ari ya kuanzisha mambo; kwa Melankoli katika urafiki wa uaminifu, ubunifu na utayari wa kujitoa; na kwa Flegmatiki katika utulivu, uchangamfu wa kudumu, utayari wa kusikiliza, utaratibu na busara ...

Licha ya tafiti zote za miundo ya kibaioolojia na ya kisaikolojia, na ... hulka na aina za haiba, mwanadamu si roboti aliyepangwa tayari, aliyeachwa kabisa chini ya pande mbaya za tabia yake. Hapa pia Biblia, na vilevile uzoefu wa huduma ya kichungaji, vinatufundisha kwamba kila kitu kinategemea mwelekeo wa moyo. Kwa kweli hulka ya mwanadamu imewekwa na maumbile aliyoyarithi; kwa hiyo karibu haibadiliki (ingawa mabadiliko madogo yanaweza kutokea katika maisha, lakini mwanadamu hana uwezo juu ya hayo). Lakini ni lazima kutofautisha vizuri **hulka** na **tabia**. Tabia ni matokeo ya sifa za mwenendo wa mwanadamu, ambazo hazitokani na hulka peke yake, bali ... zaidi ya yote zinaamuliwa na moyo.

Mwanadamu anapomwamini Kristo, na hivyo kuzaliwa mara ya pili, hapati hulka mpya (kama vile hapati mwili mwingine), lakini anapata ‘moyo mpya’: nia mpya kabisa ya moyo, mwelekeo mpya kabisa, mtazamo mpya, mpango mpya wa maisha. Sasa mambo mengine kabisa yanayoongoza matendo na nia yanaanza kuwa na nafasi katika maisha yake, pamoja na ufahamu mpya na fikira mpya (yaani ‘utambuzi’ mpya) na mapenzi yaliyoelekezwa upya (kipengele cha ‘konativ’¹⁰¹). Hivyo mtu aliyefanywa upya anaweza, ndani ya mipaka (mipana!) ya maumbile ya hulka yake, kukuza tabia mpya kabisa, ambayo ndani yake, kama tulivyosema, Kristo anapata sura kwa namna ya pekee kabisa.”¹⁰²

Hulka – yaani maumbile aliyoyarithi mtu na mwelekeo wake wa asili – inatakaswa kwa muumini, na hivyo inakuwa ya kufaa kwa Mungu. Kwa mfano, upole wa Sanguini unamfaa Mungu. Kwa kukaa ndani yake na kwa uongozi wa Roho, unakuwa hata tunda kwa ajili ya Mungu. Ndivyo ilivyo kwa pande zote “nzuri” za kila hulka. Upande wa ubinadamu unaotokana na maumbile na hulka ni sehemu ya uumbaji wa kwanza wa Mungu, na kwa hiyo ulikuwa tayari sifa ya Adamu kabla ya anguko. Kwa bahati mbaya dhambi imeiletea pia hulka kasoro, nasi tunapaswa kuziondoa kwa uthabiti.

101. “Konativ” (Kijerumani) lina maana ya “-enye msukumo wa ndani”, “-enye kujitahidi kufikia lengo”.

102. W. J. Ouwencel, *Psychologie, Ein bibelorientiert-wissenschaftlicher Entwurf*, uk. 168 (mkazo umeongezwa).

15.2 Tabia na kubadilika kwake

Tabia ni sifa ya mtu inayoweza kutambulika. Tunalijua neno hili, kwa kiasi kikubwa au kidogo. Mara nyingi linahusishwa na sifa nzuri za kibinadamu zinazostahili kutafutwa, yaani zile zinazokosekana katika jamii, na katika miaka ya karibuni hasa katika ulimwengu wa fedha. Tamaa isiyozuliwa, kujipenda na ubinafsi vinatupa ladha ya kile kitakachokuja bado. Jamii inahisi kwamba tabia njema na thabiti, inayoweza pia kupinga jaribu, ingeweza kupunguza mwendo wa kuporomoka kwa maadili, kama si kuuzuia kabisa.

Lakini hebu tuyatazame maisha yetu wenyewe. Neno la Kijerumani *Charakter* (tabia) linatokana na muhuri wa kugonga ulioitoa umbo kwa sarafu au kwa muhuri. Ni nini kinachotutengeneza, na watu wanaona nini ndani yetu? Swali lililo muhimu zaidi ni hili: Sisi ni nani, na tukoje kwa tabia yetu, mtu asipotuona? Methali moja inasema: “Uso wa mtu unauona mwangani, tabia yake gizani.”

Kile ambacho ulimwengu unakihitaji kimekuwa kweli ndani ya Yesu. Asili yake inaweza kuwa kweli ndani yetu. Tabia njema imetengenezwa na tunda la Roho Mtakatifu, na kwa hiyo na Yesu. Lakini haiji tu ikiruka yenyewe. Wala Mungu haiweki ghafla ndani ya moyo wetu kama kwa kiinimacho, akiyapita mapenzi yetu. Anatupa kila kitu ili tuikuze chini ya uongozi wake, kwa nguvu zake na kwa neema yake. Tunapaswa kuifanyia mazoezi tabia, na hivyo kuitia nguvu. Huo ndio wajibu wetu. Tunda la kiroho la upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi tunapaswa kulijifunza kama lugha mpya au lugha ya pili, hadi tuweze kuisema kwa mazoea kutokana na kujifunza na kufanya mazoezi. Tabia ya kiroho inapaswa kuwa jambo la kawaida katika maisha yetu.

Tabia inaonekana pale jambo linapokuwa muhimu, na tunapokuwa chini ya shinikizo au katika jaribu. Ndiyo sababu Paulo anasema pia kwamba tusiiangalie tabia ya mwili, bali tumvae Bwana Yesu Kristo (Warumi 13:14). Tabia iliyoimarishwa (yaani iliyofanyiwa mazoezi na kutafutwa kwa uvumilivu) inaweza kulipinga jaribu la kuziacha, katika hali ngumu kupita kiasi, kanuni za kiroho ambazo imejifunza tangu kuzaliwa mara ya pili na inazothamini kama njia ya Mungu.

Tunaifanyiaje tabia mazoezi? Kwa kujifunza na kutekeleza. Ni lazima tujifunze ili tuelewe jinsi “tabia hii ya kiroho” ilivyo. Kwa namna fulani

nimeagizwa kuifanya kuwa sehemu ya ndani yangu. Kwa hatua ndogondogo tunazitumia sifa hizi zaidi na zaidi, kwa sababu tunataka.

Wakati hulka inabaki karibu bila kubadilika maisha yote, tabia inapata mabadiliko, kuwa bora au kuwa mbaya zaidi. Msingi wa tabia ni mapenzi na nguvu yake ya kuweza kushinda. Tunao moyo mpya na mapenzi yaliyofanywa upya. Huo ndio mwanzo wa maisha mapya, ambayo hadi mwisho yanapaswa kuambatana na nia ya kubadilika.

Kama ilivyo kwa nadharia ya hulka, neno *tabia* (Charakter) halipatikani katika Biblia. Kinachokaribiana nalo zaidi ni neno la Biblia “wema” (kwa Kiyunani *aretē*) (Wafilipi 4:8; 1 Petro 2:9 [sifa ya Mungu]; 2 Petro 1:3, 5). Biblia haifuati mafundisho ya wanafalsafa wa wakati wake kuhusu wema. Mambo yanayofanana yako kwa sehemu katika kile ambacho wema unajulikana kwacho, na kwa sehemu katika ukweli kwamba unazoezwa na kufanyiwa mazoezi. Kwa mtazamo wa Biblia, wema – au tabia – na kubadilika kwake hadi kufanana na Kristo kunalenga Mungu mwenyewe na ufalme wake. Si juhudi zetu wenyewe kwa ajili yetu wenyewe, bali nguvu ya mapenzi iliyofanywa upya na Roho Mtakatifu, na matendo yanayotokana nayo kwa utukufu wa Mungu na kwa faida ya wengine – hilo ndilo linalolingana na picha ya Biblia na lengo la kubadilishwa kwetu, ambako kutaishia katika lengo la mwisho, ulimwengu mpya wa Mungu.

“Yaangalie mawazo yako, kwa maana yanakuwa maneno.

Yaangalie maneno yako, kwa maana yanakuwa matendo.

Yaangalie matendo yako, kwa maana yanakuwa mazoea.

Yaangalie mazoea yako, kwa maana yanakuwa tabia yako.

Iangalie tabia yako, kwa maana inakuwa hatima yako.”

16. Neno la mwisho

Kuna nyakati ambapo mambo yanatulemea, na hatujui tena tufanye nini na tuache nini. Wakati mwingine tabia ya mwili inaibuka, hata tunashangaa na kujiogopa wenyewe. Wakati mwingine tunashtushwa vilevile na kutojali kwetu. Haya yote yatatukuta na kutuandama, maadamu tuko katika maisha yetu ya duniani, njiani kuelekea ukamilisho. Kusema hivi hakukusudii kuhalalisha chochote. Lakini tunataka pia kubaki waaminifu tunapozungumza juu ya kiasi gani cha kweli ya kiroho kinachokua katika maisha yetu.

Tujipe moyo, bila kukata tamaa! Hata kama ndani yetu tunajisikia kukata tamaa, hilo ndilo suluhisho baya kuliko yote. Kukata tamaa na kusalimu amri kuna asili yake katika tabia ya mwili na kwa Ibilisi!

Baba anatusaidia katika kila hatua – iwe ndogo au kubwa. Tunapaswa kusonga mbele katika njia kuelekea lengo. Hata tunapopitia nyakati ambapo tunajitenga naye, yeye yu karibu nasi, na daima inatosha hatua moja kurudi mikononi mwake.

Huenda safari za milimani zilichukua muda mwingi na zilikuwa ngumu kiasi kwamba sasa hamwezi tena kuuona msitu kwa sababu ya miti mingi. Ni kweli, mkiyakusanya maandiko yote ya Biblia juu ya somo hili, ni jambo pana. Lakini tunaona ukuaji katika ufahamu wa kiroho unaoletwa na Mungu. Na jambo hilo linahitaji muda tu. Hatuwezi kulilazimisha wala kulifupisha. Mungu anatembea njia yake pamoja nasi. Yeye yuko upande wetu, nasi tuko chini ya ulinzi wake. Hasimami nyuma yetu kama msimamizi wa watumwa anayejali makosa yetu na kushindwa kwetu tu. Kinyume chake: Ametupokea kama wana wake, yaani watoto wake, na anatupa kila kitu mikononi ili tuweze kuishi kwa utukufu wake.

Hata Paulo anatuambia, ili kutufariji, kwamba katika njia kuelekea utukufu bado hajalifikia lengo hilo, wala hajawa mkamilifu bado. Lakini mwelekeo wake ni sahihi; analikaza mwendo kuelekea lengo, kwa sababu ameshikwa na kukamatwa na lengo hilo – yaani na Kristo. Hiyo ndiyo siri yake.

Kubadili upande, na juhudi zote pamoja na kujitoka kote, taabu zote, kujinyima kote na uthabiti wote – vyote vitakuwa na faida. Katika utukufu hatutakuwa tena na nafasi hii ya pekee. Kwa hiyo wakati wetu “katika mwili” (2

Wakorintho 5:10), katika maisha yetu ya duniani, una thamani kubwa ajabu. Hauwezi kurudiwa, na nafasi zilizomo ndani yake hazitatolewa kwetu tena.

“Mungu bikutupa robo ya woga

(kufa moyo, masiwasi),

bali (robo)

ya nguvu,

na ya upendo,

na ya moyo wa kiasi

(nidhamu, kujitawala, utulivu).”

2 Timotheo 1:7



Njia yetu kuelekea lengo si kupanda mlima mfululizo tu katika ukuaji wa kiroho na katika utakaso. Kuna kushuka mlima, kuna kusimama na kukwama, lakini pia kuna kupanda. Mwelekeo lazima uwe sahihi, nalo lengo lenyewe linatuvuta – tukimtaazama Yesu, mwenye kuanzisha imani na mwenye kuitimiza!

17. Bibliografia¹⁰³

- Adams, Jay E., *Grundlagen biblischer Seelsorge*, Gießen, 1983.
- Anderson, Neil T., *Neues Leben – neue Identität*, Lage, 1994.
- Anderson, Neil T., *Restored, Experience Life with Jesus*, Franklin, USA, 2007.
- Anderson, Neil T., *Spiritual Warfare*, Ventura, California, USA, 2000.
- Anderson, Neil T., *Steps to Freedom in Christ*, Oxford, 2000.
- Anderson, Neil T., *Winning the Battle within*, Eugene, Oregon, USA, 2004.
- Barclay, William, *Geist oder Fleisch*, Augsburg, 1967.
- Binde, Fritz, *Vom Geheimnis des Glaubens*, Wuppertal, 1979.
- Bullinger, Dr. E. W., *Die zwei Naturen in dem Kind Gottes*, Düsseldorf, 1907.
- Burkhardt, Helmut, *Christ werden, Bekehrung und Wiedergeburt*, Gießen, 1999.
- Custance, Arthur C., *Man in Adam and in Christ*, Grand Rapids, 1975.
- Edman, V. Raymond, *Das ausgetauschte Leben*, Kassel, 1963.
- Eldredge, John, *Der ungezähmte Christ*, Gießen, 2005.
- Gahan, M. C., *The Soul's Transfer from Adam to Christ*, Michigan, 1957.
- Gibson, Jean, *Training im Christentum 3*, Bielefeld, 1990.
- Heijkoop, H. L., *Der Heilige Geist*, Zürich, 1955.
- Hession, Roy, *Nicht ich – sondern Christus*, Bad Liebenzell, 1980.
- Hille, Rolf (mh.), *Ein Mensch, was ist das?*, Wuppertal, 2004.
- Hole, F. B., *Das große Heil Gottes*, Zürich, 1979.
- Ironside, Henry Allen, *Heiligung – Zerrbild und Wirklichkeit*, Bielefeld, 1989.
- Käser, Ernst, *Rechtfertigung des Lebens*, Herblingen, 1989, toleo la 2.
- Kelly, William, *Die Lehre des NT über den Heiligen Geist*, Neustadt, 1975 (1880).
- Kettling, Siegfried, *Wer bist du, Adam?*, Wuppertal, 1978.
- Lutzer, Erwin W., *Das widerspenstige Ich*, Bielefeld, 2011.
- MacDonald, William, *Der vergessene Befehl: Seid heilig!*, Bielefeld, 1988.
- Markmann, Otto, *Weiter zu etwas Höherem*, tathmini ya kiukosoaji ya kitabu “Das normale Christenleben” cha Watchman Nee.
- Mauerhofer, Erich, *Der Kampf zwischen Fleisch und Geist bei Paulus*, Frutigen, 1980.

103. Nimetumia vitabu vilivyotajwa, na kwa sehemu nimevinukuu. Lakini orodha hii haimaanishi hata kidogo kwamba ninakubaliana na kila kinachosemwa katika vitabu vilivyoorodheshwa.

Medema, H. P., *Romeinen 7; Het normale en het abnormale christelijke leven*, Vaassen, 1998.

Modersohn, Ernst, *Die herrliche Freiheit der Kinder Gottes*, Bielefeld, 2008.

Nee, Watchman, *Befreiung*, Stuttgart, 1978.

Nee, Watchman, *Das normale Christenleben*, Wuppertal, 1972.

Nee, Watchman, *Der geistliche Christ*, Juzuu 1 – 3, Heerbrugg, 1975.

Nee, Watchman, *Freiheit für den Geist*, Winterthur, 1969.

Nee, Watchman, *Geistliche Erkenntnis*, Berneck, 1978.

Nitsche, Walter / Peters, Benedikt, *Dämonische Verstrickungen – Biblische Befreiung*, Berneck, 1989.

Nitsche, Walter, *Versagen und innere Zerrissenheit*, Berneck, 1989.

Ouweneel, Willem J., *Geestelijke Strijd*, Vaassen, 1998.

Ouweneel, Willem J., *Geloofs-Zekerheid*, Vaassen, 1996.

Ouweneel, Willem J., *Hoe lief heb ik uw Wet!*, Vaassen, 2001.

Paxson, Ruth, *Life on the Highest Plane, God's Plan for spiritual Maturity*, Grand Rapids, 1983.

Pink, Arthur, *Practical Christianity*, Michigan, 1974.

Ryrie, Charles C., *Ausgewogen statt abgehoben*, Dillenburg, 1994.

Ryrie, Charles C., *Hauptsache gerettet?*, Dillenburg, 1998.

Ryrie, Charles C., *Ihr werdet Kraft empfangen*, Dillenburg, 2003 (1965).

Schirmacher, Thomas, *Ethik*, Juzuu 1, *Das Gesetz der Liebe*, Nürnberg, 2001.

Steidl, Grant, *Konflikt!*, *Der Christ im Widerstreit*, Hückeswagen, 1992.

Steinberger, Georg, *Das Geheimnis eines siegreichen Lebens*, Stuttgart, 1983.

Stott, J. R. W., *Men Made New*, London, 1966.

Thomas, Major W. Ian, *Christus in euch – Dynamik des Lebens*, Holzgerlingen, 2008.

Thomas, Major W. Ian, *The Indwelling Life of Christ*, Colorado Springs, 2006.

Thomas, Major W. Ian, *The Saving Life of Christ*, Grand Rapids, 1961.

Thomas, Major W. Ian, *Tote können nicht sterben*, Neuhausen-Stuttgart, 1973.

Trumbull, Charles G., *Befreiung von der Macht der Sünde*, Basel, 1986.

Willard, Dallas, *Aus dem Herzen leben* (jina la asili: *Renovation of the Heart*), Gießen, 2004.

Willard, Dallas, *The Divine Conspiracy, Rediscovering our hidden Life in God*, New York, 1997.

Vijitabu, makala na insha kuhusu mada hii

- Blackburn, John S., *Die Befreiung im Römerbrief*.
 Böhm, Heinz, *Die geleugnete Wirklichkeit*, Berneck, 1993.
 Cutting, George, *Die beiden Naturen*, Zürich.
 Cutting, George, *Freedom from Sin: What is it?*
 Ebertshäuser, Rudolf, *Mit Christus gekreuzigt und auferweckt*, Leonberg, 2009.
 Glassford, Greg, *Hey, Fleisch! Hier spricht dein Geist!*, Hamburg, 2004.
 Grant, F. W., *Deliverance: What is it?*
 Grant, F. W., *Life in Christ and sealing with the Spirit*, Bedford.
 Grant, F. W., *Some Themes on the second Part of Romans*, Bedford.
 Grant, F. W., *The two Natures and what they imply*, Bedford.
 H. E. C., *The Believer's two Natures*.
 Herrick, Greg, *Old Man and New Man in Paul*, 1999.
 John MacArthur's One Nature Teaching,
<http://www.middletownbiblechurch.org/doctrine/1natjm01.htm>
 Lüscher, Albert, *Der alte und neue Mensch*, Langenthal, 1971.
 Lüscher, Albert, *Euer Leben ist verborgen*, Langenthal.
 Pink, Arthur W., *The Christian in Romans 7*.
 Scofield, C. I., *The two Natures*.
 Trachsel, Walter, *Ein reines Herz?*, Frutigen.
 Trachsel, Walter, *Gibt es ein Leben im Sieg*, Frutigen, 2003.
 Trachsel, Walter, *Heilig sein oder heilig werden?*, Frutigen, 2009.
 Trachsel-Pauli, Ernst, *Heiligung nach Geist, Seele und Leib*, Frutigen, 2000.
 Wallis, Reginald, *The new Life, Talks with Christians about Practical Victory*, New Jersey, 1932.

Tovuti

- <http://www.bibelkommentare.de>;
<http://www.biblecentre.org/>;
<http://www.bodedesheils.nl/>
<http://www.soundwords.de/>
<http://www.streitenberger.com/>: orodha ya barua pepe Bibelgriechisch
 (Kiyunani cha Biblia; kuingia ni bure; mahali pa kubadilishana mawazo kati ya

wanaojua Kiyunani; nafasi ya kuuliza maswali kuhusu lugha ya maandishi ya Biblia na kupata majibu).

Vitabu vya ufafanuzi

Brockhaus-Kommentar zur Bibel, Wuppertal, 1985.

Calvin, Johannes, *Auslegung der kleinen paulinischen Briefe*, Neukirchen, 1963.

Cecil, A. P., *A Summary of the Epistle to the Romans*.

Coates, C. A., *Ein Überblick über den Brief an die Römer*, Leipzig.

Cousar, Charles B., *Galatians, A Commentary for Teaching and Preaching*, Atlanta, 1982.

Darby, J. N., *The Collected Writings*, Winschoten, 1972 (chapa mpya).

Ellicott, Charles John, *Bible Commentary*, London, 2004 (chapa mpya).

Grant, F. W., *The Numerical Bible*, New Jersey, 1901.

Greijdanus, Dr. S., *Korte Verklaringen*, Kampen, 1932.

Hoehner, Harold W., *Ephesians, An exegetical Commentary*, Michigan, 2002.

Jantzen, Herbert, *Vorträge zu Röm 6 – 8*, 1997.

Kelly, William, *Lectures Introductory*, 1869.

Kelly, William, *Lectures on the Epistle to the Ephesians*, Oak Park.

Kelly, William, *Notes on the Epistle to the Romans*, Sunbury, 1981 (1873).

Kelly, William, *The Bible Treasury*, Winschoten.

Kelly, William, *The Epistles of Peter*, London, 1904.

Kramer, G. H., *Christus ons leven*, Vaassen, 1994.

Lee, Witness, *Der Brief des Paulus an die Epheser*, Stuttgart, 1980.

Lincoln, William, *Assembly Writer Library*, Glasgow, 1980.

MacDonald, William, *Kommentar zum NT*, Juzuu 1, Bielefeld, 1992.

Medema, H. P., *De nieuwe Mens*, Vaassen, 1991.

Medema, H. P., *Der Brief an die Römer*, Bielefeld, 1992.

Medema, H. P., *Het leven is geopenbaard, De Eerste Brief van Johannes*, Vaassen, 1993.

Nicholson, J. B., na Waugh, G. P., *Was die Bibel lehrt, 1. und 2. Petrusbrief*, Dillenburg, 1991.

Ouweneel, W. J., *De vrijheid van de Geest*, Vaassen, 1997.

Ouweneel, W. J., *Christus unser Leben*, Schwelm, 1984.

Remmers, Arend, *In Christus gesegnet*, Hückeswagen, 2004.

Schaeffer, F., *Allein durch Christus, Die zentralen acht Kapitel des Römerbriefs*, Holzgerlingen, 1999.

Smith, Hamilton, *The Epistle to the Ephesians*, Edinburgh.

Smith, Hamilton, *The Epistles of Peter, An Expository Outline*, Edinburgh.

Stadelmann, Helge, *Der Epheserbrief*, Neuhausen-Stuttgart, 1993.

Stallan, Fred, *Was die Bibel lehrt, Römerbrief*, Dillenburg, 2001.

Stanley, Charles, *On the Epistle to the Romans*, London, 1885.

Stott, John R. W., *Die Botschaft des Epheserbriefes*, Nürnberg, 2001.

Stott, John R. W., *The Letters of John, Tyndale New Testament Commentaries*, Nottingham, 1964, 1988.

Wasserzug, Gertrud, *Der Römerbrief*, Böblingen, 1984.

Witmer, John A., *Romans, The Bible Knowledge Commentary*, 1983.

Wolston, W. T. P., *Simon Peter, His Life and Letters*, Edinburgh, 1892.

Wuest, Kenneth S., *Romans in the Greek New Testament*, Michigan, 1955.

Vifupisho vilivyotumika kwa tafsiri nyingine za Biblia

Elb *Elberfelder Übersetzung, nicht revidiert*, Berlin, 1961.

ER *Elberfelder Übersetzung, revidierte Fassung*, R. Brockhaus Verlag Wuppertal, toleo la 8, 2001.

Luther 1912 *Die Heilige Schrift nach der deutschen Übersetzung Martin Luthers*, Stuttgart, 1912.

Menge *Die Heilige Schrift Alten und Neuen Testaments*, imetafsiriwa na Dr. H. Menge, Berlin, 1960.

NeÜ *Neue evangelistische Übersetzung* ya Karl-Heinz Vanheiden, Dillenburg, 2010.

Schl 2000 *Die Bibel, übersetzt von F. E. Schlachter (Version 2000)*, Genf, toleo la 1, 2003.

Schlachter *Die Heilige Schrift des Alten und Neuen Testaments*, imetafsiriwa na F. E. Schlachter, Genf, 1990.

Kuhusu mwandishi

Hans-Jörg Ronsdorf, aliyezaliwa mwaka 1964, ameo; mke wake anaitwa Christine. Wana watoto 5 na wanaishi katika eneo la Allgäu, jimbo la Bavaria. Baada ya mafunzo yake ya ufundi wa kutengeneza zana za mashine, alifanya kazi katika sekta mbalimbali. Kwa zaidi ya miaka 10 amejajiri kama mshauri na msambazaji katika sekta ya upakaji rangi.

Yeye ni mmoja wa wazee wa kanisa la Christliche Gemeinde huko Kempten, na anahudumu katika kuhubiri na katika kufundisha Biblia.

Hans-Jörg Ronsdorf

Hata Hivyo, Wafu Wako Hai (Und die Toten leben doch)



Kutokufa kwa Nafsi

Kurasa 240, jalada laini

ISBN 978-3-89397-227-2

Je, wafu wako hai – au kifo ndicho mwisho wa kuwepo kwote? Je, mwanadamu anaingia katika usingizi wa nafsi – au ana ufahamu hata baada ya kifo? Haya ni maswali yanayomhusu kila mwanadamu. Kusudi la kitabu hiki ni kujibu maswali haya, na pia kuleta tumaini. Somo kuu la kitabu ni swali la kutokufa kwa nafsi. Wafu walio hai – Biblia inalifumbua fumbo hili: Kifo si mwisho, bali ni mwanzo wa maisha yasiyokoma kamwe. Ukweli wa maneno haya unathibitishwa na Mtu aliyekufa na kufufuka – Yesu Kristo, aliyerudi kutoka katika ufalme wa mauti na kuifungua njia inayoongoza kwenye uzima.